BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Ishirini na Mbili - Tarehe 2 Julai, 2010

(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Anna S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILLIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Kamati ya ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano,Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MHE.MAGDALENA H. SAKAYA, MSEMAJI MKUU WA KAMATI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Msemaji wa Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadiro ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIKANO WA AFRIKA YA MASHARIKI PAMOJA NA NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Randama za Makadiro ya Matumizi ya Wizara ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MHE SEIF ALI IDDI (K.n.y. WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI):

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Benki Kuu ya Tanzania kwa Mwaka 2008/2009 *[The Annual Report and Audit Accounts of the Bank of Tanzania for the Year 2008/2009]*.

MASWALI NA MAJIBU

Na.155

Kampuni za Biashara Kutoa Asilimia 0.3 ya Mapato Yake kwa Halmashauri

MHE. OSCAR R. MUKASA aliuliza:-

Sheria Na. 9n ya LGFA ya Mwaka 1998 inazitaka Kampuni za Biashara kutoa asilimia 0.3 ya Mapato yake (baada ya kulipa kodi zote) kwenye Halmashauri wanapofanyia shughuli zao,lakini zipo kampuni ambazo zimekuwa hazitoi malipo hayo kwa sababu tu shughuli zao ziko kwenye Miji mikubwa kama Mwanza, Dar es Salaam, na baadhi ya kampuni za jinsi hiyo pamoja na *TIGO,ZAIN* na *VODACOM* ambazo zimeshindwa kulipa kiasi hicho kwa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo.

Je, Serikali iko tayari kufanya marekebisho haraka kwenye utaratibu uliopo sasa ili sheria hiyo iweze kutekelezwa kulingana na kusudi lake?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mbunge wa Biharamulo napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya fedha za Seriakli za Mitaa Sura 290 ilitungwa na Bunge mwaka 1982 na hivyo kutumika kwa zaidi ya miaka 28. Kwa muda wote huo yametokea mabadiliko mbalimbali ya kisera, kiuchumi, kijamii, kisheria na kihasibu ambayo yameifanya sheria hiyo kuonekana imepitwa na wakati.

Kufuatia hali hiyo na kutokana na hitaji la utekelezaji wa sera ya *D by D*, ilionekana kuna haja ya kupitia sheria hiyo ili kuyaingiza mabadiliko mbalimbali katika mfumo wa sheria, pamoja na *Memorandum* ya fedha za Mamlaka za Serikali (*Local Authority Financial Memorandum of 1997).*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290 kwa mujibu wa kifungu cha 7(1) (z) inazitaka kampuni za biashara kutoa asilimia 0.3 ya mapato yake (baada ya kulipa kodi zote) kwenye Halmashauri wanapofanyia shughuli zao, lakini zipo kampuni ambazo zimekuwa hazitoi malipo hayo kwa sababu tu Makao Makuu ya shughuli zao yako kwenye Miji mikubwa kama vile Mwanza na Dar es Salaam.

Tatizo hili sio kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo peke yake bali lipo karibu kwenye Halmashauri nyingi nchini na Wizara yangu imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwenye Halmashauri hizo mfano, Kahama, Mtwara, Mikindani,Geita na kadhalika zikilalamikia baadhi ya makampuni kutolipa kodi ya huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Halmashauri hazina sheria ndogo zinazoiwezesha kukusanya ushuru huo wa huduma na hivyo makampuni hayo kutumia mwanya huo wa kugoma kulipa na wakati mwingine ni suala la tafsiri ya sheria yenyewe na sheria ndogo za Halmashauri.

Napenda kusisitiza kwamba msingi Mkubwa wa ushuru huo ni mahali ambapo kampuni na taasisi inafanyia shughuli au biashara zake ili mradi kampuni na taasisi hizo zina ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua changamoto hizo Wizara yangu tayari ipo katika mchakato wa kuifanyia marekebisho sheria ya fedha za Serikali za Mitaa Sura 290.

Baadhi ya mambo muhimu katika mapendekezo ya sheria hiyo ni kupanua wigo wa kulipa ushuru na kuweka mfumo mzuri wa ulipaji wa ushuru,(*service levy*) kwa kuondoa migongano iliyokuwepo ambayo ushuru huo ulikuwa unalipwa kwenye Halmashauri ambayo kampuni hiyo ina Makao Makuu hata kama shughuli zake zinafanywa nje ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya marekebisho haya yataziongezea mapato Mamlaka za Serikali za Mitaa, yataziwezesha Serikali za Mitaa hizo kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo, yataziondolea Mamlaka hizo migogoro juu ya Halmashauri ipi inapaswa kulipwa ushuru kwa huduma na kupunguza ukwepaji wa kulipa ushuru mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mapendekezo ya marekebisho hayo kwa sasa yanajadiliwa na wadau mbalimbali kwa kupata maoni ambayo yataboresha utekelezaji mzuri wa sheria hiyo. Baada ya kupokea maoni hayo tutaleta hapa Bungeni mapendekezo ya marekebisho ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati huu ambapo wadau wanaendelea kutoa maoni yao kwa lengo la kuifanyia marekebisho sheria. *(Makofi)*

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru na nashukuru majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba kuwa na swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa, Naibu Waziri amekiri hapa kwamba hili ni tatizo na ni tatizo ambalo ni pana kwa maana linatokea kwenye Halmashauri nyingi na kwa kuwa tatizo hili limekuwa la muda mrefu na hivyo Halmashauri zetu zimekuwa zinakosa mapato hasa ukichukulia kuna baadhi ya Halmashauri kama ya Biharamulo ambayo wigo wa mapato ni mdogo.

Je, Serikali ipo tayari sasa baada ya kukiri kuanza mchakato wa kurekebisha sheria hii, iko tayari kututhibitishia ni lini mchakato huu unatarajiwa kukamilika ili kuepuka uwezekano wa mchakato kwenda kwa muda mrefu bila ukomo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, labda niweke vizuri hapa jambo hili tusije tukafika mahali watu wakaanza kufikiri kwamba sasa kwa vile tunaanza marekebisho. Kwa hiyo, tunamaanisha kwamba huu ushuru usilipwe. Nimecheki na Dodoma, nimecheki na Arusha, nimecheki na maeneo mbalimbali yanaendelea kuokota ushuru huu pamoja na mapungufu haya ambayo nimekiri kwamba yako hapa. Sasa anataka kujua ni muda gani itachukua, wewe mwenyewe unafahamu na Wabunge wenzangu wote tunafahamu kwamba kipindi hiki huwa hatuleti sheria hapa, tunazungumzia mambo ya Bajeti tu. Kwa hiyo, tuombe tena Mungu akitujalia tena huko mbele ya safari kama tutakwenda, tutapita salama mimi ninaamini Serikali ipo na tutafanya marekebisho hayo.

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yanaleta mategemeo, na kwa kuwa swali lililoulizwa linahusiana na simu za mkononi na kwa upande wangu mimi naipongeza Serikali kwa kutoa muda wa kutosha kabisa kuhusu usajili wa simu, lakini lililojitokeza ni kwamba wenyewe wenye kampuni za simu watu wamesajili, lakini wanapouliza namba zao na wanapopiga simu wanasema hazijasajiliwa. Je, zitakapofungwa simu zao baada ya tarehe 16 Julai, 2010 nani atachukua dhima ya fidia ya gharama ambazo anakula hasara mteja?

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, juzi wakati nikiwasilisha Bajeti yangu nilieleza kwamba kikomo cha kusajili simu ilikuwa ni siku ya tarehe 30 Juni, 2010 ifikapo saa sita usiku, lakini nikaongeza kwamba kutokana na usikivu ya Serikali ya awamu ya nne ya Chama cha Mapinduzi, imetafakari kilio cha watu walio wengi na kuongeza majuma mawili hadi

kufikia tarehe 15 Julai, 2010. Tamko hili limepokelewa kwa hisia mbalimbali, wengi mtakuwa mmesikiliza kipindi cha redio jana asubuhi na kwenye magazeti. Watu walio wengi zaidi wamelaumu kwa kuongeza huo muda kwamba Watanzania tunaonekana kwamba hatupendi kufuata *discipline* ya maamuzi tunayoyafanya na kwamba tumeongeza muda wa watu kutukana zaidi wakati huu tunapoelekea kwenye uchaguzi. Kwa hiyo, sio nia ya Serikali tena kuongeza muda wa kusajili simu na ifikapo tarehe 15 saa sita ya usiku simu ambazo hazijasajiliwa zitazimwa na mpaka pale watu watakapoweza kulipia tena.

Mheshimiwa Naibu Spika,napenda kutoa hayo maelezo.

Na. 156

Ujenzi wa Kituo cha Afya kila Kata na Zahanati kila Kijiji

MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y. MHE. DR. IBRAHIMU S. MSABAHA) aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa ujenzi wa vituo vya Afya katika kila Kata na Zahanati katika Kijiji unatekelezwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ibrahimu Said Msabaha, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) umeanza kutekelezwa mwaka 2007 na unategemewa kukamilika mwaka 2017.

Moja ya mambo ya muhimu yanayotekelezwa ni ujenzi wa kituo cha Afya katika Kata na Zahanati kwa kila Kijiji na ujenzi wa Hospitali za Wilaya. Ili kuhakikisha kuwa lengo hilo linatimia, Serikali kupitia MMAM imepanga kutekeleza kwa hatua mambo yafuatayo:-

(i) Uimarishaji wa vituo vya Afya na Zahanati zilizopo ili ziweze kutoa huduma bora. Uboreshaji huu unafanyika kwa kukarabati Vituo vya Afya na Zahanati.

(ii) Kusomesha na kuajiri wataalam wa fani mbalimbali za Afya, katika vituo vya Afya na Zahanati ambavyo vimeshajengwa na kwa ajili ya vile vituo vitakavyojengwa.

(iii) Ununuzi wa vifaa na madawa kwa ajili ya vituo hivyo vya kutolea huduma za Afya.

(iv) Kuimarisha usimamizi na kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora.

(v) Kushirikisha Wananchi katika ujenzi wa vituo hivi na uchangiaji wa gharama za dawa kupitia mfuko wa Afya ya Jamii na Mfuko wa Bima ya Afya.

(vi) Kushirikisha sekta binafsi na Mashirika ya Dini katika kujenga na kuendesha vituo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha utekelezaji huo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeendelea kutoa ruzuku ya kutekeleza programu wa MMAM kama ifuatavyo, mwaka 2008/2009 jumla ya shilingi 29,383,519,720/= zilitolewa kukarabati Zahanati na Vituo vya Afya na kwa mwaka 2009/2010 Serikali imetenga jumla ya shilingi 23,000,000,000/=. Hivyo, Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka ili kuhakikisha kuwa mpango huo inaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2008/2009, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha walipatiwa shilingi 52,557,410/= na kwa mwaka 2009/2010 wametengewa shilingi 42,943,096.68. Aidha, mpango wa Kijiji kipi au Kituo kipi cha Afya kipatiwe fedha ni maamuzi ya vikao vya Halmashauri husika.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na maelezo mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, naomba nimwulize ametaja mambo matano yatakayo saidia kuendelea huwo mradi mpaka mwaka 2017 uwe

umekamilika, laikini nataka nimuulize ni sababu zipi zinazopelekea kupunguza pesa badala ya kuongeza kama alivyosema yeye mwenyewe, kati mwaka wa fedha 2008/2009 zilitengwa shilingi bilioni 26.4, mwaka uliofuata wa fedha wakatenga bilioni 27 lakini hata kwenye zahanati kwenye Mji wa Kibaha badala ya kuongeza wakapunguza.

Mwaka wa fedha 2008/2009 52 milioni zilitengwa lakini mwaka uliofuata zikapunguzwa bilioni 42. Ni kwa nini Serikali badala ya kuongeza pesa inapunguza pesa, kitu amabcho kinahathiri utekelezaji wa kazi hizi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani ili swali ni rahisi kwa sababu sisi wote tumeshiriki katika kupitisha Bajeti hizi, ninajua kabisa kwamba Mheshimiwa Ndassa anazungumzia eneo ambalo ni muhimu sana na tukifanya mchezo hapa watu wetu watakufa, hilo natambua yani siwezi kusahau hapa kwamba ukipunguza maanayake ni kwamba huduma kwa akina mama wanaojifungua watapata matatizo.

Lakini sasa sisi wote tunafahamu kabisa kwamba sasa hivi Bajeti tuliyopitisha hapa imekuwa na *Constrains* na mnajua kabisa kwamba tumejibana na Waziri wa Fedha alitueleza hapa.

Kwa hiyo, zimekuwa zinapungua kwa sababu tu kwamba uwezo wetu wa kiuchumi bado umekuwa uko chini na kwa hiyo, Halmashauri ilipokuwa ipanga imewekewa na *ceiling* hapa haikuweza kupanga nje ya kiasi hicho, ndivyo ilivyopangwa kwa maana ya Bajeti hii.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi wana utaratibu mzuri, wana mpango wa MESS MEMM na fedha zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu zinapelekwa kwenye Halmashauri.

Je, kwa nini Wizara ya Afya isiwe na mapango kama huo, fedha za kujenga vituo vya afya zingefahamika ili ziweze kupelekwa katika Halmashauri za Wilaya badala ya kusema kwamba Serikali ina mpango wa kusaidia kujenga vituo vya afya? *(Makofi)*

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliopo ni wa uwazi na tunafikiri unatekelezeka, kwa sababu hivyo vituo wanaovijua ni Halmashauri na watakaoviendesha ni Halmashauri na tunavyopeleka pesa katika Halmashauri ndio wanatambua ni vituo vipi ambavyo viko katika hatua nzuri wavisaidie.

Katika mtazamo wetu ni kwamba wananchi waanze halafu tunaweza tukuwasaidia mabati na vitu ambavyo vinahitaji pesa kutoka mfukoni na mpaka hivi sasa wengi wamefanya kazi nzuri na ningependa kuwapongeza.

Katika hotuba yangu siku ya Jumatatu kwenye jedwali niliambatisha katika hotuba yangu niliionyesha kwamba Halmashauri ya Iringa wao wamekamilisha vituo 21 na tunavipatia dawa na Urambo vituo 20.

Lakini kwa mwuliza swali kwa maana ya Mheshimiwa Dr. Msabaha mwaka jana na mwaka huu hakuna kituo ambacho wamekiombea, ina maana kwamba hakuna kilichojengwa.

Na. 157

Mawaziri kutokuwa na Mamlaka ya Kutoa Maamuzi ya Kiutendaji katika Wizara

MHE. ZUBEIR ALI MAULID (K.n.y. MHE. MUSSA A. ZUNGU) aliuliza:-

Baadhi ya Sheria zilizotungwa na Bunge hili zinawanyima Mawaziri kutoa maamuzi katika Wizara na hivyo kuisababisha mgongano baina yao na Makatibu Wakuu katika Wizara, jambo ambalo huchelewesha maendeleo na pindi linaapotokea tatizo huwajibishwa Waziri na siyo Katibu Mkuu:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuzipitia Sheria hizo zinazokwaza Maendeleo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri huteuliwa na Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 55(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo

pia majukumu yao ya msingi yameelezwa katika ibara ya 54(3) ya hii katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya Mawaziri umeelezwa pia katika Sheria ya *The Ministers (Discharge of Ministerial Functions) Act*, Sura ya 299 na kufafanuliwa zaidi katika Waraka wa Rais Na. 2 wa mwaka 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Miongozo hii Waziri ni Kiongozi wa Wizara ambaye wajibu wake ni kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera kulingana na Ilani ya Chama kilichoko madarakani wakati huo. Katika kutekeleza dhamana hiyo, Waziri ni Msimamizi Mkuu wa Shughuli husika na kuhakikisha kuwa malengo ya Wizara yanafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Waziri hawezi kumudu shughuli zote za Wizara peke yake, Katibu Mkuu ndiye Mtendaji Mkuu wa Wizara. Kwa maana hiyo, Katibu Mkuu ndiye Msaidizi Mkuu wa Waziri katika kutekeleza majukuu ya Wizara na kwa msingi huo, analo jukumu la uendeshaji wa shughuli zote za kila siku za Wizara kulingana na Sera za Serikali chini ya uongozi wa Waziri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondokana na migongano ambayo ingeweza katika utekelezaji wa kazi za Serikali, utaratibu na mgawanyo wa majukumu na kazi za Serikali pamoja na mipaka ya utekelezaji umeainishwa bayana katika miongozo niliyoitaja hapo juu. Kwa kuzingatia miongozo hiyo majukumu ya Waziri na yale ya Katibu Mkuu yamebainishwa wazi na hayana mgongano hata kidogo bali huongeza uwajibikaji na kumpunguzia Waziri jukumu la kufanya kila kitu yeye mwenyewe.

Aidha, Waziri anabakiwa na dhamana yake kubwa ya uongozi kwa kufuatilia utekelezaji na kuhakikisha malengo yanafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kutokana na maelezo hayo, siyo kweli kuwa Sheria zilizotungwa na Bunge hili zinawanyima Mawaziri nafasi ya kutoa maamuzi katika Wizara na hivyo kusababisha mgongano baina yao na Makatibu Wakuu wa Wizara. Kuwajibika kwa Waziri maana yake ni kukubali kutekeleza mambo yote yanayotokana na dhamana aliyopewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ukamilifu hata kama hakuhusika nayo moja kwa moja. *(Makofi)*

MHE. ZUBEIR ALI MAULID: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika jibu la msingi Mheshimiwa Waziri anasema kwamba migongano haipo. Lakini kuna ushahidi kwamba kuna migongano ambayo inatokezea ya kiutendaji baadhi ya maamuzi ambayo yanatolewa na Mawaziri yanapofuatiliwa kwa Makatibu Wakuu, Makatibu Wakuu huonekana kama wao ni wenye mamlaka ya juu kabisa ya ile Wizara husika.

Je, inapotokezea hali kama hii Mheshimiwa Waziri haoni kwamba haja ya sasa kubadilishwa hizo Sheria ili kumpa mamlaka Waziri peke yake katika ile Wizara au

tubadilishe Sheria ili Wizara iwe na kiongozi mmoja tu wa juu. Aidha kusiwe na Mawaziri ili Wabunge tuweze kusimamia vizuri hizo Wizara au Mawaziri wawe na Mamlaka ya mwisho kama zilivyo katika baadhi ya nchi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hakutoa mfano halisi wa pale ambapo mgongano umetokea. Lakini hata hivyo ikumbukwe kwamba Mawaziri na Makatibu Wakuu nao ni wanadamu na hakuna binadamu aliyekamilika. Inawezekana katika hali hiyo kumetokea migongano ambayo Mheshimiwa Mbunge anaisemea. Lakini haya yasichukuliwe kwamba ni udhaifu katika Sheria ni udhaifu wa kibinadamu tu. Lakini pale tu anapoona mfano atuletee ili tuweze kutatua tatizo linalotokana na migongano hiyo.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafisi niulize swali moja la nyongeza. Ni kwa nini Sheria zinazopitishwa na Bunge hili Tukufu zinachelewa sana utekelezaji wake hata baada ya kutiwa sahihi na Mheshimiwa Rais. Kwa mfano Bodi ya Mazao Mchanganyiko, Sheria ambayo imepitishwa toka Mkutano wa Bunge wa Kumi na Nane hadi leo, hata Bodi yenyewe haijaundwa, Bodi ambayo ina majukumu makubwa ya kununua bidhaa za wakulima.

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, Mawaziri wamegongana na Katibu Mkuu. Tafadhali hilo ni swali jipya kabisa. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais. Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir atauliza swali hilo.

Na. 158

Mafuta ya Petroli kuwa Suala la Muungano Kikatiba

MHE. HAFIDH ALI TAHIR aliuliza:-

Kwa mujibu wa *Hansard* za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1968, Bunge liliridhia mafuta ya petroli kuwa ya Muungano Kikatiba pindi yatakapogundulika katika ardhi ya Tanzania; na kwa kuwa, Baraza la Wawakilishi Zanzibar katika moja ya vikao vyake lilipitisha Muswada na kuutangazia umma juu ya kukubaliana mafuta na petroli kutokuwa ya muungano pindi yatakapogundulika:-

(a) Je, Serikali inatoa majibu gani juu ya ndio au hapana kwa jambo hilo kuwa la Muungano?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya maneno makali na ya kashfa yaliyotumiwa na baadhi ya viongozi wa Muungano wakati wa kupitisha Muswada huo ndani ya Baraza la Wawakilishi, Zanzibar?

(c) Je, nini kifanyike ili matakwa ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wa Tanzania, Zanzibar yaweze kufanikiwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mafuta na petroli liliingizwa katika orodha ya mambo ya Muungano mwaka 1968 katika kikao cha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na lilipigiwa kura na Wabunge kutoka pande zote mbili za Muungano.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Nyongeza ya Kwanza imeorodheshwa mambo 22 ya Muungano likiwemo suala la maliasili ya mafuta, pamoja na mafuta yasiyochujwa ya matokaa na mafuta ya aina ya petroli na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa na gesi asilia. Kwa maelezo hayo, Serikali inatambua kuwa suala la mafuta na petroli bado ni la Muungano hadi itakapoamuliwa vinginevyo. Hivyo Serikali haina jibu sasa la ndio au hapana.

(b) Serikali haina taarifa ya baadhi ya viongozi wa Muungano waliotoa maneno makali na ya kashfa wakati wa kupitisha Muswada ndani ya Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.

(c) Kiutaratibu kwa kuwa Muungano huu ni wa ubia na wa hiyari linalotakiwa kufanyika ni kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuiandikia Serikali ya Muungano rasmi kuonesha dhamira ya kuliondoa jambo hilo katika orodha ya mambo ya Muungano. Serikali ya Muungano ikiafiki, itabidi jambo hilo lipelekwe Bungeni ili watoe Baraka zao kwa kura kwa mujibu wa taratibu. Endapo Wabunge wa pande zote watakubali kila upande theluthi mbili yake jambo hilo litaondolewa katika orodha ya Mambo ya Muungano.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa jawabu lake linalokwenda sambamba na Katiba.

Lakini kwenye Sherehe za Mapinduzi kule Pemba ambazo zilikuwa ni za mwisho kwa Rais aliyopo sasa hivi anamaliza muda wake. Katika maelezo yake alitamka kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yeye wamekubaliana kuliondosha suala hili katika Mambo ya Muungano.

Je, Mheshimiwa Waziri unasemaje juu ya kauli hiyo ambayo kiutaratibu inakwenda kinyume na Katiba. Wewe kama Waziri unasemaje?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO: Mhesihmiwa Naibu Spika, swali la Mheshimiwa Hafidh ni suala gumu, tena rafiki yangu sana jamaa huyu sijui naona mambo yamebadilika leo. Kwa mujibu wa Katiba yetu huo ni utaratibu ambao nimeuelezea hapa lazima ufuatwe. Kauli ya Karume nimesikia kule Pemba na kauli ya Rais Kikwete nimesikia. Lakini wote hao wanasema tu, lakini ni wajibu wake, wote hawa wanafuata Sheria, Taratibu, hatima yake lazima ipite katika Bunge letu la Muungano. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Na sheria inaanza na mazungumzo.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa tamko hili limetoka ndani ya Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Waziri kama Waziri anayeshughulikia mambo ya Muungano anatoa tamko gani katika hili?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wa kushughulikia mambo makubwa kama haya unaeleweka. Mambo haya ni ya Sera na yataanzia kwenye Chama ambacho kina Serikali. Kwa hiyo, kama ma-Rais hawa ambao wote wanatoka kwenye Chama Cha Mapinduzi wanapaswa kulipeleka suala hili kwenye chama chao na kuanzia hapo ndiyo mchakato wa kuliondoa kwenye Katiba utafanyika. Huu ndiyo utaratibu ambao tumejiwekea ambao hautegemei ukubwa wa kambale na sharubu zake. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 159

Kuandaa Programu ya Utalii Hifadhi ya Taifa Kitulo

MHE. JANET B. KAHAMA (K.n.y. CYNTHIA H. NGOYE) aliuliza:-

Kwa kuwa Hifadhi ya Taifa Kitulo inaunganishwa na mtandao wa safu za Milima ya Livingstone ambayo inasambaa katika Wilaya za Rungwe, Kyela, Makete, Ludewa na Mbinga pamoja na Milima ya Rungwe na kwa kuwa maeneo haya hayajatangazwa ili kuvutia utalii wa ki-ikolojia unaovutia watu wengi wanaobahatika kutembelea maeneo hayo:-

Je, ni lini Serikali inaandaa program maalum ya utalii wa safu za Milima ya Livingstone, Milima ya Rungwe na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo kwa pamoja?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mbeya, kama ifuatavyo:-

Kitulo ni Hifadhi yenye hadhi ya kipekee Barani Afrika kutokana na maumbile yake ya mwinuko au uwanda ulio juu kabisa Barani Afrika. Uwanda wa Kitulo hujulikana pia kama Bustani ya Mungu kutokana na mimea yake ya asili isiyopatikana

popote duniani, ambapo upekee huo unawafanya wataalam wa mimea kuipa jina ya Serengeti ya Maua kwa sababu ya wingi na aina tofauti za mimea.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa Sekta ya Utalii nchini unaongozwa na Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999. Sera hii imeeleza bayana mikakati ya kukuza na kuendeleza mazao ya utalii ikiwa ni pamoja na kuendeleza mazao yaliyopo na kukuza mazao mapya. Ardhi, upo mpango wa kuendeleza utalii *(Tourism Master Plan)* ambapo kuanzia mwaka 2000 umetilia mkazo kuendeleza Utalii wa Kanda wa Kusini. Tayari Wizara, Bodi ya Utalii yaani *TTB* na *TANAPA* imeanza kuhamasisha wageni kutembelea nyanda za juu Kusini kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Wizara kwa kushirikiana na wadau na uongozi wa Mkoa wa Iringa, iliadhimisha Siku ya Utalii Duniani Kitaifa mjini Iringa Septemba, 2009 ambapo Mkoa wa Iringa ulitamkwa rasmi kuwa kitovu cha utalii wa Ukanda wa Kusini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuchapisha makala zenye kusifu uzuri na mvuto wa Hifadhi ya Kitulo na safu za milima ya nyanda za juu Kusini. Makala na picha zimechapishwa kwenye vipeperushi mbalimbali kama vile *TANAPA brochures*, *TTB – Tantravel*, *TTB – selling Tanzania*, *Tanzania Toursim and Trael Directory* na Ramani ya Tanzania.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, safu ya milima ya Nyanda za juu pamoja na Kitulo zimetajwa kwenye tovuti za kutangaza utalii za *TTB* na *TANAPA.*

(d) Filamu za kutangaza vivutio vya utalii hapa nchini zimejumuisha Hifadhi ya Taifa ya Kitulo. Filamu hizo ni pamoja na Filamu zilizopigwa na *Tanzania Safaris Channel* na Filamu ya *TANAPA* inayotangaza sifa za Hifadhi zote ikiwemo Hifadhi ya Kitulo.

(e) Bodi ya Utalii na *TANAPA* zimekuwa zikihamasisha wakala wa biashara ya utalii, kujumuisha eneo hili katika misafara ya kutembeza watalii hapa nchini. Baadhi ya wakala wa utalii tayari wameanza kujumuisha safari za Kusini Magharibi mwa Tanzania (ikiwemo eneo la Kitulo) katika mauzo yao ya safari *(Safari Packages).*

(f) Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Utalii yaani *TTB* iko mbioni kufungua Ofisi ya Utalii ya Kanda ya Kusini itakayokuwa Iringa katika mwaka ujao wa fedha ili kuwahudumia kwa karibu watalii watakaotembelea eneo hilo.

MHE. JANET B. KAHAMA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. Nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri na mipangilio mizuri ambayo Wizara inayo katika kuvutia utalii katika eneo la Kitulo.

Je, Serikali ina mpango gani basi katika kuhakikisha kwamba wawekezaji wanakuja kujenga hoteli nzuri kwa ajili ya watalii pamoja na kujenga barabara nzuri ambayo itatoka Chimala kwenda Kitulo na barabara ambayo itatoka kupita Madaba, Mlangali, Lupila, Ikonda, Lupalilo, Kisinga, Ndulamilo, Make, Ujuni, Kitulo mpaka Isonje? *(Makofi)*

Swali la pili. Kwa kuwa madhumuni ya kwanza katika kuanzishwa mradi huu mkubwa wa Kitulo ilikuwa pamoja na kilimo cha ngano pamoja na ufugaji wa kondoo ambao wanazalisha pamba kama *wool* ambayo inatumika kutengeneza nguo.

Je, Serikali ina mpango gani au imelifuatiliaje jambo hili ili kusudi na sisi tuwe kama Australia tuweze kuzalisha kwa ajili ya biashara kuzalisha *wool?*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hafidh Ali unakata katikati ya Spika na Msemaji. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, labda kabla ya kujibu nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kujua maeneo hayo vizuri sana, hasa kwenye maeneo ya miundombinu. Hakuna yawezekana amewahi kuishi huko. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameulizia kuhusu suala la wawekezaji. Sisi katika Wizara mwaka 2008 tumepitisha Sheria mpya ya Utalii, Sheria Na. 11. Katika Sheria hiyo pamoja na mambo mengine inaweka vigezo vya ubora unaotakiwa katika utoaji wa huduma za *hospitality.*

Katika kanuni ambazo tayari zimekwishakuandaliwa na zinatumika, Wizara inasimamia hoteli zinazojengwa na mwekezaji anachagua hoteli ya namna gani kutegemea na mtaji alionao ili mradi sisi kama Wizara tunaangalia ubora wake na kuipa *grade* inayostahili.

Kwa hiyo, changamoto iliyoko ni kwa wananchi wa eneo hilo kuwahamasisha wawekezaji sisi tunasimamia zaidi ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la barabara, kwa kweli naona hapa mama kanionea kidogo, maana hili suala sisi ni wadau tu na tunahamasisha Halmashauri na sisi wenyewe tunashughulikia barabara ambazo ziko ndani ya hifadhi. Kwa maana ya zilizoko ndani ya *Kitulo National Park.* Kwa hiyo, nilichukue hili, Mheshimiwa Waziri

wa Miundombinu yupo hapa amesikia. Lakini pia nitamdokezea kwa sababu tupo karibu ili aweze kulitazama eneo hili kwa sababu ni la muhimu sana kwa utalii, ambao unaongeza uchumi mkubwa kwa taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuzalisha *wool.* Baada ya shamba lile kubadilishwa kuwa hifadhi, sheria iliyoanzisha *TANAPA* inasema kulinda kilichopo na kwa sasa kilichopo kwa kiasi kikubwa ni maua pamoja na mimea ya asili. *TANAPA* kwa kutumia sheria yake, wataendelea kulinda hivyo kama ambavyo tunafanya kwenye hifadhi nyingine.

Kwa hiyo, suala la kuzalisha *wool* linaweza likaangaliwa kwenye maeneo mengine yatakayokuwa nje ya hifadhi kwa maana sasa sheria inazungumzia kulinda rasilimali ambazo ziko kwenye hifadhi.

Na. 160

Kampuni za Utalii na Malipo ya Tour Guides

MHE. ALOYCE B. KIMARO aliuliza:-

Kwa kuwa, Bunge limepitisha Sheria ya Utalii, ambapo mojawapo ya kipengele cha Sheria hiyo kinasema kuwa kampuni yoyote inayopandisha watalii mlimani ni lazima imilikiwe na Watanzania kwa asilimia 100 na pia waongozaji watalii *(Tour Guides)* ni lazima wawe Watanzania:-

(a)Je, kabla ya kuanzishwa kwa Sheria hiyo kulikuwa na Kampuni ngapi za kigeni zilizokuwa zikifanya biashara hiyo?

(b) Je, bado kampuni hizo zinafanya biashara hiyo?

(c) Je, Kanuni zinasemaje kuhusu malipo ya *Guides* na *Porters?*

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii na kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c), ningependa kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya utalii nchini imekuwa ikisimamiwa na Sheria Namba 2 ya Wakala wa Utalii ya mwaka 1969 pamoja na Sheria ya Hoteli ya mwaka 1963 kwa miaka iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwezi Februari mwaka 2008, Bunge lako lilipitisha Sheria mpya ya Utalii ambayo imeanza kutumika mwezi Julai, 2009. Ni matumaini yangu kuwa hatua ya kutekeleza Sheria hii, itaimarisha usimamiaji wa biashara ya utalii pamoja na kukabiliana na mapungufu yaliyokuwepo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kupitishwa kwa Sheria ya Utalii ya mwaka 2008, idadi ya kampuni za utalii zinazoendesha biashara ya kupandisha mlima, ambazo hazimilikiwi na Watanzania kwa asilimia 100 zilikuwa nane (8).

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuanza utekelezaji wa Sheria ya Utalii, 2008, Kampuni hizo hazikufungiwa mara moja kufanya biashara hiyo. Kwa mujibu wa Kanuni za Utalii, 2009 kampuni hizo zitahitajika kuendelea na biashara hiyo kwa kipindi cha miaka miwili na baadaye kusitisha biashara hiyo ifikapo mwaka 2011.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni za Sheria ya Utalii Na. 11 ya mwaka 2008 hazijataja kiasi halisi cha fedha kinachotakiwa kulipwa kwa waongozaji watalii *(Tour Guides)* na wapagazi *(porters)* kwa kujua kuwa suala la malipo ya wafanyakazi linasimamiwa na Sheria za kazi. Hata hivyo, Kifungu 20(2) na jedwali Na. 4 la kanuni za Sheria hiyo kinaelekeza kuwa wapagazi walipwe walau kiasi cha fedha za Kitanzania sawa na dola 10 kwa siku. Kanuni pia zinazitaka Kampuni za kitalii kuajiri wapagazi ambao ni wanachama wa vyama vya wapagazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza matakwa ya kanuni hizi Wizara imekuwa ikiwahamasisha wafanyakazi wa kada hizi wajiunge kwenye vyama vyao vya wafanyakazi ili kuweza kuwa na nguvu ya umoja katika kudai haki zao za kikazi. Aidha, mnamo mwezi Mei 2008, Mheshimiwa Waziri Maliasili na Utalii alifanya mkutano mjini Moshi, ambao uliwajumuisha wenye kampuni za biashara ya utalii wa kupanda Mlima Kilimanjaro na pia waongoza wageni.

Katika majadiliano ilionekana kuwa ili kuwawezesha wafanyakazi kutekeleza wajibu wao ipasavyo, itakuwa ni stahiki viwango vya malipo viwe $ 10 kwa wapagazi, $ 20 kwa mwongoza watalii na $ 15 kwa mpishi kwa siku. Hivyo, ilikuwa jukumu sasa la vyama vyao kuendeleza majadiliano na waajiri kwa lengo la kuafikiana juu ya ujira stahiki kwa kuzingatia mapendekezo haya na kwa mujibu wa sheria za kazi.

MHE. ALOYCE B. KOMARO: Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni je, Serikali inatambua ya kwamba bila *guides and poters* utalii Mlima Kilimanjaro utakuwa haupo?

Mheshimiwa swali la pili ni, kama hivyo ndivyo Serikali inavyotambua, ni kwa nini sasa Serikali inakuwa mbali sana na vijana hawa kwa kutosimamia mishahara yao, huku Serikali ikisimamia mavuno yake. Kwa mfano mwaka 2003 – 2006, Serikali ilivuna shilingi bilioni 97, maana yake ni shilingi milioni elfu 97. Sasa ni kwa nini, Serikali inasimamia mapato yake na kutosimamia mishahara ya *guides and poters?*

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatambua kwa hakika kwamba biashara ya utalii hasa wa kupandisha wageni mlimani, kwa kiasi kikubwa inategemea ubora wa huduma zinazotolewa na wasaidizi wa wageni hawa; wakiwemo wapagazi, wapishi pamoja na waongozaji, yaani *tour guides.* Ndio maana sisi kama Wizara katika Kanuni zetu, tumelibainisha jambo hili na tukatoa mapendekezo au bei elekezi kwamba ingefaa sana wapagazi walipwe viwango hivyo ambavyo nimeshavitaja, lengo ni kwamba wakifanya kazi kwa utulivu na kwa morali huduma zitakuwa nzuri na wageni wengi wataweza kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, utekelezaji wa usimamizi wa Sheria za kazi kama nilivyosema, uko kwenye Wizara nyingine. Sisi kama Wizara tutaendelea kuwahamasisha wapagazi wawe kwenye vyama vyao ili waweze ku-*bargain* kwa pamoja. Lakini pia niwaombe sana wanaofanya biashara ya kuleta wageni; wawalipe vizuri wapagazi kwa sababu, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, umuhimu wa kuwalipa ndio msingi wa ubora wa huduma watakazokuwa wanazitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwamba Wizara iko mbali; niseme kwamba si kweli kwa sababu tayari Wizara imeshatengeneza Kanuni, tumeshakutana nao kuzungumza, tumekuwa tukiwahamasisha kila wakati waweze kuwa kwenye vyama vyao vya wafanyakazi, yote haya ni kuonesha kwamba tuko *concerned* na afya zao na tutaendelea kufanya hivyo.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni jambo lililo wazi kwamba yapo makampuni yakupandisha milima hasa Mlima Kilimanjaro, yaliyoko Arusha na Moshi. Na ambayo yana wanahisa Watanzania bandia au wa kwenye makaratasi tu. Na kwa kuwa, tabia hii ni kuvunja sheria. Je, Serikali inalishughulikia vipi jambo hili?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Utalii na Maliasili, naomba kujibu swali la nyongeza la Ndugu yangu, kaka yangu, Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Kahama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii, pamoja na mambo mengine, inasimamia uendelezaji wa utalii. Wadau wanaojitokeza kufanya shughuli na Wizara, wako katika sura mbalimbali, wako *individual* na Kampuni. Uhalali wa wadau au wanahisa katika kampuni hizo, unafuatiliwa na kusimamiwa na taasisi nyingine za Serikali. Kwa hiyo, sisi kama Wizara na Serikali kwa ujumla, tunalichukua jambo hili na

ni changamoto kwa mamlaka zinazohusika, kuangalia kama taratibu za umiliki wa hisa kwenye Kampuni hizi ambazo ziko ndani ya sheria zilizoko nchini, zimefuatwa. Hili litakuwa ni jambo la kufanyia kazi. Sisi kama Wizara tunalichukua na tutazungumza na wenzetu katika Serikali.*(Makofi)*

Na. 161

Upungufu wa Vitendea Kazi Kituo cha Polisi cha Shelui

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Kwa kuwa, Tarafa ya Shelui ina kituo cha Polisi kimoja tu ambacho kipo Makao Makuu ya Mji Mdogo wa Shelui. Na kwa kuwa, Tarafa hiyo yenye Kata tatu na Vijiji kumi na sita vyenye wakazi wengi, ina matukio ya ujambazi na wizi wa mifugo; na kwa kuwa, mkuu wa sasa wa Kituo hicho ambacho ni kikubwa ana cheo cha *ASP:*-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza vitendea kazi hasa vyombo vya usafiri ili polisi hao waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo:-

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mkakati wa kuvipatia Vituo vyote vya Polisi nchini, kikiwemo kituo cha Shelui, vyombo vya usafiri hasa magari na pikipiki ili askari waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Hili linafanyika kwa awamu kwa jinsi Bajeti inavyoruhusu, kama Waheshimiwa Wabunge, mnavyofahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa Kituo cha Polisi Shelui, kina pikipiki moja, lakini hakina gari. Kwa kuwa, Kituo hicho kipo katika barabara kuu, *High Way*, mara kwa mara kinaongezewa nguvu ya doria zinazofanyika kwa magari na pikipiki kutoka Makao Makuu ya Mkoa. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, kituo hicho kitapewa pikipiki nyingine moja kwa ajili ya kuimarisha ulinzi.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba kati ya Vituo Vikubwa, vinavyohitaji kupatiwa usafiri ni pamoja na kituo cha Shelui. Na katika mpango wao Shelui nayo imo, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana na mimi kwamba kwa kuwa, kituo hicho kina matukio mengi na juzi Mheshimiwa *IGP* Mwema, alizomewa. Je, katika kutoa magari kituo hicho kitapewa kipaumbele? Kwani pikipiki zinashindwa kutimiza wajibu wake, kama juzi lilipovamiwa duka moja la mwananchi, pikipiki ilishindwa kufanya kazi zake ipasavyo. Gari lingefaa zaidi katika kituo hicho ambacho kinahudumia Kata sita na wala sio tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; kwa kuwa Kituo hicho ni kimoja tu katika Kata Sita, kwa maana ya Kata ya Kidaru, Kata ya Turia, Kata ya Mtwike, Kata ya Shelui, Kata ya Mtoa na Kata ya Mtekente. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba kuna kila sababu ya kuanzisha hata vituo vingine viwili vidogo, kimoja kijengwe Mtwike na kingine kijengwe Mtoa, ili viweze kukidhi haja ya matukio haya mengi ya wizi wa mifugo pamoja na ujambazi wa mara kwa mara? *(Makofi).*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri; hili ni jambo ambalo niseme kwamba Mheshimiwa Mbunge, tumelizungumza na tumefanya kila jitihada ya kumhakikishia kwamba tutatizama ni nini kinachoweza kufanyika. Lakini ningependa nirejee kauli aliyoitoa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hapa wakati tulipokuwa tunatoa Bajeti yetu na kusema kwamba kila wilaya, na hapa niuzungumzie Mkoa wa Singida, ni kwamba kila Wilaya katika Mkoa wa Singida itapata gari jipya. Sasa nafikiri itategemea na jinsi Mkuu au Kamanda wa Mkoa ule, atakavyokuwa anapanga magari haya na jinsi atakavyokuwa anapanga vituo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimhakikishie kwamba kiwilaya magari mapya yatakuwepo, ambayo yatapatikana mwezi wa saba. Sasa mpangilio wa mle ndani, nafikiri ni jambo lingine ambalo Mkuu wa Polisi pale au *RPC* wataweza kutizama itakuwaje. Lakini nikwambie kwamba hilo tumelipokea na nikuhakikishie kwamba jitihada zinafanyika katika vituo vidogo tulivyokuwanavyo juu ya vitendea kazi. Hayo magari yatakuwepo. Lakini sio kwamba yatakuja katika Kituo, lakini nikuhakikishie kwamba katika zile wilaya za Singida, zitapata magari mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, nikimjibu Mheshimiwa Mbunge Chilolo; ni kwamba siwezi nikalitamkia hapa kwamba nikubaliane na yeye ama la, kuhusu kuanzisha vituo vingine viwili vipya. Kwa sababu, tunajua tatizo tulilokuwa nalo kuhusu uanzishwaji wa hivyo vituo, na hili linatokana na uhaba wa fedha tulizokuwanazo katika Bajeti tunayoipangilia ambayo ndio tuliyokuwanayo. Isipokuwa nimwambie tu kwamba, kilio chake nimekisikia na tumekipokea, lakini itabidi tutizame katika mtizamo mkubwa wa mgawanyo wa vituo katika Tanzania yetu. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba, hilo nimelipokea. Lakini pia nikushukuru kwamba kila mara tunapokutana hali ya usalama katika Mkoa wa Singida limekuwa ni jambo kubwa kwako, na kwa kweli hili ni jambo zuri kuona kwamba unatusukuma mara kwa mara. *(Makofi)*

Na. 162

Polisi wa Ulinzi wa Majini Kutotoa

Huduma Zake Ipasavyo

MHE. RAJABU HAMAD JUMA aliuliza:-

Kwa nini kikosi cha Ulinzi wa Majini, *Police Marine*, hakionekani kutoa huduma zake katika baadhi ya Mikoa ambayo imezungukwa na Bahari au Maziwa hata pale Viongozi wa nchi wanapotembelea maeneo hayo ya kivuko kama vile ziara zinazofanyika Kisiwa cha Tumbatu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rajabu Hamad Juma, Mbunge wa Tumbatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kikosi cha Polisi Wanamaji *(Police Marine),* hakionekani kutoa huduma zake katika baadhi ya mikoa ambayo imezungukwa na bahari au maziwa. Zipo sababu nyingi za kutokufanya hivyo. Kwa upande wa Zanzibar, Kikosi hicho kimekuwa kinakabiliwa na tatizo la kuharibikiwa kwa boti ya Ngunguri. Kwa sasa, Kikosi kinatumia boti ndogo ya aina *Fibre* na *Rubber boat* kwa doria. Kwa sasa, boti ya Ngunguri, inahitaji matengenezao na hili niliwahi kulitamka hapa Bungeni awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa matatizo tuliyonayo Kamanda wa Polisi wa Kaskazini Unguja, ambaye ndiye anayehudumia eneo la Tumbatu, amekuwa akiusimamia mkakati wetu wa ulinzi shirikishi Polisi Jamii kwa vitendo, kwani amekuwa akitumia boti za *KMKM* kwa shughuli za doria na boti za Mamlaka ya Bandari Zanzibar, kwa ajili ya kubebea Viongozi pamoja na askari wa kuwalinda Viongozi hao. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba askari wetu katika maeneo yote wanakuwa na vitendea kazi vya kutosha.

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo boti ya Ngunguri, itamaliza lini matengenezo yake? Kwa sababu inaonesha iko kwenye matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuwa wanatumia boti ya *KMKM* na ya Mamlaka ya Bandari katika ziara za viongozi. Je, doria za kila siku wanatumia boti gani kwa kuwasaidia hawa Polisi ili kuhakikisha kwamba wanafanya doria za kila siku? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ni lini hii meli ya Ngunguri matengenezo yake yatakamilika:

Nipende kumwambia kwamba katika taarifa ambazo tumezipata baada ya kufuatilia sana, niseme kwamba inaonekena matengenezo yake ni makubwa. Na sasa hivi bado tuna mjadala ambao tunajaribu kutizama kama itakuwa ni *value for money* kuweza kutengeneza kitu kama hicho ama tutizame utaratibu wa kuweza kupata meli nyingine.

Kwa hiyo, tuko katika kutizama kama tutakuwa tukiweka pesa pale tutakuwa tunapoteza kwa hiyo tusiendelee na matengenezo, kwa maana nyingine tupate meli nyingine, au tuendelee kuitengeneza meli hii. Kwa hiyo, kwa sasa hivi ndilo suala ambalo tunajaribu kulitizama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pili ambalo ameliulizia Mheshimiwa Mzee, kwamba tunaendelea kutumia hizi meli za *KMKM* na Mamlaka ya Bandari, kwa kweli ningependa niseme kwamba, na ninalisema kwa nia nzuri, yako masuala mengine ambayo ni masuala ya kiusalama. Na nitahadharishe kidogo tu kwamba yapo mambo ambayo tunaweza kuyazungumza hapa, kweli kwa niaba ya kutoa taarifa, lakini pia ni lazima tuwe makini kwamba hizi taarifa zinakwenda mbali sana.

Tanzania ni nchi ambayo ni lazima iwe makini, hatuwezi kujua hizi taarifa watu ambao hawatutakii mema wanaweza kuzitumia namna gani. isipokuwa niseme tu kwamba jitihada zinafanyika, usalama wetu uko salama na tunafanya kila jitihada kuboresha pale ambapo tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba nisiende katika undani zaidi wa yepi ambayo ni mapungufu au ni wapi ambapo tumekuwa na nguvu. Isipokuwa nimuombe Mheshimiwa Mbunge, kwamba awe na imani, jitihada zinafanyika kuhakikisha kwambausalama wa nchi yetu uko sawa sawa. *(Makofi)*

Na. 163

Huduma ya Mawasiliano ya Simu katika Mji wa Bungu

MHE. LAUS O. MHINA aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji wa Bungu na Vitongoji vyake una wakazi takribani 5000 hauna huduma muhimu ya mawasiliano ya simu licha ya kuwepo ahadi ya muda mrefu ya kupatiwa huduma hiyo:-

(a)Je, ni lini kampuni za simu zitajenga minara katika eneo hilo ili kuwapatia wananchi hao huduma hiyo muhimu?

(b)Je, ni lini minara ya simu itajengwa katika eneo la Kizara kwa ajili ya kutoa huduma katika vijiji vya Kizara, Kwemkole, Bombo Majimoto pamoja na vitongoji ili kutekeleza ahadi hiyo ya muda mrefu?

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Kampuni ya simu *ZAIN* imefanya tathimini ya kibiashara na kubaini kuwa maeneo hayo yanastahili kuboreshewa mawasiliano. Juhudi za kuboresha mawasiliano hayo yatafanywa na kampuni hiyo ya *ZAIN*.

Aidha, kampuni ya simu ya *VODACOM* itafanya tathimini ya kibiashara mwaka huu wa 2010/2011 katika mji wa Bungu na Kizara ili kubaini maeneo muafaka kwa ajili ya minara ya mawasiliano ambayo itaiwezesha vijiji vya Kwemkolo, Bombo Majimoto na maeneo mengine kupata huduma ya mawasiliano. Kampuni ya *ZATEL* litaliweka eneo la Bungu kwenye mipango ya kufanyiwa tathimini ya kibiashara katika mwaka huu wa 2010/2011.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya simu ya *TIGO* imeahidi kuyaweka maeneo hayo kwenye malengo ya kufanyiwa tathimini ya kibiashara katika mwaka 2010/2011. Vilevile kampuni ya *ZAIN* itayajumuisha maeneo ya vijiji vya Kizara, Kwemkolo, Bombo Majimoto pamoja na vitongoji vyake kwenye orodha ya kufanyiwa tathimini ya kibiashara katika mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na kampuni za mawasiliano ya simu za mkononi yaliyopo hapa nchini ili kufikisha huduma za mawasilano sehemu mbalimbali hapa nchini.

MHE. ENG. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri ninalo swali moja wa nyongeza, mji wa Korogwe tunafahamu unakua kwa haraka sana, Je, ni lini mji ule utapata huduma ya simu ya viganjani kwa kutumia mitambo ya *TTCL?*

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Mhina kama ifuatavyo. Mji wa Korogwe kweli unakua kwa haraka na hauna huduma za mawasiliano ya simu za *TTCL*.

TTCL iko mbioni katika kujikwamua kutoka kwenye hali ambayo ni ngumu kidogo ya fedha na sasa hivi iko njiani humo kutaka kupata msaada kutoka Serikalini kwa maana ya *guarantee* na ndipo ambapo wataweza kufikisha huduma katika sehemu mbalimbali za hapa nchini.

Pamoja na hayo, kuna simu ambazo zinapatikana kwa makampuni mengine. Kwa hiyo, huduma ya simu si kwamba haipatikani kabisa pale Korogwe, lakini pili ni faraja kwake kujulishwa kwamba mkongo wa mawasiliano ya taifa katika *northern ring* unapita Korogwe kwenda Tanga na kutoka Tanga kwenda Dar es Salaam.

Mkongo tuko katika juhudi sasa ya kuunganisha sehemu mbalimbali hata vijijini. Kwa hiyo, sio muda mrefu huduma ya mawasiliano itakuwa imefika kwa ukamilifu pale Korogwe lakini vilevile huduma hiyo itapunguza sana gharama za mawasiliano ya simu kwa asilimia kubwa na *internet* itashuka kwa asilimia 50.

Na. 164

Viwango vya Ubora katika Ujenzi wa Barabara Nzuri Nchini

MHE. MKIWA A. KIMWANGA aliuliza:-

Serikali imeweka viwango vya ubora ambavyo wajenzi wa barabara na madaraja wanapaswa kuvizingatia wakati wa ujenzi ikiwa ni pamoja na kuandaa mipango mizuri ya hifadhi ya barabara zenyewe:-

Je, kama viwango hivyo vinazingatiwa ipasavyo, kwa nini basi barabara nyingi hapa nchini huharibika muda mfupi baada au hata kabla ya kujengwa na kufanya mawimbi na baadhi ya sehemu hufanya mashimo juu ya barabara ambayo yanahatarisha usalama wa watumiaji wa barabara hizo?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adamu Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka viwango vya ubora ambavyo wajenzi wa barabara na madaraja wanapaswa kuvizingatia wakati wa ujenzi.

Hata hivyo, kutokana na utendaji hafifu wa baadhi ya makandarasi hutokea baadhi ya maeneo machache katika mradi yakaharabika mapema kuliko ilivyotarajiwa.

Katika mikataba yote ya ujenzi vipo vifungu vinavyomtaka mkandarasi kurekebisha kasoro zinajitokeza wakati wa ujenzi, marekebisho hayo hufanywa na mkandarasi kwa gharama zake kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika mkataba.

Aidha, katika miradi yote ya ujenzi wa barabara mkandarasi huwajibika kufanya marekebisho ya sehemu zinazoharibika katika kipindi chote cha matarajio kilichoainishwa kwenye mkataba ama *defect liability period*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itaendelea kusimamia makandarasi kwa karibu ili kuhakikisha kuwa barabara na madaraja yanajengwa kwa kuzingatia viwango. Wizara yangu pia haitasita kuwachukulia hatua kali makandarasi wabovu ikiwa ni pamoja na kufuta usajili wao.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wakandarasi wengi huchelewa kufanya marekebisho pindi barabara zinapoharibika na hadi kupelekea uharibifu ule kuwa mkubwa.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa muda mfupi wakandarasi hawa kufanya matengenezo pindi tu barabara zinapoharibika?

Je, Serikali imemchukulia hatua gani mkandarasi aliyejenga barabara ya Mwanza - Shinyanga, kwa kuwa barabara huharibika maramara maeneo ya kona ya kwenda Misasi, maeneo ya Mabuki na maeneo mengine na hata kupelekea kuonekana barabara hii imetengenezwa chini ya kiwango?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mkiwa Adamu Kimwanga kama ifuatavyo. Moja napokea ushauri wa kuendelea kusisitiza na kusimamia vizuri makandarasi ili pale ambapo panahitaji kufanyiwa matengenezo na ni wajibu wao kufanyia matengenezo wafanye kwa wakati muafaka na kwa ukamilifu.

Kuhusu barabara, mkandarasi aliyetengeneza barabara hii ya Shinyanga kupitia Mabuki, niseme tu kwamba sina uhakika ngazi ambayo imefikiwa sasa hivi katika urekebishaji wake katika barabara hiyo, nitalifuatilia na wenzangu Wizarani ili tupate matetengenezo ambayo ni ya uhakika. *(Makofi)*

Na. 165

Stahili za Wafanyakazi wa Tazara

MHE. GOFREY W. ZAMBI (K.n.y. MHE. BENSON M. MPESYA) aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya wafanyakzi wa *TAZARA* hawajalipwa stahili zao kiasi cha shilingi bilioni 60 mpaka sasa:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya kulipa wafanyakazi hao?

(b) Je, Serikali imejiandaa kwa mikakati gani ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi hao?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benison Mpesya Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba hadi kufikia mwezi Desemba, 2009 *TAZARA* ilikuwa inadaiwa jumla ya shilingi bilioni 56.3 ikiwa ni pensheni za wastaafu kuanzia mwaka 2005.

Hali hiyo inatokana na hali mbaya ya mapato ya *TAZARA* ambayo ilisababisha shirika kushindwa kupeleka fedha kwenye mifuko husika fedha ambazo zilikuwa zinakatwa kutoka kwenye mishahara ya wafanyakazi kwa ajili ya pensheni za wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hali mbaya ya kifedha ya shirika la *TAZARA*, Baraza la Mawaziri wa *TAZARA* linalojumuisha Serikali ya Tanzania na Zambia liliamua kwamba Serikali za nchi hizo mbili zichukue jukumu la kugharamia malipo ya pensheni ya wastaafu hao. Kwa hiyo, Baraza likaagiza mchakato wa kuhakiki madeni yote madai yote ya pensheni ya wastaafu ufanyike.

Kazi ambayo inafanywa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kazi ya kuhakiki mahesabu hayo itakapokamilika Wizara itaandaa waraka na kuwasilisha Serikali ili fedha hizo ziweze kutafutwa na kuwalipa wafanyakazi hao.

Wakati mchakato huo unaendelea wafanyakazi wamekubaliana na menejiment ya *TAZARA* kuwalipa stahili zao kwa mafungu madogo kila mwezi ili waweze kujikimu kimaisha wakati mchakato wa kutafuta fedha za malipo ya stahili zao unaendelea. Hivi sasa *TAZARA* inalipa shilingi milioni 150 kila mwezi kama pensheni ya wafanyakazi kupitia shirika la Bima la Taifa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa *TAZARA* Serikali kupitia Bodi ya Wakurugenzi ya *TAZARA* mwezi Julai, 2009 iliidhinisha nyongeza ya mishahara ya wafanyakazi kwa asilimia tano na kwa kuzingatia kuwa mishahara ya *TAZARA* imewekwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani, Bodi pia iliidhinisha kiwango kipya cha kubadilisha fedha kwa dola moja ya Kimarekani kiwango kitakachotumika au kinachotumika sasa kwa upande wa Tanzania kubadilisha dola moja ni shilingi 1300 badala ya shilingi 1200 iliyokuwa ikitumika hapo awali. *(Makofi)*

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali atakapomaliza kufanya kazi hiyo atawasilisha taarifa yake Wizarani na

Wizara itaandika Waraka kupeleka Serikalini ili pesa ziweze kutafutwa na kwa kuwa wafanyakazi wa *TAZARA* wameteseka muda mrefu toka 2005 mpaka leo. Waziri anaweza kuwaeleza wafanyakazi hawa kwa hakika kabisa kwamba ni lini sasa kazi hiyo itakamilika ili wafanyakazi hao ambao wameteseka sana waweze kulipwa haki zao?

Kwa kuwa, wanatumia dola kulipa mishahara, na kiwango ambacho kimetumika kwa muda mrefu dola 1200 kimedumu sana, hivi ni kwa nini kisitumike kiwango kile kama ni kwa mwezi au kwa mwaka ndiyo wachukue kiwe kigezo kuliko kukaa miaka mitatu minne, wakitumia kiwango kimoja, na Waziri huku pia kunaweza kukawa kuwadhulumu wafanyakazi hao?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zambi kama ifuatavyo. Moja kuhusu lini Wizara itapeleka Waraka Serikalini ili kuwezesha wastaafu hawa kupatiwa fedha za mafao mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu kwamba tutalichukulia suala hili kwa umuhimu wake na mara taratibu zote zitakapokamilika kwa sababu ni suala la *TAZARA* Baraza la Mawaziri la *TAZARA* lazima liidhinishe uhakiki ule wa mahesabu kwa pande zote mbili. Ingawa Baraza hili linakaa mara moja kwa mwaka tutajitahidi kuliitisha la ziada ili lihakikishe kwamba hesabu hizi zimekuwa tayari tutaitisha Baraza la Mawaziri la ziada ili jambo hili lisichelewe na ili Serikali zote mbili ziweze kuwasilisha katika Serikali zao na kupata pesa mapema iwezekanavyo kwa ajili ya wastaafu hawa.

Kuhusu kigezo cha dola, kwa sababu dola ya Marekani inabadilika mara kwa mara, wakati mwingine inapanda wakati mwingine inashuka na haitokuwa sahihi kwamba kiwango kikishuka basi na sisi mishahara tuiteremshe. Kwa hiyo, taratibu tunayoitumia sasa hivi ni kuangalia ule wastani kwa kipindi fulani na kila itakapokuwa wastani huu umebadilika basi tutakuwa tunabadilisha kiwango hicho kama ipasavyo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumezidi muda naona ofisi nayo iliweka maswali zaidi ya kawaida waliweka maswali kumi na moja. Kwa hiyo, menejimenti yake inakuwa ngumu.

Sasa tuwatambue wageni tulionao katika ukumbi huu tunao wageni wa Mheshimiwa Shamsa Mwangunga Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na wageni wa Mheshimiwa Ezekieli Maige, Naibu Waziri Maliasili na Utalii ambao ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Ladslausi Komba.

Waheshimiwa Wabunge, tuna Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Makumbusho ya Taifa Ndugu Costansia Rugumamu, tuna Mkurugenzi wa Idara ya Sera na Mipango, Ndugu Januari Mrema, Mkurugenzi wa Idara ya Wanyama pori, Ndugu Erasmos

Tarimo, Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimali watu Ndugu Abdulrahman Mdimu.

Wageni wengine ni Mkurugenzi wa Idara ya Malikale, Ndugu Donatius Kamamba, tuna Mkurugenzi wa Idara ya Utalii, Ndugu Maria Mmari, Kaimu Mkurungezi wa idara ya Misitu na Nyuki Ndugu Monica Kagya, tuna mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Taifa ya Utalii Tanzania *TTD*, Dr. Aloyce Nzuki, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Makumbusho la Taifa Dr. Norbet Kayombo, tuna Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utalii wa Wanyamapori, Tanzania Tawiri, Dr. Samson Mduma na tuna Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania *TAFORI* Ndugu Evarist Sabasi,

Waheshimiwa Wabunge, sasa tuna mhifadhi mkuu wa Mamlaka ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro Ndugu Benard Mrunya, tuna kaimu Mkurugenzi wa Hifadhi za Taifa *TANAPA*, Ndugu Alan Kijazi, tuna Mkuu wa Chuo cha Wanyamapori - Mweka, Ndugu Emmanuel Savere. Tunawashukuru sana hawa ni wale wanaohusika na Wizara hiyo ya Maliasili na Utalii na wale wastaafu wote wa Wizara hiyo.

Lakini wafuatao ni wageni binafsi wa Mheshimiwa Ezekiel Maige, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, ambao ni mke wake Bibi Ribereta Ezekiel Maige na wale wa juu ambao mmoja ameamua kutangaza nia hapa hapa. Lakini pamoja na wale watoto wa Mheshimiwa, lakini tunaye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Ndugu Hamis Mgeja. *(Makofi)*

Aidha, wapo maafisa waandamizi 30 kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, pamoja na Taasisi zilizoko chini ya Wizara hiyo wote hawa tunawakaribisha sana hasa kwa kuzingatia kuwa leo ni siku ya Wizara yenu. Karibuni sana hapa Bungeni.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Haroub Masoud ambao ni wafanyabiashara kutoka Oman. Naomba wasimame popote walipo, yuko Shekh Hilal, yupo Miss Sharifa, yuko Miss. Fadia na yupo Bwana Aziz Abdallah, yeye anatoka Dar es Salaam ahsante sana karibuni sana nadhani mnafanya mawasiliano mazuri ya kibiashara na Tanzania. *(Makofi)*

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Felix Mrema, ambao ni Wawakilishi wa Wafanyakazi walioachishwa kazi *General Tires* Arusha hao ni Salim Self na Frank Kimaro. Jana mlimsikia aliwasemea kwa nguvu zake zote nadhani Serikali imesikia.

Kuna wageni wa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, ambao ni Mwenyekiti wa *CUF wa* Wilaya ya Musoma Mjini Ndugu Didi Koko, ahsante sana, tuna katibu wa *CUF* Musoma Mjini Jumanne Magafu, tuna Katibu wa *CUF* Wilaya

ya Magu, Ndugu Dominic Bubeshi, tuna Mjumbe wa Mkutano Mkuu *CUF* Taifa, Ndugu Maimuna Matola, ahsante sana tunajua kwamba mlikuwa na Mkutano wenu mkamchagua Bwana Lipumba kuwa Mgombea pekee wa *Rais - CUF*. *(Makofi)*

Tunao Wanafunzi 50 wakiongozwa na Walimu pamoja na Wakuu wa Chuo kutoka Chuo cha *Dodoma Association Training Institute (DATI).* Mimi sijawahi kukisikia chuo hiki, wako wapi wanafunzi na walimu? Tumefurahi sana kuwaona na tunawaomba mjitahidi kusoma kwa sababu enzi hizi bila elimu huna kitu.

Tuna jumla ya maskauti 28 ambao wameambatana na Viongozi wao. Maskauti wote pamoja na Viongozi wao tunaomba wasimame popote walipo. Ahsante sana mnapendeza sana Maskauti lakini inapungua nguvu siku hizi. Karibuni sana.

Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, uwe unapeleka kunakohusika haya majina, lakini anaomba nimtangazie wageni wake ambao ni Mheshimiwa Kaimu Diwani wa Kata ya Ngokolo, Saganda Khalid Saganda. Wageni wengine ambao sijui uhusiano wao na Mbunge ni Bwana Jumanne Maziku, Bwana George Mwandu, Bwana Mbassa Lugenji na Bi. Esther Nkalango. Bila shaka hao ni wapiga debe wa Mheshimiwa Mbunge, karibuni sana na wengine wote ambao hatukuwataja hapa, Bunge letu liko wazi kila mtu anakaribishwa na wote mjisikie mko nyumbani.

Tangazo moja la kazi ni kwamba, Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, naona kuna Kamati labda lakini hii ni Kamati Ndogo, anaomba niwatangazie kwamba, anayo heshima kubwa kuwasilisha Taarifa ya Kamati Ndogo ya Nishati na Madini, baada ya kukamilisha kazi za uchunguzi kuhusu matumizi ya mashine za ukaguzi zinazotumia mionzi. Hili halikuwa tangazo ni taarifa, kwa hiyo, utampelekea Spika ofisini kwake. Ninadhani haikupaswa kuja hapa.

Tunaendelea na ajenda ya leo.

KAULI ZA MAWAZIRI

Kauli Kuhusu Utekelezaji wa Miradi Mipya ya Kupeleka Umeme Vijijini

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, Kanuni Namba 49, naomba kutoa Kauli ya Serikali Kuhusu Utekelezaji wa Miradi Mipya ya Kupeleka Umeme Vijijini Inayofadhiliwa na Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)*, Miradi Inayofadhiliwa Kupitia *Millennium Challenge Cooperation (MCC)*, Miradi Inayofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) pamoja na Shirika la Maendeleo ya Serikali ya Sweden (SIDA) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi mipya ya kupeleka umeme vijijini chini ya ufadhili wa Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)*, itatekelezwa kwenye Mikoa 16 ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Mbeya, Rukwa, Tabora, Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara na Shinyanga. Miradi hii itahusisha ujenzi wa njia za umeme zenye msongo wa Kilovolt 33 pamoja na 11 zenye jumla ya takriban kilomita 1600. Ufungaji wa *transformer* 350 za ukubwa tofauti, ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kilovolt 0.4 zenye jumla ya kilomita 900 na uunganishaji wa wateja wapya wanaokadiriwa kufikia 20,000. Ujenzi wa miradi hii yote, umekadiriwa kufanywa na Wakandarasi wa ndani na nje ya nchi. Usimamizi wa utekelezaji wa miradi hiyo, utakuwa chini ya Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO).*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofikiwa ya utekelezaji wa Miradi; majadiliano ya mikataba kati ya TANESCO na Wakandarasi walioshinda zabuni yameshakamilika. Utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya Ngorongoro katika Wilaya ya Loliondo na Mkoa wa Arusha kwa ujumla, utafanywa na TANESCO, ingawa wanaweza kuwashirikisha Sekta Binafsi kwa kadiri watakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa, Wilaya na maeneo yatakayonufaika katika miradi hii pamoja na makisio ya gharama za utekelezaji mradi kwa kila Mkoa na muda, yameainishwa kwenye jedwali ambalo tutaliwasilisha hapa muda si mrefu. Vilevile majina ya wakandarasi wanaoshinda zabuni yameoneshwa katika jedwali ambalo Waheshimiwa Wabunge watalipata. Kwa kuanzia, Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Same Magharibi, maeneo yatakayopatiwa umeme ni pamoja na Vijiji vya Mhezi, Ijinyu, Kiyom, Msindo, Mbakweni, Kizungwa na Dido. Wilaya ya Mwanga kuna Vijiji vya Kwakoa, Kigonigoni, Toloha na Ngulu. Katika Wilaya ya Siha ni Vijiji vya Donyo, Moruaki, Nangumbaru, Ngaritati, Kandashi, Orikoriri, Oromeriri, Dikremuni, Magadini na Wiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Kilimanjaro, fedha zilizotengwa ni shilingi bilioni 7.2 na Mkandarasi atakayesambaza umeme katika maeneo haya tuliyoyataja ni Kampuni inayoitwa *SPENCON Services*. Muda wa kukamilisha miradi yote kwa ujumla ni kipindi kisichozidi miezi 12.

Mkoa wa Manyara, Wilaya ya Simanjiro, Vijiji vya Msitu wa Tembo na Magadini. Wilaya ya Babati, Vijiji vya Himiti, Bonga, Managa na Haraa. Wilaya ya Mbulu, Vijiji vya Gahandu, Tilawi na Shule ya Sekondari. Kiteto, Vijiji vya Ndareta, Mbeli, Mwakisabe, Ilongia na Itolwa. Fedha iliyotengwa katika Mkoa wa Manyara ni shilingi bilioni 2.9 na kampuni itakayofanya shughuli za usambazaji kwa kipindi kisichozidi miezi 12 ni Kampuni ya *NAMIS Cooperate Services* ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tanga katika Wilaya ya Handeni kuna Vijiji vya Chanika, Kibaoni, Msasa, Kwamnyanganje Secondary School, Magamba na Kwedikazu. Mkoa huu umetengewa shilingi bilioni 2.9 na mkandarasi katika Mkoa huu

ni *INTERCITY Builders*, Kampuni ambayo ni ya Tanzania. Utekelezaji utafanywa kwa kipindi kisichozidi miezi 12.

Mkoa wa Pwani katika Wilaya ya Kisarawe, maeneo ambayo yatafikishiwa huduma hii ya umeme ni pamoja na Maneromango Hospitali. Kutokea Mzenga ni Mzenga Sekondari, Masaki Sekondari, Msonga Sekondari na Kazimzumbwi, Ulongoni na Buyuni. Katika Wilaya ya Mkuranga ni maeneo ya Kilimahewa Mission, Hoyohoyo na vijiji vilivyopo katika eneo hilo. Katika Mkoa wa Pwani, fedha iliyotengwa ni shilingi bilioni 7.7 na mkandarasi ni Kampuni ya *SIMBIONI Power* inayotoka Marekani.

Mkoa wa Morogoro nikianzia na Wilaya ya Ulanga, vijiji vitakavyonufaika na mradi huu ni pamoja na Vijiji vya Mwaya, Mwanya Ginnery, Mahenge na Ulanga. Kilombero vijiji vitakavyohusika ni Vijiji vya Malinyi na vijiji kandokando ya njia itakayopita umeme. Katika Wilaya ya Kilosa ni pamoja na Hospitali ya Berega. Katika Wilaya ya Morogoro fedha iliyotengwa ni bilioni 11.6.

Mkoa wa Dodoma Wilaya ya Mpwapwa, vijiji vitakavyonufaika ni pamoja na Vijiji vya Godegode, Berege, Chitemo, Mima na Mzase na fedha iliyotengwa kwa ajili ya kuwahudumia Wananchi hawa ni shilingi bilioni 4.1. Kampuni itakayofanya ujenzi katika usambazaji wa umeme katika maeneo hayo ni Kampuni ya *INTERCITY Builders* ya Tanzania. Kipindi cha utekelezaji wa mradi ni kipindi kisichozidi miezi 12.

Mkoa wa Singida kuanzia Wilaya ya Manyoni Vijiji vya Mgandu, Itigi, Manyoni, Hospitali ya Kilimatinde na Kintinku, fedha iliyotengwa ni shilingi bilioni 6.4. Mkandarasi atakayefanya kazi hiyo ni *SPENCON Services*, kampuni inayotoka Kenya, muda wa utekelezaji ni muda usiozidi miezi 12. *(Makofi)*

Mkoa wa Mbeya Wilaya ya Chunya ni Vijiji vya Kongorosi, Lupa na Tingatinga. Wilaya ya Rungwe, Vijiji vya Lutabe na Matamba. Wilaya ya Mbozi, Vijiji vya Luanda hadi Idwili, Mahanje, Igunda, Mloo, Isanza, Saganda na Mlima Njiwa. Katika Wilaya ya Mbeya Vijijini ni Vijiji vya Santilya, Ilembo, Tembela, Imezu na Horongo. Fedha iliyotengwa ni shilingi bilioni 4.3 na kampuni inayoshughulika na usambazi wa umeme katika maeneo hayo ni Kampuni ya *ROSANT International* kutoka Afrika ya Kusini. Kipindi cha utekelezaji ni muda usiozidi miezi 12.

Mkoa wa Rukwa katika Wilaya ya Nkasi huduma hii itafikishwa katika Makao Makuu Wilaya ya Nkasi katika Mji wa Namanyere na vijiji vyote vilivyoko njiani. Kiasi cha fedha kilichotengwa ni shilingi bilioni 4.5 na kampuni itakayohusika ni kampuni ya *ROSANT International* inayotoka Afrika Kusini na kipindi cha utekelezaji ni miezi isiyozidi 12.

Mkoa wa Tabora katika Wilaya ya Nzega, Mji wa Bukene na Vijiji vya Ndala, Shabela, Bora Kilimi na vijiji vilivyopo kandokando itakapopita njia ya umeme. Katika Wilaya ya Urambo, Vijiji vya Mabatini, Vumilia, Usoke Mlimani, Kalemera na Urasa. Pia kuboresha njia ya umeme itokayo Urambo hadi Kaliua na kuwa *free phase* badala ya *single phase*. Fedha iliyotengwa ni shilingi bilioni 8.8, kampuni inayofanya kazi hiyo ni

Kampuni ya *NAMIS Cooperative Service* ya Tanzania, kipindi cha utekelezaji ni miezi isiyozidi 12.

Mkoa wa Kagera Wilaya ya Bukoba Vijijini, vijiji vitakavyonufaika ni pamoja na Vijiji vya Ibwera, Kafunjo, Izimbya na Katoro. Wilaya ya Karagwe ni Vijiji vya Bisheshe, Nyaishozi na Ihembe na fedha iliyotengwa ni shilingi bilioni 9.9. Kampuni inayofanya kazi hiyo ni Kampuni ya *Mufindi Power* ya Tanzania, utekelezaji ni kipindi kisichozidi miezi 12.

Mkoa wa Mwanza, Vijiji vya Nyamikoma na Kalemela vitanufaika katika Wilaya ya Magu. Wilaya ya Sengerema ni pamoja na Vijiji vya Buyagu, Nyamasale, Mlaga, Kalangalala, Isole, Bitoto na *Buyagu Ginnery*. Wilaya ya Ukerewe ni Vijiji vya Buzengwe na Bugombe na fedha iliyotengwa kwa ajili ya maeneo haya ni shilingi bilioni 4.4, kipindi cha utekelezaji ni miezi isiyozidi 12 na kampuni inayofanya kazi hii ni Kampuni ya *SIMBION Power* kutoka Marekani.

Mkoa wa Mara, Wilaya ya Rorya, Vijiji vya Nyanchabakanye, Marasibora, Nyarombo, Masonga na Hospitali ya Masonga. Wilaya ya Tarime, Vijiji vya Irilo na vijiji vya njiani vyote ambavyo vinapitiwa na njia hiyo kuelekea Itiryo. Wilaya ya Bunda, Vijiji vya Kung'ombe, Ncharo, Unyari, Chanjwige, Kichumpwa na Shule za Sekondari za Kung'ombe, Salama Kati, Ncharo Sizaki na Unyari Sekondari. Fedha iliyotengwa ni shilingi za Kitanzania bilioni 4.4. Kampuni inayofanya kazi hiyo ni *NAMIS Cooperate* ya Tanzania na utekelezaji ni kwa kipindi kisichozidi miezi 12.

Mkoa wa Shinyanga tukianza na Shinyanga penyewe; Shinyanga Vijijini, Vijiji vya Solwa, Kituli, Samile, Islamagazi hadi Salawi katika Jimbo la Solwa. Wilaya ya Bariadi ni Vijiji vya Ngulyati, Sapiwi na Igegu. Wilaya ya Kahama ni pamoja na Vijiji vya Isageng'e, Mpera, Mwakata na Katunguru.

Wilaya ya Meatu ni Vijiji vya Mwandoya na Pampu ya Maji. Fedha iliyotengwa ni shilingi za Kitanzania bilioni 9.4. Kampuni inayofanya kazi hii ni Kampuni ya *SIMBION Power* kutoka Marekani na utekelezaji ni kwa kipindi kisichozidi miezi 12. *(Makofi)*

Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Ngorongoro, kazi itakayofanyika ni kufikisha na kusambaza umeme katika Makao Makuu ya Wilaya Ngorongoro, Wilaya ya Loliondo, ambayo tayari *Generator* ziko njiani zinaletwa. Lakini fedha hizi ninazozisema hapa ni kwa ajili ya usambazaji katika Mji wa Loliondo. Fedha iliyotengwa ni shilingi milioni 719,470,496,000. Mradi huu katika Wilaya ya Loliondo utatekelezwa na Shirika la TANESCO.

Mkoa wa Kigoma katika Wilaya ya Kasulu, mashine ziko njiani zinaletwa lakini fedha kwa ajili ya usambazaji katika Mkoa wa Kigoma na hasa Wilaya ya Kasulu na Kibondo ni shilingi bilioni 8.7. Kampuni inayofanya kazi hii inaitwa *NAMIS Cooperate* na utekelezaji wake Waheshimiwa wa Mkoa wa Kigoma wanafahamu, inatarajiwa

kwamba, kufikia mwezi wa Novemba umeme utakuwa umeshawaka katika Wilaya ya Kibondo pamoja na Wilaya ya Kasulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya ujenzi wa miundombinu ya umeme kwenye Mikoa 15 itakayotekelezwa na wakandarasi inakadiriwa kufikia jumla ya shilingi bilioni 97.7 na gharama ya ujenzi wa miundombinu ya umeme kwenye Mkoa mmoja wa Arusha utakaotekelezwa na Shirika la TANESCO inakadiriwa kufikia jumla ya shilingi milioni 720. Hivyo, gharama kuu kwa miradi yote katika Mikoa 16 inakadiriwa kufikia shilingi bilioni 98.468. Kazi ya ujenzi wa miundombinu ya umeme kwenye Mikoa yote 16 itachukua miezi 12 kwa pamoja, tangu kuanza kazi hadi kukamilika kwa kila mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine ya umeme iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni pamoja na miradi ifuatayo:-

Miradi ya umeme Wilayani Bagamoyo. Katika Wilaya ya Bagamoyo kuna miradi miwili mikubwa ya ujenzi wa miundombinu ya umeme vijijini. Mradi wa kupeleka umeme Magindu pamoja na Mbwewe. Mradi wa kufikisha umeme katika Kijiji cha Magindu unahusu ujenzi wa kilomita 23 za njia ya umeme, msongo kilovolt 33 kutoka Kijiji cha Magwila Chalinze, ufungaji wa *transformer* 6 pamoja na ujenzi wa kilomita 12 za njia ya umeme wa msongo wa kilovolt 0.4, kukipatia umeme Kijiji cha Magindu pamoja na Vijiji vya Magwila, Chahuwa, Gwata, Gumba na Magindu Sekondari. Gharama za ujenzi huo zinakaribia kufikia shilingi za Kitanzania bilioni 1.3.

Mradi wa kufikisha umeme Mbwewe unahusu ujenzi wa kilomita 24 za njia ya umeme msongo wa kilovolt 33 kutoka Kijiji cha Makole Wilayani Bagamoyo, ufungaji wa *transformer* 6 na ujenzi wa kilomita 12 za njia ya umeme msongo wa kilovolt 0.4, kukipatia umeme Kijiji cha Mbwewe pamoja na Vijiji vya Makole, Lupungwi, Kimange na Shule ya Sekondari Changalikwa. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa shilingi za Kitanzania bilioni 1.4. Miradi yote miwili; yaani Magino na Mboye, inafadhiliwa na Serikali ya Tanzania na inatekelezwa na Shirika la TANESCO. Upimaji wa njia za umeme kwenye miradi yote miwili ulikamilika mwezi Oktoba, 2009 na Machi 2010 sawia. Ujenzi wa miundombinu ya umeme kwa Miradi ya Magino na Mboye umeshaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Longodi unahusu ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovolt 33, umbali wa kilomita 30 kutoka Mji wa Namanga hadi Makao Makuu ya Wilaya ya Longido. Ufungaji wa vipoza umeme 8, ujenzi wa kilomita 10 za njia ya umeme kilovolt 0.4 pamoja na kuunganisha wateja wapatao 291. Maeneo yatakayofaidika na mradi katika Mji wa Longido na Kijiji cha Kimokua, gharama za mradi zinakadiriwa kuwa shilingi za Kitanzania bilioni 1.4. Upimaji wa njia za umeme umekamilika kwa 100%. Utekelezaji wa mradi huu unaofanywa na TANESCO unaendelea na unakadiriwa kukamilika katika kipindi cha miezi saba.

Mradi wa kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu. Kazi ya upimaji wa njia za miundombinu ya umeme kuwezesha Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu kupata umeme imekamilika. Mradi huu utahusisha ujenzi wa miundombinu ya

umeme kilomita 3.6 za msongo wa kilovolt 33, kilomita 8.1 za msongo wa kilovolt 0.4 na ufungaji wa *transformer 3.* Mradi huu unagharimiwa na Serikali na kutekelezwa na Shirika la TANESCO utagharimu jumla ya shilingi za Kitanzania 342.7 milioni. Utekelezaji wa mradi huu umeshaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi inayofadhiliwa na *Millennium Challenge Cooperation* (*MCC*). Kuhusu ukarabati wa upanuzi wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Dodoma, Morogoro, Mwanza na Tanga, makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kupoozea umeme yalifunguliwa tarehe 7 Mei, 2010 na uchambuzi unaendelea. Matarajio ni kusainiwa kwa mkataba na mkandarasi aliyeshinda ifikapo mwishoni mwa mwezi huu wa Julai, 2010. Gharama halisi za mradi zitajulikana baada ya kukamilika kwa majadiliano na mkandarasi atakayekuwa ameshinda.

Kuhusu ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme katika Mikoa hiyo 6, makabrasha ya zabuni yatafunguliwa tarehe 9 Julai, 2010. Mkataba kati ya Mkandarasi na *MCC* kwa ajili ya ujenzi wa *Sub Marine Cab* ya kutoka Dar es Salaam hadi Unguja, ulisainiwa tarehe 30 Aprili, 2010 na matarajio ni kukamilika kwa ujenzi wa mradi mwezi *August 2012*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upembuzi yakinifu wa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Mto Malagarasi ulikamilishwa mwezi Machi 2010 na kubainisha kuwepo kwa konokono adimu. Kwa mujibu wa taratibu za masuala ya mazingira, utekelezaji wa Mradi huo ulisimama. Hata hivyo, Wafadhili wa Mradi *MCC* wamekubali kufadhili upembuzi yakinifu mpya katika eneo lingine kwenye Mto Malagarasi, wanaofahamu eneo hili linaloitwa *Igamba Three* ili kutimiza azma ya kuzalisha umeme kutokana na maporomoko ya maji katika Mto Malagarasi. Mradi unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika ADB na Mradi huu unajulikana kama *Electricity Five*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu unahusu ujenzi wa kilomita 932 za njia za kusambaza umeme msongo wa kilovolt 33 na 11 katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Dar es Salaam na Arusha. Aidha, Mradi huu utahusisha ukarabati wa miundombinu ya usambazaji wa umeme kwenye Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam. Mradi huu unakadiriwa kugharimu Shilingi za Kitanzania bilioni 60 na utafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).* Mkataba kati ya Serikali na Benki ya Maendeleo ya Afrika ulisainiwa Machi 2008. Mradi utatekelezwa na wakandarasi watapatikana kwa njia ya ushindani wa zabuni zitakazoandaliwa na kutangazwa mara baada ya kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi wa Mradi, yaani *Project Consultant.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kumpata Mshauri Mwelekezi wa Mradi uko katika hatua za mwisho, Serikali na *TANESCO* wameshakamilisha masharti yote ya mkopo kuhusu Mradi huu. Taarifa ya uchambuzi wa zabuni ya kumpata Mshauri Mwelekezi wa Mradi imepelekwa kwa mfadhili *(ADB),* kwa mapitio na kutoa ridhaa ya ufunguzi wa *Financial Proposal* ili kumpata mshindi. *TANESCO* inasubiri majibu kutoka Benki ya *ADB* ambayo yanatarajiwa kupatikana wakati wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Mradi wa Makambako Songea ni kupeleka umeme wa *grid* katika Miji ya Songea, Namtumbo, Ludewa na Mbinga. Mradi unahusu ujenzi wa kilomita 250 za njia za msongo wa kilovolt 132 kutoka Makambako hadi Songea. Vituo vya kupoozea umeme katika maeneo ya Madaba na Songea, upanuzi na usambazaji wa umeme katika miji ama Wilaya za Songea, Namtumbo, Mbinga, Makambako Njombe na Ludewa. Gharama za Mradi zinakadiriwa kuwa Kroner za Kiswidi milioni 458 au zaidi ya Shilingi za Kitanzania bilioni 85. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Maendeleo SIDA na Tanzania. Mradi utahusisha kusambaza umeme vijijini katika Wilaya za Njombe, Namtumbo, Ludewa ikiwa ni pamoja na Vijiji vya Mlangali, Diganga, Lugalawa, Milo na Kilosa. Katika Wilaya ya Songea Vijijini, maeneo yatakayohusishwa ni pamoja na Vijiji vya Madaba, Wino na Mahanje. Mbinga ni Vijiji vya Mbinga na Mbamba Bay. Mradi huu kwa kuanzia utawaunganisha wateja wa awali wanaokadiriwa kufikia 30,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu ulichelewa kuanza kutokana na kuanza kwa makubaliano kati ya Serikali na Wafadhili kwenye vipengele vya ufadhili. Kwa hivi sasa, tayari Serikali imekamilisha mazungumzo na mfadhili wa mradi na kufikia muafaka kwenye vipengele vya mkopo. Kazi inayoendelea kwa sasa ni kutayarisha zabuni, tathmini ya mazingira na kuteua wakandarasi wa ujenzi wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa ya Mtwara na Lindi inapata umeme unaozalishwa kutokana na Gesi Asili ya *Mnazi Bay* katika eneo la Mtwara na inasimamiwa na Kampuni ya ARTUMAS pamoja na Shirika la TANESCO. Mazungumzo yanaendelea kati ya Kampuni ya ARTUMAS na Wakala wa Nishati Vijijini (rea) kwa ajili ya kusambaza umeme kwenye Vijiji vya Mikoa hii. Wilaya ya Kilwa itaanza kupata umeme kutokana na Gesi ya Asili ya Songosongo kutoka Kituo cha Somanga Fungu ndani ya mwezi huu wa Julai, 2010 wakati Wilaya ya Liwale inapata umeme unaotokana na mafuta mazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, baada ya kusema haya, jumla ya fedha ambazo Serikali imetumia katika hii Mikoa 16 pamoja na Miradi hii ya Bagamoyo, Kishapu na Longido ni zaidi ya shilingi bilioni 103. Huu ndiyo uwekezaji ambao umefanywa na Serikali kwa fedha yetu ya ndani na kama nilivyosema, utekelezaji wa Miradi hii utafanyika kwa kipindi kisichozidi miezi 12 na baadhi ya wakandarasi tayari wameshafika kwenye maeneo ya kazi na maandalizi yanaendelea na utekelezaji kimsingi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ni kwa baadhi ya maeneo ambayo tulidhani ni muhimu tuyaseme kwa sababu ni Miradi ambayo imekuwa ikisemewa kwa muda mrefu. Ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba, yako maombi mengi na miradi mingi ambayo sasa hivi tunaendelea kuifanyia kazi kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini *(REA).* Waheshimiwa Wabunge ambao Miradi yao haaijatajwa, siyo kwamba huko Serikalini hatuifanyii kazi, tunaendelea kuifanyia kazi; Waheshimiwa Wabunge wawe watulivu na Wananchi wazidi kuvuta subira.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ahsante sana. *(Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Katibu tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011 – Wizara ya Maliasili na Utalii

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, baada ya kuzingatia Taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, inayohusu Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa lijadili na kukubali Taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka 2009/2010. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Maliasili na Utalii na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Mwaka 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2010/2011 katika kikao chake kilichofanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 1 Juni, 2010. Maelekezo na ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii, kuwapongeza Wabunge wapya walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao ni Mheshimiwa Janet Mbene Zebedayo wa CCM na Mheshimiwa Jussa Ismail Ladhu wa *CUF*. Napenda pia kuchukua fursa hii, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa michango na ushirikiano mkubwa walionipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, napenda kuwatakia kila la kheri Waheshimiwa Wabunge wote, watakaorudi majimboni kuomba ridhaa ya Wananchi ya kuendelea kuwawakilisha katika Bunge lijalo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, naomba nitoe pole kwenu Waheshimiwa Wabunge pamoja na Wananchi, kwa kuondokewa na Kiongozi Muasisi wa Taifa letu, Mzee Rashid Mfaume Kawawa na Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Sigfrid Seleman Ng'itu, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ruangwa. Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii, kuwashukuru kwa dhati, Watumishi wote wa Wizara yangu ya Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano walionipa na wanaoendelea kunipa. Kwa namna ya pekee, ninawashukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Katibu Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Ladislaus C. Komba, Wakuu wa Idara, Taasisi na Vitengo. Vilevile, napenda niwashukuru wadau wote wa Sekta ya Maliasili na Utalii, wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa, Asasi Zisizo za Kiserikali, Sekta Binafsi pamoja na Wananchi wote kwa

ujumla, kwa ushirikiano na michango waliyotoa katika kuiendeleza Sekta hii. Kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kuwahakikishia kuwa, Wizara itaendelea kuwa nao bega kwa bega katika kuhakikisha mchango wa Sekta hii katika Pato la Taifa unaongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza, inazungumzia utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, sehemu ya pili ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa kazi wa mwaka 2009/2010, ambao umezingatia utekelezaji wa ahadi pamoja na maelekezo yaliyotolewa Bungeni na maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali. Sehemu hii imezungumzia pia changamoto ambazo Wizara ilikabiliana nazo katika utekelezaji. Sehemu ya tatu ni Mpango wa Utekelezaji na Malengo kwa mwaka 2010/2011. Sehemu ya nne ni hitimisho, ambapo Bajeti inayoombwa kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2010/2011 imewasilishwa.

Utekelezaji wa Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 imeainisha maeneo yanayohitaji kutekelezwa na Wizara. Napenda kuchukua fursa hii, kuwasilisha kwa muhtasari taarifa ya utekelezaji kama ifuatavyo: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuhifadhi, kulinda, kuendeleza na kuvuna maliasili kwa manufaa ya Taifa kwa kuzingatia Sera, Sheria na Kanuni. Aidha, katika utekelezaji, Wizara ilishirikiana na Serikali za Mitaa na Wananchi kwa ujumla, kwa lengo la kuhakikisha kuwa, wananufaika na rasilimali za maliasili kama ambavyo Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 inavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuhimiza utekelezaji wa usimamizi shirikishi wa maliasili, jumla ya Shilingi 148,082,319 zilitolewa katika Jumuiya 10 za Hifadhi ya Wanyamapori *(WMAs)*, zenye vitalu vya uwindaji wa kitalii mwaka 2009. Jumuiya hizo ni IKONA (Serengeti), MBOMIPA (Iringa Vijijini), JUHIBU-BURUNGE (Babati), ENDUIMET (Longido), NGARAMBE-TAPIKA (Rufiji), JUHIWAI (Sikonge), NALIKA (Tunduru), MBARANG'ANDU (Namtumbo), MAGINGO (Liwale) na UYUMBU (Urambo). Vilevile, jumla ya Shilingi 2,393,846,307.17 zilitolewa katika Halmashauri za Wilaya 44 kati ya mwaka 2005/2006 hadi 2008/2009. Fedha hizo zimetolewa kama sehemu ya asilimia 25 ya mapato yatokanayo na ada za wanyamapori waliowindwa na watalii katika vitalu vilivyopo katika Wilaya husika. Madhumuni ya kutoa fedha hizo ni kuziwezesha Halmashauri zenye vitalu vya uwindaji wa kitalii kugharamia miradi ya maendeleo na kuhakikisha kuwa, Wananchi wanaoishi maeneo yenye wanyamapori wanafaidika na rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza lengo la Ilani linaloelekeza kuendeleza ufugaji wa nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali na nta kibiashara, Wizara iliendelea kutekeleza mpango wa udhibiti wa kemikali katika asali, likiwa ni sharti la lazima kwa nchi kuweza kuuza asali katika Soko la Nchi za Ulaya. Jumla ya sampuli 64 za asali zilikusanywa kutoka katika wilaya 25 pamoja na wafanyabiashara wakubwa wa asali. Wilaya hizo ni Kongwa, Manyoni, Sikonge, Uyui, Urambo, Kahama, Bukombe, Mufindi, Njombe, Makete, Chunya, Ileje, Mpanda, Nkasi, Simanjiro, Kiteto, Mwanga, Monduli, Kigoma, Rufiji, Kasulu, Kibondo, Singida, Dodoma na Same. Mpango huu umewezesha

mauzo ya asali katika masoko ya nje kuongezeka kutoka tani 430 kwa kipindi cha Januari mpaka Desemba mwaka 2008 hadi kufikia tani 620.5 kwa kipindi kama hicho mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ubelgiji, inatekeleza mradi wa kuboresha uchakataji, ufungashaji na utafutaji wa masoko *(processing, packaging and marketing)* ya mazao ya nyuki katika Wilaya za Rufiji, Kibondo na Kigoma. Mradi huu umesaidia ubora wa asali kuongezeka kufikia kiwango cha kimataifa kutokana na uchambuzi wa maabara uliofanyika nchini Ubelgiji mwaka 2009. Aidha, uboreshaji wa uchakataji na ufungashaji wa mazao ya nyuki umechangia kuongeza bei ya asali kwa mfugaji nyuki kufikia shilingi 3,000 kwa lita mwaka 2009, ukilinganisha na shilingi 800 hadi 1,000 kwa lita mwaka 2008. Vilevile, Wizara iliendelea kuboresha mashamba ya ufugaji nyuki ya mfano yenye makundi ya nyuki 1,015 katika Wilaya za Handeni, Kondoa, Manyoni na Kibondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Ilani la kuweka utaratibu shirikishi wa upandaji miti, uvunaji na udhibiti wa moto lilitekelezwa kwa kuchukua hatua kadhaa zikiwemo kushirikisha Wananchi kupanda miti na kuhakikisha wanapata mbegu bora za miti kwa ajili ya kuanzisha vitalu binafsi vya miche. Kwa kuzingatia haja ya kuongeza kasi ya upandaji miti nchini, Serikali ilibadilisha Siku ya Taifa ya Kupanda Miti kutoka Januari Mosi na kuwa Aprili Mosi ya kila mwaka kwa kuwa sehemu nyingi nchini kwa kipindi hicho zinakuwa na mvua za kutosha. Aidha, elimu ya kuzuia moto ilitolewa kwa umma kupitia mabango, sinema, vipeperushi na vipindi vya redio na televisheni. Vilevile, zoezi la kuzima moto limefanyika katika maeneo ya Misitu ya Hifadhi ya Pugu/Kazimzumbwi hekta 240, Mlima Rungwe hekta 200, Chome hekta 30, Magamba hekta 400, Shamba la Miti Shume hekta 55, Kilima na Mlima Meru hekta 500, Sao Hill eneo la shamba la binafsi (*Green Resource*) hekta 1900.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea na jitihada za kukuza utalii na kutafuta masoko mapya ya utalii kwa kuendesha kampeni ndani na nje ya nchi kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kupanua wigo wa Mazao ya Utalii kwa kubainisha aina nyingine za utalii kama vile utalii wa mikutano, fukwe za bahari, ikolojia, malikale na michezo. Baadhi ya mikutano mikubwa iliyofanyika ni pamoja na Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uvumbuzi wa Fuvu la Zamadamu (*Zinj*), Kongamano la Tano la Kimataifa la Mtawanyiko wa Watu Wenye Asili ya Afrika Duniani (*African Diaspora Heritage Trail*) na pia Mkutano wa Uchumi wa Dunia kwa Afrika (*World Economic Forum for Africa*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mikutano hii, nchi yetu imeweza kunufaika kimapato na kujitangaza kimataifa katika nyanja za utalii, uwekezaji na kuvutia wageni. Katika kuhamasisha Watanzania kupenda kutembelea vivutio vya Utalii, Wizara ilizindua kampeni ya kukuza utalii wa ndani kwa kuhamasisha kampuni za kitalii kuanzisha safari maalum za kitalii kwa gharama nafuu. Vilevile, Bodi ya Utalii ilianzisha chapisho liitwalo *Utalii Leo* ambalo hutolewa mara moja kwa mwezi na kuwekwa kwenye magazeti nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii wa michezo pia umeanza kuonekana baada ya kukamilishwa kwa uwanja wa mpira wa hadhi ya Kimataifa wa Taifa. Katika mwaka huu, timu mashuhuri za mpira wa miguu za Ivory Coast na Brazil zimeweza kuja Tanzania kucheza na timu ya mpira ya Taifa. Ujio wao uliambatana na wageni wengi wa kitalii. Aidha, kufuatia kufanyika kwa michezo ya kombe la dunia nchini Afrika ya Kusini, nchi yetu imenufaika na watalii wanaopitia Tanzania wakati wa kwenda na au kurudi toka Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika mwezi Mei pekee watalii 500 wa namna hiyo kutoka nchi mbalimbali za Ulaya walitembelea Tanzania ili kujionea vivutio mbalimbali vya utalii kabla ya kuendelea na safari ya kwenda Afrika Kusini. Ili kuwahamasisha zaidi Serikali imeamua kutoa visa ya kuingia na kutoka zaidi ya mara moja (*multiple visa*) ya mwezi mmoja ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama toka Dola za Kimarekani 50 hadi 25 kwa watalii wa aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuhakikisha kuwa Sekta ya Utalii inachangia ipasavyo katika kukuza uchumi wa Taifa, Wizara iliendelea kudumisha masoko ya asili ya utalii pamoja na kujitangaza katika masoko mapya kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo kushiriki maonesho ya kitaifa na kimataifa. Bodi ya Utalii Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa utalii ilishiriki katika maonesho ya utalii 17 nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) kupitia kipindi cha zamadamu kinachorushwa hewani mara tatu kwa wiki, iliendelea kutangaza umuhimu wa kuhifadhi na kuendeleza urithi wa utamaduni. Maeneo yaliyotangazwa kupitia kipindi hiki ni pamoja na Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara, Njia Kuu ya Kati ya Biashara ya Utumwa na meno ya tembo, Bonde la Olduvai, na Nyayo za Zamadamu katika eneo la Laetoli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha mafunzo, Chuo cha Taifa cha Utalii kimepata msaada toka Hanns Siedel Foundation wa kuwekewa mfumo wa teknolojia (*Fidelio Hotel Software)* kwa ajili ya kufundishia wanachuo wa fani ya ukarimu. Mfumo huu hutumiwa katika hoteli nyingi za kitalii duniani. Aidha, ili kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa katika Sekta ya Utalii na kuongeza uwingi wa watumishi wenye sifa, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa inakamilisha ujenzi wa chuo kipya jijini Dar es Salaam. Mradi huo upo katika hatua ya kuweka vifaa vya kisasa vya kufundishia na inatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa utoaji wa huduma za hoteli na huduma nyingine za malazi unazingatia viwango vya kimataifa, Wizara ilifanya zoezi la kupanga hoteli katika daraja kwa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kuanzia mwezi Machi, 2009. Zoezi hili lilihusisha uhakiki wa hoteli 203 ambapo hoteli 99 kati ya hizo zilikidhi vigezo vya kupewa daraja. Kati ya hizo, ni hoteli na huduma nyingine za malazi

66 tu ndiyo zimestahili kupewa nyota na zilizosalia hazikupewa kutokana na kasoro ambazo iwapo zitarekebishwa, zitakuwa na sifa ya kupewa nyota.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuhamasisha wawekezaji katika sekta ya utalii, msukumo zaidi umewekwa katika kukuza utalii Ukanda wa Utalii wa Kusini. Ukanda huu umejaliwa kuwa na vivutio anuai kama vile wanyamapori, fukwe, maeneo ya kihistoria, tamaduni, misitu ya asili na maeneo yenye mandhari nzuri na mvuto wa kipekee. Katika Maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani mwaka 2009 yaliyofanyika kitaifa mkoani Iringa, na kwa kuzingatia vivutio hivyo, Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika nyanja za utalii katika ukanda huo. Mpaka sasa mwelekeo unaridhisha kwani sekta binafsi inaendelea kuwekeza katika ujenzi wa hoteli na mahema ya kulaza wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea na jitihada za kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kufanya tathmini ambayo ilibaini maeneo yanayohitajika kuboreshwa. Hatua kadhaa zimekwisha chukuliwa ikiwa ni pamoja na kuainisha vifungu vidogo vya kukusanya mapato na kuhakikisha wateja wanafanya malipo kupitia benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2009/2010, Wizara ilizingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA-I), Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015. Vilevile, utekelezaji ulizingatia Sera, Sheria, Kanuni na Mpango Mkakati wa Wizara (2007-2010). Napenda kutoa taarifa ya utekelezaji kisekta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ndogo ya Wanyamapori iliendelea na jukumu la kusimamia, kuhifadhi, kuendeleza na kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho. iIi kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2009, Wizara iliandaa rasimu za Kanuni tisa. Kati ya hizo, rasimu za Kanuni nne zinazohusu Uwindaji wa Kitalii, Uwindaji wa Wenyeji, Ukamataji wa Wanyamapori hai, na Leseni ya Biashara ya Nyara zimewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki wa mwisho kabla ya kuchapishwa rasmi ili tarehe ya kuanza kutumika sheria yenyewe iweze kutajwa. Rasimu ya Kanuni tano kuhusu Kifuta Jasho/Machozi, Ufugaji wa Wanyamapori, Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo Katika Hatari ya Kutoweka Duniani, Utalii wa Picha na Maeneo ya Hifadhi ya Jamii zipo katika hatua ya kujadiliwa na wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi 176 ambazo ni wanachama wa Mkataba wa Kudhibiti Biashara ya Kimataifa ya Wanyama na Mimea iliyopo hatarini kutoweka (*Convention on International Trade in Endangered Species of Wild Fauna and Flora – CITES*) kuanzia mwaka 1980. Katika mkutano wa 15 wa nchi wanachama wa *CITES* uliofanyika Doha, Qatar Machi, 2010 Tanzania iliwasilisha ombi la kuruhusiwa kuuza tani 89.8 za meno ya tembo. Lengo kuu la ombi hilo lilikuwa kupata fedha zinazokadiriwa kufikia shilingi bilioni 20 kwa ajili ya uhifadhi wa tembo na

wanyamapori wengine na kuimarisha ushirikishwaji wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ombi hilo halikufikia theluthi mbili za kura ya Ndiyo za wanachama wa *CITES* na hivyo kutokupita. Kwa sasa Serikali imejipanga kuimarisha maeneo manne yafuatayo: Kwanza, kuimarisha doria ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Pili, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Serikali, kuimarisha mfumo wa ukaguzi mipakani na bandarini ili kudhibiti meno ya tembo na nyara nyingine zinazopitishwa hapa nchini kwenda nje ya nchi. Tatu, kuimarisha mfumo wa kuidadi tembo na kuweka takwimu sahihi za tembo hapa nchini na mwisho kuongeza kampeni za kushawishi na kuomba kuungwa mkono na nchi wanachama wa *CITES*. Wizara itayafanyia kazi masuala haya yote katika kipindi hiki cha miaka mitatu ili ombi hilo liwasilishwe tena kwenye mkutano wa 16 wa CITES utakaofanyika nchini Thailand mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza dhamira ya uhifadhi na matumizi endelevu ya wanyamapori na mazingira yake, hadi Machi 2010 siku za doria 47,722 ziliendeshwa ndani na nje ya Mapori ya Akiba. Kutokana na doria hizo jumla ya kesi 568 zenye watuhumiwa 602 zilifunguliwa. Aidha, kesi 215 zenye jumla ya watuhumiwa 375 zilimalizika kwa watuhumiwa kukiri makosa na kulipa faini ya jumla ya shilingi 33,151,000. Kesi 353 zilifikishwa mahakamani ambapo kesi saba zilimalizika na watuhumiwa 13 kuhukumiwa kifungo cha jumla ya miezi 392 jela na kesi 346 zinaendelea kusikilizwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha na kupanua mtandao wa barabara na viwanja vya ndege katika mapori ya akiba, barabara zenye urefu wa kilomita 425 zilikarabatiwa katika Mapori ya Akiba ya Selous na Mpanga-Kipengere. Vilevile, viwanja vya ndege vitano katika Pori la Akiba Selous na kimoja katika Pori la Akiba Rungwa vilikarabatiwa na kuwekewa alama za kuongoza ndege. Wizara iliendelea kukabiliana na changamoto ya upungufu wa nyumba za watumishi kwa kujenga nyumba mbili katika Mapori ya Akiba ya Maswa na Mkungunero.

Aidha, hatua ya kuboresha huduma za maji kwa watumishi wa Pori la Akiba Rungwa zilichukuliwa kwa kuanzisha mchakato wa kukarabati bwawa la kuhifadhi maji ya Mto Rungwa lililobomoka. Katika kuboresha upatikanaji wa umeme kwa watumishi wa Pori la Akiba Maswa, jenereta mpya ilinunuliwa na kufungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ina jukumu la kulinda maisha na mali za wananchi kwa kufanya doria za msako wa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Hadi Machi 2010, jumla ya siku za doria 2,111 ziliendeshwa katika Wilaya 16 zilizokuwa na matatizo ya wanyamapori wakali na waharibifu. Wilaya hizo ni: Mkinga, Kilombero, Sikonge, Rombo, Siha, Masasi, Biharamulo, Serengeti, Bukoba, Songea, Bunda, Hai, Karagwe, Nachingwea, Manyoni na Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utafiti wa kudhibiti tembo waharibifu wa mazao kwa kutumia pilipili kali iliyochanganywa na oili chafu unaendelea na umefanyika katika vijiji 22 vya Wilaya za Bunda, Serengeti na Liwale. Utafiti huo umeonesha mafanikio makubwa na utaendelezwa katika wilaya nyingine zenye matatizo ya tembo waharibifu wa mazao. Aidha, wananchi wanahamasishwa kutumia njia hizo katika kuwadhibiti wanyama hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kutekeleza utaratibu wa kutoa kifuta machozi kwa wananchi walioharibiwa mazao na kufiwa na ndugu waliouawa na wanyamapori wakali. Jumla ya Shilingi 155,200,000 zilitolewa kama kifuta machozi katika Wilaya za Nanyumbu, Masasi, Kilwa, Dodoma, Iramba, Bahi, Manyoni, Singida (V), Morogoro, Mkuranga, Shinyanga, Kigoma, Bukoba, Tunduru, Kilombero, Ruangwa, Kondoa, Misenyi, Liwale na Serengeti. Hata hivyo, Wizara imepokea malalamiko mengi kuhusu viwango vidogo vinavyotumika kwa sasa. Katika kutambua ukubwa wa tatizo nchini kote na pia kufuatia suala hili kuingizwa kwenye Sheria mpya ya Wanyamapori ya mwaka 2009, Wizara inalifanyia kazi suala hilo kuangalia uwezekano wa kuboresha viwango hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kudhibiti kunguru weusi liliendelea katika maeneo ya Jiji la Dar es Salaam na Bagamoyo ambapo jumla ya kunguru weusi 17,158 waliuawa. Wizara pia iliunda kamati ya kupanga na kusimamia mikakati ya kudhibiti kunguru weusi. Kamati hiyo inahusisha Idara ya Wanyamapori, Halmashauri ya Jiji, Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke, Shirika lisilo la Kiserikali la Kuhifadhi Wanyamapori (*WCST*), Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu katika nchi za Kitropiki (*TPRI*) na Kituo cha Kudhibiti Baa la Panya (Morogoro).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Idara ya Wanyamapori ilikadiria kukusanya jumla la Shilingi 21,443,269,000. Aidha, hadi kufikia mwezi Mei 2010, kiasi kilichokusanywa kilikuwa ni Shilingi 15,392,449,649.86 ikiwa ni asilimia 71.78 ya lengo. Wizara inatarajia kukusanya Shilingi 30,015,900,000. kutokana na rasilimali za wanyamapori katika mwaka wa fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori uliendelea kugharamia shughuli za kulinda wanyamapori, utafiti, mafunzo, kutoa elimu kwa umma na kuimarisha miundombinu. Katika mwaka 2009/2010, Mfuko ulikadiria kukusanya Shilingi 9,908,913,067.33 ambapo hadi kufikia Aprili, 2010 Mfuko ulikuwa umekusanya Shilingi 12,793,265,705.43. Aidha, Mfuko unakadiriwa kukusanya kiasi cha Shilingi 12,994,051,019.50 mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo kilikamilisha mitaala ya Stashahada za Utalii wa Wanyamapori na Astashahada ya Utaalamu wa Uwindaji wa Kitalii. Mafunzo hayo yalianza mwezi Agosti 2009. Stashahada ya Utalii ni mafunzo ya miaka miwili na Astashahada ya Utaalamu wa Uwindaji wa Kitalii ni mwaka mmoja. Aidha, Chuo kwa

kushirikiana na wahisani kiliwezesha wakufunzi sita kupata mafunzo katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*) na sita katika masomo ya Shahada ya Uzamili (*MSc*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori katika mwaka 2009/2010, iliendelea na zoezi la kuhesabu wanyamapori nchi nzima na kutathmini ubora wa vitalu vya uwindaji wa kitalii. Sensa 10 za wanyamapori zilifanyika katika Hifadhi za Taifa za Serengeti, Ruaha, Katavi, Mikumi, Tarangire, Ziwa Manyara na eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na maeneo ya wazi yanayozunguka hifadhi hizo. Maeneo mengine ambayo yalifanyiwa sensa ni pamoja na Mapori ya Akiba ya Selous, Rungwa, Moyowosi, Kigosi, Rukwa, Ikorongo, Grumeti, Maswa na Ugalla. Hali kadhalika, sensa zilifanyika katika maeneo ya West Kilimanjaro, Ziwa Natron, Malagarasi-Moyowosi pamoja na Ushoroba wa Selous –Niassa.

Taasisi pia ilifanya tathmini ya kutambua ubora wa vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa vitalu 159 nchini. Tathmini ilifanyika kwa kuzingatia aina na idadi za wanyamapori na ubora wa miundombinu yaani barabara na viwanja vya ndege katika vitalu hivyo. Kufuatia tathmini hiyo, vitalu vimegawanywa katika makundi manne, kulingana na ubora wake. Katika zoezi hilo pia mipaka ya vitalu imehakikiwa ili kuondoa migogoro ya mipaka iliyojitokeza kipindi cha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi iliendeleza utafiti kuhusu mienendo ya mbwa mwitu, athari yao kwa jamii ya wafugaji katika Pori Tengefu la Loliondo pamoja na kutathmini uwezekano wa kuhamisha baadhi ya makundi kwa lengo la kuyapeleka Hifadhi ya Taifa Serengeti. Tafiti ilifanyika katika vijiji 16 vilivyoko katika Pori Tengefu la Loliondo na maeneo yaliyo karibu na Hifadhi ya Taifa Serengeti, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Pori la Akiba Maswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa idadi ya mbwa mwitu imepungua kutoka 192 kwa mwaka 2008/2009 hadi kufikia mbwa mwitu 150 kwa mwaka 2009/2010. Sababu kubwa ya kupungua kwa mbwa mwitu hao ni migogoro kati ya mbwa mwitu na wafugaji, hali ambayo imewafanya wafugaji kutumia sumu kupunguza idadi ya mbwa mwitu katika kudhibiti uharibifu kwa mifugo yao. Mradi wa kukusanya taarifa za Wanyamapori Wanyonyeshao uliendelea kutekelezwa. Aidha, Mpango Mkakati wa kuendeleza uhifadhi wao kitaifa umekamilika tayari kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa liliendelea kusimamia uhifadhi wa maliasili na mazingira pamoja na kusimamia mwenendo wa shughuli za utalii ndani ya hifadhi. Katika mwaka 2009/2010, jumla ya siku za doria 112,208 zilifanyika ndani ya hifadhi za Taifa pamoja na maeneo yanayozunguka hifadhi hizo. Katika doria hizo, jumla ya majangili 3,773 walikamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. Shirika liliwezesha askari na wahifadhi kushiriki mafunzo maalum ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na wimbi la ujangili na ujambazi kwenye Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utoaji wa huduma za utalii, Shirika liliendelea na uboreshaji wa miundombinu ikiwemo barabara na sehemu za kulala wageni. Barabara mpya ya kuelekea Loji ya Bilila – Kempinski ilijengwa katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Vilevile, Shirika lilikamilisha ujenzi wa mabanda ya watalii katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa lengo la kupunguza gharama za malazi kwa wageni hususan kwa ajili ya watalii wa ndani. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Shirika lilishiriki maonesho 27 kwa lengo la kujitangaza na kuvutia watalii katika mabara ya Ulaya, Amerika na Asia. Nchi zilizohusika ni Korea, Japan, Russia, China, Canada, Singapore, Uingereza, Hispania, Uholanzi, Ureno, Uturuki, Marekani, Ubelgiji, India, Italia, Ujerumani, Ufaransa, Sweden na Falme za Kiarabu (Dubai).

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mpango wa Ujirani Mwema, Shirika la Hifadhi za Taifa lilitumia jumla ya Shilingi 3,470,873,720/= kuchangia utekelezaji wa miradi 109 ya maendeleo ya jamii kwa vijiji vinavyozunguka hifadhi za taifa. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa, mabweni, nyumba za walimu na waganga, zahanati na malambo ya maji. Kati ya miradi hiyo, 27 imekamilika na 82 ipo katika hatua za mwisho za utekelezaji. Katika kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa hifadhi za taifa, Shirika limeandaa rasimu ya Mipango ya Usimamizi wa Hifadhi za Taifa za Mkomazi na Saadani. Zoezi la kufanya mapitio ya Mipango ya Usimamizi wa Hifadhi za Taifa za Tarangire na Udzungwa linaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ina jukumu la kusimamia uhifadhi wa maliasili na mazingira, kutangaza na kukuza utalii pamoja na kuwaendeleza wananchi wanaoishi ndani ya eneo la Mamlaka. Katika kuimarisha doria dhidi ya ujangili wa wanyamapori na misitu, Mamlaka ilinunua nyenzo za doria za kisasa na kufanya matengenezo ya kawaida katika barabara zake ili zipitike vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka iliendelea na mpango wake wa kugharamia miradi ya maendeleo ya jamii ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi, nyumba ya Mkuu wa Kituo na nyumba za askari kwenye makao makuu ya Hifadhi ya Ngorongoro. Kiasi cha Shilingi 260,049,460 kilitumika katika ujenzi huo. Vilevile, jumla ya Shilingi 464,734,952 zilitumika katika ujenzi wa madarasa manne, ofisi mbili, nyumba ya Mwalimu Mkuu na nyumba nne za walimu. Aidha, Mamlaka ilitumia Shilingi 249,838,622 kugharamia ujenzi wa zahanati yenye vyumba kumi na tatu (13), nyumba ya Daktari na Nyumba mbili za Wauguzi katika makazi mapya ya wananchi waliohamishwa kutoka ndani ya eneo la Ngorongoro, yaani Jema-Oldonyo Sambu.

Mamlaka, kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa wa Arusha na Wilaya ya Ngorongoro, inaendelea na zoezi la kutafuta maeneo mengine ya kuishi nje ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa ajili ya makazi na kilimo. Lengo la hatua hii ni kupunguza msongamano wa shughuli za binadamu ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Mamlaka ilitumia jumla ya Shilingi 70,392,000 kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya jamii

inayozunguka Hifadhi ya Ngorongoro. Miradi hiyo ni ya majengo katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Michaud, Shule za Sekondari za Malambo, Slahamo, Oltiga, Loliondo na Mlima Oldonyo Sambu pamoja na Shule za Msingi za Endulen na Oldonyo Sambu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha na kudhibiti mapato, Mamlaka imekamilisha mchakato wa kuweka na kutumia mfumo wa *smart card* ulioanza kutumika Mei, 2010 sambamba na mfumo uliokuwepo. Mfumo huu unasaidia kupunguza upotevu wa fedha unaoweza kutokea kwa kupokea malipo kwa fedha taslimu pamoja na kuhakikisha usalama katika ukusanyaji mapato. Katika kuunga mkono mkakati wa Serikali wa kuboresha elimu ya Sekondari, katika mwaka 2009/2010, Mamlaka ilitenga Sh. 653,000,000 kwa ajili ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa shule ya Sekondari ya Kisasa Nainokanoka. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba jengo la utawala, nyumba za walimu mbili, mabweni mawili, madarasa manne, na vyoo vipo kwenye hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, soroveya kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki iliendelea na jukumu lake la kusimamia, kuhifadhi na kutunza rasilimali za Misitu na Nyuki. Sekta hii iliendelea kuhakikisha upatikanaji endelevu wa huduma na mazao kwa kusimamia na kuhifadhi misitu ya asili pamoja na misitu ya kupandwa. Pia iliendelea na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kuuzwa kwa rasilimali za Misitu na Nyuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998. Rasimu ya mwisho imewasilishwa kwenye Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Misitu ili kuipitia kabla ya kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri kwa uamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea na shughuli za utunzaji wa mashamba 16 ya miti ya kupandwa yanayomilikiwa na Serikali kwa kupanda jumla ya miche 8,941,700. Aidha, kiasi cha hekta 5,950 zilitayarishwa na kupandwa miti ya aina mbalimbali, hekta 5,289 za mashamba ya miti inayoendelea kukua zilipogolewa matawi na hekta 14,200 za miti michanga zilipaliliwa. Pia, katika kipindi hicho mipaka na barabara za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 873 zilifyekwa na barabara zenye urefu wa kilomita 926 zilitengenezwa. Kwa ujumla katika kutekeleza shughuli hizi, Wizara iliweza kuvuka lengo la utekelezaji kutokana na matumizi ya fedha zinazotokana na shughuli za uvunaji katika mashamba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa uvunaji endelevu wa rasilimali za misitu unazingatiwa, Mipango ya Usimamizi kwa mashamba 15 ya miti ya kupandwa inayosimamiwa na Serikali isipokuwa Shamba la Ruvu imekamilika na sasa inatumika. Mipango hii inaonyesha shughuli zote za usimamizi na uvunaji wa rasilimali katika mashamba haya. Mwaka 2009/2010 miti yenye ujazo wa mita 12,634,393 ilikuzwa (*growing stock)* katika mashamba hayo na kati ya hizo, miti yenye ujazo wa mita 1,200,000 ipo tayari kwa uvunaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kulinda rasilimali za Misitu na Nyuki, Wizara iliendelea kuimarisha kikosi cha doria katika Kanda nane na kukijengea uwezo. Hali kadhalika, Wizara imekamilisha ujenzi wa ofisi za kudumu katika vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu vya Kamanga na Usagara na kujenga vituo vya Busisi mkoani Mwanza, Maweni mkoani Tanga, Isaba mkoani Mara, Nyangao mkoani Lindi, Msijute mkoani Mtwara, Shamwengo mkoani Mbeya, Vikindu na Kisarawe mkoani Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kutilia mkazo matayarisho na utekelezaji wa mipango ya usimamizi na matumizi ya mazao ya misitu. Aidha, wilaya 29 ziliandaa mipango ya usimamizi na matumizi ya mazao ya misitu ambapo wilaya 27 kati ya hizo ziliwezeshwa kuendesha vikao vya uvunaji wa mazao ya misitu vya Wilaya. Wilaya hizo ni Bagamoyo, Biharamulo, Bukombe, Chunya, Geita, Handeni, Kasulu, Kigoma Vijijini, Kilindi, Kilombero, Kilosa, Kilwa, Kisarawe, Liwale, Manyoni, Masasi, Mkuranga, Mpanda, Mvomero, Nanyumbu, Rufiji, Sikonge, Sumbawanga, Tunduru, Ulanga, Urambo na Uyui.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujenga uwezo wa viwanda vya kuchakata mbao, Wizara kupitia Chuo cha Viwanda vya Misitu iliendesha mafunzo kwa wafanyakazi wa viwanda hivyo kwa ajili ya kuongeza tija na ubora wa bidhaa za mbao zinazozalishwa. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wafanyakazi wa viwanda vya kuchakata mbao katika maeneo ya Rongai, Lushoto, Njombe na Mafinga. Hii ni hatua mojawapo katika kukabiliana na changamoto za viwanda vingi vya kuchakata magogo kutoendeshwa kwa ufanisi na kusababisha upotevu wa malighafi ya mbao katika matumizi kutokana na kukosa teknolojia ya kisasa, ambapo upotevu huo unafikia hata asilimia 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea na zoezi la kupandisha hadhi misitu ya hifadhi kuwa hifadhi za mazingira asilia (*Nature Reserves).* Kama nilivyoliahidi Bunge lako tukufu, taratibu za kisheria za kutangaza misitu ya hifadhi ya Magamba na Chome kuwa misitu ya mazingira asilia zimekamilika. Aidha, mchakato wa kutangazwa kwa misitu ya Tao la Mashariki kuwa katika Orodha ya Urithi wa Dunia umekamilika na kuwasilishwa kwenye Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*) kwa hatua zaidi za kutangazwa. Kutokana na juhudi hizi, maeneo ya utalii ikolojia yataongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwezesha usimamizi endelevu wa hifadhi za mazingira asilia na misitu ya hifadhi, mipango ya usimamizi ya misitu 14 ya Amani, Nilo, Kilombero, Uluguru, Magamba, Chome, Rungwe, Palaulanga, Nawenge, Mkingu, Igombe River, Mpanda Hill, Monduli na Nyahua-mbuga imekamilika na inatumika. Kazi hii bado inaendelea kwa misitu 30 kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara, kwa ushirikiano na sekta binafsi (*Public - Private Partnership),* imeendelea kuhifadhi rasilimali za misitu. Kupitia Programu ya

Taifa ya Misitu na Ufugaji Nyuki, Wizara iliandaa rasimu ya mpango wa kuwezesha sekta binafsi kusimamia misitu na biashara ya hewa ukaa. Aidha, Ushirika wa Wakulima wa Miti (*Tree Growers Association*) uliundwa kwa lengo la kuwa na sauti moja katika kupanga bei na kupata fursa za teknolojia na ujasiriamali. Chini ya umoja huo, wanachama 495 katika vijiji 11 vya majaribio kwenye Wilaya za Njombe, Mufindi, Kilolo na Rungwe, walipewa miche ya miti ya mbao 297,000 ambapo kila mwanachama alipata miche 600 na kuipanda kitaalamu katika mashamba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara, katika kuwezesha sekta binafsi kusimamia misitu na biashara ya hewa ukaa *(Private Forestry and Carbon Trading Project*), ilikamilisha andiko la mradi ambao utagharimiwa na Serikali ya Finland kwa kipindi cha mwaka mmoja. Lengo la mradi huu ni kuwezesha sekta binafsi kuzalisha malighafi za viwanda vya misitu na kuwezesha wakulima wadogo kunufaika na rasilimali za misitu wanayomiliki kwa lengo la kuinua kipato chao. Mpango huu unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2010/11 katika Mikoa ya Iringa na Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kutekeleza Mradi wa Tathmini ya Rasilimali za Misitu (*National Forest Resource Monitoring and Assessment - NAFORMA*) kwa kutoa mafunzo kwa wataalamu watakaoshiriki zoezi la kuhesabu miti. Aidha, utaratibu utakaotumika kuhesabu miti umekamilika na maeneo yatakayohusika yameainishwa (*sampling design and sampling plots*) na kubainisha mahitaji halisi ya zoezi zima. Kazi ya kuhesabu miti ilianza mwezi Mei 2010 katika ukanda wa mashariki unaohusisha Mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Tanga na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara kwa kutumia fedha za Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (*FAO*) iliwezesha Mashirika yasiyo ya kiserikali (*NGOs*) kutekeleza shughuli zinazohusu Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki. Jumla ya mashirika saba yasiyo ya kiserikali yalichaguliwa baada ya kushinda zabuni. Mashirika hayo ni ITISO *Women Group, Former District Commissioners* Forum (*FODICO*), Tanzania *Chamber of Commerce Industry and Agriculture, Tanzania Association of Women Leaders in Agriculture and Environment* (*TAWLAE*), *ENVIROCARE, Tanzania Forest Conservation Group* (*TFCG*) na Chanika CDM *Associates.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inajihusisha na utoaji elimu ili kuwaongezea ufahamu wananchi juu ya utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za usimamizi, utunzaji na matumizi ya rasilimali za Misitu na Nyuki. Aidha, Wizara kwa kutumia maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, Sabasaba na Nanenane, iliendelea kuelimisha jamii ambapo elimu ya uhifadhi na utunzaji wa misitu, ufugaji nyuki na ubora wa asali ilitolewa kwa wadau wote waliotembelea banda la Wizara. Pamoja na kutumia kanda saba za uenezi, jumla ya vipindi 72 vya redio na sita (6) vya televisheni vinavyohusu Misitu na Nyuki vilirushwa hewani.

Vilevile, kalenda 3,000, majarida 9,500 ya misitu ni mali, 6,000 za jarida la Maliasili, na mabango 10,000 ya kampeni ya kuzuia moto yalichapishwa na kusambazwa kwa wadau. Katika juhudi za kulinda na kurudisha uoto wa asili katika hifadhi za

mikoko, kamati za mazingira katika vijiji 191 vinavyozunguka maeneo ya Delta ya Mto Rufiji, ilipatiwa mafunzo ya uhifadhi kupitia mradi wa *MACEMP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki pia inahusika na ukusanyaji wa maduhuli. Hadi kufikia mwezi Mei 2010, Wizara kupitia Idara ya Misitu na Nyuki ilikusanya kiasi cha shilingi 28,406,865,318.30 ambayo ni asilimia 119.23 na hivyo kuvuka lengo la mwaka la kukusanya Shilingi 23,825,361,000. Katika mwaka 2010/2011 matarajio ni kukusanya shilingi 38,958,900,000. Ili kuongeza ufanisi na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli hasa yale yatokanayo na mkaa, Wizara itashirikiana na wadau mbalimbali katika ukusanyaji kwa njia ya ubia (*outsourcing*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa *LMDA – Logging and Miscellaneous Deposit Account* ulianzishwa mwaka 1984 kwa madhumuni ya kuimarisha usimamizi na kuhudumia mashamba 16 ya miti. Fedha za *LMDA* zinatumika kwa upandaji miti maeneo yaliyovunwa, kupogoa matawi, kupunguza miti, kupalilia, kujenga na kukarabati barabara na madaraja. Aidha, hutumika pia kujenga na kukarabati nyumba za watumishi mashambani, kununua na kukarabati magari na mitambo na ulinzi wa misitu dhidi ya moto.

Kwa mwaka 2009/2010, mapato ya *LMDA* hadi Aprili 2010 kwa mashamba nane kati 16 yenye miti iliyofikia umri wa kuvunwa yalifikia shilingi 9,543,783,556 ambazo ni sawa na asilimia 76 ya makadirio ya mapato ya shilingi 12,456,794,000 kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

SHAMBA LA MITI	**MAKADIRIO YA LMDA (TAS)**	**MAKUSANYO HADI APRILI 2010 (TAS)**
1. SAO HILL	9,838,144,000	7,500,193,130
2. LONGUZA	369,180,000	582,657,260
3. MTIBWA	483,100,000	392,647,802
4. BUHINDI	303,600,000	225,709,315
5. MERU/USA	323,310,000	252,990,358
6. SHUME	235,700,000	174,618,491
7. WEST KILIMANJARO	328,760,000	207,401,270
8. NORTH KILIMANJARO	575,000,000	207,565,930
JUMLA	**12,456,794,000**	**9,543,783,556**

Chanzo: Idara ya Misitu na Nyuki

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kutunza na kuhudumia mashamba ya ufugaji nyuki ya mfano na hifadhi za nyuki zilizopo katika Wilaya za Handeni, Kondoa, Manyoni na Kibondo. Vilevile, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wafugaji nyuki katika wilaya 30 kwa takriban miaka mitatu sasa. Katika mwaka 2009/2010, wataalamu wa ufugaji nyuki katika Wilaya za Kongwa, Same, Kahama na Geita walipatiwa pikipiki ili kuwawezesha kuwafikia wafugaji kirahisi. Aidha, wananchi wapatao 2,947 katika vijiji 134 vya wilaya 29 walipatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki na

kuunda vikundi 227 vya ufugaji nyuki. Jumla ya mizinga ya kisasa 931 na zana za kuvunia asali jozi 220 vilinunuliwa na kusambazwa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupanua wigo wa soko la asali nchini, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Asali Tanzania ilifanya maonesho ya asali na kongamano Jijini Dar es Salaam. Maonesho hayo yaliwakutanisha wafugaji nyuki 150 kutoka mikoa 18 ya Tanzania na Kongamano lilikutanisha wataalamu 70 kutoka ndani na nje ya nchi ili kujadili maendeleo ya sekta ya ufugaji nyuki nchini. Aidha, rasimu ya mkakati wa Baraza la Asali Tanzania ilijadiliwa na kuboreshwa.

Kwa kipindi cha mwaka 2009/2010, mauzo ya asali na nta nje ya nchi yalikuwa tani 291.2 za asali zenye thamani ya shilingi 686,418,795.10 na tani 252.5 za nta zenye thamani ya shilingi 1,527,354,277. Mauzo haya yalipungua kwa tani 138.8 za asali na tani 249.836 za nta ikilinganishwa na mwaka 2008/2009 kutokana na ukame uliokumba maeneo mengi ya nchi, kuongezeka kwa matumizi ya asali nchini, kushuka kwa bei ya nta katika soko la dunia na mtikisiko wa hali ya uchumi duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Wizara yangu iliendelea kuboresha mafunzo ya taaluma ya Misitu na Nyuki. Jumla ya wanafunzi 128 walidahiliwa katika vyuo vya Misitu kama ifuatavyo; Chuo cha Misitu Olmotonyi wanafunzi 108 na Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi wanafunzi 20. Katika kipindi hicho mitaala ya Misitu na ya Ufugaji Nyuki ilipitiwa ili kuendana na mfumo mpya wa *NACTE* wa kufanya mitaala iliyojikamilisha kila mwaka, ambapo mwanafunzi akimaliza mwaka mmoja na kufaulu anapata cheti (*Basic Certificate).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora unaendelea ambapo hadi sasa ujenzi wa jiko na bwalo la muda umekamilika. Katika mwaka 2010/11, Chuo kitaanza kutoa mafunzo kwa wanafunzi 20 watakaodahiliwa kwa mafunzo ya ufugaji nyuki ngazi ya Astashahada. Matarajio ya kudahili wanafunzi 35 wa fani ya ufugaji nyuki kama ilivyoainishwa katika mpango wetu wa utekelezaji wa 2009/10 hayakufikiwa kutokana na kutokukamilika kwa Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2009/10, Wizara ilianzisha Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Misitu. Kamati hii ilizinduliwa rasmi mwezi Mei 2010 na imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 kifungu cha 10. Kazi za Kamati kwa mujibu wa sheria hiyo ni kumshauri Waziri juu ya mambo yote yanayohusiana na ukodishwaji wa misitu, kutangazwa kwa hifadhi za misitu, usimamizi wa misitu ya hifadhi, mapitio ya Sera ya Misitu na mambo ambayo Waziri atahitaji ufafanuzi wake. Aidha, Kamati itaandaa taarifa ya mwaka ya utendaji wa kazi zake, na kuwasilisha kwa Waziri. Vilevile, taarifa ya utekelezaji wa kamati itajumuishwa katika taarifa ya mwaka ya utekelezaji ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeanzisha Mfuko wa Misitu Tanzania (*Tanzania Forest Funds*) kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002, kwa lengo la kuongeza uwezo wa Idara ya Misitu na Nyuki katika kukabiliana na changamoto za kusimamia rasilimali za misitu nchini. Mfuko umefungua akaunti na unatarajiwa kuzinduliwa na kuanza kufanya kazi Julai 2010. Vyanzo vya mapato ya mfuko vimeainishwa katika Sheria ya Misitu ya mwaka 2002, ambavyo ni; Ushuru wa asilimia mbili ya kila ada inayotozwa; Ushuru wa asilimia tatu ya mrahaba; Misaada, michango au kiasi chochote cha fedha kitakachochangiwa na watu binafsi, mashirika, mifuko, asasi/mashirika ya kimataifa au mifuko kutoka ndani na nje ya nchi; mapato yatokanayo na mauzo ya mazao ya misitu yaliyotaifishwa na mapato yatokanayo na miradi iliyofadhiliwa na kusimamiwa na mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika; katika mwaka 2009/10, Wizara imefanikiwa kukamilisha mchakato wa kuanzisha Wakala wa Misitu Tanzania (*Tanzania Forest Service*). Wizara ipo katika hatua za mwisho kutangaza uanzishwaji wa Wakala huu kwenye gazeti la Serikali. Lengo la kuanzisha Wakala ni kuendeleza na kusimamia rasilimali za Misitu na Nyuki kwa kushirikiana na wadau kwa kutoa huduma bora kiufanisi na kiufasaha zaidi ili kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi na kimazingira nchini na kimataifa. Wakala unategemewa kuanza kazi rasmi katika mwaka wa fedha 2010/11.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania iliendelea na utafiti na usambazaji wa teknolojia zinazohusu mimea ya miti kupitia vituo vya Kibaha, Dodoma, Lushoto, Moshi, Malya, Mufindi na Tabora. Katika mwaka 2009/2010, Taasisi ilitoa elimu ya uchomaji mkaa kwa kutumia teknolojia ya matanuru bora aina ya *Kasamansi* katika eneo la Maji Chumvi, kwenye vijiji vya Manyemba na Njovu wilayani Mvomero. Jumla ya wachomaji mkaa 20 walinufaika na elimu hiyo ambayo inatoa ufanisi mkubwa kati ya asilimia 25 - 30 ukilinganisha na uzalishaji kwa njia za jadi ambazo ufanisi wake ni chini ya asilimia 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa nishati ya kuni na mbao, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Taasisi ilifanya utafiti juu ya bioteknolojia ya miti aina ya mikaratusi chotara. Miti hiyo inayokua haraka inaendelezwa katika bustani ya Kwamwarukanga, wilayani Korogwe ambapo viunga nane vya uzalishaji wa miti hiyo vilianzishwa na miche 300,000 ilikuzwa. Pia, miche 48,000 ya mitiki na *Grevillea* ilioteshwa. Aidha, Kilimo Misitu kiliendelezwa katika Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza na Shinyanga. Vilevile, majaribio ya aina ya miti isiyo maarufu ingawa ina matumizi mengi (*lesser-known tree species)* pamoja na miti ya dawa yalianzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Taasisi kwa kushirikiana na taasisi za utafiti za Afrika Mashariki chini ya Jumuiya ya Kimataifa ya Kuhifadhi na Kuongeza Ubora wa Miti (*CAMCORE*) imeanzisha majaribio ya jamii 63 ya mikaratusi (*Urophylla*) na jamii 70 za mitiki kutoka nchi mbalimbali. Ustawishaji wa

miti hii utasaidia kuongeza miti ya kupandwa kwa ajili ya matumizi ya mbao na nishati na hatimaye kupunguza ukataji ovyo wa miti ya asili.

Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Taasisi ilianzisha utafiti kubaini ubora wa uhifadhi wa misitu kwa njia ya jadi. Katika utafiti huo, tathmini ya uhalisia wa mimea na bioanuwai katika misitu inayohifadhiwa kwa njia ya jadi ya Kabale na Ibasa na ule wa Hifadhi ya Taifa wa Sawago Wilayani Rungwe ilifanyika. Utafiti wa aina hiyo ulifanyika pia katika msitu unaohifadhiwa kwa njia ya Jadi wa Nyumba – Nitu, wilayani Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Wakala wa Mbegu za Miti nchini ni kuwezesha upatikanaji endelevu wa mazao ya misitu na utunzaji wa mazingira nchini kwa kuzalisha na kusambaza mbegu bora, miche ya miti pamoja na vipandikizi vingine. Katika mwaka 2009/2010, Wakala uliendelea kuzalisha na kuuza mbegu na miche bora ya miti. Hadi Mei, 2010 kiasi cha mbegu za miti kilichouzwa ndani na nje ya nchi ni kilo 11,369 zenye thamani ya Shilingi 285,201,000. Kati ya hizo, takriban Shilingi 148,782,255 zilipatikana kwa kuuza kilo 2,889 za mbegu katika nchi za Australia, Afrika ya Kusini, Msumbiji, Guatemala na Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wakala ulinunua kilo 212 za mbegu zenye thamani ya Dola za Kimarekani 55,403 kutoka Zimbabwe. Malengo ya Wakala hadi Juni 2010 yalikuwa ni kuuza kilo 11,500 zenye thamani ya Shilingi 180,000,000. Hadi kufikia Mei, 2010 kiasi cha mbegu kilichohifadhiwa katika maghala ya Wakala kilikuwa kilo 14,500 kwa ajili ya wateja wanaoagiza mbegu kwa dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, aina za mbegu za miti zilizouzwa imeongezeka kutoka 70 mwaka 2008/2009 na kufikia 96 mwaka 2009/2010. Kati ya hizo, miti ya kienyeji ni 38 ambayo ni sawa na asilimia 40 na miti ya kigeni ni 58 sawa na asilimia 60. Mbegu za Msindano, Mkangazi, Mwerezi na Mtiki, ziliendelea kuongoza katika kupendwa, zikifuatiwa na Mkenge, Mgunga na Mkongo. Kwa upande wa miche, hadi kufikia Mei, 2010, Wakala iliuza miche 39,171 yenye thamani ya Shilingi 28,765,093. Miche iliyouzwa zaidi ni mitiki, miembe, michungwa, mikangazi na mwalambe. Idadi ya miche iliyouzwa ilishuka ukilinganisha na mwaka 2008/2009 ambapo miche 192,462 iliuzwa kwa kuwa Wakala ilipata zabuni ya kuuza miche kwa ajili ya mashamba ya chai ya Mponde na Lupembe wilayani Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kusimamia utoaji huduma bora na uendelezaji utalii ili kuhakikisha sekta ya utalii nchini inachangia ipasavyo katika kukuza Pato la Taifa. Katika kutekeleza majukumu haya, Wizara inaongozwa na Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999 na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Utalii ya mwaka 2008 pamoja na Kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Sheria ya Utalii, Kanuni tano zilizoandaliwa ni za Mfuko wa Maendeleo ya Utalii, Wakala wa Utalii, Ada na Tozo, Waongoza Misafara ya Utalii na Huduma za Malazi na Vyakula. Aidha, Wajumbe 45 wa vyombo vya usimamizi wa Sheria ya Utalii (Bodi ya Utoaji Leseni za Wakala wa Utalii,

Mamlaka ya Rufaa na Kamati ya Ushauri) walielimishwa juu ya Sheria ya Utalii ya mwaka 2008 na vigezo vya kuweka hoteli katika daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zoezi la kuhakiki hoteli lilianzia kwenye eneo lenye hoteli nyingi na huduma nyinginezo za malazi katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Jumla ya hoteli 99 zilihakikiwa katika zoezi hilo kwa lengo la kuinua viwango vya ubora wa huduma. Katika idadi hiyo, jumla ya hoteli 66 zilizokidhi vigezo zilipangwa katika daraja na kukabidhiwa Vyeti na Nyota. Katika zoezi hilo Hoteli ambazo zilipatiwa daraja la chini kuliko matarajio yao, wahusika walishauriwa maeneo ya kuboresha ili zipande daraja.

Aidha, katika kuboresha huduma na kukuza utalii, Wizara iliendesha mafunzo ya mapishi, huduma ya vyakula na vinywaji, usafi wa nyumbani na huduma kwa mteja katika Wilaya za Dodoma na Mpwapwa. Mafunzo kama haya pamoja na yale ya mapokezi ya wageni na uongozaji watalii yalifanyika pia mkoani Iringa katika Wilaya za Iringa na Njombe. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya ujasiriamali na utalii kwa vikundi vinne Wilayani Pangani. Mafunzo hayo yalihusu uongozaji watalii, kutengeneza batiki na sanaa nyingine za mikono, huduma kwa mteja, usafi na mapishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utalii wa kitamaduni ni eneo mojawapo ambalo Wizara yangu imeweka mikakati ya kuliendeleza. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), ilifanya tathmini ya awali katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Iringa, Morogoro, Mbeya na Pwani kwa lengo la kuibua miradi ya utalii wa kitamaduni. Tathmini hiyo imebaini kuwa maeneo ya Kilwa (Lindi), Msimbati (Mtwara), Lituhi (Ruvuma), Madunda (Iringa) na Mlingotini (Pwani) yana fursa ya kuendelezwa kuwa miradi ya Utalii wa Kitamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuhimiza na kuvutia uwekezaji katika sekta ya utalii. Aidha, Wizara inaendelea na mazungumzo ya kuwezesha upatikanaji wa miundombinu muhimu kwa maendeleo ya utalii. Kwa sasa kuna uwekezaji mkubwa wa hoteli na huduma za malazi katika maeneo ya Temeke, Kinondoni na Ilala katika Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo ya Arusha, Mwanza, Iringa Mjini, Tungamalenga na Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Idara ya Utalii ililenga kukusanya Shilingi 1,990,870,000 kutokana na leseni mbalimbali za wakala wa utalii nchini. Hadi kufikia mwezi Mei 2010, jumla ya fedha zilizokusanywa ni Shilingi 1,914,147,532.10 sawa na asilimia 96.15 ya lengo. Katika mwaka 2010/2011, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi 2,793,200,000. Jukumu la Bodi ya Utalii Tanzania ni kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi, kwa kushirikisha sekta binafsi na wadau ili kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea vivutio vya utalii nchini.

Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Bodi ilishiriki katika maonesho 17 ya kimataifa ya utalii ambapo maonesho 14 yalifanyika katika masoko yetu ya asili na maonesho matatu katika masoko mapya. Katika masoko ya asili, maonesho yalifanyika katika nchi za Marekani, Uingereza, Uholanzi, Italia, Hispania, Ujerumani, Urusi, China, Ubelgiji, Japan, Afrika Kusini, Zimbabwe, Canada na Nchi za Scandinavia. Aidha, Bodi ilishiriki maonesho yaliyofanyika katika masoko mapya ya nchi za Uturuki, Jamhuri ya Czech na India. Ili kutangaza vivutio vya utalii nchini, Bodi ilitumia magazeti ya kimataifa katika nchi za Marekani, Uingereza, Afrika Kusini, Kanada na Afrika Kaskazini na Mashariki ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi iliratibu matembezi yaliyohusisha makundi kumi ya waandishi wa habari na wapiga picha kutoka katika nchi za Hispania, Canada, China na Uingereza. Lengo la matembezi hayo lilikuwa ni kuwawezesha kufahamu nchi yetu pamoja na vivutio vya utalii ili vitangazwe katika vyombo vya habari vya nchi zao.

Aidha, kwa kushirikiana na Shirika la Ndege la Uingereza, Bodi iliratibu ziara ya wapiga picha kutoka kampuni ya *Knucklehead* ya Uingereza kuja nchini kwa ajili ya kuandaa filamu ambayo huonyeshwa katika ndege za Shirika hilo. Bodi pia iliingia mkataba na kampuni ya *Newsgroup Inc*. ya Marekani ambayo iliandaa filamu inayoonyesha vivutio vya utalii nchini. Filamu hiyo ilionyeshwa katika stesheni mbalimbali za kimataifa za *Global Business and Financial News, National Geographic na Discovery Channel.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Utalii kwa kushirikiana na Sekta Binafsi nchini iliratibu safari za Mawakala 40 wa utalii kutoka Afrika Kusini. Lengo la ziara hii lilikuwa ni kuwawezesha mawakala hao kujifunza na kujionea vivutio vya utalii vya Tanzania ili waweze kuwashawishi watalii watakaokwenda kushuhudia fainali za Kombe la Dunia kuja kutembelea Tanzania wakati na baada ya mashindano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Bodi kwa kushirikiana na Shirika la Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ilidhamini mashindano ya urembo Tanzania (Miss Tanzania 2009) ambapo alipatikana balozi wa kutangaza utalii wa ndani (*Miss Domestic Tourism).* Kwa kupitia balozi huyo, Wizara imehamasisha utalii wa ndani katika shule za Msingi zipatazo 9 na Sekondari 12 Visiwani Zanzibar na katika Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii una jukumu la kutoa mafunzo yenye hadhi ya kimataifa katika fani ya hoteli na utalii ili kuongeza ubora wa utoaji huduma katika sekta ya utalii. Wakala unatoa mafunzo ya Astashahada na Stashahada katika fani ya utalii na ukarimu na unatumia mitaala iliyoidhinishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala uliongeza udahili wa wanachuo kutoka 148 mwaka 2008/2009 hadi 340 mwaka 2009/2010. Aidha, jumla ya washiriki 74 walihitimu kozi za muda mfupi katika fani za hoteli na utalii. Vilevile, kwa sasa Chuo kina wanafunzi 29 wa Stashahada ya Ukarimu, 48 wa Stashahada ya Utalii na 263 wa mafunzo ya Astashahada katika fani za ukarimu na utalii. Katika juhudi za kujijengea

uwezo, Wakala uliwezesha watumishi watatu kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu ya Shahada ya Uzamili na wawili katika ngazi ya Astashahada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ndogo ya Malikale imeendelea kutoa mchango wake katika kukuza utalii nchini kwa kulinda, kutafiti na kuhifadhi urithi wa malikale kupitia utalii wa kihistoria na tafiti za malikale.Kufuatia kukamilika kwa Sera ya Malikale, Wizara iliandaa rasimu ya marekebisho ya Sheria Na. 10 ya Mambo ya Kale ya mwaka 1964 na marekebisho yake Na.22 ya mwaka 1979. Aidha, Wizara imeanza kufanya tafsiri ya Sera ya Malikale katika lugha ya Kiingereza kutoka katika lugha ya Kiswahili na kuandaa mkakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010, Wizara iliandaa Mpango Mkakati wa uendelezaji wa eneo la Bonde la Oldupai na Mpango Kazi wa ufukuaji wa nyayo za Zamadamu katika eneo la Laetoli. Aidha, Wizara ninayo furaha kutoa taarifa kuwa nyayo nyingine za zamadamu zimevumbuliwa katika eneo la Sugaresero, karibu na Ziwa Natron. Mpaka sasa hivi nyayo 308 zimefukuliwa na wananchi wanahamasishwa kwenda kuziona. Nyayo hizo zina umri wa miaka takribani 120,000. Wizara ilianza ukarabati wa jengo la kihistoria la Caravan Serai na kuendelea na uimarishaji na ukarabati wa magofu ya Kaole na makaburi ya Bagamoyo. Pia, kazi ya kutayarisha michoro ya ujenzi wa vituo vya taarifa na kumbukumbu kwa vituo vya Kimondo cha Mbozi, Kalenga, Kilwa Kisiwani, Mapango ya Amboni na Engaruka ilianza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ilikamilisha ukarabati wa jengo la *Arab Tea House* na kuendelea kuratibu ukarabati wa jengo la kihistoria la Boma la Kijerumani lililopo mjini Bagamoyo. Vilevile, Wizara iliendelea na ukarabati wa ngome ya Kireno (Gereza), Msikiti wa Malindi na kuzuia mmomonyoko unaotokana na mawimbi ya bahari katika eneo la Kilwa Kisiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kushirikiana na wananchi na wadau katika uhifadhi wa Michoro ya Miambani Kolo – Kondoa na Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Wananchi wa Kondoa wameshiriki katika upandaji wa miti katika maeneo ya Pahi, Mnenia na Kolo ambapo jumla ya miche ya miti 2,754 imepandwa kama hatua ya kupunguza uharibifu wa michoro ya miambani kutokana na mahitaji ya kuni. Katika Kituo cha Kilwa, wananchi wamekuwa wakishiriki kufanya usafi na ukarabati wa magofu. Aidha, Wizara ilisaini mkataba wa makubaliano na Shirika lisilo la Kiserikali la *Trust for African Rock Art* (*TARA*) kwa ajili ya kuhifadhi michoro ya miambani Kolo. Makubaliano hayo yanatoa fursa kwa ushiriki wa wananchi katika kuhifadhi na kuendeleza maeneo ya malikale.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza ahadi ya kurejesha malikale zilizohifadhiwa katika Makumbusho ya Taifa la Kenya Nairobi, Wizara iliandaa eneo na vifaa vya kuhifadhia malikale hizo. Taratibu za kurejesha malikale hizo nchini zinaendelea na inatarajiwa kuwa ifikapo mwezi Desemba 2010, zitakuwa zimerejeshwa nchini. Nchi yetu imejaliwa historia ya pekee kwa kuwa na masalia ya Zamadamu. Katika mwaka 2009/2010, Wizara iliadhimisha kumbukumbu ya miaka 50 ya uvumbuzi

wa fuvu la Zinj katika Bonde la Oldupai Mkoani Arusha kuanzia tarehe 13 hadi 17 Agosti, 2009. Aidha, maadhimisho hayo yalihusisha kongamano la kimataifa la siku tatu na kufuatiwa na uzinduzi wa eneo lilipogunduliwa fuvu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Oktoba 2009, Wizara ilikuwa mwenyeji wa Kongamano la Tano la Kimataifa la Mtawanyiko wa Watu Wenye Asili ya Afrika Duniani (*Diaspora*). Kongamano hili lilifanyika Dar es Salaam na Zanzibar kuanzia tarehe 25 hadi 30 Oktoba na kujumuisha washiriki kutoka nchi 22 duniani wenye asili ya Afrika. Washiriki walipata fursa ya kubadilishana uzoefu katika masuala ya elimu, biashara ya utumwa na jinsi ya kuhifadhi na kuendeleza maeneo yaliyotumika katika biashara ya utumwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara ilishiriki katika mkutano mkuu wa Taasisi ya Kimataifa ya Mafunzo ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Rasilimali za Urithi wa Utamaduni (*ICCROM*) uliofanyika kuanzia tarehe 25 hadi 27 Novemba, 2009 huko Rome - Italia. Katika mkutano huo, Tanzania ilichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Uongozi wa Taasisi hiyo kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kutambua umuhimu wa kupanua wigo wa vivutio vya utalii na kukuza utalii, iliendeleza jitihada za kuhamasisha wananchi na wageni kutembelea maeneo ya vivutio vya utalii vya Malikale. Aidha, watalii wanaotembelea maeneo ya Malikale wamekuwa wakiongezeka mwaka hadi mwaka ambapo hadi kufikia Mei, 2010 idadi ya wageni waliotembelea maeneo ya malikale ilifikia 103,777 ikilinganishwa na mwaka 2008/2009 ambapo wageni 90,520 walitembelea vituo hivyo kwa kipindi cha kufikia Aprili, 2009. Katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Idara ya Mambo ya Kale iliweka lengo la kukusanya shilingi 264,801,000. Hadi mwezi Mei, 2010, Wizara ilikusanya shilingi 190,663,709.38 ikiwa ni asilimia 72 ya lengo. Katika mwaka 2010/2011, Wizara imeweka lengo la kukusanya shilingi 327,400,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania liliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuhifadhi, kutafiti na kuelimisha Umma kuhusu urithi wa Taifa letu. Ushauri wa kitaalam uliotolewa na Shirika kuhusu uhifadhi na uanzishaji wa makumbusho katika wilaya kadhaa hapa nchini umeanza kuonyesha mafanikio. Mwezi Novemba 2009, Shirika lilikabidhiwa rasmi makumbusho ya Maji Maji yaliyopo Mjini Songea, mkoani Ruvuma. Baada ya kukabidhiwa, Shirika lilianza kuyaboresha makumbusho hayo kwa kukarabati majengo, makaburi ya mashujaa wa Vita vya Maji Maji na ujenzi wa mnara wa kumbukumbu ya Mashujaa. Pia, Shirika liliboresha vionyeshwa vya historia ya mapambano ya kutetea Utu na Uhuru wa nchi yetu. Aidha, ushauri wa kitaalam uliendelea kutolewa kwa Makumbusho ya Bujora katika Wilaya ya Nyamagana, mkoani Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoahidi Bunge lako Tukufu mwaka jana mchakato wa kupata eneo la kujenga Makumbusho ya Kisasa Mkoani Dodoma

unaendelea. Aidha, mchakato wa kuanzisha Makumbusho ya Mwalimu Julius K. Nyerere kijijini Chamwino uko katika hatua ya kuandaa michoro ya majengo. Hatua zaidi zitaendelea katika mwaka 2010/2011. Ujenzi wa Nyumba ya Utamaduni uliendelea kutekelezwa kwa kukarabati majengo matatu na upo katika hatua za mwisho kukamilika. Ukarabati wa jengo la Makumbusho ya Azimio la Arusha ambao umeboresha mazingira ya jengo na mfumo wa umeme umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kijiji cha Makumbusho ulianzishwa mradi wa kufuga samaki na wanyama hai. Pia ukarabati wa nyumba za jamii za Wangoni, Waswahili, Wafipa, Wazaramo na Wachagga ulifanyika. Tamasha la watoto wenye mahitaji maalum ambalo lilihusisha wanafunzi kutoka shule za msingi zilizopo Dar es Salaam ilifanyika tarehe 4 hadi 6 Machi, 2010. Kumbukizi ya miaka 10 tangu kifo cha Baba wa Taifa Mwl. Julius K. Nyerere ilifanyika Kitaifa Butiama. Maonyesho maalum ya Kumbukizi hiyo yalifanyika katika Makumbusho ya Butiama na Makumbusho ya Azimio la Arusha. Kumbukizi hiyo, sanjari na maonyesho ya wiki ya vijana Kitaifa yaliyofanyika mwezi Oktoba 2009, vilihamasisha Umma kuhusu urithi wetu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya majadiliano yaliyochukua takriban miaka 20 kati ya Serikali ya Tanzania na Uswisi hatimaye sanamu ya Kimakonde iliyoibwa kutoka Makumbusho ya Taifa na baadaye kupatikana katika Makumbusho ya Barbier – Mueller, Geneva (Switzerland) ilirejeshwa nchini mwezi Mei, 2010. Sanamu hiyo imehifadhiwa katika Makumbusho ya Taifa, Dar es Salaam. Aidha, mchakato wa majadiliano kuhusu Tanzania inavyoweza kunufaika na masalia ya Mjusi yaliyopo katika Makumbusho ya Berlin, Ujerumani yameanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika kipindi cha mwaka 2009/2010 imeendelea kusimamia masuala ya watumishi katika maeneo ya ajira, upandishwaji cheo, utendaji kazi, nidhamu, mafunzo, maslahi, utawala bora, ustawi na afya kwa watumishi wote pamoja na kusimamia masuala ya jinsia. Katika mwaka 2009/2010, Wizara ilipewa kibali cha kuajiri watumishi 217 wa kada mbalimbali ambapo jumla ya watumishi 211 waliajiriwa. Aidha, nafasi sita hazijajazwa kutokana na waliofaulu kutokuripoti katika vituo vya kazi walivyopangiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuona umuhimu wa kuwaongezea watumishi uwezo wa kielimu na kuboresha utendaji kazi, kwa mwaka 2009/2010 Wizara iliwezesha watumishi 428 kuhudhuria mafunzo ambapo watumishi 77 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na 98 mafunzo ya muda mrefu. Aidha, katika kutekeleza Waraka wa Utumishi Na. 4. wa mwaka 2005, Wizara ilitoa mafunzo elekezi ya awali kwa watumishi wapya 211.Mwaka 2009/2010 watumishi 1,101 walipatiwa mafunzo ya utaratibu wa kupitia na kupima utendaji kazi wa watumishi wa umma (*Open Performance Review and Appraisal System* – OPRAS). Mafunzo yalilenga kuwawezesha watumishi kujaza fomu za mkataba wa utekelezaji wa majukumu yao kwa mwaka. Kwa kuzingatia utaratibu wa *OPRAS* na Miundo ya Utumishi wa Umma, katika kipindi cha 2009/2010, watumishi 179 wa kada mbalimbali walipandishwa cheo. Pia, watumishi 318 walithibitishwa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010, watumishi 70 walishiriki Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara (SHIMIWI) Mkoani Morogoro. Lengo

la kushiriki mashindano hayo lilikuwa ni kuboresha afya za watumishi na kujenga mahusiano mazuri na watumishi wengine wa umma. Vilevile, Wizara iliendelea kutoa huduma kwa watumishi walioathirika na Virusi vya UKIMWI na kuhamasisha watumishi kupima kwa hiari ili kujua afya zao. Hadi sasa, watumishi 35 waliojitokeza kuwa wanaishi na Virusi vya UKIMWI wanapatiwa msaada wa fedha kwa ajili ya kununulia dawa, virutubisho na lishe bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha utendaji kazi, mwaka 2009/2010, Wizara ilifanya vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi vilivyohudhuriwa na wajumbe 70. Katika vikao hivyo, hoja mbalimbali za watumishi zilijadiliwa na maazimio ya utekelezaji kufikiwa. Aidha, Wizara ilifanya mkutano wa Watendaji wake wakuu mkoani Morogoro ambao ulishirikisha jumla ya wajumbe 103 ambapo maazimio yaliyohitaji kufanyiwa kazi ili kukuza tija na utendaji kazi yalifikiwa. Vilevile, Wizara iliandaa Mpango Mkakati (2010-2013) na kufanya mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja ili kuendana na hali halisi pamoja na kukidhi mahitaji ya wateja. Katika kutoa huduma bora, Wizara iliendesha mafunzo ya Huduma kwa Mteja kwa viongozi na Maafisa waandamizi wa wizara na mafunzo haya yataendelea kutolewa kwa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kukabiliana na changamoto ya upungufu wa watumishi, hii ikihusisha pia katika ngazi ya Wilaya. Jitihada zinaendelea kuchukuliwa katika kujenga uwezo wa vyuo vya Wizara ili kuongeza uwezo wa kudahili wanafunzi wengi zaidi. Maslahi ya Watumishi yataendelea kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kuwakopesha kwa masharti nafuu vifaa kama samani, televisheni na vifaa vya usafiri kama vile pikipiki, baiskeli na kuimarisha huduma katika zahanati na kuboresha huduma za maji na umeme katika vituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuimarisha mtandao wa miundombinu hususan barabara, mipaka na viwanja vya ndege kwa kufyeka mipaka yenye urefu wa Kilometa 500 katika Mapori ya Akiba 24, kukarabati barabara zenye urefu wa kilometa 800 na kukarabati viwanja vya ndege 17 katika Mapori ya Akiba. Aidha, ili kuhakikisha kuwa uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori unaendelea kuimarika, mchakato wa uanzishwaji wa Pori la Akiba la Piti katika Wilaya ya Chunya utakamilishwa. Ili kuendelea kushirikisha wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori, Wizara itaanza mchakato wa kuanzisha Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (*WMA*) manne. Vilevile, itaendelea na mchakato wa utoaji wa haki ya matumizi ya rasilimali za wanyamapori (*user right*) kwa WMA mbili na kuanzisha Jumuiya za Kijamii (*CBO*) nne. Lengo ni kuhakikisha kuwa pamoja na wananchi hao kunufaika na shughuli za uhifadhi, wanakuwa na uwezo wa kujilinda dhidi ya wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na Serikali ya Msumbiji pamoja na wadau katika uhifadhi wa wanyamapori, Wizara pia itaendelea kutekeleza mradi wa kuhifadhi ushoroba wa wanyamapori unaounganisha Pori la Akiba Selous na Pori la Niassa la Msumbiji. Ushoroba huo wa Selous-Niassa unaunganisha hifadhi mbili ambazo zinatenganishwa na Mto Ruvuma na huwezesha uhamaji wa wanyamapori hususan tembo kutokana na mabadiliko ya kiikolojia. Katika kutekeleza mradi huo, *WMA* mbili za

Songea na Tunduru zitaimarishwa na mchakato wa kuanzisha *WMA* moja wilayani Tunduru na mbili wilayani Namtumbo utaendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi katika Mapori ya Akiba, nyumba mpya nne na vituo vya doria viwili vitajengwa. Aidha, nyumba mbili zilizoanza kujengwa zitakamilishwa pamoja na kukarabati nyingine 16. Vilevile, uboreshaji wa mtandao wa kusambaza maji katika vituo vya Matambwe katika Pori la Akiba Selous, Rungwa na kituo cha Kwamtoro katika Pori la Akiba Swagaswaga utafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau katika kuhifadhi maeneo ya Ardhioevu yaliyopewa hadhi ya kimataifa na kuwa *Ramsar Sites*. Mwaka 2010/2011, mpango endelevu wa usimamizi wa ardhioevu nchini utatekelezwa kwa kusaidia wilaya 10 katika uhamasishaji wa shughuli za kiuchumi zinazozingatia matumizi bora ya maeneo ya ardhioevu na kusaidia kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vitano vilivyopo katika *Lake Natron Ramsar Site*. Aidha, utekelezaji wa mradi wa *Kilombero Valley Ramsar Site* utaendelea kwa kushirikiana na Wilaya za Ulanga na Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori, Wizara katika kipindi cha mwaka 2010/2011 itaendesha siku za doria 60,000 ndani na nje ya mapori ya akiba na siku za doria 3,000 za msako kwa ajili ya kudhibiti wanyama wakali na waharibifu katika Wilaya 44 zenye matatizo. Vilevile, Wizara itanunua nyenzo za doria za kisasa pamoja na vitendea kazi. Aidha, ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za wanyamapori mipakani katika mwaka 2010/2011, Wizara itajenga kituo cha doria katika eneo la Mtambaswala, wilayani Nanyumbu karibu na Daraja la Umoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kujenga na kukarabati nyumba za watumishi na kujenga vituo vitatu vya doria katika eneo la KIA, Nangurukuru na West Kilimanjaro. Aidha, zoezi la kudhibiti kunguru weusi litaendelea katika maeneo ya Kibaha, Morogoro na Jiji la Dar es Salaam kwa kutumia mitego na sumu aina ya DRC 1339. Kwa mwaka 2010/2011, Chuo kitakamilisha mitaala ya Shahada ya Utalii wa Wanyamapori na Shahada ya Uhifadhi na Usimamizi wa Wanyamapori. Mafunzo ya Shahada hizi mbili yanatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2010 iwapo Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi litapitisha mitaala husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori itakamilisha mapitio ya Kanuni za Utafiti wa Wanyamapori na kuainisha maeneo ya kipaumbele ya utafiti wa wanyamapori nchini. Aidha, Taasisi itaendelea na uandaaji wa mkakati wa kuhifadhi tembo nchini pamoja na kuanza utekelezaji wa Mpango wa Kuwahifadhi Wanyamapori Wanyonyeshao.

Vilevile, itaendelea kufanya tafiti na kuendesha mafunzo mbalimbali ya ufugaji wa nyuki kwa njia za kisasa. Katika mwaka 2010/2011, Shirika litafanya mapitio ya Mipango ya Usimamizi ya Hifadhi za Taifa za Arusha na Ziwa Manyara na kuimarisha shughuli za ufuatiliaji wa mabadiliko ya mazingira ndani na nje ya hifadhi. Shirika

litaendelea pia kuimarisha uwezo wa Idara ya Hima Sheria kwa kuhakikisha kuwa vifaa na nyenzo muhimu zinapatikana, pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika litaendelea kupanua wigo wa shughuli za utalii, kuratibu shughuli za wawekezaji binafsi kwenye hifadhi na kuendeleza shughuli za utalii wa ndani. Aidha, utalii wa kiikolojia na kiutamaduni utaendelezwa kwa kushirikiana na jamii zinazozunguka hifadhi. Elimu ya uhifadhi itatolewa kwa kutumia njia mbalimbali kama vile majarida na kampeni kwa wanavijiji waishio karibu na hifadhi. Katika kuendeleza ujirani mwema, Shirika litachangia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika vijiji vinavyozunguka hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mamlaka itaendelea na matengenezo ya barabara ndani ya eneo la hifadhi pamoja na ununuzi wa mitambo ya kutengeneza barabara. Mamlaka itaendelea kutekeleza miradi ya ujirani mwema kwa kujenga mabweni katika Shule ya Sekondari ya Embarway na ujenzi wa bwalo, jiko na mtambo wa *biogas* katika Shule ya Msingi ya Olbalbal. Vilevile, ujenzi wa mabwawa ya maji (malambo) na majosho utafanyika pamoja na uendelezaji wa miundombinu katika eneo la Jema – Oldonyo Sambu ambapo baadhi ya wakazi wa Ngorongoro wamehamia kuendelea na shughuli za kilimo. Pamoja na hayo jitihada za kuimarisha utalii zitaendelea ambapo Mamlaka itaendelea na mchakato wa kujenga kituo cha Makumbusho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mpango kazi wa mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuhifadhi misitu na mazingira yake hususan yale ya hifadhi za bionuai na vyanzo vya maji, ikiwa ni pamoja na misitu ya hifadhi ya mikoko. Zoezi la kuondoa wavamizi katika misitu ya hifadhi iliyovamiwa itaendelea katika mikoa 10. Aidha, kazi ya kupitia mipaka yenye urefu wa kilomita 3,000 na kuboresha ramani za misitu 17 ya asili na mashamba ya miti ya kupandwa itatekelezwa pamoja na kuhudumia na kuongeza idadi ya Hifadhi za Mazingira Asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuhudumia mashamba yake 16 ambapo jumla ya miche 10,670,000 itaoteshwa, hekta 8,760.4 zitatayarishwa na kupandwa. Hekta 21,457.7 zitapaliliwa, hekta 8,527.1 zitapogolewa, hekta 1,740.19 zitapunguziwa miti na barabara za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 1,884 zitafyekwa. Vilevile, barabara zenye urefu wa kilomita 400 katika mashamba matano ya miti zitakarabatiwa. Ukarabati huu pia utahusisha nyumba 10 katika mashamba matano ya miti na nyumba nne katika vituo vinne vya nyuki. Aidha, zoezi la kuhamasisha upandaji miti wa kibiashara litaendelea kwa njia ya ushirikishwaji wa sekta binafsi na sekta ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kukiwezesha kikosi cha doria katika kanda nane kufanya ukaguzi wa mazao ya misitu kwenye maeneo ya uvunaji, usafirishaji na masoko ili kudhibiti wafanya biashara wa mazao ya misitu wasio waaminifu. Vilevile, vizuizi vipya 20 vya mazao ya misitu na nyuki vilivyoanzishwa nchini vitaendelea kuwezeshwa. Ili kuhakikisha kuwa uvunaji wa mazao ya misitu unafanywa kwa njia

endelevu, Wizara itaendelea kuwezesha kamati za uvunaji katika wilaya zenye mipango ya usimamizi wa misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuhamasisha wananchi juu ya matumizi endelevu ya rasilimali za misitu ikiwa ni pamoja na kutahadharisha kuhusu madhara yaletwayo na uchomaji moto misitu. Majarida 6,000 ya makala mbalimbali za misitu na nyuki yatachapishwa na vipindi 78 vya redio na programu 100 za televisheni vitarushwa hewani. Aidha, kanda saba za uenezi zitawezeshwa kutekeleza shughuli za uenezi na ugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kutunza makundi 2,800 ya nyuki kwa kuhudumia vituo vinne vya maonesho ya ufugaji nyuki katika Wilaya za Kondoa, Manyoni, Handeni na Kibondo. Katika kuhakiki ubora wa mazao ya nyuki, kazi ya kudhibiti mfumo wa mabaki ya kemikali katika asali itaendelea kwa kuongeza idadi ya sampuli zitakazofanyiwa uchunguzi kutoka 35 hadi 55 kutoka kwenye wilaya 30. Aidha, wadau 100 watapatiwa mafunzo juu ya njia bora za uvunaji, uchakataji na uhifadhi wa mazao ya nyuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010, Chuo cha Misitu Olmotonyi kinatarajia kudahili wanafunzi 60 katika taaluma ya Misitu, ambapo 30 ni wa Astashahada na 30 ni wa Stashahada. Aidha, wanafunzi 20 watadahiliwa kwenye taaluma ya Ufugaji Nyuki ngazi ya Astahashada katika Chuo cha Ufugaji Nyuki cha Tabora. Vilevile, Chuo cha Viwanda vya Misitu *FITI* – Moshi kinatarajia kudahili wanafunzi 20. Taasisi itaendelea kuzalisha vitalu vya miche kwa ajili ya utafiti, kufanya utafiti kuhusu mabadiliko yanayoweza kutokea katika udongo kutokana na aina ya miti inayopandwa, kufanya utafiti kuhusu jinsia na uhifadhi wa misitu katika maeneo kadhaa nchini, kufanya utafiti kuhusu uchangiaji wa dawa za asili katika kupunguza umasikini pamoja na uhifadhi wa misitu katika Wilaya ya Mvomero.

Katika mwaka 2010/2011, Taasisi ya Utafiti wa Misitu itaendelea kufanya utafiti juu ya upatikanaji na mwenendo wa masoko kwa mazao ya misitu nchini hasa katika Mikoa ya Iringa, Pwani, Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro na Morogoro. Ili kuimarisha rasilimaliwatu, Taasisi itaendelea kuwezesha mafunzo kwa watafiti na watumishi wa taasisi, kutoa machapisho na kuyasambaza, na kuendeleza tafiti kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi. Elimu ya uchomaji mkaa kwa teknolojia ya kisasa iitwayo Kasamansi itaendelea kusambazwa katika sehemu nyingine za nchi kwa kuanzia na Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha katika mwaka 2010/2011. Katika jitihada za kukuza sekta ya utalii ili ichangie ipasavyo katika kukuza uchumi, mwaka 2010/2011 Wizara itafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999, kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria ya Utalii ya mwaka 2008 na Kanuni zake pamoja na kuandaa mwongozo wa utalii ikolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuharakisha zoezi la upangaji hoteli katika daraja, Wizara itatoa elimu kwa wadau kuhusu uwekaji hoteli katika daraja kwa Mikoa ya Arusha na Manyara na kuwezesha mafunzo kwa wataalam watakaopanga hoteli katika

daraja. Katika kutekeleza Mkakati wa Utalii Endelevu – Punguzo la Umaskini, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Utalii Duniani itaendesha mafunzo katika nyanja za Sera, uendelezaji mazao ya utalii na utafutaji masoko. Mwaka 2010/2011, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii unatarajiwa kuwa na Kampasi tatu; moja ya Arusha na mbili za Dar es Salaam. Hatua hii itawezesha Wakala kuongeza udahili, hivyo kuongeza idadi ya wataalamu katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Utalii itaendelea kutangaza vivutio vya utalii na kuwavutia watalii nchini kwa kushiriki maonesho pamoja na misafara ya utangazaji utalii ndani na nje ya nchi. Vilevile, Bodi itaandaa machapisho, CD's, DVD's na majarida katika lugha za Kiswahili, Kiingereza, Kihispania, Kiholanzi, Kijerumani, Kiitaliano, Kirusi, Kichina na Kijapani ili kutangaza vivutio katika masoko hayo. Aidha, Bodi itaendelea kutangaza vivutio vya utalii nchini kupitia tovuti yake *www.tanzaniatouristboard.com* katika lugha mbalimbali za Kimataifa. Bodi itaendelea kuimarisha tovuti yake kwa kuiwezesha kusomeka katika lugha mbalimbali za Kimataifa kama vile Kijerumani, Kifaransa, Kihispaniola na Kiitaliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi inakusudia kupitia upya Mpango wa Masoko na Mpango Mkakati wake kwa lengo la kuufanya uende na wakati. Aidha, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Bodi itaanza mchakato wa kufungua ofisi ya utalii kwa Ukanda wa Utalii Kusini mjini Iringa kwa ajili ya kuongeza kasi ya utangazaji utalii kusini. Kwa mwaka 2010/2011, Wizara inakusudia kuendelea na mchakato wa kurekebisha Sheria ya Mambo ya Kale. Mikutano miwili ya wadau itafanyika kwa lengo la kupata maoni yatakayowezesha maandalizi ya Sheria hiyo. Vilevile, Wizara itakamilisha kazi ya kutafsiri Sera ya Malikale kwa Kiingereza na kuichapisha kwa ajili ya kuwasambazia wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na uhifadhi endelevu wa malikale, Wizara itaandaa orodha ya urithi wa utamaduni katika maeneo ya wapigania uhuru katika Mikoa ya Mbeya na Iringa. Vilevile, Wizara itawezesha upimaji wa viwanja katika eneo la hifadhi ya Mji mkongwe Bagamoyo na kuendelea na mchakato wa ufukuaji wa nyayo za zamadamu katika eneo la Laetoli. Ujenzi wa kituo cha taarifa katika Kituo cha Mapango ya Amboni pamoja na uzio katika Kituo cha Kumbukumbu ya Dr. Livingstone Ujiji utafanyika.

Aidha, ujenzi wa banda la mihadhara, langoni na mnara wa kumbukumbu ya uvumbuzi wa fuvu la Zinj utafanyika katika Kituo cha Oldupai. Wizara, kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu, itaendelea na ukarabati wa Boma la Kijerumani mjini Bagamoyo na kuanza ukarabati wa jengo la Tembe la Kwihara mkoani Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea na jitihada za kutoa elimu kwa jamii kuhusu malikale kwa njia ya vipindi vya redio, televisheni na vipeperushi kwa lengo la kuhamasisha utalii wa ndani. Kwa mwaka 2010/2011, Wizara itaandaa na kurusha

vipindi vya televisheni kuhusu malikale katika Mikoa ya Lindi, Tanga, Tabora, Pwani na Iringa.

Aidha, nakala 10,000 za vipeperushi kuhusu malikale zitachapishwa na kusambazwa. Katika mwaka 2010/2011, Shirika litaanza mchakato wa kupanua Makumbusho ya Azimio la Arusha ili yawe endelevu na kuonyesha historia pana ya mageuzi ya kisiasa na kiuchumi nchini. Shirika litaendelea na maandalizi ya kumbukizi ya miaka 50 ya Uhuru wa Taifa letu na kutoa elimu kwa Umma kupitia vyombo vya habari na kuandaa machapisho mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara inatarajia kuajiri jumla ya watumishi wapya 260 na kujaza nafasi zilizoachwa wazi pamoja na kupandisha cheo watumishi 295 wa kada mbalimbali. Vilevile, Wizara itaendelea kuhamasisha na kuwagharamia watumishi wake ili waweze kujiendeleza kitaaluma kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kulingana na mpango wa mafunzo ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa Mwaka 2010/2011, itaendelea kuwashirikisha watumishi wake kwenye michezo mbalimbali ya Kiwizara na Kitaifa ili kuendelea kuboresha afya zao na kuimarisha uhusiano mzuri kazini. Katika jitihada za kupambana na UKIMWI, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa watumishi kuhusu mbinu za kujikinga na maambukizi ya UKIMWI na kupima kwa hiari. Aidha, watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI wataendelea kuhudumiwa ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa watumishi katika kujadili masuala mbalimbali ya kuimarisha utendaji kazi utaendelezwa kwa kuwawezesha kushiriki vikao mbalimbali pamoja na Baraza la Wafanyakazi. Katika kuboresha utoaji huduma, Wizara itaanzisha mfumo wa kielektroniki wa kushughulikia malalamiko *(Complains Management System)* yatakayowasilishwa na wateja wake. Vilevile, itaendelea kuimarisha ofisi zake za masijala kwa kuimarisha mfumo wa kieletroniki wa kufuatilia majalada *(File Tracking System)* ili kuboresha mawasiliano ndani na nje ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kushiriki katika maonesho mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wiki ya Utumishi wa Umma, Sabasaba na Nanenane. Kupitia maonesho haya, Wizara itapata fursa ya kutangaza vema shughuli zake kwa jamii na kutoa elimu ya uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili, malikale na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwashukuru wale wote ambao wameshirikiana na Wizara yangu katika kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Shukrani za dhati ziwaendee washirika wetu wa maendeleo wafuatao, kwa michango yao ya kifedha na kitaalam; Serikali za Finland, Denmark, Ujerumani, Ufaransa, Marekani, Sweden, Ubelgiji, Japan na Norway. Taasisi na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *UNESCO, FAO, IUCN, UN -WTO, WMF, ILO,*

ICCROM, WWF, AWF, TARA, SES na Asasi zisizokuwa za Kiserikali pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee ningependa kumshukuru mume wangu Bwana Patrick Mwangunga pamoja na watoto wangu Monica, Mbonike, Mwangunga na mwanangu Mtwa Kabole Mwangunga kwa ushirikiano na upendo ambao wamenipa na hivyo kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu kwa kuzingatia mpango kazi wake wa mwaka 2010/2011, naomba Bunge lako tukufu liafiki kupitisha Shilingi 65,506,240,000 kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Taasisi zake. Kati ya fedha hizo, Shilingi 55,398,980,000 zitatumika kugharamia mishahara na matumizi mengineyo na Shilingi 10,107,260,000 zitagharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

WAZIRI WA USHIRIKIANOWA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, hoja hiyo imeungwa mkono, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ambayo ilipitia Wizara hii, Mheshimiwa Kimbita kwa niaba ya Mwenyekiti.

MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA –(K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira naomba kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii katika mwaka wa fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na Maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana na watendaji wakuu wa wizara hii wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri, katika Ofisi Ndogo ya Bunge Jijini Dar es Salaam na kupitia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2009/2010 pamoja na kupitia makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii inasimamia sekta ndogo za Wanyamapori, Misitu na Nyuki, Utalii na Mambo ya Kale ambapo mchango wa Sekta ya Utalii peke yake ni takriban asilimia 17.2 kwenye pato la Taifa. Aidha, katika majadiliano, Kamati ilifahamishwa kuwa Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Wizara ambayo ni kuwa na "Maliasili na Malikale Zilizohifadhiwa Vizuri, Kusimamiwa na Kutumika Kiendelevu na Kuwa na Utalii Unaowajibika" pamoja na Dhima ya Wizara ambayo ni "Kusimamia Uhifadhi na Matumizi ya Maliasili na Malikale na Kuendeleza Utalii kwa Manufaa ya Kizazi cha Sasa na Kijacho".

Mheshimiwa Naibu Spika, dhima hii itatekelezeka kwa kufanya yafuatayo:-

· Kuandaa na kudurusu sera, mikakati na miongozo ya usimamizi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii;

· Kuandaa, kudurusu na kusimamia sheria na kanuni zinazolenga kuleta uhifadhi na matumizi endelevu ya Maliasili na Malikale na maendeleo ya utalii; na

· Kufuatilia na kutathmini utekelezwaji wa Sera, Sheria, Programu na miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2010/2011 umetayarishwa kwa kuzingatia Dira ya Wizara ambayo imefafanuliwa katika Sera mbalimbali za kisekta ambazo ni Sera ya Wanyamapori ya Mwaka 2001, Sera ya Misitu ya Mwaka 1998, Sera ya Ufugaji Nyuki ya Mwaka 1998, Sera ya Utalii ya Mwaka 1999, Sera ya Malikale ya Mwaka 2008. Mpango huu pia umezingatia Malengo Makuu Matatu kama yalivyoainishwa katika MKUKUTA ambayo ni:-

· Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato;

· Kuboresha hali ya maisha na maendeleo ya jamii; na

· Utawala bora na uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 Kamati yangu ilitoa maoni, ushauri na maagizo kwenye maeneo mbalimbali hasa yanayohusu Utalii, Wanyamapori, Misitu na Nyuki, Mali Kale, na Utafiti katika sekta ya Maliasili na utalii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara kwa kiasi kikubwa imefanyia kazi maeneo husika na hatua za utekelezaji kufanyika. Hata hivyo, yapo maeneo mengine ambayo Kamati iliona juhudi zaidi zinahitajika na ikatoa ushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini yake ziliidhinishiwa na Bunge, Bajeti ya Shilingi 70,803,337,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 44,791,000,000 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Idara, Vitengo, Taasisi, Vyuo na Wakala wa Wizara na Shilingi 26,012,337,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2010, Wizara ilikuwa imepewa jumla ya Shilingi 34,930,918,109 sawa na 49.34 % tu ya bajeti iliyoidhinishiwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi 30,988,167,027 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 3,942,751,082 zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, Wizara ilikusudia kukusanya Shilingi 47,570,100,000 ikiwa ni Makusanyo ya Maduhuli ya Idara na Mifuko ya Wizara. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2010, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi 39,886,513,929 sawa na asilimia 83.8 ya makisio. Aidha, Wizara ilikadiria kufikia lengo kwa kukusanya jumla ya Shilingi 47,810,087,099 ifikapo Mwezi Juni, 2010 sawa na asilimia 100.5 ya makisio ya makusanyo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Mafanikio. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2010, Wizara ilifanikiwa kutekeleza malengo mengi iliyojiwekea. Naomba niyataje baadhi ya yale ambayo walifanikiwa kutekeleza ikiwa ni pamoja na:-

(i) Wizara kufanikisha kujenga uwezo wa watumishi na watendaji wa idara mbalimbali kwa kuwapatia mafunzo katika fani zinazohitajika na pia kuwapatia vitendea kazi.

(ii) Jumla ya Wilaya 37 zenye vitalu vya uwindaji wa kitalii na Wilaya 10 zenye Jumuiya za Uhifadhi Wanyamapori (*WMAs*) zilipewa asilimia 25 ya mapato yatokanayo na uwindaji.

(iii) Jumla ya Kilomita 110 za barabara zilikarabatiwa katika Pori la Akiba Selous na pia Km 101.5 za mipaka zilifyekwa katika mapori ya Akiba ya Ikorongo/Gurumet (51.5 Km) na Likwika (50 Km).

(iv) Tafiti mbalimbali zilifanyika ikiwa ni pamoja na Hesabu ya Tembo Katavi - Rukwa, Ruaha - Rungwa, Selous – Mikumi, Tarangire – Manyara na jumla ya tembo 110,000 walihesabiwa. Sensa ya wanyamapori imefanyika katika ardhioevu za Bonde la Mto Kilombero ili kuweka takwimu za wanyamapori na mtawanyiko wake.

(v) Wizara imefikia hatua za mwisho katika mchakato wa mapitio ya Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998 ambao ulianza mwaka 2006. Rasimu ya mwisho imewasilishwa kwenye Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Misitu ili kuiboresha kabla ya kuwasilishwa kwenye ngazi ya Makatibu Wakuu.

(vi) Ushirikishaji jamii katika kusimamia rasilimali za misitu unaendelea ambapo jumla ya wilaya 63 zimewezeshwa kutekeleza Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu. Utekelezaji wake unahusisha vijiji 2,328 vyenye jumla ya hekta 4,122,500.

(vii) Sampuli 46 za asali zilikusanywa katika wilaya 19 za Manyoni, Kongwa, Sikonge, Uyui, Urambo, Kahama, Bukombe, Mufindi, Njombe, Makete, Chunya, Ileje,

Mpanda, Nkasi, Simanjiro, Kiteto, Mwanga na Same na kufanyiwa uchambuzi katika maabara teule iliyoko nchini Ujerumani. Matokeo ya sampuli yameonyesha kutokuwa na viwatilifu katika asali.

(viii) Sheria mpya ya Utalii ilianza kutumika Mwezi Julai, 2009 baada ya kukamilishwa kwa baadhi ya Kanuni zake.

(ix) Wigo wa Mazao ya Utalii uliendelea kupanuliwa kwa kuainisha aina nyingine za utalii kama vile utalii wa mikutano, fukwe za bahari, ikolojia na malikale.

(x) Wizara ilifanikiwa kutafsiri Sera ya Malikale katika lugha ya Kiingereza kutoka katika lugha ya Kiswahili na Rasimu ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Malikale imeandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio ambayo Wizara iliyapata, changamoto zifuatazo zilijitokeza katika kutekeleza Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010:-

(i) Ufinyu wa fedha zinazotengwa katika Bajeti ya Serikali, hivyo kutokidhi utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa na dharura za uhifadhi.

(ii) Wizara kutokuwa na watumishi wa kutosha kushughulikia utekelezaji wa programu zake katika baadhi ya idara.

(iii) Matumizi yasiyokuwa endelevu na uvunaji haramu wa rasilimali za maliasili na malikale.

(iv) Ushiriki usioridhisha wa baadhi ya wadau katika matumizi na kuhifadhi maliasili na malikale.

(v) Kuwepo kwa mwamko mdogo wa Watanzania wazawa kutembelea vivutio vya utalii, hivyo kupata mapato madogo yatokanayo na Utalii wa Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa fedha 2010/2011. Kamati inaendelea kusisitiza Wizara kujenga uwezo wa Idara na Taasisi zake pamoja na watumishi wake. Aidha, Serikali iendelee kuwawezesha watumishi wake kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani mbalimbali ili kuboresha utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapongeza juhudi ambazo Wizara imekuwa ikizifanya kwa kuanza kuutangaza Utalii wa Ndani katika maonyesho mbalimbali pamoja na kuwapeleka waandishi wa habari kwenye vivutio vyetu vya utalii. Tunaishauri Wizara kuandaa mkakati maalum wa kuhamasisha Utalii wa Ndani kwenye mashule, vyuo pamoja na taasisi za serikali na zisizo za serikali ili idadi ya Watanzania wanaotembelea vivutio vyetu vya utalii iwe kubwa zaidi. Aidha, tunaishauri Wizara pamoja na Taasisi na Mashirika yaliyo chini yake kubuni njia za kuweza kuwasafirisha watalii hawa kwa bei

nafuu kwenda kwenye vivutio hivi, kwani pamoja na kuwa viingilio katika vivutio hivi ni nafuu, gharama za usafiri bado ziko juu kwa wananchi walio wengi kuzimudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada ambazo Wizara inazifanya kuilinda misitu yetu dhidi ya matumizi mabaya ikiwemo uchomaji moto na ukataji miti hovyo kwa matumizi mbalimbali, bado kumekuwepo na uhujumu mkubwa wa maliasili hii. Wizara ina uhaba mkubwa wa vitendea kazi pamoja na rasilimaliwatu ukulinganisha na ukubwa wa misitu tuliyo nayo. Kamati inashauri Wizara kufanya tathmini kujua kwa usahihi aina, ukubwa na maeneo mahususi ambayo yanakabiliwa na hujuma hii ili kuweza kubuni njia za kukabiliana na tatizo hili pamoja na kugawanya rasilimali walizonazo kwa uwiano ulio sahihi ili kupunguza na kisha kutokomeza tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza kuwa kuna umuhimu mkubwa wa Wizara kuziwezesha taasisi za utafiti inazozisimamia ili kuwezesha taasisi hizi kufanya kazi kwa ufanisi. Aidha, taasisi zenyewe zinapaswa kubuni njia mbalimbali zitakazoweza kuwasaidia kupata mapato kwa ajili ya kufanya tafiti. Kamati inashauri kuwa suala hili liende sambamba na utungwaji wa Kanuni mbalimbali zitakazowezesha taasisi hizi kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi ambazo Wizara imezifanya, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali iharakishe utafutwaji wa maeneo mbadala ili kuhamishia watu waliohamia ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya mkaa mijini ni suala linalochangia kwa kiasi kikubwa katika kutokomeza misitu yetu. Matumizi ya nishati mbadala ni jambo ambalo litasaidia sana kupunguza matumizi ya mkaa. Kwa kuwa suala la nishati mbadala ni suala mtambuka, kamati inashauri Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira na asasi zisizo za kiserikali kubuni mpango wa uhamasishaji wa matumizi ya nishati mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Wizara kwa kukifungua Chuo cha Nyuki Tabora. Tuanaishauri Wizara ijitahidi kuandaa mkakati wa kudahili wanafunzi wengi zaidi ili kupata wataalam wazalendo katika sekta hii muhimu kwa pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Idara ya Mambo ya Kale iko katika hatua za mwisho za ukarabati wa Makumbusho na Jumba la Utamaduni Dar es Salaam. Pamoja na juhudi ambazo Wizara imefanya kujitangaza kwenye mitandao ya kijamii yaani blogs, Kamati inaishauri Wizara kuandaa programu endelevu ya kuwafikia wananchi wengi zaidi ili waweze kuhamasishwa kutembelea Makumbusho haya ili kujifunza historia yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza uharakishwaji wa kuanzishwa kwa Mamlaka ya Wanyamapori ili kufanikisha kikamilifu zoezi zima la usimamizi wa mapori ya Akiba na Tengefu nchini. Aidha, Kanuni za uendeshwaji wa Mamlaka hii ziandaliwe mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Utali Tanzania (*TTB*) ni chombo muhimu sana katika sekta ya utalii nchini. Kwa kuwa jukumu kuu la Bodi ya Utalii, pamoja na mengineyo, ni kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini ili kuvutia watalii wa ndani na nje, Kamati inashauri Bodi kuimarisha mfuko wao kwa kubuni mbinu mpya za kuongeza vyanzo vya mapato yao kwani mapato wanayoyapata kutoka katika vyanzo vilivyopo hayatoshelezi kukidhi malengo ambayo wamejiwekea. Aidha, uwepo ubunifu mkubwa zaidi kutangaza vivutio vyetu vya utalii. Bodi izingatie ukuaji wa teknolojia hasa teknohama kwa kuanzisha vitu kama mitandao ya kijamii (*social networks*) na *blogs* ambazo zitaweka mada mbalimbali kuzungumzia vivutio vinavyopatikana Tanzania na mada nyingine zinazoathiri utalii wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na uchumi, kuangalia na kufanya marekebisho ya kodi mbalimbali zinazotozwa kwenye mazao ya mbao zinazovunwa kwenye mashamba ya miti ya Serikali ili kusaidia wananchi kuweza kumudu gharama za mbao na kujenga nyumba bora ili kusaidia kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2010/2011 chini ya Mpango wa Muda wa Kati wa Bajeti (*MTEF*) yamezingatia maelekezo yanayolenga katika kutekeleza Sera na Mikakati mbalimbali ya Serikali na maeneo ya kipaumbele yanayolenga katika kutekeleza sera na mikakati ya utekelezaji wa MKUKUTA na miongozo mingine ya utayarishaji wa bajeti Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi wa kina, Kamati inakubaliana na Makadirio ya Bajeti ya Wizara, Fungu 69, jumla ya Shilingi 68,071,891,000 kati ya fedha hizo Shilingi 55,398,980,000 ni Fedha za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 12,672,911,000 ni Fedha za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha fedha zinazoombwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kipekee napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii kwa kunichagua kuwa mwenyekiti wao kwa kipindi chote tulichofanya nao kazi. Napenda kuwashukuru sana kwa michango yao, busara zao, uvumilivu wao na ushauri wao kwa Wizara na taasisi zake ambao mara zote umekuwa ukilenga kutetea maslahi ya Taifa katika sekta ya maliasili na utalii na pia kuichambua bajeti hii kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwatambua wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao ndio walioichambua bajeti hii ambao ni:-

Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti; Mheshimiwa Hassan R. Khatib, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Archt. Fuya G. Kimbita, Mjumbe; Mheshimiwa James Daudi Lembeli,Mjumbe; Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mjumbe; Mheshimiwa

Zakia Hamdani Meghji, Mjumbe; Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. Charles O. Mlingwa, Mjumbe; Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mjumbe; Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi,Mjumbe; Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mjumbe; Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mjumbe; Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mjumbe; Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mjumbe; Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Said Salim,Mjumbe; Mheshimiwa Ali Khamis Seif,Mjumbe; Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii,Mjumbe; Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti,Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda,Mjumbe; Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud,Mjumbe; Mheshimiwa Anastazia J. Wambura , Mjumbe; Mheshimiwa Aziza S.Ally , Mjumbe; Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mjumbe na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, napenda kumshukuru Mhe. Shamsa S. Mwangunga, Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu wake Mheshimiwa Ezekiel Maige, Katibu Mkuu wa Wizara Dr. Ladislaus Komba, Wakurugenzi wa Idara na Watumishi wote wa Wizara hii na Taasisi ama Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashililah na Makatibu wake wasaidizi wa Kamati hii Ndugu Grace Bidya na Ndugu Yona Kirumbi kwa kazi nzuri walioifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa kipekee naomba niwashukuru wananchi wenzangu wa Wilaya ya Hai wanaoishi ndani na nje ya Wilaya ya Hai kwa ushirikiano ambao wamenipa katika kipindi chote cha miaka mitano nazidi kuwaahidi kwamba tutaendelea kushirikiana hatimaye kuleta maendeleo endelevu katika Wilaya ya Hai na kwa ahadi yao hawatababaishwa na ngonjera za wapita njia. Naomba pia nimshukuru mke wangu Monica, watoto wetu Nancy, Godwin na Gideon kwa ushirikiano walionipatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba kuwasilisha na naunga hoja mkono. (*Makofi*)

MHE: MAGDALENA H. SAKAYA – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu na hekima tele kwa kunilinda, kunipagania na kuniwezesha kutimiza wajibu wangu wa uwakilishi ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi chote cha miaka mitano. Sifa na utukufu namrudushia yeye mweza wa vyote.

Mheshimiwa Spika, kadhalika nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani

kuhusu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kwa mujibu wa kanuni za Bunge kifungu cha 99(7) toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, Nichukue nafasi hii kukupongeza wewe, Naibu Spika na Makatibu wa Bunge kwa kutuongoza vyema hapa Bungeni kwa ufanisi mkubwa. Hakika Bunge limekuwa la viwango, lenye kutia hamasa na kuvuta hisia za Watanzania wote. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuishukuru familia yangu, kwa namna ya pekee namshukuru Mume wangu mpenzi Undule Twisa Mwampeta na mwanangu Nazarety Mwampeta kwa moyo wao wa uvumilivu kwa kipindi chote ambacho nimekuwa mbali nao nikiwa natimiza majukumu ya Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Mwenyekiti wa *CUF* Taifa, Profesa Ibrahim Haruna Lipumba mchumi wa dunia kwa kuteuliwa kuwa Mgombea pekee wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nampongeza Katibu Mkuu wa *CUF*-Taifa, Maalim Seif Sharif Hamad, kwanza kwa kuleta maridhiano yeye na Dr. Aman Abeid Karume ya watu kuishi kindugu kuelekea Uchaguzi Mkuu ujao, pia kuteuliwa kwake kuwa mgombea pekee wa nafasi ya Urais Zanzibar. (*Makofi*)

Aidha napenda kuchukua nafasi hii kukishukuru Chama changu cha Wananchi (*CUF),* Chama Kikuu cha Upinzani nchini Tanzania kwa kunipatia fursa ya kuwa mwakilisha kwa muda wa miaka hii mitano. Pia niwashukuru wananchi wa Mkoa wa Tabora hususani wale wa Wilaya ya Urambo kwa kuendelea kuniunga mkono katika kutetea maslahi yao na ya Watanzania wote kwa ujumla. Ushirikiano wanaonipa umenisaidia kutekeleza majukumu yangu ya kila siku na kwa ufanisi mkubwa. Nawaahidi kwa uwezo anaonipa Mwenyezi Mungu nitaendelea kuwatumikia kwa uaminifu tena kwa juhudi zangu zote na kwamba sitowaangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani kwa kutuongoza, kutuelekeza na kutusimamia vyema katika shughuli zetu za kila siku. Pia nawashukuru Waheshimiwa wabunge wote kwa mashirikiano mazuri baina yetu, naomba Mwenyezi Mungu abariki nia zenu na kuwasimamia katika uchaguzi ujao.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru waandishi wa habari kwa kuibua hoja na hisia na kufikishia Watanzania habari mbalimbali zinazojadiliwa hapa Bungeni. Nawaomba waendelee na moyo huo wa kuwasaidia watanzania, Mwenyezi Mungu atawalipa.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara kwa kuandaa bajeti hii, japokuwa baadhi ya watendaji katika wizara na idara zake wanachangia kwa kiasi kikubwa Taifa kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, maduhuli yaliyobakizwa ya kiasi cha shs.19,619,837,995 hayakuonyeshwa matumizi wala kiasi husika kujumuishwa katika bajeti ya wizara,

maduhuli yasiyokusanywa ya USD46,000 kutoka kwa wakala wa Utalii. Pia mishahara isiyolipwa ya shs.414,561,666 ya wastaafu waliofariki na waliofukuzwa haikurejeshwa hazina. Shamba la Sao hill halikutengewa bajeti ili kuhalalisha matumizi ya shs.5,127,118,191, aidha, shs.1,388,076,273 zilihamishwa na uongozi wa Sao Hill hazikuthibitishwa matumizi yake. Manunuzi ya *Computer* zenye thamani ya shs. 287,830,836 hazikupokelewa toka kwa mnunuzi.

Mheshimiwa Spika, hizi ni fedha nyingi sana, Kambi ya Upinzani, inasema huu ni uzembe wa kiutendaji tu unaotokana na kutokuja au waliokabidhiwa madaraka kuona kuwa wako juu ya sheria. Hivyo tunaitaka Serikali ilieleze Bunge ni hatua gani zimekwishachukuliwa kwa watendaji hao na je, kitengo cha ukaguzi wa ndani kinafanya kazi gani hadi Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndio agundue mapungufu haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhifadhi wa Wanyapori. Suala zima la uhifadhi hapa nchini kwa wananchi wengi hawalielewi, wapo wanaoona ni suala lisilowahusu na kwamba maeneno yaliyotengwa kisheria hayastahili kuwepo. Kutokana na kukosekana uelewa wa kutosha kumekuwepo migogoro mingi sana kati ya wananchi waishio jirani na hifadhi. Migogoro ya ardhi kati ya hifadhi na wananchi ipo karibu hifadhi zote hapa nchini. Hii ni hatari sana kwa uhai wa wanyama waliopo pamoja na usalama wa watumishi wa hifadhi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia mauaji ya kinyama yakifanywa na wananchi dhidi ya askari wa wanayamapori kwenye hifadhi zetu, tukio mojawapo ni lile lililotokea kwenye hifadhi ya Kitulo. Wananchi wenye hasira kali wamemshambulia askari aliyekuwa doria na kumuua kwa mapanga. Jambo la kusikitisha Serikali kuanzia ngazi ya Wilaya imeyanyamazia matukio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge ni hatua gani zilizochukuliwa dhidi ya matukio haya ya mauaji ya askari wa wanyamapori yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha baadhi ya wanasiasa wamekuwa wanaungana na wananchi kupinga uhifadhi. Kila tunapoelekea kwenye uchaguzi wananchi wamejenga kasumba ya kuvamia maeneo ya hifadhi kwa shughuli mbalimbali kama kulima, kukata miti, kuwinda wanyama na kadhalika. Hatua zinapochukuliwa dhidi yao wanasiasa wanakuja juu na kuwalinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Sadan inakabiliwa na tatizo kubwa la uharibifu mkubwa linalosababishwa na uchimbaji wa chumvi pembezoni mwa hifadhi hiyo. Kwenye ramani ya awali ya hifadhi ya Sadan Mto Wami ulikuwa ni sehemu ya hifadhi hiyo, Mto huu ni muhimu sana kwa uhai wa hifadhi hii pia kwa uhifadhi wa mikoko, mazalia ya samaki na viumbe wengine. Kwa sababu ya siasa mto huu umeondolewa kwenye hifadhi na sasa uharibifu mkubwa sana unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kuwa sekta ndogo ya wanyamapori imeonyesha kukua vizuri kwa kipindi chote cha kuanzia mwaka 2006 hasa kwenye uwindaji wa kitalii na utalii wa picha. Mwaka 2006, sekta hii ilikusanya jumla ya shs. 23,575.7 milioni ikilinganishwa na shs.18,387.4 milioni zilizokusanywa mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ilikwishatoa mapendekezo yake kuhusiana na jinsi gani sekta hii inavyoweza kuchangia fedha zaidi katika pato la Taifa, kwani kiasi hiki kilichopatikana ni kidogo mno kwa kulingana na kipato halisi wanachopata wanafanya biashara katika sekta hii ya wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhifadhi wa Tembo Tanzania. Tanzania bado tuko nyuma sana katika suala zima la uhifadhi. Ujangili umeendelea kwa kasi kubwa sana katika kona zote, mikoa yenye rasilimali ya wanyamapori (Arusha, Morogoro, Iringa, Mara) Serikali haijaweka mkakati wowote wa makusudi kuhakikisha kunakuwepo na nguvu ya kutosha kulinda wanyama hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujangili wa Tembo unaendelea kwa kasi kubwa na hivyo kutishia uhai wa wanyama hawa. Kila leo meno ya tembo yanakamatwa maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu zilizopo idadi ya tembo tuliyonayo sasa hivi ni 110,000, lakini mwaka 1970 Tanzania ilikuwa na tembo wanaokadiriwa kufikia 300,000 kutokana na ujangili kuzidi idadi hiyo ilipungua na kufika takriban 55,000 mwaka 1989. Kutokana na hali hiyo ililazimika Tembo kuwekwa kwenye kundi la wanyama walio katika hatari ya kutoweka (*Appendix* I).

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati bado tembo wanawindwa kwa kasi kubwa, uhifadhi bado ni hafifu na hatujaweza kufikia hata nusu ya tembo tuliokuwa nao miaka ya nyuma, Serikali inakuja na mpango wa kutaka kuwaondoa Tembo kwenye *APPENDIX* I na kuwapeleka kwenye (*APPENDIX* II) yaani viumbe ambao hawatishiwi na tatizo la kuwa hatarini kutoweka iwapo biashara yake haitadhibitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Serikali haikuwaeleza ukweli Waheshimiwa Wabunge jambo halisi walilotaka kulifanya kwenye Mkutano wa DOHA, nchini QATAR. Suala lilikuwa sio kuruhusiwa kuuza tu vipusa vilivyoko kwenye maghala yake, bali pia kuomba kibali cha kuhalalisha biashara ya meno ya tembo na bidhaa zake zote. Kambi ya Upinzani inasema huku ni kuwadanganya Watanzania kwa manufaa ya wachache wanaofanya biashara ya nyara za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli uliowazi kuwa Tanzania ilikwishapiga marufuku biashara yeyote inayohusu pembe za ndovu ama vipusa. Kama ikitokea ndovu au tembo wamekuwa wengi kiasi cha kuhatarisha maisha ya binadamu, utaratibu wa kuvuna upo na unaeleweka na sio rahisi kuvuna zaidi ya tani moja ya vipusa. Lakini kwa mshangao ni kuwa wenzetu nje wamekuwa wakikamata shehena kubwa ya vipusa toka Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zilizokusanywa na shirika liitwalo *Elephant Trade Information System* inaonyesha kuwa Tanzania imekubuhu katika biashara haramu ya vipusa, kwani mwaka 2007 kati ya tani 27 zilizokamatwa toka pande zote za Dunia, tani 11 zilisafirishwa kutoka Tanzania, na mwaka 2009 kati ya tani 24 zilizokamatwa, tani 12 zilitoka Tanzania. Matukio yote haya yanaonyesha kuwa biashara hii inamtandao mkubwa na kitovu cha mtandao huo ni Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwindaji haramu wa tembo katika mbuga zetu hasa katika hifadhi ya Selous ambayo ni kubwa kuliko hifadhi zote Tanzania ikiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 54,600 na ni kivutio kikubwa sana kwa watalii kwa kuwa na tembo wa kijivu, nyoka adhimu wasiopatikana sehemu nyingine duniani na mambo mengi mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa muda mrefu uliofanywa na Shirika la Marekani liitwalo *"Environmental Investigation Agency"* kwa kushirikiana na waandishi wa habari za mazingira Tanzania *JET* uligundua kuwa, ujangili na biashara ya vipusa unafanywa na mtandao ambao umeota mizizi kati ya wafanyabiashara wa ndani na nje pamoja na viongozi wakubwa Serikalini kwa kushirikiana na watendaji katika idara ya wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti unaonyesha kuwa kwa mwezi tembo 50 wanauawa, hivyo basi hii inafanya asilimia ya kuuawa kwa tembo kuongezeka kutoka asilimia 18 mwaka 2004 hadi asilimia 60 mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo inaeleza wazi kuwa watendaji wakuu katika idara ya wanyamapori wananufaika na biashara hii ya ujangili. Kuna matukio kadhaa yanayohusiana na ujangili ambayo yamekwishafikishwa katika vyombo vya dola yanayowahusu watendaji katika idara hii ya wanyamapori, lakini mara zote hizo haijawahi kutokea kuwa wahusika wamesimamishwa kazi wakati uchunguzi unaendelea. Je, kwa njia hii haki inaweza kutendeka? Kwa ubadhirifu wa njia hii ni kweli nchi yetu inaweza kunufaika na maliasili zetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atueleze ni kesi ngapi zinazowahusu viongozi waandamizi na watendaji wa idara zimefikishwa polisi na wahusika kuchukuliwa hatua?

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya *Selous* tangu 1982 ilitangaziwa na Shirika la Uhifadhi duniani *UNESCO* rasmi kuwa urithi wa Dunia *(World Heritage Sites)* kwa lengo la kuhifadhi utajiri uliyopo kwa faida ya Taifa na pia kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *UNESCO* imepiga marufuku kufanyika kwa shughuli yoyote inayoweza kuathiri mazingira au viumbe hai vilivyoko katika maeneo ambayo yametangazwa kuwa ya kihistoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana Serikali ya Awamu hii ya Nne imetoa kibali na kuruhusu uchimbaji wa madini ya *Uranium* kwenye pori tengefu la *Selous*. Kibali hicho kimetolewa kwa Kampuni ya *Manta Resources* ya Australia. Kampuni hiyo imepewa eneo la kilomita za mraba 3,325 za hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tumepitisha hapa Bungeni Sheria ya Wanyamapori. Wakati wa kujadili Sheria hii kuanzia ngazi ya Kamati tulikataa kata kata kipengele cha uchimbaji wa madini ndani ya hifadhi zote hapa nchini. Serikali ilipenyeza tena kipengele hicho kwenye *miscellaneous amendment,* Bunge likakataa na Waziri akakiondosha kifungu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze Bunge hili ni Sheria gani wameitumia kuruhusu uchimbaji wa madini ndani ya hifadhi ya Selous? Sambamba na hilo Serikali ieleze kwa nini imekiuka mkataba tulioingia na Shirika la *UNESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka Bunge lipewe maelezo ya kina na tunataka wahusika wote wawajibishwe kwa mujibu wa sheria, hatuwezi kuendesha nchi kwa mwendo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi za Jamii za Wanyamapori (*WMA's*) ni maeneo yaliyotengwa kisheria na yanahifadhiwa kwa kufuata taratibu na kanuni. Wamefanya mpango wa matumizi ya ardhi ya vijiji vyao na kutenga maeneo haya kuwa hifadhi za wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tunaitaka Serikali ieleze Bunge ni Sheria ipi inayoihusu Serikali kutoa leseni ya utafutaji madini kwenye maeneo yaliyotengwa kisheria kuwa hifadhi bila kushirikisha wananchi wa vijiji husika? Mfano, Serikali imetoa leseni kwa mwekezaji kutafuta madini kwenye eneo la Jumuiya na Maliasili Mbarang'andu – Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gawio toka uwindaji wa kitalii. Serikali lazima itambue kwamba wananchi ndio walinzi wa kwanza wa maliasili zinazowazunguka. Hata kama kungekuwa na vikosi vingi kiasi gani vya doria kama wananchi wa maeneo hayo wasiposhirikishwa vizuri hakuna ufanisi na rasilimali hizo haziwezi kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Serikali kutotoa stahili ya gawio la fedha zitokanazo la uwindaji wa kitalii kwenye Hifadhi za jamii na Halmashauri zinazohifadhi wanyama hao siyo sahihi na kufanya hayo ni kukatisha tamaa wananchi hawa na kuendeleza vitendo vya ujangili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze Bungeni kwa nini haijatoa asilimia 25%, stahili ya gawio kwa Halmashauri zote zenye vitalu vya utalii kwa 2008/2009, wakati fedha hizo zimelipwa zote na makampuni ya uwindaji? Kwa mwaka 2009/2010 hadi Juni kati ya fedha kiasi cha sh. 1,516,839,511.1 ambazo ni

stahili ya Halmashauri 37 zenye vitalu vya utalii, zilizotolewa ni Sh. 890,000,000.00 tu. Je, Serikali kutotoa fedha hizi kwa Halmashauri kwa wakati haioni inarudisha nyuma maendeleo ya Wilaya hizi kwani baadhi ya miradi ya maendeleo hutekelezwa kwa fedha zitokanazo na vyanzo zilivyoko ndani ya Wilaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utalii. Tanzania imejaliwa kuwa na vivutio vingi kila kona, tumejaliwa kuwa na misitu minene, hifadhi za mwanyamapori zenye wanyama wa kila aina, tunayo maeneo ya ardhi oevu *(Ramsa sites)* ambazo ni vyanzo vya maji, milima, malikale na vingine vingi. Kati ya maajabu saba ya Dunia *(World heritage sites)* yanayohifadhiwa kihistoria, maajabu matano yapo nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vivutio tulivyo navyo bado hatujaweza kutumia fursa hizo kuhakikisha sekta ya utalii inaingiza pato la kutosha kwa Taifa na kuinua hali ya maisha ya Watanzania wengi walio maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la kutangaza utalii, bado hatuna mikakati mizuri pamoja na fedha nyingi zinazotumika kutangaza vivutio vyetu ndani na nje, bado hakuna mbinu mpya zinazoibuliwa ili kuleta ufanisi. Tumekuwa tunatangaza vivutio vile vile siku zote (Mlima Kilimanjaro, Serengeti National, Zanzibar *Spice Island*) wakati tuna vivutio lukuki ambavyo havitangazwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kutangaza utalii kwenye maonyesho mbalimbali nje na ndani hatuendi kama timu. Kila kitengo kinakwenda kujitangaza chenyewe. Nchi za Kenya na Uganda wamepewa nishani ya Kimataifa kwa kuwa na mikakati mizuri ya kutangaza vivutio vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji wa Serikali wanaporudi kutoka kwenye maonyesho, hawakai chini kwa pamoja kufanya tathmini kama timu kuona kama kuna mafanikio au hakuna, wapi wameshindwa na wapi wamefanikiwa na jinsi gani ya kujipanga vizuri, hili nalo ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu yetu kwenda kwenye vivutio ni dhaifu sana, licha ya hifadhi hizi kuingiza pato kubwa kwa Taifa, lakini barabara zinazotumiwa na watalii kutembelea vivutio hivi hazifai na zimeharibika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ruaha *National Park* ni hifadhi ya pili kwa ukubwa nchini Tanzania baada ya Serengeti lakini hakuna barabara ya kwenda Ruaha, iliyopo imeharibika vibaya, ukipita siku moja hutatamani kupita tena. Katavi *National Park* ni hifadhi ya Tatu kwa ukubwa Tanzania, hakuna barabara, hakuna hata kiwanja cha ndege wala hata ndege inayokwenda kule. Mtalii akitaka kwenda Katavi ni lazima akodi ndege binafsi, Je, ni watalii wangapi wenye uwezo huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inauliza Hifadhi ya Katavi, Gombe na zinginezo ambazo hazifikiki kwa sababu ya kukosa miundombinu na

watumishi wanalipwa na Shirika kusimamia na kulinda vivutio vilivyopo, je, hii si ni hasara kwa Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi hatuna utaratibu wa kutembelea mbuga zetu, tunategemea sana watalii kutoka nje waje kutembelea mbuga zetu na kuongeza pato. Hii ndio sababu kubwa ya uchumi kuyumba mara nchi za wenzetu zikiyumba kiuchumi na sisi tunayumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za Serikali kuhamasisha utalii wa ndani zinahitajika sana na isiwe wakati wa maonyesho ya sabasaba na nanenane tu kama inavyofanyika sasa, inatakiwa iwe utamaduni wetu wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu misitu na Nyuki. Nchi yetu imejaliwa kuwa na misitu minene katika maeneo mbalimbali ambayo ni vyanzo vya maji ya mito, kuleta mvua, makazi ya wanyamapori na hata hali ya hewa tuliyo nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana misitu yetu mingi iko kwenye hatari ya kutoweka na dalili za wazi zinaonekana kwa sababu ya uharibifu mkubwa na ukataji wa miti inayotokana na shughuli za bishara zikiwepo uchomaji mkaa, ukataji miti kwa ajili ya mbao, kilimo kisichojali mazingira na kadhalika. Zipo Sheria za misitu na Sera za Misitu zinazoongoza utunzaji wa matumizi endelevu ya misitu lakini zipo kwenye vitabu makabatini utekelezaji hakuna. Sekta ya misitu na nyuki imeshindwa kuchangia pato stahili kutokana na baadhi ya watendaji kushirikiana na majangili kuhujumu rasilimali kwa manufaa yao binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha mauzo ya mazao ya misitu nje ya nchi kilishuka toka Dola za Kimarekani 700,914.5 mwaka 2008 hadi Dola 70,247.7 mwaka 2009. Sababu ni kutokana na kuzuiliwa uuzaji wa magogo nje ya nchi, kudorora kwa uchumi wa dunia na ushindani mdogo wa bidhaa za mazao ya misitu zinazozalishwa hapa nchini katika masoko ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa misitu yetu ya asili imesheheni miti mizuri yenye mbao zenye thamani kubwa lakini Serikali imeshindwa kusimamia sekta hii ili ilete ajira kwa vijana wengi wanaozunguka mijini bila kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbao ya Tanzania ina thamani kubwa na inapendwa sana hata Ulaya. Ni ngumu na inadumu kwa muda mrefu na uasilia wake. Samani iliyotengenezwa na mbao iliyovunwa hapa nchini huwa ni imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatumia fedha nyingi sana kununua samani za maofisini kutoka nje ya nchi tena kwa gharama kubwa. Meza moja ya ofisini kutoka China ambayo siyo imara wala haina ubora inanunuliwa 500,000 – 1,000,000/-. Meza hiyo hiyo ikitengenezwa hapa nchini ambayo ni imara itagharimu 200,000 – 300,000/-. Wakati huo huo tungetoa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasumba hii imejengeka hata kwa wananchi wengi pia wanaona baidhaa za nje ni bora kuliko za hapa, tubadilike tuthamini mali zetu kuinua uchumi wetu na maendeleo yetu. Ni aibu kwa nchi kuagiza hata vijiti vya meno *(tooth pick)* toka nje ya nchi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge imeandaa mkakati gani kuhakikisha kuwa samani za maofisini na majumbani zinanunuliwa hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kukosa uzalendo viwanda vyetu vya mbao, vyote vimekufa hapa nchini. Tunategemea kununua kila kitu kutoka nje. Hatuwezi kuinua uchumi kwa kutoa fedha za ndani kununua mali nje bila kuuza ili kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze ni mikakati gani ya dhati iliyopo ya kufufua viwanda vyetu vya mbao?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana kwenye bajeti yangu nilizungumzia suala la Kiwanda cha Mbao cha Mkata Sao Hill kilichopo Tanga. Nililieleza Bunge lako Tukufu kwamba kiwanda hicho kilichobinafsishwa Machi 1998 hakijawahi kufanya kazi wala kulipa chochote Serikalini. Serikali ilijibu hapa kwamba kiwanda hicho kinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nililazimika kutembelea kiwanda hicho kujionea hali halisi, ni kuwa kiwanda hicho kilichobinafsishwa mwaka 1998 kwa kampuni ya *ANISHAS* hakijawahi kufanya kazi hata siku moja, mali za mabilioni zilizokuwepo zimeoza pale kiwandani, yakiwepo magari mapya *E-Vehicle* -4, Matrekta aina ya *Fiat double tyres-2, Valmet* -1, gari *double cabin* mpya na mashine zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati kiwanda hiki kinabinafsishwa na wafanyakazi wote walibinafsishwa pamoja na baadaye waliachishwa kazi kinyemela bila kulipwa chochote, hadi leo hii watumishi 75 walioachishwa kazi hawajalipwa stahili zao. Kwa miaka yote wananchi hawa wamefuatilia madai yao bila mafanikio. Wameshindwa kurudi makwao, wamebaki wanahangaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze hatma ya wafanyakazi hawa kuhusu kulipwa haki zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sao Hill ni shamba la Serikali na hivyo basi tulitarajia liwanufaishe Watanzania wote bila kubagua. Jambo la kushangaza ni kwamba bei zinazotumika kuuza magogo zinatofautiana kati ya wananchi wa kawaida na wafanyabiashara wakubwa. Wafanyabiashara wadogo wananunua *cubic* mita moja ya gogo shs.34,000 wakati Kiwanda cha Mgololo kinanunua *cubic* mita hiyo kwa shs.10,000. Tunaitaka Serikali itueleza utofauti huo wa bei unatokana na nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mfuko ulioanzishwa kwenye shamba hili kwa kila anayevuna mbao kuchangia sh.10,000 kwa ajili ya kuendeleza bustani za miti na kutengeneza barabara, wafanyabiashara wadogo wanalipa lakini Kiwanda cha Mgololo

hawachangii wakati wao ndio wanaovuna kwa wingi na ndio wanaharibu barabara kwa magari makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la mfuko huu ni kuendeleza shamba hili na miundombinu yake, lakini cha ajabu ni kuwa Serikali imekuwa inazichukua kwa matumizi mengine. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge ni kwa nini inachukua fedha hizo zote na kusababisha dhamira nzima ya mfuko huo kukosa maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hatari kubwa ya misitu yetu ya asili kutoweka yote ikiwa Serikali haitatafuta njia mbadala ya matumizi ya nishati kwa wananchi wengi wa hali ya kati. Matumizi ya mkaa yanaongezeka kwa kasi kikubwa kila kukicha, wananchi wengi hawawezi kumudu gharama za umeme na majiko ya gesi. Vijana wengi wanaomaliza shule wanajiingiza kwenye uchomaji wa mkaa. Maeneo mengi yaliyokuwa na misitu yamebaki vichaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuacha maneno ya vitabuni na kutekeleza haraka mipango ya matumizi ya makaa ya mawe pamoja na gesi asilia ambayo ipo kwa wingi hapa nchini, vinginevyo nchi itakuwa jangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana pamoja na Serikali kutambua mchango mkubwa wa zao la tumbaku kwenye uchumi wa Taifa hili. Serikali imeshindwa kuwa na mpango maalum wa kunusuru misitu ya Mkoa wa Tabora isiteketee kwa ajili ya kukaushia tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Misitu inasema Kata mti panda miti. Ni nani anafuatilia na kuwezesha kuhakikisha miti inayokatwa kwa ajili ya kukausha tumbaku inarudishiwa? Suala la upandaji wa miche ya miti limeachwa kwa makampuni yanayonunua tumbaku. Makampuni haya yanagawa kwa wakulima miche miwili kwa kila mfuko wa mbolea. Wakulima wakishapata mbolea wanawahi mashambani hawana mpango wa miche ya miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali itenge fedha zitokanazo na tumbaku kupeleka kwenye mikoa inayolima tumbaku kurudishia misitu inayopotea na hapo hapo itakarahishe nishati mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufugaji wa nyuki. Sekta ya ufugaji nyuki bado ina fursa kubwa sana kwa maendeleo ya Watanzania na uchumi wa nchi kwa ujumla. Kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na Kampuni inayojihusisha na Maendeleo ya Sekta Kilimo inayoitwa (*PASS*), inaonyesha kuwa Tanzania ina uwezo wa kuzalisha tani 138,000 za asali zenye thamani ya shilingi 133.3 bilioni kila mwaka na kuzalisha nta tani 9,200 zenye thamani ya shilingi 35.5 bilioni kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya hali ya uchumi ya mwaka 2009 inaonyesha kuwa uzalishaji wa asali umeongezeka kutoka tani 430 mwaka 2008 yenye thamani ya sh. 605.6 milioni hadi kufikia tani 621 mwaka 2009 yenye thamani ya sh. 1.223 bilioni. Uzalishaji wa nta ulipungua kutoka tani 502.4 mwaka 2008 ya thamani ya sh. 2.9 bilioni, hadi kufikia tani 296.502 mwaka 2009, yenye thamani ya shs.1.96 bilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi za Serikali kuhusiana na mapato kutoka katika sekta ya nyuki, ukilinganisha na takwimu zilizofanyiwa utafiti na *PASS* ni dhahiri kuwa bado tunahitaji watendaji makini Serikalini, vinginevyo miaka yote tutaendelea kuletewa takwimu zinazoonyesha kuwa hatuzalishi na hivyo kutoa mwanya kwa biashara ya njia ya panya kushamiri na kuwanufaisha watendaji katika idara hizo. Aidha, Serikali bado haijaweza kutumia fursa zilizopo za kuhakikisha zao la asali linaingiza kipato kikubwa kwa Taifa na kuinua maisha ya Watanzania wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti zinaonyesha kuwa kuna zaidi ya hekta 34 milioni za mapori yanayofaa kutunza makoloni 9.2 millioni ya nyuki wa asali. Aidha, tafiti zinaonyesha iko mikoa mingi hapa Tanzania inayofaa sana kwa ufugaji wa nyuki. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge ni mikakati gani ya uhakika kuwa fursa hii inawanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utafiti. Suala zima la utafiti hapa nchini bado halipewi uzito unaostahili. Hakuna uhifadhi endelevu bila ya kuwepo utafiti makini wa rasilimali zetu. Kuelewa rasilimali zetu tutaweza kupanga mipango endelevu ya kuzilinda na kuzitumia pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi za utafiti wa Wanyamapori *TAWIRI* na ile ya misitu (*TAFORI*) zimekuwa miaka yote hazipati fedha za kutosha kutekeleza mipango yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TAWIRI* inakabiliwa na matatizo mengi kiasi cha kushindwa kujiendesha kwa ufanisi kituo kinakabiliwa na tatizo kubwa la ufinyu wa bajeti. Kwa miaka yote fedha zinazotolewa ni kidogo sana na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kama yanavyopangwa. Mfano, 2009/2010 waliomba Sh.3,591,593,424/- walizopewa ni 2,064,590,371 sawa na 57%, lipo tatizo la uhaba wa rasilimali watu, wataalamu wa utafiti waliopo ni wachache sana na hivyo kupelekea tafiti nyingi za wanyamapori kufanywa na wataalam kutoka nje jambo ambalo ni hatari sana kwa uhifadhi wetu. Ni aibu kwa taasisi muhimu kama hii kutegemea misaada ya Wafadhili na hatuwezi kuwa na uhifadhi endelevu kwa mwendo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la ajabu na aibu kwamba wanakuja watafiti kutoka nje wanakuwa na takwimu za kina *(detailed data),* kuhusu rasilimali zetu hapa ndani kutuzidi wakati tuna chombo/taasisi ambayo tukiwezesha inaweza kufanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili limejidhihirisha wazi hata kwenye mkutano wa *CITES* (Cop.15) uliofanyika Qatar Doha 13 – 15/3/2010 wakati wataalam wetu walitoa *data* kidogo kuhusiana na uhifadhi wa tembo watafiti wa nje walitoa ripoti yenye takwimu za kina kuhusu hali ya ujangili wa tembo hapa nchini na biashara haramu ya meno ya Tembo hali iliyyopelekea washiriki kuona Tanzania hatuko makini na hii ndiyo hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

MHE.FELIX N. KIJIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitoe shukrani zangu za dhati kwa kunipatia nafasi hii. Lakini pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Muhambwe ambao waliniwezesha kufika hapa. Nina hakika bado wanahitaji niendelee kuwa mwakilishi wao kwa sababu naendeleza msemo wangu ninaosema kwamba kila kwenye msafara mamba, kKenge hawakosekani kwa hiyo, wale kenge walie tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa dhati kabisa, niipongeze Hotuba ambayo tumesomewa na Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, hotuba ambayo kusema ukweli ni nzuri sana. Hotuba imeandaliwa kwa umakini na kwa mantiki hiyo sina budi kupongeza uongozi mzima wa Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Waziri Mheshimiwa Mwangunga, nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizi nazozitoa kwa niaba ya wananchi wa Kibondo katika Mkoa wa Kigoma. Wananchi wa Kibondo walikuwa na tatizo kubwa wakaja kwangu kama mwakilishi wao na sikusita kwenda kwa Waziri na Naibu Waziri, wakaitisha kikao, tukaa na Mkurugenzi wa Wanyapori, Tarimo sijamuona, leo tukawa na uamuzi mzuri sana ambao wamekwenda wakapeleka semina nzuri kabisa ambayo imewatoa gizani wananchi wa Muhambwe na hususan Wilaya ya Kibondo nzima kuelewa wajibu wa wale wananchi wanaokaa kwenye vijiji ambavyo vinapakana na hifadhi, nawashukuru sana na nawapongeza sana kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalosema basi ni salamu za wanachi wa Kibondo. Napenda nitoe shukrani nyingine za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Nne. Serikali ya Awamu ya Nne maana yake hitimisho kwetu sisi kwetu Kigoma tumepata leo na hasa Kibondo na Kasulu kutoka katika Wizara ya Nishati na Madini, wakati watu wanazungumzia umeme wa vijijini, mimi kwangu ninalilia umeme wa Makao Makuu ya Wilaya, hata Kasulu kwa ndugu yangu Nsanzugwanko lakini kwa huruma kubwa kabisa ya Serikali ya Awamu ya Nne tunapozungumza ni kwamba kazi ya kuwapatia wananchi wa Kasulu na Kibondo umeme inaendelea na Waziri ametuthibitishia na wananchi wamesikia naipongeza kabisa kwa dhati awamu hii ya nne kwamba imeweza kuwaonea huruma wananchi wa Kigoma kwa sababu ni wananchi ambao wametoka katika matatizo kuanzia enzi za ukoloni ama tangu tupate uhuru mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi upo kwamba hapa karibia Mbunge kila kinachotajwa ni umeme wa kijiji fulani kwangu Kasulu na Kibondo ndiyo Wilaya tunapata umeme. Kwa hiyo, nadhani hata Waheshimiwa Wabunge mngeweza kutuhurumia mkasema kwamba hapana kwetu msipeleke vijijini tuwasaidie hawa ambao hawajapata Makao Makuu ya Wilaya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ulishawahi kusikia mtu anasema mama yako wee, kila mtu anasema mama yangu wee!

MHE.FELIX N. KIJIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Sasa niupongeze kabisa kwa dhati uongozi kuanzia ngazi ya juu wa Awamu ya Nne kwamba kwa kweli wameonyesha mabadiliko makubwa sana katika nchi yetu na nina hakika ndiyo mwendo tunaotoka nao. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awajalie huko tuendako tuendelee kupata fadhila hizi ambazo tunapewa. Lakini nina mambo mawili, matatu ya kushauri tu kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwangu katika Wilaya ya Kibondo nimekuwa na wafugaji ambao wanatoka Ilunde, wamekuwa wakifuga ng'ombe kuanzia miaka ya 1960, ni wafugaji wapatao 6,000. Wana ng'ombe wapatao 40,000, hawa wananchi katika kufuga kwao wameweza kutekelezewa mambo kadhaa na Serikali walijengewa shule, zahanati, ikiwa ni pamoja na mambo mengine muhimu ambayo yanatolewa na Serikali kwa vijiji ambavyo vimetengwa ni kweli kabisa nakubali kwamba katika ukumbi huu kuna Sheria ambazo zinamiliki sasa Hifadhi zetu kwamba watu hawawezi kuishi kiholela kama ambavyo tumekuwa tukiona kwamba wafugaji wanatoka Mwanza wanakwenda mpaka Mtwara, ni katika kutekeleza hili kwamba Wafugaji hawatakiwi kukaa hifadhini na kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa mfano huu ambao nimeutoa naomba sasa Wizara ya Maliasili na Utalii wajaribu kuangalia. Sisemi kwamba hawa watu ni lazima wakae katika Hifadhi hapana, Sheria inasema lakini basi katika kuwataka waondoke watafutiwe eneo ambalo watakwenda na mifugo yao watu 6,000 kuwaondoa mahali ambapo walikuwa wamekaa zaidi ya miaka 40, ukawaondoa na mifugo kwa kweli ni kutowatendea haki, wale watu wanahangaika wengine wamekwenda Kaliua, wengine Nguruka wanahangaika na mifugo inakufa. Mimi kama mwakilishi wao kwa sababu walikuwa ni wapiga kura wangu wamekuwa wakinifuata hapa Dodoma naingia gharama za kuwasafirisha, kuwatunza hapa wakiwa wanatafuta msaada wa kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara na uongozi wa Wizara ni uongozi ambao kusema kweli nasema kuwa ni watu wenye busara kabisa na huruma ya hali ya juu. Wajaribu kuangalia kama siyo lazima basi watafutiwe mahali ambapo watakwenda kuishi pamoja na mifugo yao ili waweze kuepukana na mateso ambayo wanayapata sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo ningeomba Wizara ijaribu kutazama wale wananchi wa kule Kibondo wamekuwa na matatizo mengi sana. Kwanza walikuwa hawajui Sheria ambazo zinalinda hifadhi wao walifikiria kuinga katika hifadhi ni kwenda kienyeji nimesema mwanzoni kwamba kuna semina ambayo imefanyika, wameelewa kinachotakiwa kwamba vibali vinatakiwa vipatikane vya uhakika vya kuwaruhusu hawa watu waweze kuingia kwenye hifadhi na kupata mahitaji wanayotaka, sasa kwa kule Kibondo na Hifadhi ya Movoza ambayo inakwenda mpaka kule Kahama ni pori kubwa sana, naomba hao watu waweze kupata utaratibu wa kwenda kuvua samaki, ndiyo kilio cha wananchi wangu wa Kibondo. Miti imo ndani ya hifadhi kwenda kurina asali, ikiwa

ni pamoja na kutafuta kuni, akina mama wanahangaika sana kwa kufanya hivyo, hii itawasaidia sana hilo ni ombi nimelileta kwa niaba ya wananchi wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kulikuwa na tatizo kubwa la wananchi kuzaliana sana, sasa wao baada ya kunithibitishia hilo zoezi la kuzaliana wanaliendeleza vizuri, wanaomba mpaka uweze kurudishwa nyuma kwa kumega sehemu ya pori kwa sababu ukiangalia vijiji vyote vinavyopakana na hifadhi vimeshajaa wananchi wanakosa ni wapi wakalime. Hilo likiangaliwa wananchi wa Kibondo na Kasulu wataendelea kuishukuru Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema wananchi wa Kibondo wamekuwa wanakwenda kienyeji hawajui sheria ambazo zinalinda hifadhi, lakini sasa hivi wamekuwa na uelewa mkubwa sana, lakini hii itaweza kuendelea kuwajenga endapo Wizara itendelea kutoa semina za namna hii, sisemi kwa Kibondo sasa hivi naweza nikasema ni Mkoa mzima wa Kigoma ikiwa ni pamoja na maeneo mengine ambayo yana vijiji vinavyopakana na hifadhi za wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niipongeze Wizara hiyo kwa hayo na naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nikianza kwa kumshukuru sana Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Watalaam wote katika Wizara hii, Taasisi zake kwa kazi nzuri sana ambayo wamekuwa wakiifanya katika mazingira ya fedha chache, mazingira ya watumishi wachache na mahali pengine maslahi yasiyoridhisha. Nawapongeza sana na ningependa kuwapa moyo muendelee kwa bidii zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana wananchi wa Kongwa kwa kuendelea kuniamini na niendelee kuwahakikishia kwamba uwakilishi ninaofanya kwa niaba yao hapa Bungeni ni wa uhakika natumaini tutaendelea kuwa pamoja kwa kipindi kijacho 2010-2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kadhaa nimesema na sitachoka kurudia tena, inanipa tabu tunapokuwa na Shirika la Hifadhi za Taifa, Tanzania *National Parks*, ambalo madhumuni yake ni kuhifadhi maeneo yale ambayo tumekubaliana kwamba yana umuhimu wa kipekee Kitaifa, yakae katika daraja hilo chini ya Shirika hilo la Taifa, lakini tunazo hifadhi za bahari, *Marine Park* na Marine *Reserves* ambazo ziko nje ya *TANAPA,* ningependa kusisitiza tena baadhi ya *marine parks* kama ile ya Mafia au ile ya Mnazi *Bay* ni vizuri sasa wakati umefika ziwe chini ya *TANAPA* kwa sababu ndilo shirika ambalo linapaswa kimsingi kushughulikia hifadhi hizi pia za bahari, isiwe *TANAPA* ni hifadhi za bara tu na hofadhi za majini pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwenye hotuba ya Waziri ukurasa wa 28 ametupa takwimu zinazotia moyo sana za makusanyo ya fedha inayoitwa *LMDA* kwenye masuala ya misitu. Makadirio ni kukusanya bilioni 12. Fedha hii kazi huwa ni kusaidia sana katika upandaji na uoteshaji wa vitalu vya miche ili kuhakikisha kwamba mashamba yetu ya misitu yanaweza kupandwa miti mipya kwa uhakika kinyume na hali ilivyokuwa mwanzo. Kwa kuwa tuna fedha nyingi namna hii tulikuwa tumekadiria bilioni 12, tumekusanya bilioni tisa mpaka Aprili, kuna mahali palikuwa na *negotiations* zinaendelea kwenye shamba la Sao Hill, kwamba kampuni ya *Green Resources* ipewe zaidi ya ekari 5470 kwa utaratibu wa *concession*, najiuliza *concession* ya nini, kwa kuwa una fedha tayari za kuweza kupanda miti huna tatizo, sasa *concession* ya nini, hata kama huwezi kupanda kwa mwaka mmoja bado unaweza kuendelea kidogo kidogo, mwaka huu, mwakani, mwaka kesho kutwa katika miaka miwili hadi minne tayari utakuwa umeshapanda Sao Hill nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huhitaji *green resource* wala kampuni nyingine yeyote kukusaidia kwa kuipa ardhi kwa miaka tisini au miaka sitini wakae nayo wakati una uwezo wa kupanda wewe mwenyewe na kuvuna wewe mwenyewe. kwa hiyo hii sera ya *concession* kwa ujumla wake haitupeleke popote, mimi siiungi mkono hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulisemea hapa ni kule Ngorongoro, kuna eneo la *Olduvai Gorge* na kule Laitoli, maeneo haya yako chini ya Idara ya Mambo ya Kale, ningeshauri sana kwamba idara hiyo ikabidhi *Olduvai Gorge* na Laitole uendeshaji wake kwa mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro ili utoaji wa huduma ulingane katika mamlaka nzima idara isaidie katika masuala ya utalaam wa namna ya kuhudumia maeneo hayo ambayo yana umuhimu wa kipekee kabisa wa utalii katika nchi yetu na kiuhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la barabara ya Mugumu-Loliondo mpaka Mto wa Mbu. Tumeelezwa mara kadhaa hapa kwamba Serikali imeshafanya uamuzi na safari hii zimetengwa shilingi bilioni moja kwa ajili ya barabara hiyo. Mimi kama mhifadhi jambo hili linanitatiza, naomba radhi sana watu wa maeneo hayo, lakini ukweli, barabara ile kwa ajili ya huduma ya watu wa Musoma ingepita eneo ambalo lina watu wengi zaidi kutoka Karatu unateremka kuelekea Mbulu, Yaeda Chini, unapita makao *open*, unapita Meatu, unaingia Maswa, Bariadi unatokea Lamadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lile ni eneo lenye ufugaji, ni eneo lenye kilimo cha pamba, kilimo cha vitunguu, ni eneo lenye uzalishaji mkubwa mno. Ukitazama *mileage* ya kutoka Musoma kuja Arusha kwa kuunganisha Lamadi mpaka Karatu inawezekana labda ni kilomita 400 au 500 maximum, na hii ambayo inatoka Mugumu kuelekea Mto wa Mbu na yenyewe ni kama kilometa 400 hivi tofauti yake wala siyo kubwa sana. Kwa hiyo sijui, ushauri ni kwamba ni vizuri Serikali ikalitazama jambo hili, badala ya kulitazama kisiasa zaidi ikalitazama kiukweli kiuchumi na kwa faida kubwa zaidi.

Ukishafungua barabara ile juu, sahau habari ya kuwa na Serengeti, lazima itafungua maeneo yote ya kule juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, masuala ya *immigration* ya Serengeti sahau, Loliondo ni maeneo mazuri sana kwa Kilimo ukishaweka barabara ya lami Loliondo yote italimwa, *migration* kwa kheri. Kwa hiyo, jambo hili Serikali ilitazame vizuri. Nazungumza kama mhifadhi maeneo yale nayajua sana, inanipa tabu kidogo kulinga mkono jambo hili. Naiomba Serikali ilitazame jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sheria tuliyoipitisha mwaka jana ya wanyamapori, tulisisitiza sana suala la kuunda shirika jipya kwa ajili ya kuangalia *game reserves* zetu. *Selou Game Reserve* ni hifadhi kubwa usawa wa Burundi na Rwanda kwa pamoja, hifadhi moja. Ina kilomita za mraba zaidi ya elfu hamsini (50,000). Pori lile lina umuhimu wa kipekee, lenyewe pekee sina takwimu halisi lakini linaingiza karibu bilioni sita, saba, nane kwa mwaka, wao wanapewa bilioni moja au chini ya bilioni moja kwa uendeshaji matokeo yake ni nini? Hali ni mbaya na hali inazidi kuwa mbaya, inabidi tumtegemee Kamanda Tossi kwenda kufanya doria kule ndiyo kuwe na *discipline* kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri pori hili lipandishwe hadhi lifanane na Ngorongoro, liwe na Bodi yake na hizo *reserves* zingine kama tulivyosema katika sheria ile, liundwe Shirika ama mamlaka kwa haraka iwezekanavyo ili iweze kusimamia *reserve* zetu zilizobaki. Zina uwezo kabisa wa kujiendesha, hazina wasiwasi, masuala ya wasiwasi wa watumishi yataondoka, masuala ya fedha itakuwa kuna unafuu mkubwa zaidi, lakini vile vile masuala ya maslahi ya watumishi yatakuwa ni historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, tulipokwenda Doha tulikwenda na maombi mawili, moja tu-*down grade* tembo atoke appe*ndix one* aende *appendix two*, yaani atoke kwenye *total protection* aende kwenye eneo ambalo anaweza akawindwa. Lakini jambo la pili lilikuwa la kuuza meno ya tembo. Ushauri wangu ni kwamba tutakapoandika maombi mengine ya kwenda kwenye kikao cha aina hiyo tuandike maombi ya kuuza meno ya tembo yale ambayo yapo kwenye *stock*, ombi moja peke yake la kuuza ile *stock.* Tunapoenda na masuala ya ku-*down grade* ndiyo maana hata jirani zetu wa Kenya wanatuletea matatizo, kwa sababu wanaamini Kenya hawawindi tembo wala mnyama yeyote, wanaamini kwamba tembo wao wanaotoka Amboseli na hifadhi kama hizo wanao-*cross* kuja Tanzania na kurudi, wanapoingia Tanzania kuna vitalu vya uwindaji, kwa hiyo, wanawindwa. Kwa hiyo, ukisema jambo la kuruhusu tembo awindwe ni lazima utapata matatizo tu. Majirani watakupiga saa hiyo hiyo, kwa sababu wanyama hawa wana-*cross* mipaka na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile mimi kama ni mhifadhi, habari ya kuwinda tembo bado siifurahii sana, ningependa tuendelee kumhifadhi mnyama huyu na wanyama wengine, kwa ajili ya faida kubwa zaidi ya nchi yetu kwa sasa na siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuiomba Serikali iitazame kipekee Wizara hii, izitazame hifadhi, maslahi ya Bwana Nyama na Bibi Nyama wanaokaa katika maeneo ya mapori ndani kabisa katika mazingira magumu sana kwani ni maslahi madogo sana, wanaishi katika mazingira magumu sana, kuna Mbung'o kule,

kuna wanyama wakali, wana *risk* mambo mengi, maslahi yao yaangaliwe kipekee. Kuna kila sababu ya kupata mishahara ambayo ni bora zaidi, kupata marupurupu ambayo ni bora zaidi hasa wale ambao kwenye *game reserves,* wanaishi katika mazingira magumu, tuwajengee nyumba bora zaidi na tuhakikishe kwamba mazingira yao ya kazi ni mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya watumishi katika *game reserve* ni ndogo mno na haya masharti ya *game scout* kuwa *form four* siyo lazima. Darasa la saba anaweza, matokeo yake tunakuwa na kila mtu Afisa. Kila anayeingia *form four* anachukua cheti anataka achukue *diploma* afanye hivi mtu wa ku-*patrol* atakuwa hayupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Kuna mambo mawili mazito umeyazungumzia, habari ya barabara ambayo inaweza ikapita kwenye hifadhi, halafu jambo la pili ni kibali cha kuwinda tembo, nilifikiri Kamati yako ndiyo yenye mamlaka ya kushauri *serious* kwa maandishi na *research* inayostahili. Nafikiri ungefanya hivyo kwa sababu ukizungumza hapa sisi tunapiga makofi tu, lakini ninyi mnaweza kuchukua hatua. Nadhani ungefanya hivyo. (*Makofi*)

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Lindi, wanawake kwa wanaume kwa namna moja au nyingine wameniwezesha mimi kufika hapa leo, kwa kweli nasema ahsante sana. Vile vile natangaza nia kwamba nitagombea tena Ubunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kupongeza Wizara hii, Waziri, Naibu Waziri, pamoja na uongozi wake wote kwa kufanya mambo makubwa na mazuri. Kwa kweli ni budi kumsifia binadamu mwenzio pale anapoweza kuliko kulaumu kila kitu kila siku utaambiwa una kasoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imefanya mambo makubwa mazuri na mimi ni shahidi, kwamba mara tu baada ya umoja wa nchi za Afrika na Bunge la Afrika kupitisha Azimio la kuunga mkono mwaka 2004 kwa nchi zote Barani Afrika zinazotaka kurejeshewa mali zao, Wizara hii ilikuwa ya kwanza kuweka mikakati ya kurudisha mali za Tanzania. Ushahidi ninao wameweza kurudisha kile kinyago ambacho sasa hivi amekizungumzia Waziri kipo ndani ya picha ya kitabu cha bajeti ambacho kiliibiwa ufaransa kwa miaka 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, kile kinyago ni mali halafu kinatakiwa sana katika nchi za nje kwa sababu ile *museum* ambayo tumekikuta kinyago hiki ni *museum* inayoonesha tamaduni za binadamu wote Duniani. Sasa ile ilikuwa inaonesha utamaduni wa Mwafrika ulivyo, kilikuwa inaonesha Mwafrika alivyo. Kwa hiyo kilikuwa ni mali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukirejesha nchini Tanzania baada ya miaka 20 mmefanya jambo kubwa sana. Wakati wanakirudisha mimi ni shahidi walikuwa wanatuambia kitaibiwa na kweli mzigo mmoja uliibiwa walidhani kinyago kile kipo katika mzigo ule, lakini kinyago kilifika salama Tanzania, kinyago cha Newala- Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi mwingine ni kwamba tulitembelea Ufaransa, Ujerumani kuangalia Mjusi yule ambaye anazungumziwa kila siku, yule mjusi ni mkubwa sana, tulipokwenda kule tulijaribu kupiga naye picha, kidole cha mwisho cha mguu wake ndiyo ukubwa wangu, Waafrika saba tuliokwenda kule wote waliishia urefu wa kidole cha kwanza na kidole cha pili ndiyo urefu wetu sisi. Kwa hiyo, nasema ile ni mali na inatakiwa na watu wote kule wanaithamini. Hayo ndiyo mambo waliyofanya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamejaribu kuzungumza na Ujerumani na sasa hivi ninavyozungumza tayari *memorandum of understanding* imeshawekwa ya kutaka kufanya ushirikiano wa Tanzania na Berlin *Museum*. Vile vile, mafunzo kati ya Tanzania na Berlin kubadilishana wafanyakazi kwa maana ya kujifunza wafanyakazi wa Tanzania na wafanyakazi wa kule kuwa pamoja katika mafunzo ya makumbusho. Kwa hiyo, tayari mambo makubwa hayo ya kwenda katika mwelekeo wa kurudisha mali za Tanzania zilizopo nje ya nchi ukiacha Mjusi na sanamu kuna mali zingine Kenya, kuna mali zingine Uingereza. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuwapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nachukua nafasi hii kuwashukuru Wizara kwa kunipeleka Berlin kwenda kuona Mjusi, vile vile kushiriki katika kurudisha kinyago kile cha Mtwara, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa kweli nashukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amezungumzia mambo sita ambayo yapo katika Wizara yake, sitaweza kuyazungumzia mambo yote lakini angalau niweze kuzungumzia mambo matatu. Amezungumzia wanyamapori, Misitu na Nyuki, Utalii, Malikale, Makumbusho. Naomba nizungumzie suala la utalii, malikale na makumbusho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la utalii. Watalii sasa hivi wanapenda sana masuala ya utamaduni. Nafikiri tuangalie maeneo yale ambayo yana utamaduni wa mambo mbalimbali katika nchi ya Tanzania, kuna sehemu nyingi sana ambazo zina utamaduni huo ili kuongeza kupanua wigo wa utalii ni budi sasa twende katika maeneo yale ambayo yana mambo ya utalii wa kitamaduni. Mfano, mmoja mdogo ambao upo katika Mkoa wa Lindi, katika Mkoa wa Lindi kuna mifano kadhaa ya vivutio ambavyo

tungeweza kufanya utalii, kuna *beach* nzuri ya Lindi, pili magofu ya Waarabu Kilwa ambayo sasa ni *heritage of the world* yapo kule pamoja na kwamba watalii wenyewe wanakuja lakini matunzo hayo hayapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni Makonde *Carvings*, hii ni *culture*, Makonde *plateau*, hii ni *culture*, kuna pango kubwa wanasema kwamba lilitumika wakati wa vita ya maji maji, lile pango ni kubwa katika Afrika ndani yake kuna mapango 20 na kuna njia mbalimbali za kuweza kujificha na ndani kuna kaburi. Yaani wakati wa vita ya majimaji watu walikuwa wanatupwa ndani, sasa hivi utalii ni mkubwa sana, lakini kunatakiwa juhudi ya kuendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Tendegulu, Lindi ambalo huyu Mjusi, mnyama wa ajabu aliyeishi miaka milioni 150 alionekana lipo, ni eneo zuri ambalo tungefanyia utalii kwa sababu dunia nzima wanapenda utalii wa mjusi aina ya *Dinosaur*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale pangekuwa kivutio kikubwa kwa sababu mpaka sasa Waingereza na Wajerumani wanakuja kuchimbua vitu fulani fulani, hatujui ni nini lakini hawachukui kitu kikubwa, wanachukua udongo na nyasi, sisi tukiuliza vitu hivi vya nini? Kumbe wanakwenda kupamba kwenye *museum* yao kwa sababu walichukua mijusi mitano (5) kwenda Ujerumani kabla ya Vita ya Kwanza ya Dunia na walichukua mijusi mingine iko Uingereza na ni kivutio kikubwa. Kule ukiangalia kuna utaalam mkubwa ambao wameufanya, wameweka kitu kinaitwa *Jurascope* ni kipindi ambacho kinaonyeshwa katika Runinga, walionyesha Mjusi huyo angali mzima na unamwangalia anafanya vitendo mbalimbali mfano kula, kucheza, kukimbia n.k. ni kivutio kikubwa sana.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, hayo mambo ni mazito sana. Sasa Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, atafuatiwa na Estherina Kilasi, Mheshimiwa Ndesamburo atafikiwa na baadaye Mheshimiwa Lembeli.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kipindi chote tulichokuwa nao nikiwa miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Pamoja na taabu nyingi na maelekezo mengi tuliyokuwa tukiwapa, lakini nashukuru wameungana nasi na wamefanya kazi kwa juhudi kubwa kabisa na hivyo ninapenda niwapongeze sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninapenda nitumie nafasi hii, niwapongeze Wapigakura wangu wa Jimbo la Jang'ombe ambao wamenistahimilia kwa vipindi viwili hivi sasa na ninashukuru kwa salamu zao walizonitumia kwamba, wako tayari na wanachangishana ili nichukue fomu kwa ajili ya awamu ya tatu. Ninawaahidi kwamba, nitapokea mchango huo na nitawatumikia zaidi ya hivi nilivyokuwa ninawatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uharibifu wa mazingira, ukweli mazingira yanaharibiwa sana katika nyanja zote. Pamoja na mikakati ya Wizara katika kujitahidi ili mazingira yetu yawe mazuri, bado uchafuzi wa mazingira upo na hasa misitu yetu inakatwa sana. Lakini uchafuzi huu na ukataji wa miti unatokana na wafanyakazi kuwa wachache na kukosa vitendea kazi vya kuwawezesha kuzungukia maeneo yote na kuweza kufanikisha kazi hizi. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iitazame kwa jicho la huruma Wizara hii ili kuweza kuwapa mfuko wa kuweza kuajiri kwa sababu mapori yetu ni mengi, makubwa lakini Watendaji ni wachache kuliko ukubwa wa mapori yenyewe. Tungewajalia hawa wenzetu nguvu zaidi ya kuweza kufanya kazi ya kuhakikisha kwamba mazingira yetu yanalindwa kwa sababu ndiyo uhai wetu, bila ya hivyo uchafuzi wa mazingira ambao pia ndiyo uchafuzi wa maisha yetu unakwenda sambamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninataka niipongeze Wizara kwa kazi kubwa waliyofanya Ngorongoro kwa sababu tulikuwa katika hali mbaya sana kiasi cha kuondolewa katika urithi wa dunia. Nashukuru jitihada imefanywa, niwashukuru viongozi wote wa Ngorongoro kwa kupitia uongozi wa Wizara kwa kuwezesha kufanikisha kazi hiyo pamoja na kwamba nguvu ya Kamati ilikuwepo, Kamati ilikuwa inatoa mikakati tu lakini utekelezaji wote ulitekelezwa na watendaji wetu kupitia kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake. Ukweli hali hivi sasa ni nzuri na inaridhisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujasiri huo wa Mheshimiwa Waziri, sina wasiwasi kwa nia yake aliyoitangaza ya kwenda Ubungo, ninaamini anaweza akaifanya kazi hiyo vizuri zaidi na sasa ninataka niwaombe wananchi wa Ubungo wampokee Mheshimiwa anakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika matatizo makubwa ya uhifadhi hasa yanakuja kati ya uongozi wa Wizara na Vijiji, Waziri amethibitisha hapa kwamba jitihada kubwa imechukuliwa na hivi sasa hali ni nzuri kabisa na hasa Ngorongoro ambako tofauti hizo zilikuwepo pamoja na sehemu nyingine nyingi tu. Kwa sababu huwezi kulinda wanyama kwa kutegemea Maafisa wake wa Wizara tu, ni lazima ulinzi shirikishi uwepo na ulinzi shirikishi unatoka kwenye vijiji na vijiji sasa vimefikia hatua ya kukubali kulinda. Kama ushirikiano huo upo tatizo lilikuwa ni mipaka tu, kwa hiyo, ninaamini kuwa kuna utaratibu mzuri kabisa unaowezesha wanyama wetu kuwa salama zaidi kuliko hapo ilivyokuwa siku za nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nimpongeze tu Mheshimiwa Waziri pia kwa jitihada hiyo na inatuwezesha sasa kujua kwamba, wanyama wetu wako salama, japo

si salama sana kwa sababu wewe ukiziba huku, jangili anazibua kwingine. Lakini watakapopata zana na vitendea kazi nafikiri tatizo hilo pia linaweza kuondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeandaa na kutengeneza mpango mzuri kabisa wa kuweka Wakala wa Mfuko wa Misitu. Nafikiri vitu hivi pamoja na mbegu bora, vitatusaidia sana kuwa na miti yenye ubora inayoweza kuishi katika mazingira yetu kwa wingi zaidi. Mimi ninataka nipongeze tu kwamba, mfuko huu tuutumie vizuri ili tuweze kuwa na miti mizuri inayotokana na usimamizi mzuri tutakaokuwa nao katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sera yetu, tunasema kutangaza utalii ni Kilimanjaro, Serengeti na Zanzibar. Lakini jambo la kusikitisha sana ambalo pia ninamuomba Mheshimiwa Waziri na Wizara yake waliangalie, katika utalii kuna madaraja mengi, sasa mpaka hii leo Zanzibar hakuna hoteli ya *Five Star*. Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi katika hili kuwashawishi wenzetu wa Zanzibar kule ili nako kuwa na hoteli ya *Five Star* kwa sababu kuna madaraja mengi ya watalii. Yule mtalii mwenye hamu ya kwenda Zanzibar anapoambiwa hakuna hoteli ya *Five Star* anaweza akaghairi, lakini kama sehemu zote kutakuwa na hoteli mpaka za hadhi ya *Five Star* basi tutadumisha hii kauli tunayosema, utalii ni Kilimanjaro, Serengeti na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, nami nichangie katika hoja hii ambayo ni muhimu sana kwa utalii wa Tanzania na hususani utalii wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Maliasili, pamoja na Katibu Mkuu na viongozi wote wa idara zote, kwa kufanya kazi nzuri ya kuendeleza utalii na uhifadhi na pia kwa kutengeneza bajeti nzuri. Ninapenda nimshauri Waziri kwamba aendeleze kwa haraka ule mpango wa kuunda Mamlaka ya Wanyamapori kama tulivyokubaliana hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, niwapongeze viongozi na wafanyakazi wote wa *TANAPA* pamoja na Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro, kwa kazi nzuri wanazofanya. Mashirika haya yanaongozwa na wazalendo, wafanyakazi wake wengi karibia 98% ni wazalendo na kwa kweli mashirika haya yanafanya kazi kwa faida. Mashirika mengi yamekufa, lakini haya yanafanya kazi kwa faida na hivyo yanahitaji pongezi na kuungwa mkono na Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije sasa katika hoja na nianze na Mlima Kilimanjaro. Utalii wa Kilimanjaro au tunaweza kusema Kilimanjaro ni Mkoa wa Utalii. Kilimanjaro imekuwa Mkoa wa utalii kwa sababu ya mandhari nzuri ya Mlima Kilimanjaro. Sasa tujiulize Mlima Kilimanjaro unatunzwa na kama unatuzwa watu gani wanautunza? Mlima Kilimanjaro umezungukwa na Halmashauri tano; Longido, Siha, Hai, Moshi Vijijini na Rombo. Mlima Kilimanjaro kwa miaka mitatu (3) ambayo nina kumbukumbu

nayo, mwaka 2003 -2007 ulizalisha takribani shilingi bilioni 97,000 (bilioni 97) lakini mapato waliyopata Halmashauri hizi zinazozunguka Mlima Kilimanjaro ni shilingi bilioni mbili tu kwa njia wanayosema ni njia ya huruma, njia ya ujirani mwema maana yake huyu ni jirani hivyo tunamuonea huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliwahi kuuliza swali la nyongeza hapa Bungeni kwamba, kwa nini mapato yanayopatikana kutoka Mlima Kilimanjaro, 25% isiende kwenye Halmashauri zinazozunguma Mlima huo? Lilikuwa swali la nyongeza la Swali Na.100 katika Kikao cha Kumi na Moja cha Bunge, Waziri alijibu kama ifuatavyo na ninaomba ninukuu:-

"Ni kweli kwamba kuna baadhi ya Halmashauri zinazozunguka sehemu zetu za utalii na sehemu mbalimbali za wanyamapori na wanapata percent kama hivyo na pia napenda kumuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili tutaliangalia na pia tutaona uwezekano uliopo na tutakaa nao wenyewe ili tuweze kuzungumza masuala hayo."

Mheshimiwa Naibu Spika, Kikao cha Kumi na Moja na hiki ni Kikao cha Ishirini, kikao cha mwisho, hatujawahi kukaa, wala Waziri hajawahi kukaa na mamlaka zinazohusika yaani hizo Halmashauri tano. Sasa mimi ninashauri, Mheshimiwa Waziri atimize ahadi yake na ninaomba tu Watanzania waelewe kwamba, ng'ombe kadri unavyomlisha ndivyo anavyotoa maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mlima Kilimanjaro unalishwa na wananchi wanaouzunguka na ili Mlima Kilimanjaro uweze kutoa mapato zaidi, ni lazima wale wananchi wajisikie nao wanapata faida kutokana na Mlima huo kwa maana ya ile 25% ambayo Mheshimiwa Waziri aliahidi. Mimi ninaomba asilimia hiyo ishirini na tano iende kwenye Halmashauri zinazozunguka Mlima huo ili waweze kuutunza zaidi na uweze kuzalisha zaidi. Kama mwaka 2007 kwa miaka mitatu(3) walizalisha shilingi bilioni 97, sasa wakipata hiyo *incentive* watazalisha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, katika Kikao cha Kumi na Sita, niliuliza swali kuhusu njia ya watalii ya Maua. Mheshimiwa Waziri, akaniomba nivute subira na atalifanyia kazi. Ni kweli Mheshimiwa Waziri alitembelea eneo hilo na aliahidi kwamba njia hiyo itafunguliwa. Sasa ninamwomba alieleze Bunge hili kwamba, ni lini njia hiyo itafunguliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni utalii kwa ujumla Tanzania. Wenzetu wa Kenya wanaelewa kwamba barabara ya Marangu – Tarakea iko mbioni kufunguliwa na wao wameshatengeneza barabara kutoka Emali mpaka Tarakea, wameshajenga Kituo kikubwa cha Forodha, wanajipanga kutengeneza uwanja wa ndege Holili. Wenzetu sasa wanajitayarisha kuelekea kwenye utalii wa Mlima Kilimanjaro, sisi tunajitayarisha kuvuna bila kupanda, je, sisi matayarisho yetu ni nini? Tumeshajenga barabara kutoka Tarakea - Kamwanga, barabara hiyo ndiyo Kenya wanataka kuitumia kwa ajili ya Utalii wa Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utalii ni lazima tuwe na mahoteli…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. ESTHERINA J. KILASI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuungana na wenzangu kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Nianze kwanza kwa kutoa salamu za rambirambi kwa kuondokewa na Katibu wetu mpendwa wa Wilaya Bageorge Zacharia, kwa wale wote ambao sikufanikiwa kuwaona siku ya mazishi, naomba wapokee salamu za rambirambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mengi sana ya kuchangia lakini la msingi ni moja. Labda nianze tu kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja (100%) sikusudii kutoa shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kweli kazi wanayoifanya ni nzuri sana. Kwa kipindi hiki wamebadilisha sana Taasisi na Mashirika yote ambayo yako chini yao. Ninasema hivyo kwa uhakika kwa sababu mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mashirika ya Umma, ukiona kinachofanyika Ngorongoro huwezi kuamini kwa sasa. Hali ni nzuri na uwekezaji ni mzuri. *TANAPA*, Serengeti kwa kweli kuna maajabu mazuri tu. Ninaamini tunaweza tukiweka nia na uwezo wetu. Kwa kweli, ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, niipongeze sana Serikali, nikianzia na Rais, Waziri Mkuu na Wizara husika kwa kuweza kusikiliza kilio cha wananchi wa Mbarali. Waheshimiwa Wabunge mnakumbuka mwaka 2008 tangazo la kupandisha hadhi hifadhi ya Ruaha ambayo inaunganisha na Usangu kwa jina maarufu la Ihefu. Wananchi wa Mbarali hawakuwa na tatizo lolote, walipokea vizuri kabisa tangazo hilo na walikuwa wameridhia maeneo mazuri ambayo wanafikiri walikuwa hawayahitaji sana kwa ajili ya kilimo na mifugo na serikali tulishirikiana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema hapa ni kwamba, ninaishaukuru Serikali kwa sababu sheria ile ilipotungwa ilipitishwa ikiwa na makosa makubwa sana kwa sababu vijiji vilivyokuwa vimeridhia vilikuwa saba (7) lakini vikaongezeka na kufikia 14 na imekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Mbarali na nimekuwa nikilalamika kwa muda mwingi sana hapa kwa kuchangia na kuuliza maswali. Sasa kwa mwezi uliopita nimepokea kopi ya barua ambayo imeandikwa kwa *RAS* Mkoa wa Mbeya ikiridhia vile vijiji vyote ambavyo vilikuwa vinalalamikiwa na wananchi kwamba Serikali imeridhia kuviondoa ndani ya hifadhi. Nafarijika sana na nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sio mimi tu naipongeza na Kamati ile ambayo inashughulikia chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Ndugai imeshirikiana na mimi sana kubainisha maeneo haya, kuona kweli yanahitajika kwa ajili ya kilimo. Barua ile

nimeisoma kwa makini sana na nimeona maeneo ambayo mmekubaliana na sisi, lakini ni juzi tu ambapo tumekuwa na vikao, nimeipitia na kutafakari, ninachokuomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu wewe ndio mwenye dhamana na hii Wizara ili na mimi mwenzako maana sharti mojawapo nililowekewa, Mheshimiwa Mbunge hatuna tatizo na wewe, kipindi cha tatu unaingia, lakini hakikisha kero hii inaondoka na mimi najua utaniunga mkono tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vile Vitongoji ambavyo umesema vibaki vyote vitatu, kuna Manuungu, Kijiji cha Manawala, nasema kwa sababu wewe unafahamu nini ambacho nakisema na Mwenyekiti Mheshimiwa Ndugai anajua nini nasema pale tulipofanyia mkutano, kile Kitongoji mlichokiruhusu mkasema kingine kinachofuata, kingine kinaitwa Manuungu, kiko katikati kabisa. Kwa hiyo, si busara kabisa kwamba kile kibaki, kile kiondolewe na kama vile hujafanya kitu, ninaomba hilo lirekebishwe na barua nimeileta ofisini kwako nafikiri utaielewa vizuri sana na Kijiji kile cha Manawala tumekitenga hasa hasa kwa ajili ya kufuga na kulima kizingatia mashamba yote yale muhimu ya wale wenye vijiji, liliuzwa, kwa hiyo, wananchi wamehamia kule na wamefungua mashamba makubwa na tumeweka maeneo ya ufugaji baada ya kuhamisha kwenye eneo la Ihefu**.** Kwa hiyo, hilo ninaomba sana lizingatiwe kwenye Kijiji cha Nyeregete, Kitongoji cha Magwalisi ni wale ambao wameingia ndani ya Hifadhi, ninaomba ndio waangaliwe warudi, washirikiane na wenzao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna Vijiji viwili Madundasi - Msanga ni Vijiji vikubwa vimekaliwa kwa muda mrefu na mimi naamini ukiona kwenye ramani vinaonekana viko karibu sana na Hifadhi, lakini busara zinaweza zikatumika tukahamisha tu wale ambao tunafikiri wameingia ndani ya mpaka, vile Vijiji vikaweza kubaki na watu wakaweza kuishi tu kwa amani na wakawa walinzi wazuri sana wa hiyo Hifadhi ya Taifa. Kwa hiyo, naomba hilo lizingatiwe, ile barua ambayo nimeileta ofisini kwako na ramani ya Vijiji, nafikiri ukiiona utaizingatia na unapohitimisha hapa nitafurahi sana iwapo haya maombi yetu yatajibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ombi langu kubwa kwa sababu mara nyingi tunapotoa mapendekezo, ramani zinachorwa ndio zinaletwa. Ninaomba baada ya hii Serikali kuridhia kwamba vitolewe sasa basi ile taarifa ya Kikosi Kazi ambacho uliunda, waje kule sasa washirikiane na wadau wenyewe, wananchi wanaoishi kuzunguka yale maeneo ili washirikishwe kikamilifu, kukubaliana na ile mipaka ndipo ramani ichorwe kusudi kusitokee tena mabadiliko ya kila wakati. Hilo nilitaka niliseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wananchi waliohamishwa walipata fidia, fidia zile zilikuwa na tofauti, kubwa ni ndogo sana; wengine walipata kiwango kikubwa, wengine kidogo. Ninakumbuka bajeti ya mwaka jana ilisema hapa kwamba Wizara ya Maliasili na Wizara ya Fedha, mshirikiane kutafuta pesa ili wapewe TANAPA kwa ajili ya kukamilisha malipo yale ambayo wananchi wamelalamika na sisi kwa timu ya pamoja, Madiwani na mimi Mbunge wao tuliweza kupita malalamiko yote yamefikia kama elfu moja, tulishayawasilisha sasa ni muda mrefu sana wamechukua, wananchi wanasubiri jibu, kweli tumekubaliwa kupewa au hatujakubaliwa? Lakini na mimi kama Mhasibu nafikiri ni kitu cha uhakika tu, hata ukianza tu, mtu aliyelipwa fidia elfu hamsini

kitu ambacho hakiwezekani, mtu unahama Kijiji ambacho hukupenda kuhama, hukuhama kwa ridhaa yako ulipanga ufe, uzikwe hapo lakini unalipwa elfu hamsini hata kama nyumba ingekuwa ni ya manyasi, ni ya udongo, tunafikiri kwamba fidia ile ingetakiwa iangaliwe upya. Lakini basi anzieni hata kwenye milioni moja kushuka mpaka kwenye elfu hamsini wale muwaangalie kwa nini huyu amepata milioni moja kama yale mengine yatakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi najua kuna ubinadamu, inawezekana kuna upungufu wa hapa na pale, mtu mwingine amedanganya lakini yote yangeangaliwa kwa haraka na kwa sababu kwa kipindi hiki wananchi wamesubiri sana. Tatizo lililopo wakati wanalipwa nafikiri hawakuweza kuambiwa unalipwa kwa sababu hii na hii na hii, hawakupata ile nafasi. Sasa hivi hata mimi napata shida wakisema tunalalamika tumepunjwa, ukimuuliza mwananchi umepunjwa shilingi ngapi, anakuwa hajui, kwa hiyo, wanahitaji sana elimu ya karibu ili wajue kabisa ulilipwa milioni mbili, ulitakiwa ulipwe hiki na kwa sababu hujalipwa hii, ni kwa sababu fulani. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri unapohitimisha jioni tujue mwelekeo wa Wizara, chini ya Wakala wako *TANAPA* ambaye ndiye anayeshirikiana na Halmashauri yetu ya Wilaya ya Mbarali kuona tena wananchi hawa hawaleti kilio mbele ya Serikali na tuwe walinzi. Mimi naona ile Hifadhi inachelewa kuanza kwa sababu ya migogoro hii midogo midogo, tukiimaliza hii wananchi wa Mbarali hawana tatizo, watakuwa walinzi wakubwa wa Hifadhi ya Taifa na tunaipokea kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande vilevile wa Askari sasa, umetupa yote, umeridhia kwamba hii mipaka irekebishwe, ninachokuomba basi *TANAPA* wapewe taarifa ili wawambie Askari kule kwamba maeneo yote ambayo yanasubiri kuwekewa mipaka wasiwasumbue na kuwanyanyasa wananchi wanaozunguka pale, kwa sababu bado mipaka hatujakubaliana iwe wapi. Kwa hiyo, kwa kipindi hiki uwekwe utaratibu mahsusi ambao utaondoa magomvi kati ya Askari wale wa wanyamapori na wananchi husika na nafikiri elimu ni nzuri zaidi kuliko kutumia nguvu. Sasa hawa wenzetu tumekuwa tukilalamika muda mwingi sana wanatumia sana nguvu kuliko kutumia sheria ambayo wamepewa, kuliko kutoa faini, mtu yuko radhi kupiga, kumlisha kitu chochote alichomkuta nacho, sasa hiki kinazidi kuleta uadui baina ya wananchi ambao wanazunguka Hifadhi hizo. Kwa hiyo, hilo ni jambo kwangu zito sana kwa sasa na nafikiri Waziri na watendaji wake watalifanyia kazi ili liweze kuondoa kero kwa wananchi wa Mbarali na mimi ninapokwenda sasa niondoke nikisema ile kazi mliyonituma nimeikamilisha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya utalii. Kwanza, ni *declare interest,* mimi ni mdau katika utalii. Sina mengi lakini nina machache ambayo ni maombi kwa Waziri. *KINAPA* ina mkakati wa kupunguza namba ya watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro kwa mfano kuna mkakati wa kupunguza watalii ambao wanatumia njia ambazo sio *permanent,* mfano kama njia ya Machame, kwa sasa tunapandisha

watalii 400 kwa siku na wanatarajia kuteremsha mpaka wafike 100 kwa siku. Sasa *Tour Operators* wa Moshi na Arusha wameniomba nilete haya maombi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kweli kuteremsha ile namba kutoka 400 mpaka 100 itapunguza mapato ya nchi, itapunguza ajira kwa vibarua wanaobeba mizigo na sababu wanasema kupunguza watalii ni kulinda mazingira. Mimi siamini kweli kupunguza watu kutoka 400 mpaka 100 eti tunalinda mazingira, wenzetu hata Wamarekani pamoja na kuendelea walikataa hata ku-*sign Kyoto Protocol* kwa ajili ya kulinda viwanda vyao na maisha ya watu wao. Hivi sisi Tanzania pamoja na umaskini wetu, tumefika kiwango cha kukataa watalii 400 kwa siku, kwa njia moja sasa tunazo Mjia karibu nne, tuwapunguze kutoka 400 mpaka 100, embu fikiria pato hilo litateremka kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tungeomba angalau kwa sababu mtalii mmoja lazima abebe wabeba mzigo wannne, angalau katika njia zile ambazo hazina *camp* ambazo ni *permanent*, tungeomba *KINAPA* iweke *facilities* kule Mlimani ili tusiweke vibarua wengi wa kubeba mizigo kama mahema, kama viti vya kukaa, kama meza, kama *shower*, kama choo, tunabeba mpaka vyoo vya Wazungu. Sasa kama wangeweka hizo *facilities* kule Mlimani, tungepunguza ile namba ya *Porter* ambao wanabeba mizigo, halafu tukaongeza ile namba ya Wazungu ili nchi iweze kupata pesa nyingi. Hilo ni ombi rasmi tunaliomba, mfikirie katika mkakati huo ambao mnao kwa sasa, kwa kweli utaiingiza nchi hasara kubwa na Mlima wa Kilimanjaro ndio unaotegemewa kwa kuleta *revenue* katika nchi hii kuliko *National Park* yoyote nyingine katika nchi hii, hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Moshi ndio Mji wa Mlima wa Kilimajaro, tuna kiwanja cha ndege cha pale Moshi *Airport*, mwaka jana mimi niliomba tena katika mpango wa ujirani mwema, Mheshimiwa Waziri tunaomba tusaidie kile kiwanja kiwe *repaired* kidogo tu ile *runway* ili watalii wanaoruka kutoka Nairobi waweze kuruka waje moja kwa moja. Kama hatutafanya hivyo, Kenya wanajenga kiwanja pale Holili na watalii wote sasa watarudi Kenya, watoke Holili wapande Mlima Kilimanjaro, tutakuwa tumepoteza fedha nyingi na hadhi yetu itapotea. Jamani ndugu zangu Waheshimiwa, Moshi haina kiwanda, Moshi haina chochote, ni utalii tu umebakia, sasa kama utalii utahama tena pale Moshi, uhamie Holili tutakuwa tumeuwa ule Mji wa Moshi kabisa. Mheshimiwa Waziri, naomba ombi langu na sio langu, ni ombi la watu wote wa Moshi, tusaidie kile kiwanja kitengenezwe ili watalii waweze kuruka moja kwa moja kutoka Nairobi kuja Moshi kupanda Mlima na wakitoka Moshi waweze kurudi Nairobi ambako ndio kwenye watalii wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, niliuliza swali hapa, kuhusu reli ya Mombasa kuja Moshi, nikaambiwa watalii wengi hawatoki Kenya, si kweli. *Destination* ya watalii kuja *East Africa, mostly* wanakwenda Kenya na Mombasa na ndege zinaruka moja kwa moja kutoka Ulaya zinakwenda Mombasa na watalii wengi baada ya kuchoka kuogelea wangependa kuja kuona Mlima wa Kilimanjaro na njia ambayo ni sahihi ni ile reli, hawataki kupanda mabasi yetu kwa kuwa ni hatari, wanaogopa kufa, mabasi yetu sio *safe*, reli ndio *safe* na wao watalii wamezoea reli, hawakuzoea mabasi kama huku kwetu. Kwa hiyo, mimi ningedhani tufikirie upya, wenzetu Kenya wanaweka hizi *facilities*, zimekwishafika mpaka pale Holili. Sasa kwa nini sisi tunaona tabu kuifungua ile njia na

sasa *community* ameshafungua hiyo *Common Market*. Kama tukiendelea kupoteza muda, tunapiga siasa tu, tutakuwa tunarudi nyuma badala ya kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuweka lile ombi Waheshimiwa Viongozi, naomba sana, Waheshimiwa Viongozi fungueni ile njia ya reli ya kutoka Mombasa mpaka Arusha. Watalii wengi wanaotoka pale Mombasa wangependa kusafiri na treni waje mpaka Arusha kuja kuona Mlima Kilimanjaro na kuja kuona wanyama, ni *leisure*, lakini hawapendi ku-*risk* maisha yao kupanda mabasi kutoka Mombasa mpaka Arusha. Kama kuna mtu aliwahi kusafiri kutoka Voi mpaka akaja Taveta, ile njia ni hatari, ni mbaya kabisa, ile barabara ni mbaya mno. Haifai wala mtu kuendesha gari lake. Kwa hiyo, bado naendelea kuweka lile ombi langu ili tuweze kuendeleza utalii wa Mlima wetu wa Kilimanjaro na ili wenzetu wasiweze kuchukua ile nafasi, naomba sana tufungue ile njia ya reli ili watalii waweze kutoka Mombasa waje mpaka Moshi na mizigo yetu vile vile iweze kutoka Mombasa ije mpaka Moshi au mpaka Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndio maombi yangu na sina mengine, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maombi yangu kwa Waziri. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naona muda uliobakia hatuwezi kumpa nafasi Mbunge mwingine achangie, lakini tukirudi jioni naomba wafuatao wawe wamejiandaa, atakuwa Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mheshimiwa Juma Kilimbah, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, tutaishia hapo, tutajadiliana tuone vifungu vya Wizara vimekaaje kama viko vingi basi tena tunakomea hapo, kama vitakuwa vifungu sio vigumu sana basi tutanaweza kuongeza muda kidogo tu.

Halafu jana tulikuwa tumewatangazieni kwamba zile fomu za maadili zipo, nafikiri wamewagawieni kwenye *pigeon holes*, safari hii tofauti na tunavyojaza mwezi wa Disemba kila mwaka, tunajaza nakala moja, kama utarudi basi utakuja kujaza tena, lakini unajaza nakala moja. Sasa ukishajaza fomu hizo zipelekwe chumba Na.9, jengo la Utawala. Kwa hiyo, ninasoma walivyoandika, kama wamekosea mimi nasoma yalivyoandikwa hapa, wanasema naomba watangazie Waheshimiwa Wabunge Fomu za Rasilimali na Madeni zirejeshwe chumba namba 9, jengo la Utawala. Kama kuna mabadiliko basi tutatangaza tena baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo linguine, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunarudia tena, niliwataja Waheshimiwa watakaoanza kuchangia, ni makusudio yetu kwamba tufikie mpaka saa 12

halafu tuweze kumpa Waziri aanze kujibu baadhi ya hoja. Kwa hiyo, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa James Lembeli, atafuatiwa na Mheshimiwa Oscar Mukasa, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Killimbah na Mheshimiwa Malangalila awe tayari. Mheshimiwa James Lembeli.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kwanza kuchangia hoja iliyo mbele yetu jioni ya leo, hoja ya Maliasili na Utalii. Napenda nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kahama kwa kunipa heshima kubwa ya kuwatumikia ndani ya jengo hili katika kipindi cha takribani minne na nusu iliyopita. Bado niko imara, ninaamini na wao bado wananihitaji, wananipenda na mimi nawapenda. Niko tayari kushirikiana nao katika miaka mitano mingine ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu wake, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote wa Idara, Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii, kwa kazi nzuri ambayo kwa kweli kwa muda mrefu sasa imelipatia Taifa letu heshima kubwa duniani kote. Kutokana na ambacho ninataka kuchangia leo, naomba ni-*declare interest*, *mimi* kabla ya kuingia ndani ya Bunge hili, nilikuwa mtumishi wa Hifadhi ya Taifa kwa zaidi ya miaka 12. Mchango ambao ninautoa leo, unajikita katika suala zima la uamuzi ambao umefanywa na Serikali hivi karibu wa kujenga barabara ya lami kutoka Mto wa Mbu kupita Serengeti hadi Mugumu. Nakushukuru umeshalitolea maagizo suala hili. Lakini nitakuwa sijaitendea haki nafsi yangu nisiposema yale ambayo tayari nilikwishaazimia kuyazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu licha ya kuwa masikini, lakini ina utajiri mkubwa na inasifika duniani kote kwa Sera yake nzuri ya uhifadhi. Nchi yetu Tanzania inasifika sana duniani kwa kuwa na vivutio vya kipekee ambavyo havipatikani sehemu yoyote Barani Afrika na kwingineko duniani. Vivutio hivyo ni pamoja na Mlima Kilimanjaro kutaja vichache, Hifadhi ya Serengeti, Ngorongoro na ndio maana kauli mbiu ya Kitaifa ya kutangaza utalii wa nchi hii ni Tanzania nchi ya Kilimanjaro, Serengeti na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, kauli mbiu hii haitakuwa na maana tena katika miaka miwili, mitatu ijayo pale barabara hii inayokusudiwa kujengwa itakapokuwa imeanza kujengwa. Kujengwa kwa barabara hii kwa sababu zozote zile ambazo zinatolewa, kutaiua kabisa Serengeti. *Eco-system* ya Serengeti itakuwa imesambaratika na ndio itakuwa mwisho wa Tanzania kujivuna kiutalii duniani maana Kilimanjaro nayo itakuwa haina tena theluji na Ngorongoro kama inavyofahamika hivi sasa imezongwa na mambo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kujengwa kwa barabara katikati ya Serengeti, madhara yake ni makubwa kulikoni ambayo tunayatarajia. Madhara hayo sio tu yatabadilisha *eco-system* lakini pia yataongeza ujangili wa hali ya juu. Hata zoezi la juzi la ku-*introduce* upya Faru ndani ya Serengeti, litakuwa halina maana. Iko mifano mingi, mimea ambayo siyo ya asili, itaingizwa ndani ya hifadhi kupitia matairi ya malori makubwa na ujangili utafanywa na watu wa malori makubwa. Tunaona Mikumi na juzi

mimi nilikuwepo Doha, moja ya sababu ambazo hoja ya Tanzania ilikataliwa ni kwamba *eco-system* ya *Mikumi Selous* ndiko kumeshamiri ujambazi na ujangili wa Tembo. Ukipita leo hii Mikumi ndani ya Hifadhi utakuta malori makubwa ya zaidi ya tani 50, 60 yako pale lakini huwezi kujua wanachokifanya, wanafika ndani mle wanaharibu gari, lakini kumbe wana jambo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya lami kupita ndani ya Hifadhi, siyo tu itasababisha vifo vya wanyama na binadamu lakini barabara hii itasababisha kutoweka kabisa kwa Nyumbu ndani ya Hifadhi ya Serengeti. Mimi najiuliza kama tunashindwa kudhibiti ajali zinazotokea katika barabara zetu hapa nchini, nani atafanya kazi ya kuongoza sasa wanyama wapite na baadaye magari yapite?

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tuna matatizo, matatizo ya kuwa na Sera nzuri sana, mipango mizuri sana na kufanya mambo ambayo nchi nyingine wameshindwa kuyafanya, mojawapo ni uhifadhi. Lakini Watanzania tumekuwa mahodari wakubwa kwa kusambaratisha mambo mazuri ambayo tumeyajenga sisi wenyewe. Hifadhi ya Serengeti imekuwa ni kioo cha nchi yetu, leo ninasikitika kusema watu ambao wamepewa majukumu ya kushauri viongozi katika masuala mbalimbali hawawatendei haki viongozi. Uamuzi huu, kwa hakika sidhani wenye majukumu ya kushauri walishauri hivyo na mimi, nasikitikia sana hifadhi za Taifa, najua na ninaamini kwamba jambo hili wanashinikizwa, siasa hapa inatumika kuimaliza Serengeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hayo kwa sababu tumekuwa na mambo mazuri sana nchi hii, Serikali ya Awamu ya Kwanza ilijenga viwanda vingi vya nguo, viatu, vya ngozi leo hii hakuna hata kiwanda kimoja kinaendelea, tutawaambia nini watoto wetu? Halafu tumekazana tulete wawekezaji, ni jambo la ajabu sana. Sasa tunaiua Serengeti kidogo kidogo, mimi jana nilikuwa nasoma *internat*, zaidi ya watu 2000 duniani wame-*petition* kwa Serikali ya Tanzania, isithubutu, isijaribu kujenga hiyo barabara, Watanzania wenyewe hapa tunashangilia, tunasherehekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana katika kikao hiki hiki, niliuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu barabara hii. Nimetoka nje, Kiongozi alikaribia kunipiga ngumi kwa hoja yangu hiyo lakini mimi nasema historia lazima ikumbuke watu wanaotetea maslahi ya nchi.

NAIBU SPIKA: Kiongozi maana yake utasema ni Waziri Mkuu anataka kukupiga ngumi, hapana, Kiongozi labda mwanasiasa mwenzako.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na muda umeisha, *but we have to give Serengeti a chance to survive.* Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu kwa Wizara ya Maliasili na Utalii na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia wote afya njema kwamba tunaweza kufanya shughuli hii leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, kwa mara nyingine, niwashukuru na kuwapongeza wananchi wa Biharamulo Magharibi, kwa ushirikiano na uvumilivu walioonesha kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja, kwa ushirikiano mkubwa walionipa na napenda niwatamkie rasmi kwamba mwishoni mwa mwezi huu, nitafika Biharamulo kuchukua fomu, kuomba ridhaa ya Chama cha Mapinduzi ili niweze kupeperusha bendera na nirudi kama Mbunge wao ili nikidhi haja ya kiu yao kubwa walionayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, pia napenda niishukuru Wizara ya Maliasili na Utalii, Waziri, Naibu Waziri na Timu yake nzima kwa kazi kubwa wanayofanya na kwa ujumla Serikali nzima ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi inayoendelea. Lakini pia niwashukuru wenzangu wote wasemaji wa leo waliotangulia. Tumesikia mambo mengi sana ya kisera ambayo wameyazungumza kama ushauri kwa Wizara ya Maliasili na Utalii lakini kwa sababu mahsusi kabisa, mimi nitalazimika leo kutokuzungumzia jambo la kisera. Nitazungumzia jambo linalohusu eneo maalum kwenye Jimbo langu la Biharamulo Magharibi, Kata ya Nyakaura ambako pale kwa kweli tuna tatizo kubwa. Nitalieleza kama ifuatavyo. Ninapenda Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wanasikilize kwa umakini wote kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukipata fursa ya kufika Kata ya Nyakahura, Wilaya ya Biharamulo, Kijiji chochote pale Nyabugombe, Nyakaura ya Zamani na vinginevyo, lugha pekee ambayo wananchi wa pale wanaweza kukuelewa, mkakaa mkazungumza, ni namna gani tunaweza kukabiliana na Ndovu. Hawa wanyama wanatoka kwenye hifadhi, wanakwenda kwenye makazi ya watu, wanaharibu mazao na hili limekuwa suala ni kama la kudumu sasa, miaka nenda rudi, pamoja na jitihada nyingi kabisa ambazo zinafanyika, lakini hazizai matunda. Kwa hiyo, lugha pekee wanayoelewa wananchi wa Nyakaura leo wanazungumzia kuhusu Tembo ama Ndovu wengine wanaita hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano, nilifanya ziara na kiongozi mmoja wa Mkoa wa Chama cha Mapinduzi pale, basi akafika pale, ana ajenda nzuri tu, anataka kuzungumzia kilimo, anataka kuzungumzia michango ya elimu, anaendelea na hotuba yake wananchi wanamwambia Mzee Tembo, mpaka akauliza mimi Tembo? Wakamwambia Tembo, hatutaki habari nyingine yoyote. Kwa hiyo, ndiyo lugha pekee ambayo wananchi wa Nyakaura wanaielewa. Kwa kweli hali ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyozungumza, jana wananchi wa Vitongoji vya Chamakaza na Kibamba wa Kijiji cha Nyabugombe walikesha wanapambana na Tembo kwenye mashamba yao kujaribu kufukuza ingawa jitihada hazizai matunda

mpaka asubuhi na inafikia hatua sasa mpaka watoto wa shule za msingi kwa kweli mahudhurio yao shuleni yanaanza kuporomoka kwa sababu si rahisi wewe mzazi ukamruhusu mtoto wako mwenye umri wa miaka 10, 12 kwenda shule wakati una uhakika Tembo wanamaliza mkutano kijijini saa tatu asubuhi, ndio wanaondoka kurudi kwenye hifadhi. Kwa hiyo, hali kule ni mbaya na lugha pekee ambayo wananchi wa Nyakaura na mimi Mbunge wao tunaweza kuielewa sasa hivi siyo kujadili mambo ya kisera, kwanza tutatue tatizo la Tembo kuingia kwenye makazi Nyakaura.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua jitihada ambazo zimekuwepo kuanzia ngazi ya Halmashauri, Mkuu wa Wilaya, wanakuwa wanafanya jitihada, Mkuu wa Mkoa, Mzee Babu nampongeza sana. Mara kadhaa mimi nimelazimika kumpigia simu saa saba usiku kwamba Tembo wamevamia na zaidi ya mara mbili amefanya jitihada analeta vikosi vya kusaidia kutoka Mwanza, vinakwenda vinasaidia kwa siku moja, wakiondoka Tembo wanaendelea na mikutano yao kama kawaida. Lakini pia nimeshapata fursa ya kuzungumza na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, nikapata hata nafasi ya kuzungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu na mwezi wa tano kuna jitihada zilifanyika pale, Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru lakini kwa bahati mbaya jitihada hizo hazizai matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niongelee kidogo kwa nini jitihada hizi hazizai matunda. Jitihada za ngazi ya Wilaya ni wazi hazizai matunda kwa sababu tatizo ni sugu, ni la muda mrefu, sio tukio la mara moja. Kwa hiyo, ni wazi kwa Halmashauri kama ile ambayo hata vianzo vyake vya mapato ni vidogo, haiwezi kuwa na uwezo wa kushughulika na tatizo la namna hii ambalo ni la muda mrefu, ikamudu gharama hizo. Hata ukiangalia kwenye ukurasa wa 62 wa hotuba yetu pale ambapo kuna kielelezo kinachosema kwamba fedha zilizotumwa kwenye Halmashauri za Wilaya, asilimia 25 kutokana na uwindaji wa kitalii, Wilaya yetu ya Biharamulo imepata wastani wa shilingi milioni mbili kwa mwaka. Kwa hiyo, ukiangalia kipato ambacho Halmashauri inakipata kutokana na shughuli zinazoendelea pale za utalii ukilinganisha na hiyo kazi ambayo unaweza kuibebesha Halmashauri hiyo ipambane na wanyama hawa, kunakuwa hakuna biashara nzuri kwa maana ya kipato cha Halmashauri pale. Kwa hiyo, Halmashauri haiwezi kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngazi ya Mkoa ni hivyo hivyo, hili suala lingekuwa ni ajali ya mara moja, mara mbili, ungesema ngazi ya Mkoa wanaweza wakamudu lakini hili suala limekuwa sugu. Ni la muda mrefu, limekuwa sehemu ya maisha ya wananchi wa Nyakaura. Sasa hivi imefikia hatua wakati wananchi wa sehemu zingine nchini wanaongelea ulinzi shirikishi kuungana na ili kupambana na uhalifu wa aina nyingine, wananchi wa Nyakaura wanapanga zamu ya kwenda kulinda mashamba yao kupambana na Tembo hao. Kwa hiyo, hali ni mbaya na nasikitika kwamba nadhani moja ya tatizo linalotukabili pale ni kwamba kwa ngazi ya Serikali Kuu inawezekana hatujajua uzito hasa wa lile tatizo. Tunalichukulia kama matukio mengine Tembo au wanyama wanakwenda wanafanya uharibifu, tunakwenda pale tunafanya fidia tunaondoka lakini kwa kesi ya Nyakaura Biharamulo hili ni tatizo sugu linahitaji kwenda pale kuliangalia kwa upana ili tulitatue kwa upana wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha zaidi pamoja na usugu wa tatizo hili ukiangalia ukurasa wa 14 pale ambapo hotuba hii ya Waziri inaongelea Wilaya ambazo zimepata fidia kutokana na uharibifu wa wanyama, Biharamulo ambayo tatizo hili ni sugu haikuorodheshwa pale. Kwa hiyo, sisi ni tatizo ndani ya tatizo. Tatizo linasababishwa, lakini pale anapokuja hata masuluhisho yale madogo madogo, tunasahaulika. Kwa hiyo, namwaomba Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, hili suala siyo ajali kwa Biharamulo, kama ambavyo ukiangalia ukurasa huo wa 13 na 14 yale maudhui ya ulinzi wa mali na maisha ya wananchi, ukiangalia *paragraph* ile, maudhui yake ni kwamba Wizara inatambua kwamba katika shughuli zao zipo ajali zinaweza kutokea, wanyama wakaingia kwa wananchi lakini kwa Biharamulo sisi hatuhusiki sana hapo kwa sababu siyo ajali ni suala la kawaida sasa. Ndiyo maisha ya wananchi wa Nyakaura. Sasa hivi pale huwezi kuzungumzia kilimo, huwezi kuzungumzia miradi ya maendeleo, maji na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru, ninaomba kusikia majibu ya kina kabisa wakati tumekaa kama Kamati tuone ni namna gani sasa suala hili linakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii. Awali ya yote, nashukuru kwa Mwenyezi Mungu, nimepata fursa hii muhimu na jioni ya saa hii ili kuweza kutoa mchango wangu muhimu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo adha, nimpongeze Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri mwenye dhamana, rafiki yangu Mheshimiwa Ezekiel Maige, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, niungane na wazungumzaji waliopita, nami nitumie fursa yangu kuweza kutoa shukrani tu kwa wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa namna wanavyonionyesha ushirikiano kwa kazi nzuri tuliyoifanya kwa kipindi cha miaka mitano na kama nilivyosema hata kipindi kilichopita kwamba kwa ushirikiano ambao wamenionyesha na imani ambayo wamenionyesha na siku zote Waswahili husema, imani huzaa imani, kwa sababu kazi nzuri tumefanya kwa ushirikiano na Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo, nina uhakika kabisa kwamba katika kipindi hiki kijacho, watanirejesha na nitafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mchana nimeelezwa kwamba wapo wengine wanazungukazunguka, lakini ninachotaka kusema, Kanzu ya Ijumaa hufuliwa tangu siku ya Jumatano, Alhamisi ni maandalizi, Ijumaa inavaliwa kwenda Msikitini. Pia Waswahili wanasema ng’ombe unayetaka kumpeleka mnadani huwezi kumnenepesha siku ya mnada, kwa hiyo, huwa ni maandalizi ya muda mrefu. Kwa hiyo, katika uhakika huo,

ninaamini kabisa watu wa Iramba Magharibi wanaelewa juhudi zangu na kazi ambayo nimeifanya kwa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika mada yenyewe, ninachotaka kusema ni katika mambo yaliyo muhimu na hivi sasa tulikuwa tunalia ufinyu wa bajeti, tukasema bajeti ina upungufu wa takribani trilioni moja. Lakini nataka nieleze katika eneo ambalo naliona, ni nyeti na ambalo tunaweza tukapata mapato mengi na hasa tunaweza tukaja tukajiendesha kwa kutumia hata mapato yake. Ninayo mifano baadhi ya nchi zinatumia sekta moja tu inawezekana ikawa ni utalii na nyingine labda sekta ya anga, unakuta nchi inaendelea na inafanya shughuli zake za kimaendeleo bila matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachotaka kusema ni kwamba sisi pamoja na ukubwa wa nchi tuliyonayo na maeneo mbalimbali ya nchi yetu yanayohusiana na masuala ya utalii, lakini utakuta tumeelekeza macho katika maeneo machache sana. Tumeelekeza macho kwenye mbuga za wanyama, tumeelekeza macho kwenye Mlima Kilimanjaro, tumeelekeza macho kwenye utalii wa hoteli, hasa tukiangalia zile hoteli zenye nyota tatu hadi nyota tano. Niliwahi kusema, nafikiri ilikuwa ni mwaka 2008 na nikaongelea kuhusiana na fursa ambazo zinaachwa, ambazo pengine hizi zingefanyiwa kazi, ninaamini kabisa tungeweza kuongeza mapato na tungekuwa na hali njema na hata Taifa lingeweza kupiga hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni utalii wa bahari, fukwe tulizonazo wewe utakuwa shahidi, mimi ninataka nitoe mfano mmoja, mwaka jana niliwahi kutembelea nchi ya Vietnam na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, ndio ulikuwa kiongozi wetu. Katika msafara huo tuliokwenda, tulipelekwa katika kisiwa kimoja kinaitwa *Halong Bay,* kisiwa hiki ni sehemu tu ambayo iko katika eneo la Vietnam, lakini shughuli za utalii zinazofanyika hapo, wewe mwenyewe ulijionea, ni shughuli kubwa sana na mapato mengi sana ya Serikali yanaingizwa kupitia kisiwa hicho. Huo ni mfano mzuri, pale kuna maeneo ambayo yapo katika kisiwa hicho ambayo yanatumika kama utalii. Ndani ya kisiwa hicho kuna maeneo ya mawe ambayo yapo, yapo maeneo mazuri ambayo wameweza kuyaendeleza wao wenyewe kama Serikali, lakini watalii wanafika maelfu kwa maelfu katika eneo hilo na wanakwenda kujionea hali ya utalii na wanaacha mapato ya Serikali katika eneo la kisiwa hicho cha *Halong Bay.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nilikuwa nataka tu niseme, sisi tuna maeneo kama hayo na yako hapa kandokando katika Bahari ya Hindi, Dar-es-Salaam. Tunavyo visiwa vya aina hiyo, lakini ni kwa jinsi gani tunavitumia visiwa hivyo kuweza kutuletea mapato? Visiwa hivi tumeviacha na sasa pengine vinaweza vikaja vikageuzwa vikawa ni sehemu ya uhalifu. Mimi naiomba sana Serikali, kwanza mngeweza kwenda kujifunza huko, muende Vietnam, muende *Halong* na bahati nzuri niliwahi kwenda kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na nikamueleza suala hili, ili mkajifunze na tujionee kwamba tunaweza tukafanya *transformation* gani hapa katika visiwa vyetu tulivyonavyo ili sasa na sisi tuweze kuwa tunajipatia mapato na tusitegemee tu maeneo ambayo nimeyataja.

Sasa hivi kila tukitaka kuzungumza utalii, tunakimbilia Serengeti, tukizungumza utalii Mikumi, tukizungumza utalii tunakimbilia Kilimanjaro na nakadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika eneo la Jimbo langu. Tatizo lingine tulilonalo ambalo ninaliona ni suala hili la utalii ambalo ninalizungumzia, limekuwa ni la eneo fulani. Lakini tunafanya utafiti kwa kiwango gani wa maeneo ambayo yanaweza yakawavutia watalii na wakaja wakaona mambo ya tamaduni na mambo mbalimbali yanayohusu makabila ya nchi yetu? Mfano mzuri ni sisi tuna eneo katika kijiji cha Kisharita, Kata ya Kinambanda, makazi yaliyokuwa ya Mtemi Shulwa. Haya makazi yanaeleza historia ya Mnyiramba, hasa utawala wa Kinyiramba jinsi ulivyo. Pengine watalii wangependa sana kuja na labda si kuja katika eneo fulani tu, wanapofika wakaulizwa kwamba mngependa muende katika eneo gani, wanaweza kuja pale wakajifunza sana. Lakini hata sina hakika kama hilo eneo lipo katika kumbukumbu zao, hata sina hakika kama Wizara ya Utamaduni inalijua eneo hilo, lakini ni eneo nyeti sana na ninaona ni eneo bora ambalo mnatakiwa mlijue na mliweke katika kumbukumbu ili tuweze kuliendeleza na tusiliache likipotea hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Boma la Mjerumani la Mkalama. Boma la Mjerumani la Mkalama, ni boma maarufu sana, ni moja ya maboma yaliyokuwa ni ngome za Mjerumani. Lakini boma lile kwa kadiri ya hali inavyokwenda linaendelea kupoteza hali yake. Ninaishukuru Serikali juzi mmetupatia Wilaya nyingine ya Mkalama na afadhali mmeienzi hiyo Mkalama lakini siamini kwamba Mkalama kwa sababu ni Makao Makuu ya Wilaya tutakapokwenda kuweka kule, hayatakuwa pale Mkalama penyewe, Makao Makuu ya Wilaya yatakuwa yapo Nduguti, sasa tatizo litakalokuja ni kwamba ile Mkalama na lile Boma lake litaendelea kupotea taratibu na baada ya miaka fulani inawezekana ikabakia jina na isijulikane katika historia kwamba tulikuwa tuna boma la Mkalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Hii habari ya Vietnam, Mheshimiwa Waziri, nilishawahi kukueleza yaani unavyoona yanajaa mabasi Ubungo, basi ni mabasi yamepeleka watalii na meli za kutembeza watalii kwenye bahari basi ziko vilevile. Ni mahali ambapo panapendeza sana, kama sio ninyi basi hata wataalamu wenu wanaweza wakaenda. Nashukuru sana.

Tunaendelea, Mheshimiwa Benito Malangalila, atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Bura.

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie hoja ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimeisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nimeielewa vizuri. Lakini nilikuwa na maswali machache juu ya bei ya misitu ya Serikali. Miaka mingi sana nimekuwa nikiitaka Wizara hii ijaribu kupunguza bei ya

misitu yake kwa sababu, ni kweli kwamba bei ya misitu ya Serikali iko juu sana na kwa sababu Serikali ndio ambayo ina mashamba makubwa na ya kutegemewa na wananchi, inapokuwa yenyewe imepandisha bei yake ni dhahiri kwamba bei ya mbao katika nchi inakuwa ni kubwa. Niliwahi kusema na kuuliza swali ndani ya Bunge hili, kwamba iweje Serikali iweke *VAT* kwenye miti iliyosimama? Kwa bahati mbaya sana sikupata jibu la swali langu hili, lakini natarajia leo wakati wa *wingind up* Mheshimiwa Waziri, atatupa jibu la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia bei ya misitu, hususan *Sao Hill, Sao Hill* tunazalisha karibu 60% ya *soft wood* yote inayouzwa hapa Tanzania na pia niliwahi kuzungumza ndani ya jengo hili kwamba pale Mafinga, tulikuwa tunanunua mbao kutoka Malawi, ilikuwa ni rahisi zaidi kuliko mbao kutoka shamba letu lile la *Sao Hill*. Kitu ambacho kimsingi hakikuwa kizuri na ninafurahi kwamba Serikali ilikwenda kule Malawi ikafanya uchunguzi, lakini hatujapata matokeo ya uchunguzi huo kwa sababu bei ya mbao katika bei ya msitu pale *Sao Hill* bado ni kubwa na wananchi wa Mufindi na wananchi wa Tanzania kwa ujumla wake, tunashindwa kununua msitu ule kwa sababu ya gharama yake kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona hapa kuna kitu kinaitwa Sera ya Misitu, mimi sielewi hii sera inazungumzia mambo gani, kwa sababu wakati Serikali inapandisha bei ya misitu haikuja sera. Nakumbuka nilipiga kelele sana ndani ya Bunge hili kwamba kwa hakika bei ya ule msitu ilikuwa inatufilisi wavunaji wa msitu. Maana ukinunua msitu, ukipasua mbao zako zile, kwanza haziuziki na kwa sababu haziuziki, mvunaji unapata hasara na si hivyo tu, hata Watanzania wanashindwa kupauwa nyumba zao kwa sababu ya bei ya mbao kuwa kubwa. Niliwahi kuzungumza ndani ya Bunge hili kwamba iwapo mjenzi wa nyumba anashindwa kununua ubao, itakuwaje bei ya bati?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, kwa uchungu kabisa, nataka kuishauri Wizara hii ya Maliasili na Utalii, iwaonee huruma Watanzania. Taifa letu ni moja kati ya mataifa maskini, tuwaonee huruma Watanzania ambao dunia nzima inajua kwamba ni maskini, ili angalau na wao waweze kujenga nyumba zao. Maana unaposema maisha bora kwa kila Mtanzania, mimi ninaamini moja ya vitu ambavyo ni muhimu ni kuwa na nyumba bora. Jambo hili ninalisema kwa uchungu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba kuna kuchakata mbao, ni kweli sisi Mufindi kama nilivyosema tunazalisha 60% ya mbao laini na nimeshukuru kwamba anasema pale Mafinga kuna utaratibu wa kuwafundisha wavunaji wa mbao wachakate mbao zao. Inatia uchungu sana ukiona malori yamechukua ma-tani kwa ma-tani ya mbao zinakwenda Dar-es-Salaam, ujue kwamba ile ni *labour,* ni kazi ambayo ilikuwa ifanywe na wananchi wa Mufindi wenyewe. Ubao uliochakatwa ni tofauti kabisa na ubao *two by six, two by four,* maana yake ni kwamba unapeleka kazi Dar-es-Salaam, unapeleka kazi sehemu nyingine ya Mufindi. Kwa hiyo, ninapenda kuitaka Serikali isisitize suala la uchakataji wa mbao, isisitize suala la kuwa na viwanda vya mbao Mufindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua siku moja nimekwenda Dar-es-Salaam, kuna duka moja wanauza fanicha za *soft wood* zinatoka Afrika ya Kusini, zingine milioni tatu, zingine milioni nne, kwa nini sisi Tanzania kama Taifa, tusiwe na viwanda vya namna ile? Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba Wizara hii imenielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni misitu ya asili, *natural resources.* Kule Mufindi sisi, katika ile Kata ya Luhunga tuna msitu mkubwa sana wa asili na tunautunza. Kwa miaka mingi huwa hatuchomi moto, tunautunza wenyewe, pale kuna tatizo moja kwamba, wale watu walioajiriwa kutunza ule msitu hawalipwi, wakati katika maeneo mengine watu wakiajiriwa na Serikali kutunza misitu ya asili wanalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna msitu mkubwa sana wa asili kule Ihwamasa. Juzi niliuliza swali hapa la Kihanga, Kihanga ni msitu wa kupandwa lakini Ihwamasa ni msitu wa asili. Sasa ninarudia tena kuitaka Wizara ya Maliasili na Utalii, itekeleze jibu lake kwamba itakwenda Kihanga na pia itakwenda Ihwamasa, kwenda kuzungumza kwenye mkutano wa hadhara, ili kwamba jibu la kweli na la mwisho lipatikane mahali pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nitalisema kwa haraka, ni hewa ukaa. Nimesoma hapa, Serikali au Wizara hii ya Maliasili, imeanzisha utaratibu wa kutoa miche kwa wananchi. Wanasema wametoa miche mia sita, miche 600 ni kitu gani? Mbona ni kitu kidogo sana. Mimi ningeshauri katika jambo hili katika kushirikisha jamii, Wizara ya Maliasili iende ikasajili watu wote wenye misitu katika maeneo yanayojulikana ni maarufu kwa ulimaji wa miti. Niliwahi kusema mimi nina zaidi ya heka 200 nimepanda miti, mwaka huu nimepanda zaidi ya ekari 15 za miti na mwaka huu ninapanga kupanda zaidi ya heka 30; sasa *what is 600?* Ni kitu kidogo mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, ninazo fununu kwamba mnataka kukodisha ule msitu wa *Sao Hill* kwa miaka 99; mimi sikubali. Miaka minne au mitano hivi iliyopita, niliwahi kukataa Wizara ya Maliasili kuuza mashamba matatu katika manne ya ule msitu wa *Sao Hill* na hili ninalikataa pia. Sisi tuliitoa ile ardhi bure kwa Serikali, hatukulipwa hata senti 50, sasa ni kwa nini ikodishe ile ardhi ya *Sao Hill,* zaidi ya hekta 5000 kwa mwekezaji? Hii hatukubaliani nayo kabisa, kama mmeichoka hiyo ardhi, turudishieni. Katika miaka mingi ambayo tumekaa, tumezuiwa kupanda miti, sasa ni kwa nini mkodishe miaka 99. Wakati ule Wakoloni walichukua *Rukbont* wakapanda chai miaka 99, sasa hiyo miaka 99 sijui atakuja kuchukua nani? Kwa hili, watu wa Mufindi tunasema kwamba hatukubaliani na kukodisha hilo shamba, sisi tuliitoa ardhi yetu kwa Serikali, tunajua ni mali ya Serikali na tunajua itaendelea kuwa ni mali ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndio kauli ya watu wa Mufindi. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Lakini kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa uhai na kwa afya njema aliyonijalia na pia niwashukuru sana wanawake wa Dodoma, kwa ushirikiano ambao wamenipa kwa kipindi chote nilichokuwa Mbunge na nina imani kwamba wataendelea kunipa ushirikiano huo katika kipindi hiki kilichobaki na hata kwa kipindi kinachofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze pia kwa kuwapongeza sana watumishi pamoja na uongozi wa Mashirika haya ambayo ni ya hifadhi na ambayo yanashughulika na mambo ya utalii. Tunaona kazi kubwa wanazozifanya katika nchi yetu. Shirika la *TANAPA* limefanya kazi kubwa na linaendelea kufanya kazi kubwa. Shirika la Hifadhi ya Ngorongoro wanaendelea kufanya kazi kubwa, Sekta ya Misitu, Sekta ya Nyuki, Sekta ya Wanyamapori, wanaendelea kufanya kazi kubwa katika nchi yetu na ndio maana bado tunapata wageni wengi ndani ya nchi yetu kutokana na kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na kazi nyingi wanazozifanya za kuhakikisha kwamba watalii wanaoingia nchini wako salama na wanatoka katika nchi yetu wakiwa salama, bado wameshiriki katika kuchangia miradi mbalimbali. Wanajenga shule, wanajenga mabwawa, zahanati, wamefanya mambo mengi ambayo kwa kweli yanahitaji kupongezwa. Mimi ninawapongeza sana kwa uendelezaji wa maendeleo ya jamii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lakini pamoja na yote hayo, kuna changamoto ambazo wanakumbana nazo. Kuongezeka kwa watu katika maeneo ya hifadhi, kumeleta changamoto sana kwa mashirika haya ambayo yanashughulika na hifadhi na yanayoshughulika na mambo ya utalii. Watu wameongezeka, wanaingilia mipaka ya hifadhi na kuongezeka kwa watu kumeleta migogoro mingi sana kwa mashirika haya. Mifuko ya kuhifadhi wanyamapori, wanahangaika, wana migogoro na wananchi katika baadhi ya maeneo, *TANAPA* wana migogoro na wananchi, Ngorongoro wana migogoro na wananchi, hii ni kutokana na wananchi kuongezeka kwa kasi bila kujali kwamba kuna mipaka iliyowekwa kuhusu hifadhi.

Lakini pamoja na hayo, bado kuna mavamizi katika mapori yetu, wanavamia mapori na hasa wengine wanatoka nchi za jirani wanavamia mapori yetu wamejenga humo ndani lakini mashirika haya na hata Wizara kwa ujumla hawana pesa za kutosha kulinda mapori hayo, hawana uwezo wa kuajiri watumishi wetu, na hata kwa silaha hawana uwezo wa kununua silaha za kutosheleza mahitaji kwa ajili ya ulinzi wa mapori.

Kwa hiyo, bado kuna haja ya kuongeza pesa kwa Wizara ya Maliasili na utalii kwa ajili ya kupata watumishi wa kutosha kulinda hifadhi zetu. Hifadhi haiwezi kulindwa

bila watumishi. Ukitoka wanakoishi watumishi mpaka katikati ya pori huko unaweza ukakuta ni kilomita 80 na Afisa anayehusika hana hata baiskeli, na nyumba anayolala ni nyumba ya ajabu, wengine wana-*share* nyumba wakati wana familia. Mimi nimewahi kutembelea pori la *Selous,* kwa kweli niliogopa wafanyakazi wa Wizara ya Maliasili na hasa wanaolinda kule kwenye mapori yetu wanatakiwa jamani tuwajali, mishahara ni midogo sana ukilinganisha na kazi wanazofanya wale watu. Wale wanakaa miezi hajaona lami, hajaona taa za umeme, wanakaa huko ndani kwa shida kweli! Kuna haja ya kuangalia namna ya kuwaongezea hawa watu mishahara, kuangalia namna ya kuwawezesha kuishi japo kama binadamu na kama wafanyakazi wa Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado mashirika yetu haya yanayoshughulika na mambo ya utalii na mambo ya hifadhi wanatakiwa kupeleka asilimia kumi ya bajeti yao hazina. Pamoja na mapungufu hayo yote waliyonayo, lakini bado tunawataka wapeleke asilimia kumi ya bajeti yao Hazina. Lakini tukumbuke kwamba mashirika haya ndiyo yanayoshughulika na kutengeneza barabara za hifadhi, kwa sababu Wizara ya Miundombinu haitengenezi barabara ndani ya hifadhi, ni haya mashirika. Kwa hiyo, wana kazi kubwa, wana barabara zaidi ya kilomita 1000. Ukiangalia Serengeti, Kamati yetu ilizunguka Serengeti, ni mwendo wa masaa mawili ukitoka katikati ya pori mpaka mpakani mwa Arusha -Tanzania na Kenya, mnatembea mwenendo mrefu sana masaa mawili, saa moja na nusu na gari linakwenda mwendo wa kasi. Kwa hiyo, wanahitaji pesa kwa ajili ya kutengeneza miundombinu kwa ajili ya kuwalinda watalii wetu kukagua hoteli na kadhalika.

Kwa hiyo, mimi nadhani ifike wakati tuangalie: Je, kuna haja ya shirika la *TANAPA* na hifadhi ya Ngorongoro kupeleka asilimia kumi ya bajeti yao hazina au tuwaachie hizi pesa ziwasaidie kujenga miundombinu katika hifadhi zetu ili watalii waendelee kufaidi na sisi wenyewe tuendelee kufaidi na sisi wenyewe tuendelee kufaidi matunda ya nchi yetu.

Lakini pia tujue kwamba asilimia kumi hii itakapopelekwa Hazina inaweza kuua *morale* kabisa ya wafanyakazi. Wafanyakazi hawa wanafanya kazi masaa mengi. Tulipokwenda kule tuliambiwa kwamba hawana muda wa saa za kazi. Kwa hiyo, pesa hizo kidogo wanazozipata zinawasaidia pia katika kuwapa motisha kidogo hao wafanyakazi. Lakini pia ukiangalia sekta au Mfuko wa hifadhi ya wanyamapori kama nilivyosema kwamba wafanyakazi wa kule wanafanya kazi katika hali ngumu sana na kwa sababu Wizara haina pesa za kutosha, wengine wamekaa katika vituo vyao kwa muda wa miaka 30 hawezi kuhamishwa kwa sababu Serikali haina pesa. Ninaomba hili lifikiriwe na lichukuliwe hatua za haraka ili kuwasaidia hawa wenzetu ambao wako katika maeneo yenye matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo, pia Halmashauri zetu zimefaidika. Nimesoma katika hotuba ya Waziri kwamba asilimia 25 wanapewa Halmashauri ambayo wako katika maeneo ya hifadhi. Hili ni jambo la kutia moyo, ni jambo la kupongezwa na ninawaomba mashirika haya na Wizara yako waendelee kuwasaidia wananchi na hata asilimia itakapozidi na hata ikifika asilimia 30 kwa sababu yote ni kuleta maendeleo katika maeneo yetu, maeneo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara hii ifanye kazi ya kuwahamasisha wananchi, tulipotembelea hifadhi zetu tulikuta wananchi wa Tanzania wenyewe ambao wametembelea hifadhi hizi ni wachache mno ukilinganisha na wageni. Hii inawezekana inatokana na gharama kubwa ya hoteli za kulala na kwenye hoteli za kulala kwani wanalipa kwa pesa za nje ambazo Mtanzania hawezi. Sasa tuone namna ya kuhamasisha kwanza, lakini pia gharama ipungue kama *TANAPA,* hifadhi ya Ngorongoro wakajenga...*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

NAIBU SPIKA: Asante wamesikia.

MHE. FELISTER BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kwa hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, nilitaka kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Wizara hii hasa kwa Waziri wa Utalii - Mheshimiwa Shamsa Mwangunga na Naibu wake Mheshimiwa Ezekiel Maige. Kwa kweli wameonyesha tofauti kubwa sana ya uendeshaji. Mambo yamezidi kunyooka kila siku ingawa Roma haikujengwa siku moja, lakini tuna imani kabisa kwamba hawa wawili wakiendelea kwa kipindi kijacho tutakuwa na Wizara nzuri zaidi yenye ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kwamba Mwenyezi Mungu ajalie kwamba Mheshimiwa Mwangunga na Mheshimiwa Maige na mimi mwenyewe turudi hapa, wananchi waturudishe ili tuje kusaidiana kusukuma gurudumu hili kuhakikisha kwamba maliasili na utalii inaleta ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mimi nina mifano mizuri sana na ninaomba nimsifu Mheshimiwa Mwangunga hapa kwa sababu miaka mitatu iliyopita *DC* wa Rufiji, huyu *DC* wa Rufiji nataka nimsifu katika Bunge hili, anaitwa Bwana Kassim Majaliwa, alikuja pale akafanya operesheni wahujumu maliasili katika shughuli zile Wabunge tulimpa *go ahead,* kila mtu akafurahi. Lakini kulikuwa na Afisa mmoja wa maliasili akawa analeta ukorofi, basi tulimwambia Mheshimiwa Mwangunga leo, kesho, yule bwana kwa hiyo, naomba tumpigie makofi kwa utendaji mzuri. *(Makofi)*

Barabara ndani ya *Selous* kama ilivyoelezwa, inatia moyo kwamba imejengwa, na vilevile ukarabati wa viwanja vya ndani ya *Selous* umetimizwa vizuri. Ila nilikuwa nataka kufanya maombi maalum. Miezi iliyopita nilikwenda *Selous* katika kambi ya Kingupira na kulala kule, kwa hiyo, niliona mambo ambayo nadhani lazima nimwombe Mheshimiwa Waziri aweze kuyatupia macho ili ufanisi uwe mzuri zaidi kwa wale wanaofanya kazi kule.

Kwanza barabara hii inayotoka kijiji cha Ngarambe kwenda katika *Camp* ya Kingupira ni mbaya sana. Mimi nadhani yeyote anayetaka kuhakikisha jambo hili tunamkaribisha aende, ataona mwenyewe. Halafu kuna barabara iliyopo kati ya *Camp*

makazi ya Maafisa na wafanyakazi na ofisi zao katika hapa pana bonde kubwa la mto Lung'onya, lile bonde hujaa maji, ni bonde lina udongo mfinyazi, barabara hakuna pale, Maafisa wale na wafanyakazi wanapata taabu sana na mimi nilipata taabu hiyo, nusu tukwame pale.

Sasa ombi langu mimi ni hili, kwa vile *Selous* inatoa kati ya shilingi bilioni sita mpaka nane kwa mwaka, iwezekane basi Serikali impe huyu ng'ombe anayetoa maziwa majani ili atoe maziwa zaidi, itengeneze barabara kati ya ofisi za *Camp* na makazi ya Maafisa Wanyamapori pale Kingupira. Inaweza ikafanya hivyo kwa namna nyingi. Hatuombi barabara ya lami, tunaomba barabara yenye tuta lililonyanyuka ili wafanyakazi wapite ili waende kazini bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

Vilevile, barabara ya Ngarambe kwenda Kingupira itupiwe macho na fedha kwa kweli inaweza ikapatikana kwa sababu huyu ng'ombe anatoa maziwa kila siku. Nililala pale, *alhamdulillah* asubuhi nikawa na Mkutano ndiyo nikaelezwa mambo haya. Naomba Mheshimiwa Waziri uyatupie macho sana.

Kwanza, kuna ukosefu wa maji katika *Camp*, kwenye makazi ya watumishi pale hakuna maji ya uhakika, lakini lazima niseme nyumba mlizowajengea wafanyakazi wale ni nzuri mno na kwa kweli inatia moyo kabisa. Maana ukienda pale utadhani umetoka katika pori umekwenda katika *small paradise.* Lakini maji, hakuna choo, zile ni choo za kizungu, hizi *water closet* kama huna maji haitumiki kabisa na wameniambia, mzee sasa tunachimba choo cha shimo. Ukienda uwani kwake kule ana shimo la choo, yaani mambo haya hayatakiwi katika karne hii hata kidogo. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri utoe amri pesa zipelekwe vichimbwe visima virefu yapatikane maji kwa ajili ya matumizi ya watumishi wetu pale Kingupira. *(Makofi)*

Ombi lingine naomba sana utilie maanani ni kwamba kule Rufiji, katika hifadhi ya *Selous* Rufiji kuna mabwawa makubwa yana samaki, yaani nataka kusema kindengereko, wanaombanga, yaani wanaruka ruka samaki sasa wanajifia hivi hivi, watu hawaruhusiwi kuvua. Nilikuwa nadhani jambo busara kabisa Wizara ikubali kurudia tulikoanza kule miaka ya 1970 kwamba zilikuwa zinatoka *fish per meet*, zilikuwa zinatolewa na Wizara kwa miezi kadhaa kuvua katika mabawa yale halafu mabwawa yanafungwa. Hivi nani atalima shamba halafu hata huvuni chochote? Yaani unasema wacha samaki wazeeke, wafe wenyewe tu, hali watu wana njaa? Mimi nadhani tuwe kidogo watu tunaoweza kutazama ukweli, turuhusu watu wa vijiji vya Ngorongo, Mwaseni, Mloka na hata huku Kipugira waende wakavue kwa *per meet* halafu mnafunga mabwawa wanazaliana tena. Nilikuwa nadhani hili ni ombi maalum. *(Makofi)*

Ombi lingine maalum ni jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori ya Mungata. Hii ni Ngarambe na Tapika. Kwa bahati mbaya kabisa hawa watu hawapati maduhuli. Wale wawindaji wanalipa fedha Wizarani hawa wenye jumuhia yao hawapati, ninaomba Wizara itazame pale katika sera ili hela hizi za jumuiya ziende kwa wale wanajumuiya ili wajue na wafaidi Mungu amewaletea wanyama wale nao wafaidi. Kwa hiyo, nadhani hili linawezekana.

La mwisho ni hili la jumuiya ya Mwaseni, Ngorongo, Utete. Tumefanya maombi ya kuandikishwa mpaka leo hatujapa kuandikishwa. Nilikuwa naomba Afisa wako pale utete atie mkazo kidogo ili jumuiya hii nayo ianzishwe tuwe na jumuiya mbili na halafu vilevile zilipwe fedha moja kwa moja badala ya fedha zake kulipwa Wizarani kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi ninakushukuru sana na napenda sana kumwombea sana Mheshimiwa Mwangunga na Mheshimiwa Ezekiel Maige warudi hapa Bungeni na mimi najiombea nirudi hapa Bungeni. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ili muweze kuendeleza mazungumzo! Ahsante sana.

MHE. MWANAWETU S. ZARAFI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hotuba hii ya Maliasili na Utalii. Kwanza napenda kutoa pongezi kubwa kwa Wizara hii ya Utalii kwa kazi nyingi ambazo wamezifanya na vilevile natoa pongezi kwa yale yote ambayo nimeyasoma kwenye kitabu ambayo sisi wananchi wa Mkoa wa Lindi na Kilwa tutakuwa na manufaa nayo. Mfano, ujenzi wa vituo vya doria Nangurukulu pamoja na miradi ambayo inapelekwa katika Mkoa wa Lindi, Wilaya ya miradi ya *Eastern Selous* pia tunawashukuru kwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina tatizo moja ambalo linanisumbua. Tunapenda sana tuwe na wawekezaji, lakini tuna matatizo na wawekezaji wengine. Kuna suala hapa ambalo nimelipata kwa leo hii ambalo linanitia wasiwasi kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi. Suala hili linasemekana kwamba kuna mwekezaji ambaye ametaka kuwekeza katika vijiji 22 vya Wilaya ya Kilwa. Vijiji hivyo mimi sikatai uwekezaji lakini naona inavyokuja kama kuna hitilafu ndani yake. Vijiji hivi 22, tisa kutoka wilaya Kilwa na vingine vilivyobaki Wilaya ya Lindi.

Lakini tatizo linalonisumbua, hapa kuna uharakishwaji wa huu mchakato. Madiwani wa Wilaya ya Lindi wameshapitisha tarehe 25 Ijumaa kukubali kwamba mwekezaji huyu apewe nafasi katika vijiji hivyo. Madiwani wa Wilaya ya Kilwa wao wanatakiwa wapitishe kesho, lakini mchakato umeanza kama ifuatavyo:- Kwa Wilaya ya Kilwa, wanadai vijiji vinane vimekubali, kimoja kimekataa.

Kwa mara ya kwanza tarehe 16 Juni wamepewa makabrasha ya kuelezwa mchakato huo. Tarehe 26 Juni mkutano wa dharura ulifanyika na leo tarehe 2 Julai, Mkuu wa Mkoa alikuwa pale kuwasisitiza Madiwani ambao hawakubaliani na jambo hili kwa sababu linaonekana kama vile, kwa vile sisi tunamaliza Ubunge na wenzetu Madiwani wanamaliza Udiwani, kwa hiyo lipite haraka haraka wapate kuendesha mambo yao wanayoyataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkumbuke kwamba mwekezaji huyu ambaye aliwekeza Serengeti kwa jina anajulikana Ngurumenti wa Serengeti. Mwekezaji huyu ndiye aliyewakimbiza Wabunge wasiingie kwenye eneo ambalo amewekeza. Mwekezaji huyu amehamia Kilwa kwa vijiji hivyo 22 na wananchi wa Kilwa ninavyowaelewa mimi ni wanyonge ambao hawana usemi wowote.

Mimi naliona suala hili lina utata. Utata wake ni kwamba, ningependa Wizara ipeleke Kamati ikachunguze kwamba hawa wananchi kweli wamekubali au hawakubali. Kwa sababu kikao cha leo tarehe 2 Julai, ambacho Mkuu wa Mkoa alikuwepo pale ili kuwahimiza Madiwani walikubali na kesho itokee *full council* ya dharura. Lakini Madiwani walitaka kwenda kuhakikisha kwamba vijiji hivyo vimekubali, Mkuu wa Mkoa hakukubali, kasema waende kwenye kijiji kimoja ambacho wamekataa, lakini vijiji vingine hawana sababu ya kwenda. Mimi naona hapa kuna utata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji hivi kwanza hekta zinazotakiwa ni heka 153,000 ambazo vijiji vyake ni hivyo 22. Tukumbuke kwamba katika vijiji hivyo kuna shule zimejengwa na Serikali, kuna Zahanati, kuna visima, kuna kila kitu ambacho wananchi wanaoishi mle vimejengwa na Serikali na ni mali na nguvu za wananchi. Kwa hiyo, naomba mlitilie maanani hili. Kesho wanalazimishwa Madiwani wa Kilwa walipitishe hili suala, mimi nalileta hapa mapema Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa ananisikia, naomba Kamati itengenezwe kufuatilia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina suala ambalo nimeliandika, kwani nilidhani nisingepata nafasi, lakini ninashukuru umenipa nafasi. Katika miezi mitatu iliyopita kulitokea operesheni ya kutafuta silaha haramu na operesheni hii imefika Kilwa na baadhi ya wananchi wamenyang'anywa silaha. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba, siraha hizo bado ziko Kituo cha Polisi na ninataka kukuhakikishia kwamba, kuna baadhi ya wananchi silaha zao ni halali, lakini suala la kwenda Polisi kila siku wanashindwa kupata silaha zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua operesheni hiyo ni halali, imeagizwa na Serikali na ni halali kufanywa, lakini ninaomba wale wananchi ambao wana silaha halali, basi waachiwe silaha zao kwa sababu katika Mji wa Wilaya ya Kilwa kuna wanyama wakali na kuna wanyama ambao wanamaliza mazao ya wananchi, na hawa wananchi ndio ambao wanaweza kufanya doria kwa sababu wafanyakazi sio wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi wale wale wananchi ambao wana silaha ndiyo ambao wanafanya ile kazi ya kufukuza wanyama wakali ili wasiharibu mazao. Kwa hiyo, hili ni ombi tu kwa Wizara ya Maliasili, wawasaidie hawa wananchi ili wapate hizo silaha zao ili waweze kulinda mazao yao na kulinda hali halisi ya wanyama wakali ambao wanawaathiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru pia kwa kuwa asilimia 25 na pia nimeziona kwenye kitabu zile ambazo wananchi au Halmashauri ya Kilwa inastahili ipate. Nawashukuru Wizara na ninaomba wakati mwingine fedha hizi zifike katika Halmashauri zetu kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na wote walioshiriki katika uandaji wa bajeti. Lakini pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri na mahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza wote Wizarani kwa utendaji na uendeshaji mzuri wa shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sekta hii inakua kwa haraka, pamoja na yote ambayo Serikali imekwishafanya kuwawezesha wananchi kushiriki zaidi, Serikali iendelee kuangalia njia zaidi za kuwawezesha Watanzania kujihusisha zaidi katika biashara hii ili waendelee kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujangili, napongeza jitihada zinazofanywa lakini nashauri vifaa vya kisasa vipatikane ili kurahisisha na kufanikisha zaidi shughuli hizo hasa maeneo ya *Selous*, magari yaongezwe na mbinu nyingine zitumike.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Shamsa Mwangunga (Mb), Waziri mwenye dhamana ya Maliasili na Utalii. Nimpongeze pia Mheshimiwa Ezekiel Maige (Mb), Naibu Waziri, Maliasili na Utalii. Nimpongeze Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya maandalizi ya hotuba hii ya bajeti 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya utalii, ni sekta nyeti na muhimu katika kuchangia pato la Taifa, bado kuna hali ya kusikitisha juu ya namna tunavyozitumia fursa zilizopo za utalii katika kuchangia pato la Taifa, fursa zote zilizopo zina uwezo mkubwa sana. Aidha, yapo matatizo ambayo nadhani ni udhibiti katika fursa zilizopo. Udhibiti huu ni namna ya usimamizi wa mapato, uendelezaji wa fursa hizo ili ziwe na hadhi ambavyo itawezesha kujipatia mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbuga za wanyama tunaziendeleza ama kuzilinda kwa namna ipi na uoto wa asili ili tusiwapoteze wanyama?

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii wa bahari tumeutumia kwa namna ipi katika kutuongezea pato la Taifa. Maeneo nyeti ya visiwa vidogo vidogo vilivyopo Bahari ya Hindi, Wizara ina mpango gani ili iwe sehemu ya utalii kwa wageni wajao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mlima Kilimanjaro na mingineyo imetumiwa kwa kiwango kipi kutangaza sifa ya nchi yetu Tanzania na kutuletea mapato?

Mheshimiwa Naibu Spika, maliasili, mapori tengefu na yale yaliyopo katika hifadhi, Wizara imetoa msukumo wa aina gani katika kulinda maliasili hii? Mfano mzuri ni eneo la Mlima Sekenke ambalo limetengwa eneo la Ekari 10,500 lakini inashangaza tangu Mtukufu Rais, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete azindue hifadhi hiyo, hakuna uangalizi wa aina yoyote na wala sidhani kama Wizara ina taarifa na hifadhi hiyo.

Sina hakika kama kuwekwa jiwe la msingi pekee na Rais halafu kuiacha hifadhi hiyo bila elimu kwa wananchi na uangalizi wa mara kwa mara wa Serikali, naamini hiyo ni kiini macho kwa wananchi. Naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya kina juu ya uangalizi wa hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kukosa umakini wa Serikali katika kuipa msukumo Hifadhi ya Wembere, kadri siku zinavyokwenda hifadhi inaendelea kutoweka siku hadi siku. Ni suala la ajabu kwa Serikali kutokuzingatia maeneo muhimu ambayo nayo kama yangetiliwa uzito yangechangia katika ongezeko la pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Kitangiri, Ziwa hili ni eneo mojawapo la maliasili. Mbali ya kuwa kivutio pia Ziwa hili linazalisha samaki wengi aina ya pelege, kambale na kamongo. Ziwa hili linalo vivutio vya ndege wazuri ambao ni nadra kupatikana kwenye maziwa mengine. Sasa kina cha Ziwa hilo kinaendelea kupotea, Waziri na Wizara yake wana mpango gani, kwa ushirikiano wa Wizara za Mifugo na Uvuvi na pia Wizara ya Mazingira katika kulinda maliasili hii ili eneo la Ziwa hili wananchi waweze kufaidi maliasili na kuvutia watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya fukwe za bahari ya Hindi, kwa nini yasitumike kuvutia watalii kwa kuwakaribisha wawekezaji kujenga mahoteli makubwa ambayo yatasaidia katika kuongeza pato la Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi kumpongeza rafiki yangu mpenzi, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga (Mb), Mwanangu Mpendwa, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige (Mb), Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii yenye mwelekeo wa kuinua uchumi wa nchi kupitia vyanzo vya mapato ndani ya Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa imani kubwa niliyonayo kwa Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri mwenye dhamana na Naibu wake Mheshimiwa Ezekiel Maige pamoja na watendaji wote, napenda kutamka rasmi kuwa ninaunga mkono bajeti hii kwa moyo mkunjufu. Ninawaombea Mwenyezi Mungu awapiganie ili wapiga kura wao wawape kura kwa kishindo ili warudi Bungeni na Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu arudi kwa kishindo awateue tena waendelee kutekeleza mikakati yao kama walivyoainisha kwenye hotuba yao, Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Parseko Kone, Mkuu wa Mkoa wa Singida, kwa juhudi zake ambazo zimesaidia kukamilika kwa ujenzi wa Makumbusho ya Mkoa wa Singida pamoja na viongozi wote walioshiriki kuboresha kituo hicho kwa kukusanya vivutio vyote ndani ya Mkoa na vya asili kwa kuweka kwenye kituo hicho ili vizazi vijavyo vije kuona. Ninaomba Waziri, Naibu Waziri au wataalam wa Wizara watembelee makumbusho haya ili kuja kutoa ushauri wa kitaalam. Muhimu zaidi ninampongeza Mheshimiwa Mizengo Peter Kayanza Pinda -

Waziri Mkuu, kwa kutuzindulia makumbusho haya akiwa ameongozana na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii - Mheshimiwa Ezekiel Maige.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana wananchi wa Singida, kwa jitihada zao kubwa za ufugaji wa nyuki wakiwemo wanawake hasa wa Wilaya ya Manyoni, Singida Vijijini na Iramba, Tarafa ya Ndago, Kata ya Urughu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Ezekiel Maige, Naibu Waziri, kwa ahadi yake ya kutuchangia mizinga mia moja ishirini (120) kwa akina mama ambao wana miradi ya ufugaji wa nyuki Mkoani Singida. Ninaomba ahadi hii Serikali itekeleze kabla Bunge halijavunjwa. Aidha, ninaomba soko la asali lenye uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mungu kwani kati ya Mikoa yenye vitalu vya uwindaji ni pamoja na Singida Wilaya ya Manyoni. Pamoja na vitalu vya uwindaji kuwepo Wilaya ya Manyoni bado Wilaya na Vijiji vinavyozunguka vitalu hivyo havijanufaika vya kutosha. Ninaomba asilimia ya uwindaji iletwe kwa wakati pia kiwango kiongezeke na Mfuko huu usaidie miradi ya maendelo kwenye vijiji jirani hasa vya Kata ya Rungwa na Nkonko na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vivutio vya utalii Mkoani Singida kutambuliwa, ninapenda kurudia tena kuihabarisha Serikali kuwa kati ya Mikoa yenye vivutio vya utalii ni pamoja na Mkoa wa Singida. Hivyo, ninaendelea kuiomba Serikali kuwa ni muhimu kwenda Singida kuvitembelea vivutio hivi ili viweze kuingizwa kwenye orodha ya vivutio ili tuweze kutembelewa na watalii ili kuinua uchumi wa Singida kupitia vivutio mbalimbali mfano Kitovu cha Tanzania Bara kilichopo Kijiji cha Sukamahela, Kata ya Sorya, Tarafa ya Kilimatinde, Wilaya ya Manyoni, kuona alama iliyowekwa juu ya Mlima wa Mawe na Wajerumani zamani sana.

Pili, jiwe kubwa lililoko Kata ya Heka, Wilaya ya Manyoni lenye mchoro wa picha ya Malaika anayefananishwa na Nabii Issa au Yesu Mwana wa Mungu. Tatu, Mawe ya Mjini Singida yaliyobebana na kuonesha picha mbalimbali. Nne, Maziwa yaliyopo Manispaa ya Singida yaani Ziwa Kindai ukitokea Manyoni na Ziwa Singidani ukitokea baraba ya Shelui na tano, Mapango ya Wajerumani ambayo inasemekana walizika vitu vya thamani sana. Mapango haya yako Kisiriri na Mkalama yote Wilaya ya Iramba. Nina matumaini sasa Serikali itatuma wataalamu kwenda kuona vivutio hivi mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mbuga za Wanyama kutokuingiliwa, ninapenda kuikumbusha Serikali kuhakikisha Mbuga za Wanyama haziingiliwi na makazi ya watu kama tulivyoona wakati wa ziara ya Kamati ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma huko Ngorongoro na kadhalika. Kwani ni kuhatarisha maisha ya watu pia kusababisha wanyama kuhama.

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, hongera nyingi kwa Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Naibu Waziri, Mheshimiwa E. M.

Maige, Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote wa Wizara hii. Tunashukuru sana kwa hotuba nzuri na utendaji wa kutukuka wa Wizara hii hususani utendaji kazi wa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Rufiji tulikuwa na tatizo la Afisa Maliasili aliyeleta ukorofi wakati wa kamata kamata ya wavimaji haramu iliyoendeshwa na Mkuu wa Wilaya ya Rufiji. Mheshimiwa Waziri alichukua hatua za haraka na kumtoa Rufiji Afisa huyo mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wana Rufiji tunashukuru sana kwa kutuletea mradi wa *Eastern Selous Conservation* na shughuli za ufugaji nyuki. Mradi huu ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wa Jimbo langu.

Mheshiniwa Naibu Spika, nilitembelea *Camp* ya *Selous* ya Kingupira Rufiji, wana matatizo ya barabara yao ndani ya *Selous* hasa Kingupira kwanza kutoka kijiji cha Ngarambe kwenda *Camp* (Kambi) ya Kingupira ni mbaya sana.

Aidha, barabara kati ya kambi ya makazi ya watumishi wa hifadhi Kingupira, kwenda kwenye Ofisi za *Camp* hiyo ni mbaya sana. Barabara hii inapita katika Bonde la Mto Rung'onya yaani ofisi za hifadhi ziko upande wa pili wa makazi ya watumishi. Tunaomba barabara hii ijengwe kwa ngazi ya changarawe na iwe ya kudumu (vipande vyote viwili). Barabara toka Ngarambe kwenda Kungupira na barabara kutoka Kungipira makazi ya watumishi kuvuka Mto Rung'onya kwenda kwenye Ofisi za hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Kingupira ina majengo ya kisasa. Tatizo kubwa ni ukosefu wa maji. Kambi, hasa makazi ya watumishi Kingupira wana matatizo ya maji. Mathalani wana vyoo vya ndani yaani *"water closet"* lakini wanashindwa kivitumia vyoo hivi, badala yake watumishi wanachimba vyoo vya shimo *(Pit latrines)* nyuma ya nyumba zao. Hata maana ya kuwa na nyumba ya kisasa haipo kabisa. Maji ni uhai. Naomba Serikali ichimbe visima virefu ili maji yapatikane kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabwawa ya Samaki ya Hifadhi ya *Selous*. Sisi Rufiji tuna mabwawa ya asili mengi na yako katika Hifadhi ya *Selous*. Zamani, *permit/license* zilikuwa zinatolewa kwa wanakijiji wanaozunguka pori hili ili wavue kwa muda maalum. Wanavuna samaki na kisha mabwawa yanafungwa. Tunaiomba Serikali irudishe utaratibu wa kutoa *permit* ya kuvua kila mwaka ili wananchi wavune samaki. Serikali ikumbuke kuwa huwezi kulima shamba lakini huvuni kutoka shamba hilo. Kuvua kwa *permit* katika mabwawa ya Rufiji katika hifadhi ya *Selous* sasa kuruhusiwe ili kiondoe umaskini wa wanavijiji wanaozunguka hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii 100%. Ahsante sana.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Mto Kilombero, lina umuhimu wa kipekee juu ya kuhifadhi aina mbalimbali ya wanyama. Katika bonde hilo kumekuweko wanyama wengi baadhi ya wanyama walikuwa wanapatikana hapo tu. Hivi sasa hali iliyoko katika bonde hilo ni ya kusikitisha. Wanyama wengi wametoweka kutokana na kuongezeka kwa mifugo na kupanuka kwa

kilimo hususan cha mpunga. Wanyama waliokuwa wanaonekana hapa kwa makundi hivi sasa hata mmoja mmoja huwaoni, ni taabu. Hivi sasa mazingira yanachafuliwa kwa kasi kubwa licha ya kuwa sasa wanyama hawaonekani bali hata hicho kilimo na ufugaji kina athari kwani kina cha Mto Kilombero kinapungua kwa kasi kubwa kuashiria kuwa Mto huo unakufa kidogo kidogo. Ipo haja hatua madhubuti na ya haraka ichukuliwe kukabili hali iliyoko kwenye Bonde la Mto Kilombero, mifugo ipunguzwe na kilimo kinachochagua mazingira kifuatwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna ukataji mkubwa wa miti kwa ajili ya nishati ya kupikia. Ninaelewa uhifadhi wa mazingira ulio chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais lakini suala hili ni mtambuka. Kuzuia ukataji wa miti ni sehemu moja ya uhifadhi wa mazingira, je, Wizara hii imeshirikiana vipi na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kuhakikisha ukataji wa miti unafungwa kwa kuwepo nishati mbadala ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilianzisha utaratibu wa kuzipanga hoteli kwa mujibu wa daraja zao. Zoezi hilo lilianzishwa katika miji mikuu miwili. Je, zoezi hilo bado linaendelea na ni katika maeneo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Natron ni mahali pekee ambapo kiasi cha asilimia 75% ya mazalia ya *heroe* wadogo *(lesser flamingo)* yanafanyika. Hivi sasa inavyoonekana kuna mvutano na uvunaji wa magadi, wako wanaosema kuwa mradi wa kuyachimba magadi ufanyike na wako wengine hawakubaliani. Ni hatari sana kuja kuyachafua mazingira ya Ziwa Natron na *heroe* wadogo *(lesser flamingo)* watatoweka. Iwapo mazingira yatarekebishwa na kufanya watalii kufika hapo, eneo hilo litakuwa na kipato cha milele kutokana na utalii kinyume na kipato kitachotokana na magadi kama yatachimbwa kwani hatima yake magadi yatakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii, ila napenda kujua ni siku ngapi za doria kwa mwaka zinahitajika kwa wastani katika hifadhi zetu zote ili kukabiliana na majangili kisawasawa *(effectively)* na ni kiasi gani cha gharama (fedha) kinahitajika kwa mwaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya majangili 3,773 yaliyokamatwa ni wangapi wamekamatiwa katika Mbuga za Akiba za Rungwa, Kizigo na Mhesi na pia Chaya? Je, ni hifadhi au mbuga zipi zinazoongoza kwa majangili hapa nchini na sababu zake?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kuna wazo lolote ndani ya Wizara hii la kutenganisha Mamlaka ya Hifadhi ya *TANAPA* na Mamlaka ya Mbuga za Akiba ili kuwe na mamlaka itakayosimamia *effectively* hifadhi za mbuga za Akiba kama Selous, Rungwa, Kizigo, Mhesi na kadhalika, maana nahisi *TANAPA* inasimamia zaidi *National Parks.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara iruhusu wananchi watumie mabwawa ya Itwaga na Kiyengege kule Ipande (Mkajenga na Mgamboo) kwa ajili ya

kunywesha mifugo yao. Hii ni kwa sababu mwaka huu mvua zilikuwa chache sana na tayari ukame umezidi sana kiasi cha kuwafanya wananchi wataharuki na kukumbuka ukame wa mwaka 2005/2006 ambapo mifugo mingi ilikufa kwa sababu ya ukame.

Tayari maombi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kuomba kibali yamewasilishwa Wizarani. Naomba jibu, ili Serikali iwanusuru wananchi na mifugo yao na kuwazuia wananchi wasihame maeneo yao kipindi hiki wanajipanga kupiga kura kwenye Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba na mwishoni mwa mwezi huo kwenye kura za maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri na Naibu Waziri wapokee shukrani za wananchi wa kata za Ipande, Itigi, Mgandu Mwamagembe, Rungwa na Sanjaranda kwa kazi nzuri ya kuiongoza Wizara hii ngumu. Wamenufaika na mengi katika muda wao wa utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la tembo bado kero kubwa, tatizo la simba hakuna lilimalizwa, ni kwa nini tatizo la tembo lisimalizwe pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongeza kwa Wizara kwa kazi nzuri kwa ujumla. Wananchi wa Kata ya Nyakahura katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo wamekuwa wakikabiliana na adha ya wanyama kama ndovu kuvamia maeneo ya makazi ya watu hali ambayo inaambatana na uharibifu mkubwa na endelevu wa mazao ya kilimo lakini hata kusababisha kusimama kwa shughuli za maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua jitihada za Serikali kuanzia ngazi ya Halmashauri ya Wilaya, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa na hapa Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia kwa Waziri na Naibu Waziri chini ya usimamizi wa Waziri Mkuu ambaye ameshirikiana jambo hili mara kadhaa. Hata hivyo nasikitika kuwaarifu Wizara kwamba jitihada hizo zote hazizai matunda kwani kadri siku zinavyokwenda tatizo linazidi kuwa kubwa na madhara yake yanazidi kutanuka. Usiku wa kuamkia jana tarehe 1 Julai, 2010 kwa mfano, mlinzi wa Shule ya Msingi ya Bugombe amefukuzwa na wanyama hao na akalazimika kuacha lindo kwa usalama wake. Wiki iliyopita wananchi wa vitongoji vya Chamakaza na Kibambe wameshindwa kufanya shughuli zao kabisa mashambani kwa muda wa siku tatu mfululizo kwani ndovu hao walikuwa na mkusanyiko mkubwa katika maeneo yao kwa mfululizo usiku na mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa kawaida sasa kwa wanachi na Kata ya Nyakahura kufanya ulinzi usiku kwa maana ya kuwafukuza wanyama mashambani pamoja na jitihada hizo inatokea mara kadhaa ambapo ndovu hao huendelea kuzagaa kwenye maeneo ya makazi ya watu mpaka asubuhi wanafunzi hao wale wa shule za msingi hushindwa kuhudhuria masomo kwa kuhofia usalama wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu kwa ufupi tuangalie sababu za jitihada za Serikali kugonga mwamba, katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya ufinyu wa vitendea kazi na fedha kwa Idara ya Maliasili na Misitu, ngazi ya mkoa ufinyu wa Bajeti na katika ngazi ya Wizara kutokuwa na picha sahihi ya ukubwa wa tatizo na hivyo kulishughulikia bila kulipa uzito stahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni janga na kuna aina mbili kubwa za majanga, *slow, silent process* (taratibu na kimya kimya) na *an abrupt, loud emerge* na nyuma ya aina hizi mbili za majanga kuna makundi mawili ya sababu za kutoka majanga hayo, *human made, somethings due to wrong policy choice, stem from forces of nature.*

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotokea janga la ghafla na lenye kuonesha udharura Serikali imekuwa ikiuona ukubwa wa tatizo kwa usahihi na kufanya utatuzi kwa kutoa masahihisho yenye uzito stahili. Lakini inapotokea majanga yanayotokea taratibu na yanayoweza kudhaniwa yanatokea kimya kimya kwa wale walioishi eneo husika basi hapa Serikali haipati nafasi ya kufahamu uzito hasa wa tatizo, tunakuwa na utatuzi wa namna ya zimamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Wizara ilione suala hili kama dharura na ifanye jitihada za makusudi kwenda kufahamu kiini cha tatizo hili kwa kina na kuongoza Wizara nyingine katika utatuzi kwani inasemekana kuna sababu nyingine ambazo ni mtambuka kutokea Wizara nyingine.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeze sana wewe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ambayo inafanyika sasa baada ya misukosuko mikubwa ya magogo, kuzuiwa kuuza meno ya tembo pia na ukosefu mkubwa wa vitendea kazi, pia matatizo ya uwindaji wa kitalii. Ni matumaini yangu makubwa kwamba sasa mmejipanga vizuri kufanya kazi ya kutukuka kulinda maliasili zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite upande wa wanyamapori ambacho mimi ni mtaalam na nimefanya kazi miaka 28 humo. Mpaka sasa Ashauri wa Idara ya Wanyamapori tuliona ni wachache sana kulinganisha na mapori yanayohitajika kulizidiwa pia pamoja na kuwa wachache hawana vitendea kazi vya kutosha na vya kisasa kuunganisha na vile majangili wanavyovamia magari na silaha. Kwa kuwa Serikali ingefanikiwa kuuza meno ya tembo lakini kutokana na chuki binafsi na wivu kwa nchi ya Kenya na Rwanda mpango wa Serikali mzuri ulikataliwa, Wizara yako itaendelea kujipanga na kuwaelewesha wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa *CITES* waelewe nia yetu nzuri ya uhifadhi ili mkutano ujao waturuhusu kufanya uuzaji wa meno yetu ya tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya hivi karibuni kumekuwa na malalamiko na malumbano juu ya uwindaji wa kitalii hasa kuhusiana na vitalu vya uwindaji, mapendekezo yangu ni kutumia sheria yetu mpya ya wanyamapori na kanuni zake ili kupanga upya ugawaji wa vitalu vya uwindaji ili kuwezesha Serikali kupata mapato zaidi, kuendelea kuhifadhi wanyama wetu, pia napendekeza Serikali itafute njia nzuri ambayo itatoa haki kwa wote bila kujali rangi au Utaifa.

Hapa maana yangu ni kwamba tutende haki kama kuna Watanzania wenye uwezo na waaminifu ambao hata wakipewa vitabu hawatakodisha kwa mengine kulipa kodi zote zinazotakiwa na Serikali basi wapewe. Pia kwa wenzetu waendishaji wa nje ambao kwa miaka yote wamekuwa wana wawindisha watalii bila kuvunja sheria za nchi basi nao wafikiriwe kama wawindishaji wema na wapewe vitalu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kutafutwe njia nzuri ya kugawa vitalu njia ambayo Serikali haitakosa mapato yake. Mimi nakubaliana na mpango uliowahi kupendekezwa huko nyuma kwamba vitalu viuzwe kufuatana na ubora maana kuna vitalu vingine vina wanyama wengi wa aina mbalimbali wanaotafutwa na wawindaji na kuna maeneo yenye wanyama wachache na maeneo mengine ya kupiga picha ni mazuri zaidi kuliko mengine. Nashauri utafutwe utaratibu utakao ondoa migongano kati ya Idara na wawindaji na upande mwingine kati ya Idara ya wawindaji na wanavijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze sana mpango wa kuanzisha *WMAs*, nashauri idara iwe makini maana baadhi ya maeneo hayo yameanza kutumiwa vibaya na viongozi wa vijiji, wawindaji wa kitalu wanapiga picha wanaojenga mahoteli na *camping sites* na kadhalika. Pia naomba wawindaji wenyeji wanoatafuta kitoweo nao watengewe mpango mzuri zaidi ili kutoa malalamiko kwenda kwa Serikali kwamba wanakerwa na hawapewi haki yao ya kupata kitoweo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande kwa Idara ya Mambo ya Kale tunayo maeneo mengi sana ambayo Serikali iliyafuatilia na kuyaorodhesha yatachangia sana kukuza utalii mafunzo na tamaduni zetu. Wilaya ya Mkalama ina vivutio vingi sana kama Boma ya Wajerumani, miguu kwenye miamba ambayo binadamu wa kale walipita na kukanyaga ngoma kubwa za asili ambazo zipo Tarafa za Kivumi, Nduguli na Nduruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Chuo cha Pasiansi kiendelee kuongezewa fedha ili kiendane na wakati. Naunga mkono hoja.

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Bajeti hii haitoshi kabisa, pesa iongezwe katika Kitengo cha Malikale, Makumbusho, Utalii na Utalii wa Wanyamapori. Kuhusu Malikale Tanzania, kuna maeneo mengi ya Malikale hayajafanyiwa kazi hasa katika mkoa wa Lindi kama Kilwa ni mji mmoja kati ya miji mitano iliyoendelea tangu *AD 960 – 1700(old cities)* miji mingine ni Lamu – Kenya, Momba – Kenya, Mogadishu – Kenya na Sofala Msumbiji. Nataka niambiwe Serikali inaendelezaje Kilwa, kuna uwanja wa ndege uliotumiwa wakati wa Vita vya Dunia ya Pili 1939 -1945, kuna *run way* sita, kuna bandari iliyotumiwa kusafirisha mjusi mwaka 1910 Ujerumani hii yote ni mali kale kurudisha mijusi Ujerumani.

Mheshimiwa Naibu Spika, makumbusho sita yaliyopo ni machache sana, bado kuna Makumbusho ya Falsafa ya Mwalimu Nyerere. Makumbusho ya Majimaji Songea hayajaboreshwa kwani inabidi pia makumbusho hayo yaanze Kilwa, kijiji cha Kinjekitile

ambako vita vya majimaji ilikoanza mkoani Lindi. Kwa hiyo makumbusho hayo yawepo Lindi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanyamapori, tunaomba *Selous Game Reserve* iendelezwe mkoani Lindi kwani ni matatizo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni shukrani zangu na pongezi kwa Wizara, Waziri na Uongozi wake wote kwa kunipa nafasi ya kwenda kuona mjusi Ujerumani, kwa kweli ninaishukuru pia kitengo cha Makumbusho kwa kunishirikisha kwani baada ya kumuona mjusi yule, ile kasi ya kudai mjusi arudi, inapoza kidogo, lakini bado nadai mjusi wangu wa Lindi. Ahsanteni sana.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote Wizarani pamoja na mashirika yote chini ya Wizara kwa kazi nzuri. Aidha, napenda kusisitiza yafuatayo, ugemaji wa asali, asali ni moja ya mazao muhimu yapatikanayo katika Mkoa wa Tabora naishauri Serikali iandae mpango kabambe ya jinsi ya kuliendeleza zao hili kwa kuwapatia zana za kisasa (mininga) za kufungia nyuki.

Aidha, mavazi ya kuvaa wakati wa kuvuna asali nayo ni muhimu ili kubadili teknolojia ya kutumia moto na moshi wakati wa kuvuna asali ambao matokeo yake ni kuumwa na nyuki wengi bila sababu. Aidha, asali inayotumiwa kwa utaratibu huu hupungua thamani kwa kunuka moshi. Suala la kuweka viwanda vya kusindika asali pale inapopatikana halihitaji kusisitizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Makumbusho ya Kale, Kwihara Tabora, Kwihara ni miongoni mwa sehemu za kihistoria hapa nchini. Naishauri Serikali kuyaboresha na kuyatunza mazingira ya Kwihara - Tabora kama kivutio cha watalii wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shirika la ndege, sekta ya utalii inaweza kuliingizia Taifa letu fedha nyingi za kigeni kama Serikali ningeweza kulihuisha shirika letu la ndege ili liweze kushiriki kikamilifu katika kuwasafirisha watalii wetu. Inakadiriwa kwamba takriban 60% ya matumizi ya watalii yanakwenda kwenye gharama za usafiri wa ndege.

Aidha, 40% ya matumizi ya watalii ndiyo yanayokwenda kwenye malazi (hoteli), vyakula na vinywaji, vilevile manunuzi ya zawadi mbalimbali, kwa mustakabali huu, ili nchi yetu iweze kufaidika zaidi na kipato cha watalii ni lazima sekta ya utalii iweze kuunganishwa na sekta nyingine hapa nchini hususani kilimo, viwanda na usafirishaji wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kutembelewa na watalii, sehemu kubwa ya utalii wetu ni katika mbuga za wanyama za Serengeti, Ngorongoro na Mlima Kilimanjaro yaani utalii wetu umeelekezwa zaidi Kaskazini ya nchi yetu pamoja na kwamba kuna sehemu nyingine nyingi zenye vivutio hapa nchini kama vile Mbuga za *Selous*, Katavi

(Rukwa). Tunahitaji kuyafungua maeneo haya kimiundombinu ili kuwavutia watalii wengi kuyatembelea maeneo haya vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utalii wa uwindaji, hii ni aina nyingine ya utalii tena yenye mvuto mkubwa kwa watalii. Aidha, ni eneo linalohitaji usimamizi wa makini zaidi ili kuepusha ubadhilifu, halikadhalika kuna haja ya kufanya maamuzi ya makusudi ya kuwapa kipaumbele wazalendo (Watanzania) kwa kuwagawia vitalu vya uwindaji kinyume na utaratibu wa sasa ambao unaonekana kupendelea wageni katika ugawaji wa vitalu. Ili Watanzania wenye vitalu vya kuwinda waweze kumudu gharama kubwa za kuendesha kampuni za utalii wa uwindaji, Serikali haina budi kuwawezesha wazalendo hawa kupata mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuwa na mradi huu katika mipango yake. Aidha, naishauri Serikali iongeze kasi katika kukamilisha mradi huu ambao njia inayokusudiwa ni pamoja na ile inayoanzia Ujiji kupitia Tabora (Kwihara) kuelekea Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

MHE. DR. C. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii na nampongeza Waziri, Naibu Waziri na wataalam wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuwa Serikali ifanye *operation* maalum ya kusaka majangili. Uuaji wa Tembo Tanzania unatisha, baada ya miaka michache nchi itakuwa haina tembo, ujangili Tanzania unatisha, ujangili ndani ya Selous unatisha. *Operation* maalum itakayohusisha askari wanyamapori *F.F.U.* na JWTZ iandaliwe na kutekelezwa mara baada ya uchaguzi mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya ukataji miti na kuiuza nje kwa njia ya magendo pia unaendelea, hatua kali zinatakiwa kwa watendaji wanaoshirikiana na wafanya magendo.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu kwa maandalizi mazuri ya hoja hii ya bajeti. Naelewa Wizara hii ni nyeti, lakini jitihada zilizofanywa mpaka sasa ni nzuri na za kujivunia. Msikate tamaa, fanyeni tu kazi kwa kuwa njia mnayoifuata ya kuendeleza Wizara hii baada ya muda wananchi watatambua nini mmekuwa mkifanya. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa dhati maeneo yafuatayo ambayo ningependa Mheshimiwa Waziri anisaidie katika kutoa maelezo, ni hatua zipi zitatumika ili kuendeleza na kuanza kutekeleza maombi ya Wana Rukwa kwa siku nyingi bila ya mafanikio.

Kwanza, Hifadhi ya Msitu wa Mbizi – ulioko katika eneo la Manispaa ya Sumbwanga. Msitu huu ni muhimu kwa kuwa ndicho chanzo kikuu cha maji mjini – na

pia ni msitu wenye mbega wekundu ambao wanaweza kupotea kama hawakulindwa. Tuomba eneo hili liwe Hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni lile la Ngome ya Zamani ya Wajerumani. Kule Kasanga ambako Serikali ya Ujerumani ikiwasilishiwa ushauri wa kulifanya eneo hilo la kitalii wanaweza kulikarabati na kutuingizia fedha nyingi za ndani na nje.

Eneo hili pia lina eneo lipo karibu na hapo ambalo ndilo lenye maporomoko makubwa ya Kalambo mpakani mwa Zambia. Nashauri Waziri au Naibu wake atembelee maeneo hayo kabla ya kulivunja Bunge mwisho wa mwezi huu. Eneo hili litafungua sana utalii wa Ziwa Tanganyika Kusini mwa nchi hii na kwa kuzingatia pia kuwa *Mtwara Corridor* itakuwa na vivutio vingi zaidi kama hivyo. Naomba ushauri huu uzingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Mradi wa Asali katika maeneo ya misitu ya Mpanda, Nkasi na kando kando ya Maziwa ya Tanganyika na Rukwa, ungeweza kuwakomboa watu wetu wengi kwenye lindi la umaskini. Jitihada za ziada kuwawezesha wananchi wengi wafuge nyuki kwa kuunda vikundi vya wafugaji ili kujenga soko la uhakika.

Jambo la nne ambalo ningeomba lipewe umuhimu ni kufanya utafiti wa uhakika kuhusu “Twiga Weupi” waliomo katika Mbunga ya Wanyama ya Katavi..

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji wataalam na kuwapatia zana za usafairi - magari katika eneo hilo. Bado tunadhani Serikali imetoa kipaumbele kwa mbuga za Kaskazini mwa nchi hii. Hifadhi ya Katavi na hasa baada ya Uwanja wa uhakika wa Ndege wa Mpanda kujengwa, nina uhakika kuwa sasa Wizara na Shirika letu la *TANAPA* litakuwa na mpango kamambe wa kuendeleza Hifadhi ya Katavi, Mpanda na kuwajengea uwezo wa kujiendesha hapo baadaye. Mhifadhi Mkuu wa Katavi anajitahidi sana pamoja na uwezo duni wa zana na vifaa walivyonavyo bado anafanya kazi yake nzuri na iwapo watasaidiwa watafanya kazi vizuri hata zaidi ya Hifadhi za Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Utalii ungeweza kusaidia maeneo yaliyo nyuma kama haya.

Jambo la tano na la mwisho, napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri aone namna na kupata wahisani kwa mpango wa *PPP* ili waje Rukwa kwa madhumuni ya kushirikiana na Serikali ya Mkoa na wananchi kwa ujumla kupanda miti mingi – kama *Sao Hill Forest* ilivyo. Sehemu ya Sumbawanga ina maeneo mengi yaliyo wazi na hayana kabisa miti. Sehemu hizo ni “Makuzani’, ni wazi, haina miti, wala mazao mengine kutokana na hali ya upepo na baridi. Eneo hili ni safi kwa kuanzisha mradi mkubwa kama huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na kuwatakia Waziri, Naibu Waziri, kinyang’anyiro cha Ubunge kiwe cha fanaka na baraka za Mwenyezi na mrudi humu Bungeni kuendeleza kazi nzuri mliyoianzisha.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi wanazofanya kwenye Wizara ni nzuri na wanatoa ushirikiano wa kutosha. Mchango wangu katika hotuba hii uko katika maeneo yafuatayo hususan Jimbo la Bukombe.

Kwanza, uchimbaji wa Bwawa la Nsango, Bukombe. Serikali iliahidi kwenye bajeti 2009/2010 kuchimba bwawa la kunywesha mifugo Kijiji cha Nsango jirani na Pori la Kigosi, Myowosi. Hadi leo bwawa hilo halijachimbwa. Naomba Serikali itekeleze ahadi hiyo ili kuimarisha ujirani mwema. Pili, mapato ya 25% ya uwindaji. Kwa muda mrefu Wilaya ya Bukombe haipati mapato haya kwa maelezo kwamba hakuna uwindaji maeneo ya msitu huo. Nashauri Serikali iangalie uwezekano wa kupata fedha maeneo mengine ili kuzisaidia Halmashauri zenye msitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo haliwezekani Serikali iendelee kuonesha umuhimu wa wananchi kuwa jirani na msitu. Wananchi wanatusumbua sana kuhusu mapato hayo ambayo yangewasaidia kwenye miradi yao ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu vibali kwa wavuvi na walina asali. Natumia fursa hii kuishukuru Wizara kupitia Meneja wa Kigosi/Myowosi kwa ushirikiano anaonipa, kusikiliza hoja ya wananchi. Muhimu ni mahusiano haya yaendelezwe ikiwa ni pamoja na kufuata ratiba wanazokubalina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri. Nilipata taarifa kuwa upo utaratibu wa kuwaondoa wafugaji wa nyuki mahali mizinga yao ilipo kuisogeza karibu na barabara (*main road*). Tukifanya hivyo tutaathiri uchumi wa wananchi wa Bukombe.

Wananchi wa Bukombe wanategemea sana zao la asali. Ni vizuri makubaliano kati ya Serikali na walina asali yazingatiwe bila kuwaondoa mahali walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne ni mradi wa ufugaji nyuki. Katika bajeti ya 2006/2007 Serikali iliainisha kuanzisha mradi wa ufugaji nyuki wa kisasa Bukombe. Kwa nini mradi huo haujaanza na lini unatarajiwa kuanza kazi Wilayani Bukombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Kituo cha Kutolea vibali. Naomba Serikali mtoe kibali katika Wilaya ya Bukombe. Kwani wananchi wangu wanalamika kusafiri kilomita mia moja toka Bukombe hadi Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini mnaweza kupata ofisi katika majengo ya Halmashauri au majengo ya CCM, Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema na uchaguzi ili mpate ushindi katika maeneo yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu wake na wataalam kwa ripoti na mpango mzuri wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka ya Pori la Hifadhi Mkungunero inaishia kwenye mipaka ya Wilaya ya Kondoa. Hivi sasa hifadhi hiyo imevamia na kuingia ndani ya mipaka ya Wilaya ya Kiteto katika Kijiji cha Dikiushi Dibour na mipaka ya Kijiji cha Kimotorok, Wilayani Simanjiro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ifanye marekebisho haraka ya mipaka hiyo ili kukwepa fujo kwa watu ambao hawakushiriki katika mipango ya kuunda Hifadhi ya Mkungunero

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iharakishe kutoa *user rights* kwa *WMA* ya Endema Makame.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naomba kushauri maeneo ambayo yana Hifadhi kwa mfano Ruaha *National Park*, iliyopo kwenye Halmashauri ya Iringa Vijijini, ni muhimu Halmashauri zikapata gawio la mapato yanayotokana na hifadhi au mbuga husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sera hii bado kuna changamoto ya utunzaji wa takwimu kujua ni kiasi gani cha mapato maana mapato husika hukusanywa na Serikali Kuu. Hivyo ningeomba jambo hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua, Bodi ya Utalii itaanza lini kuendeleza utalii wa utamaduni eneo la Madundo Iringa?

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii. Aidha, napenda kumpongeza Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa hotuba yake iliyofanyiwa utafiti na ninafikiri Serikali itayachukua maoni haya ili kuwa na utalii unaojali mazingira na endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Ni jambo la kusikitisha, uchafu umezidi katika hifadhi hii. Kuna baadhi ya makampuni wakati wakipandisha watalii wengine huenda kufanya/kuweka *camping* ndani ya *crater* lakini baada ya wageni kujisaidia katika vyoo hivyo vya (*Chemical toile*t) wakimaliza ma-*porter* wanamwaga kinyesi kule kule *crater*.

Hii ni hatari sana, ni baya kwa mazingira na pili ni hatari kwa afya za wageni. Je, Serikali iwe na mikakati gani kuhusu uchafu uliokithiri katika Mlima Kilimanjaro ambao unatuletea aibu ukizingatia wageni wanalipa fedha nyingi sana kwa *park fees*?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kidia ambayo imefungwa. Kwa kuwa barabara hii ilikuwa inatumika kwa watalii kuteremka lakini barabara hii ina vivutio vizuri sana (*water falls*), vipepeo na ndege wa aina tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri, kama njia ile Serikali haitaki kuitumia kwa ajili ya kupanda mlima basi sehemu ile waruhusu watu wapande kwa *day trip* wapige picha na hii itakuwa ni njia mojawapo ya wageni hawa na siku ya kuuruhusu mwili kuzoea hali ya mlima tayari kwa kupnda mlima *next day*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *NGO* iliyopo pale Moshi kutoka Marekani. *NGO* hiyo inaitwa *Kilimanjaro Ports Assistant Project (KPAR*). Kwa kweli *NGO* hii kazi yake ni ku-*promote* tu makampuni ya nje na kukandamiza wazawa. *NGO* hii ilikuwa kule Evarest wakafukuzwa, sasa wamekuja hapa Tanzania. Kisingizio wanaangalia haki za ma-*porter*.

(i) Je, tunahitaji mtu kutoka nje ya nchi kuja kuangalia haki za ma-*porter*?

(ii) Tunavyo vyama vya ma-*porter* na Vyama vya Wafanyakazi ambao wanaweza kutetea haki zao ni kwa nini mama huyu aingilie taratibu zetu na Serikali inakaa kimya.

(iii) Je, anapoomba *visa* ya kufanya kazi kama *NGO* hakuna kikomo kama ni kufundisha amekwishakaa zaidi ya miaka mitatu. Ni kigezo gani kinatumika kuwapa kibali cha kufanya kazi nchini?

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, Lazima tulinde haki zetu kama Watanzania, hivi kuna Mtanzania anayeweza kwenda Marekani akajifungulia *NGO* kuaangalia haki za wafanyakazi kule Marekani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri kwa *TTB* waongezewe fedha za kutosha ili kuweza kuitangaza nchi yetu vema kwa kuwa tumeingia katika soko la pamoja la *East Africa* wenzetu wa Kenya Mawakala wa Utalii wakati wanahudhuria maonyesho huwa wanajilipia *ticket*, malazi na vyakula.

Lakini Serikali inalipia banda. Kwa kuwa Wakala huitangaza nchi yetu na inakuwa ghali sana, je, Serikali ikiiwezesha *TTB* wakalipia banda na wakala wajilipie malazi, *ticket* na chakula haioni patakuwepo na wakala wengi na hatimaye kupata wageni wengi zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha naomba kumpongeza Mheshimiwa Shamsa Mwangunga - Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba yake nzuri na yenye uchambuzi wa kina aliyoitoa asubuhi hii. Nampongeza pia Mheshimiwa Ezekiel Maige - Naibu Waziri kwa ushirikiano mzuri anaompa Mheshimiwa Waziri na hivyo kuleta ufanisi mkubwa katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukumbushia ombi la muda mrefu la Halmashauri zinazozunguka Mlima Kilimanjaro ambalo lilitenga Halmashauri hizo kuachiwa mrabaha kwa asilimia itakayokubalika ili kuchangia maendeleo ya Halmashauri hizo. Ahsante.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu kwa utunzaji wa Maliasili ambao ni muhimu na Utalii nao pia ni muhimu kwa kipato cha nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mwangunga pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Maige kwa kufanya kazi bila kuchoka, na kazi hii ni ngumu kwani mnafanya kazi ya kuchungana na watu ambao ni Maharimia, pia kuongoza ulinzi wa kulinda Mali asili yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo la msitu wa Serikali, sehemu ya Bomba mbili Mwatolole Geita kumetokea mabishano ya eneo hilo kati ya Wizara ya Maliasili na Halmashauri ya Geita, kitendo ambacho kilipelekea Halmashauri ikalipima eneo hilo viwanja vya makazi na biashara, wananchi wakauziwa viwanja hivyo zaidi ya Sh. 300,000,000/=. Baadaye Wizara ilipofahamu hilo ikapiga marufuku eneo hilo kugeuzwa matumizi bila idhini ya Wizara. Naibu Waziri - Mheshimiwa Maige alisimamia kidete kuhakikisha kwamba eneo la hifadhi haliwezi kubadilishwa matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wananchi waliouziwa viwanja hadi leo hii wanapewa matumaini. Hivyo basi, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho alieleze wazi Bunge kama matumizi yamekwisha badilishwa: Je, kwanini Halmashauri walipima eneo hilo kabla ya kubadilishwa matumizi. Ni hatua gani wamechukuliwa watu ambao wamewaingiza wananchi kwenye shida? Na nini hatma ya wananchi ambao walidanganywa na kupimiwa eneo la hifadhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Naibu Waziri alianza kuvutana na Halmashauri na alizuia eneo hilo kutumiwa kwa matumizi mengine na kupeleka askari wa Maliasili kung'oa vigingi vilivyokuwa vimewekwa katika upimaji wa viwanja hivyo.

Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko la eneo hili la Bomba mbili Mwatolole Geita. Hivyo, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alishudia ung'olewaji wa vigingi hivyo, basi namwomba Waziri atoe tamko la Serikali ili wananchi ambao wametapeliwa na Halmashauri wajue kinachoendelea maana wamesubiri kwani bado wanatiwa moyo kuwa watajenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Wizara ndio itatoa njia. Tuwe macho na wadanganyifu wa hifadhi zetu. Ahsante.

MHE. KHADIJA S. AL-QASSMY: Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa mzima na kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Vile vile nakupongeza wewe, Naibu

Spika, Wenyeviti na Watendaji wako wote kwa jinsi mnavyofanya kazi kwa ufansi mkubwa, Mungu awasaidieni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Naibu pamoja na Watendaji wake wote kwa juhudi zao za kufanikisha hotuba hii na leo hii inasomwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho na kwa umuhimu mkubwa, nampongea Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhifadhi wa Saadan ni Serikali, haichukui jitihada za kutosha na hifadhi hii ni nzuri sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali ichukue jitihada za makusudi, waache kuwalinda wanasiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wa Wanyamapori ni kidogo sana, kiasi kwamba wananchi wanapata athari kubwa kwa kudhuriwa na wanyama hao. Kwa hiyo, naomba Serikali ijitahidi sana katika hili ili wananchi waondokane na hofu ya kufa kwa ajili ya tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sekta hii kuwa na umuhimu sana katika Taifa, lakini bado Serikali haichukui jitihada za kuboresha miundombinu kiasi kwamba kunakuwa hakufikiki kwa urahisi zaidi. Naiomba Serikali ichukue jitihada za kutosha kuboresha hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali ya Miundombinu mibovu ndio maana Watanzania wengi hawaoni sababu ya kufanya utalii wa ndani na kusababisha kukosa pato la kutosha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoteli za kitalii kwa wananchi wa Tanzania (Utalii wa Ndani) bado ni ghali sana, ukienda katika hoteli bado wananchi wanashindwa kumudu. Pamoja na Serikali kuchukua jitihada ya kuhamasisha utalii wa ndani, bado wenye mahoteli wapunguze zaidi kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ahsante.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na timu yote ya Wizara na vitengo mbalimbali kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwani kweli wanawake tunaweza tena bila kuwezeshwa. Ameongoza vyema Wizara hii na Mungu amrudishe tena hapa Bungeni Novemba, 2010 ili aendelee kutoa mchango wake katika kuleta maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, nina maswali au maoni:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wanawake wengi waishio katika maeneo ya pembezoni mwa misitu ya hifadhi mfano Rungwa, Gumanga, na kadhalika, wamekuwa

wakishiriki katika kutunza mazingira na kuhakikisha misitu hiyo haivamiwi kwa kukata miti na matokeo yake wanafuga nyuki kwa kuzalisha asali. Je, ni kwanini Wizara haiwaungi mkono kwa kuwapa mitaji midogo midogo ili ufugaji wao uwe na tija?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wanyama waharibifu wa mazao mashambani na hata kudhuru binadamu pia waishio karibu na hifadhi sababu kubwa mojawapo inayowaleta kwenye maeneo ya makazi ya watu ni pamoja na kutafuta maji: Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwachimbia mabwawa wanyama hawa ili wabaki huko huko porini?

Je, ni kivutio gani ambacho Wizara imeweza kukiweka katika vivutio vya Kitaifa na kukitangaza toka Mkoa wa Singida?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii katika kulinda, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumebarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya utalii kama hivyo vilivyoainishwa, lakini ipo haja ya kuwa na mkakati maalum wa kuhamasisha utalii kwa vivutio mbadala. Mfano Desturi za asili za makabila, mapishi, urembo, shughuli zao za kila siku na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo hivi vinaweza kukuza utalii kwa mtu mmoja mmoja, vikundi vidogo vidogo na jamii moja kwa moja kwani havihitaji gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ni miti na mimea mingi ambayo inatumiwa na waganga wa jadi kwa tiba asili, na kundi hili tayari lina utaratibu unaotambulika.

MHE. RIZIKI SAID LULIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Waziri wa Maliasili, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa rai kuwa sasa hivi tuuangalie utalii katika Mikoa ya Kusini Lindi, Mtwara na Ruvuma kutokana na ufunguzi wa daraja la Umoja la Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Serikali kuipa kipaumbele Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara/Mara wameipa kisogo Mikoa hii ya Kusini na kukosesha kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa utalii mkubwa utakuwepo Kusini, naomba Serikali iandae mpango wa maendeleo eneo la Mtwara na Lindi kwa vile italeta pato kubwa kwa kutumia utalii wa bahari na pori.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Lindi kuwa na vivutio vingi hivyo Wizara iwe makini kuangalia na kulinda raslimali zisije zikachukuliwa bila kufuata taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. FREDRICK N. WEREMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na wataalam kwa kufanya kazi ya kulinda maliasili ya nchi yetu na kudumisha utalii. Aidha, tunawapongeza kwa kurudisha nidhamu katika utendaji. Bado kuna matatizo katika hifadhi na utalii lakini bila shaka mmejipangia mikakati ya kurekebisha kasoro hizo. Mchango wangu ni katika maeneo haya:-

(a) Malambo ya maji kwa ajili ya wanyama. Nashauri kwamba yachimbwe malambo katika mbuga ya Serengeti ili kuwasaidia wanyama wakati wa kiangazi. Nafahamu kwamba zipo fikra kwamba kufanya hivyo ni kinyume na uasilia wa wanyama umefika wakati wa kubadilika kwa sababu sio wanyama wote ambao wanahama wakati wa kiangazi na hao wanaobaki hasa *Western* Serengeti wanapata shida kubwa na kupoteza maisha kwa kukosa maji.

(b) Inaonekana bado hatujaimarisha ulinzi wa wanyama hasa tembo. Inasemekana wageni wanafanya uharamia wa mauaji ya tembo. Nashauri eneo hili liangaliwe kwa uangalifu, uaminifu na kujua maeneo yanayohusika. Zinunuliwe *scan machine* kwa ajili ya ukaguzi wa magari makubwa, magari yanayoonekana ni ya kusafirisha mafuta na majahazi.

(c) Ukataji wa Mbao. Inaonekana maeneo yenye misitu na miti mikubwa ya mbao sasa inakuwa *depleted*. Tunaomba hili liangaliwe kwa lengo la kuhakikisha kwamba uvunaji wa mbao uzingatie sheria na kuhakikisha kwamba Serikali inapata mafao ya mazao ya mbao.

(d) Leseni za kukata mbao. Eneo hili linalalamikiwa sana kwamba lina harufu chafu na kutozingatia haki. Badala ya kupuuza malalamiko hayo ni vema Waziri uchunguze maeneo hayo kwa lengo la kuondoa kero hiyo.

(e) Matumizi ya nyati kama nguvu kazi. Mbona hatuna mkakati wowote wa kuwapoza nyati wetu ili wapoe na kutusaidia katika kilimo. Hili lingesaidia sana katika “dhana ya kilimo kwanza”.

(f) Mbegu za Miti. Nashauri Wakala wa Mbegu za miti zisambazwe mbegu za miti katika maeneo yasiyo na miti. Nashauri kwamba mbegu hizo ziwe zinasambazwa wakati wa mvua. Maeneo kama lile la Kijiji cha Kongoto, Buswahili, Wegero na Baranga katika Tarafa ya Kiagata (Musoma vijijini), sehemu za Shinyanga, Tabora na Mwanza. Maeneo hayo yana kila aina ya kugeuka kuwa jangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa kuwa nafahamu Waziri anayo nia, ari na moyo wa kutekeleza mambo hayo.

Mhesimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja. Hotuba hii imezingatia kwa kiasi kikubwa maelekezo yaliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 – 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia hoja hii kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuwa na utendaji kazi wa pamoja ambao kwa kiasi kikubwa umeipatia Wizara hii sifa kubwa. Kila ofisi utakayokwenda utapewa maelezo sahihi na shida iliyokupeleka kuweza kuondolewa. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru sana Serikali yetu kwa kuifungua misitu ya mikoko katika Delta ya Mto Rufiji. Mara baada ya kufungua viongozi wa Idara ya Misitu na Nyuki walitembelea vijiji karibu vyote vya eneo hilo ili kutoa taarifa hiyo kwa wadau na kuwapatia utaratibu wa namna ya kuvuna miti ya mikoko kwa kutumia uvunaji endelevu. Taarifa hii imepokelewa kwa matumaini makubwa na wananchi hao na wameahidi kutoa ushirikiano mkubwa kwa Serikali yao.

Aidha, wananchi (wadau) wameitaka Serikali yao kuweza kuangalia upya viwanja vya ushuru kwa wafanyabiashara wa mikoko kwani ushuru wa sasa uliopendekezwa ni mkubwa na hakuna soko la kuaminika wanakokwenda kuuza mikoko hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri pia Serikali ikaweka utaratibu usio wa kirasimu wa namna ya kupata leseni za bashara ya mikoko – utaratibu uliopita ulikuwa hauwatendei mema wavunaji wadogo wadogo wa mikoko kwani leseni ilikuwa inatolewa na Wizara tu pale Dar es Salaam. Ni vizuri leseni hizi zitolewe na maafisa wa mikoko waliokuwa kanda ya kati (*Central Zone*) pale Kibiti. Kwa kufanya hivyo itasababisha wavunaji wadogo kuhalalisha kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu kuendeleza ufugaji wa nyuki. Katika Wilaya ya Rufiji suala la ufugaji nyuki limepewa kipaumbele, kupitia miradi mbalimbali Wilayani hapa. Wananchi wameibua suala hili na kulipa kipaumbele. Hadi sasa kuna vikundi zaidi ya 50 ambavyo vimeanzisha ufugaji huu wa nyuki. Pamoja na kuanzishwa kwa vikundi hivyo kuna wananchi wengi wanaofuga nyuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kutoa mafunzo kwa vikundi hivi vipya, namna ya kuendesha kazi hii. Mizinga mingi ya kisasa haiwavutii nyuki na kusababisha kutoingia na hivyo asali kukosekana. Elimu au mafunzo yatakayotolewa yatasaidia sana kuboresha mizinga hiyo na kuwavutia nyuki waweze kuingia kwa wingi na hivyo kusababisha kuongezeka kwa mapato ya asali na nta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri katika sekta zote na kuboresha utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa mchango wa maliasili na utalii katika pato la Taifa ni ishara ya kukua kwa ufanisi katika sekta hizo na taasisi au kampuni zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri na maombi ya jumla katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendeleza upandaji wa miti katika mashamba yanayovunwa na kuongeza mashamba mapya. Uvunaji wa miti katika mashamba ya Lunguza, Muheza na Morogoro umelipatia Taifa pato zuri na hata Halmashauri za Wilaya. Tuendeleze kasi ya kupanda upya miti katika maeneo yanayovunwa na kuanzisha mashamba mapya. Thamani ya miti itaendelea kukua katika miaka ijayo na hivyo kukuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvunaji usipite kiasi na kuharibu mazingira na barabara za Halmashauri. Uvunaji katika shamba la Lunguza, Muheza uangaliwe upya kwa sababu zifuatazo:-

(a) Maeneo ya shamba ni sehemu ya mito mikubwa inayotegemewa kutoa maji ndani ya Wilaya ya Muheza na Jiji la Tanga, kwa mfano Mto Ziggi. Kuondoa miti yote katika eneo la mto huo ni hatari kwa kupunguza uwezo wa asili wa maji ya mto huo.

(b) Magari makubwa yanayotumika kubeba magogo kutoka maeneo ya mashamba hadi viwandani na maeneo ya usafirishaji nje ya nchi kwa mfululizo wa miaka mitatu sasa yamekuwa yakiharibu barabara zifuatazo:-

(i) Muheza – Lunguza – Mashewa (barabara ya Mkoa *TANROADS*)

(ii) Bombani – Lunguza – Mashewa (barabara ya Mkoa *TANROADS*)

(iii) Lunguza - Kamba (barabara ya Wilaya ya Muheza)

Uharibifu huu ni hasara kubwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza. Malori makubwa yamekuwa yakianguka kutokana na kubeba mizigo mikubwa zaidi ya uwezo hivyo kufunga barabara mara kwa mara na kuleta kero.

(c) Kiwango cha mavuno kwa mshindi wa tenda ya kwanza *Celmac*. Ni vizuri tukafahamu hadi sasa uvunaji umefikia kiasi gani na kama bado mzabuni wa kwanza

kabisa amemaliza kiwango cha eneo lake na jinsi maeneo mengine mapya yanavyotolewa. Lengo ni kuona mantiki ya kufanya maamuzi ya ushauri wa kuendeleza au kusitisha uvunaji kwa muda kwa kuzingatia kwamba:-

(i) Tunapashwa kuangalia hifadhi ya mazingira maliasili na misitu.

(ii) Kwamba thamani ya miti itapanda na hivyo Taifa kuweza kupata mapato zaidi kwa mauzo mapya ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika. Maombi rasmi kwa kurejesha hali ya barabara zinazoharibiwa kutokana na uvunaji wa muda mrefu. Kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, tunaomba Wizara ya Maliasili na Utalii, kutumia vyanzo vyake vya mapato kupitia taasisi zake, isaidie katika ujenzi wa barabara ya Wilaya ifuatayo inayopita ndani ya eneo la shamba la Lunguza.

(1) Lunguza – Kambai

(2) Daraja moja (ndani ya shamba la Lunguza)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imeweka katika mpango wake barabara hiyo 2010/2011, lakini itahitaji msaada kwa kuwa Mfuko wa Barabara hautaweza kukamilisha ujenzi huo kwa mwaka 2010/2011. Tunaomba ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutafuta, kutathmini, kuainisha na kutangaza viashiria vya asili na mila kwa kivutio cha utalii. Mkoa wa Tanga katika Mkutano wake wa Kamati ya Maendeleo ya mkoa mwezi March/April, 2010 ilipokea taarifa ya awali ya vivutio hivyo vya asili na mila kutoka Wilaya zote za mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vyanzo hivyo vitasaidia sana kuvutia utalii na kwa kuwa mikoa haina mafungu au kasma nzuri kwa ajili ya kazi hiyo ipo haja Wizara ya Maliasili na Utalii, kuweka nguvu na msaada katika kuwezesha zoezi hilo kufanyika kwa ufanisi na kwa haraka. Hii itawezekana kwa kupitia Ofisi za Misitu, Mkoani na Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kutekeleza kwa vitendo sheria mpya ya utalii ikiwa pamoja na kuweka madaraja katika mahoteli hapa nchini na kusimamia vizuri sekta ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kuwa Malagarasi Wetlands ni eneo la Ramsa Site. Hata hivyo, eneo hili linagusa Wilaya za Kasulu, Kigoma na sasa Wilaya mpya ya Kaliua zamani Urambo.

Eneo hili limevamiwa na mifugo mingi kupita kiasi ya Watanzania jamii ya Wasukuma. Wengi wao ni wale waliofukuzwa Lake Rukwa, Ihefu, Tabora na wanaokimbia ukame huko Shinyanga na Mwanza. Eneo hili lipo hatarini. Nimeshangaa ukurasa wa 50 wa hotuba hausemi chochote kuhusu eneo hili. Ninashauri *strongly* eneo hili, Wizara iisaidie sana Halmashauri za Wilaya za Kasulu, Kigoma na Urambo/Kaliua ili kuondoa ng'ombe wengi waliozagaa na kutoa Elimu kwa vijiji vinavyozunguka eneo hilo. Sina hakika kama katika Wilaya 10 tajwa na Wilaya ya Kasulu imehusishwa. Naomba ufafanuzi. Sehemu kubwa ya Mto Malagarasi, *wetlands* ipo katika Mkoa wa Kigoma na hasa Wilaya ya Kasulu.

Hatari iliyopo ni kwamba, endapo Wizara haitazisaidia Halmashauri za Wilaya tajwa, ipo hatari kubwa eneo hili kutoweka. *Something has to be done now.*

Hifadhi ya Misitu na Nyuki katika Mapori ya Misitu ya Akiba *(Forest Reserve)* za Makere, *North, South* na Mkuti. *(Visits done by Ministry officials in Kasulu 2009).* Ninaishukuru sana Wizara, kupitia Kurugenzi ya Misitu kwa kutuma 2009 Wataalam kuja Kasulu kuona hali halisi ya maeneo hayo ya Misitu ya Akiba.

Yapo makosa yaliyofanywa na Serikali miaka ya 1972 hadi 1974, ambapo Zoezi la Operesheni Kigoma *(Villagezation Scheme),* bila kujali maeneo hayo ya Hifadhi ya Misitu, watu walipelekwa katika maeneo hayo. Vijiji vya Kwaga, Kigembe, Zeze, Bugaga na Muzye, sehemu kubwa vipo eneo/ndani ya eneo la Mkuti South. (Ramani za 1954 zinaonesha hivyo). Aidha, Vijiji vya Makere, Mvugwe, Kagera Nkanda, Mvinza, Kabalanzwili na sehemu ya Vijiji vya Rungwe mpya navyo kwa mujibu wa Ramani tajwa, vipo ndani au sehemu kubwa ya vijiji hivyo vipo ndani ya maeneo ya *Forest Reserve.*

Tume imekamilisha ripoti yake, tunashukuru sana, mimi Mbunge nimepata nakala yake. Mapendekezo yake ni mazuri, isipokuwa yanahitaji kufanyiwa kazi kwa umakini ikizingatiwa kwamba, sasa idadi ya watu imeongezeka zaidi ya mara kumi *since 1954* na maeneo mengi sasa ni vijiji kamili. Hivyo, misitu haipo tena na kama ipo ni mashamba ya wanavijiji. Kwa mujibu wa Ripoti ile, ninashauri ramani zipangwe/zichorwe upya ili kuainisha hali halisi ya sasa.

Maeneo yenye Mashamba ya vijiji na Makazi yao ya kudumu yaheshimiwe na sasa maeneo hayo yabadilishwe na kuwekwa chini ya *Village Forest Schemes* (Misitu ya Vijiji) ili Wananchi wasipate usumbufu usiokuwa wa lazima.

Elimu ya Misitu na Nyuki itolewe kwa nguvu zaidi kwa maeneo haya ya Kasulu ili Wanavijiji wajue dhana ya Kilimo Mseto na Kilimo Misitu. Bila shaka Wananchi wanaweza kulima kilimo bora kinacholinda mazingira na misitu ya asili.

Vitendo vya kutesa/kupiga Wananchi eti wamevamia Misitu ambayo kimsingi haipo au ilishavamiwa miaka 40 iliyopita iachwe mara moja. Vikosi vya dolia vijielekeze maeneo ambayo kweli misitu hiyo bado ipo na katika Wilaya ya Kasulu baadhi ya maeneo yapo na mengi yapo karibu na Kitalu cha Nyamloha na baadhi ya sehemu za Makere South.

Wizara ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kukabiliana na tatizo la moto katika misitu. Tatizo hili ni kubwa na linaharibu misitu michache iliyobaki. Fedha zinahitajika kama nyenzo kusaidia zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa za kulinda na kuhifadhi rasilimali zetu, bado lipo tatizo kubwa la upungufu wa rasilimali fedha na watu katika uhifadhi wa rasilimali hizi. Naomba Wizara iweke mkakati wa makusudi wa kuongeza Watumishi katika kukabaliana na tatizo hili la kuwa na eneo kubwa la hifadhi za misitu na Wanyamapori, lakini wahifadhi ni wachache. Aidha, maslahi na vitendea kazi havitoshelezi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nitaomba ufafanuzi katika masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi, Wizara ina mpango gani endelevu wa matumizi ya Kituo cha Mlele katika Mradi wa Rukwa Lukwati; kwa kweli kutokitumia ipasavyo Kituo hicho ni mambo mawili ama hatuna maamuzi yetu wenyewe na kutekeleza wanavyotaka wafadhili, kwa maana uwekezaji uliopo pale na matumizi yake hayana ulinganifu, hakuna vitendea kazi magari na wahifadhi, hao wachache waliopo wanaishi kama wafungwa katika kambi ya mateso. Kama busara na utafiti wa kutosha ungefanywa, basi tusingewekeza pale mahala, bora na sahihi ilikuwa Sitalike lakini pia eneo la mradi ni kubwa, kwa namna yoyote ile ipo haja ya kupitia upya mpango wa uhifadhi wa eneo hili kwa kuwa wakati wa masika eneo kubwa halifikiki kwa urahisi na kutoa fursa kwa ujangili hata hiyo maana ya kuhifadhi inapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa niaba ya Wananchi wanataka kufahamu juu ya Mradi wa Ubende WMA. Inawezekana zikawepo faida lakini ni lazima Wananchi washirikishwe. Je, Ubende WMA iliwashirikisha Wananchi wa vijiji vinavyozunguka kwa kiasi gani; na je, zimeangaliwa faida na hasara kwa kuwanyang'anya Wananchi maeneo yao ya kilimo kupanua mipaka ya Ubende WMA?

Kama nchi ambayo haijitoshelezi kwa chakula na idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kubwa na huku upo mkakati wa makusudi wa kuwapora ardhi zao katika Mradi huu wa Ubende WMA, maeneo ya kilimo lazima yaachiwe kwa Wizara kuagiza na kuelekeza njia bora ya kumaliza mgogoro ambao upo. Hata kama mtakataa ni dhahiri tija ya kuwepo kwa Ubende WMA haitaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara isimamie jambo hili kwa faida ya wote, watu na wanyamapori. Ustawi wote unategemea watu kuwa na chakula pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ukataji holela wa misitu kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya binadamu ikiwemo nishati (mkaa); kuna mpango gani umeandaliwa kuhusu nishati mbadala na hatua au maelekezo ya Wizara juu ya Watendaji wao wanaotoa vibali vya kuvuna misitu kwa ajili ya mkaa katika hifadhi za misitu kama vile Hifadhi ya Msitu wa Kalambo na mingineyo? Umefika wakati sasa tuheshimu na kusimamia sheria zetu zilizopo. Kadhalika, ningependa kujua michango ilyotolewa katika miradi ya kijamii na makampuni ya uendeshaji na kama makampuni hayo yametekeleza wajibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

MHE. NURU A. BAFADHIL: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kidogo tu kuhusu utalii. Tanzania tuna bahati ya vivutio vingi vya kitalii ambavyo vikitumika vizuri vitaingiza tija kwa Taifa letu. Tuchukue fukwe zetu za bahari tu; tuna bahati ya fukwe nzuri za bahari ambazo ni vivutio kwa watalii, lakini kubwa nasi kama Watanzania tuwe wabunifu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna fukwe ambazo tunaweza kujenga hoteli nzuri za kitalii lakini fukwe hizo zinabaki tu kuoteshwa mikoko. Mfano, Jiji la Tanga sehemu ya Utoofu karibu ya daraja, pale kama serikali itajipanga vizuri inaweza kujenga hoteli nzuri za kisasa ambazo watalii watafika na kuliingizia Taifa fedha. Je, kwa nini hawa wawekezaji hawahamasishwi kujenga hoteli hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bandari ya Jiji la Tanga kuna Kisiwa ambacho kina mambo ya kale kama kisima kirefu sana ambacho kilitumiwa miaka kadhaa iliyopita, pia kuna handaki ambalo Waarabu walitumia kujificha. Vitu hivi ni vivutio vizuri; kwa nini Serikali haiamui kujenga au kutafuta mwekezaji ili aweze kujenga hoteli nzuri ya kisasa kama wenzetu wa nchi nyingine wanavyotumia visiwa vyao katika kuwaingizia pato la nchi zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Jiji la Tanga kuna magofu ya nyumba na misikiti ambayo yapo katika ufukwe wa Kata ya Tongoni. Hapa inaelekea yamesahauliwa kabisa, ambapo ni historia nzuri kwa vizazi vilivyopo na vijavyo.

MHE. ZAKIA H. MEGHJI: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utalii katika Mikoa ya Kusini lazima liwekewe mikakati thabiti *"Tourism going South"* isiwe tu kutangaza, bali kuhakikisha miundombinu inakuwepo kuwafikisha watalii huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam siku zote imekuwa *the transit destination,* ni muhimu Dar es Salaam ikawa pia *one of the destinations* tuangalie mambo gani tunaweza kuyatangaza na hivyo kuwahamasisha wenye Kampuni za Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingi zenye historia ndefu zimehakikisha kuwa majengo ya kihistoria hayavunjwi hata kama matengenezo yatafanyika au ujenzi basi ufuate *structure* zile zile. Kutofanya hivi ni kupoteza kabisa historia yetu. Dar es Salaam na majengo yake ya zamani ingeachwa watu wangejenga sehemu nyingine, tuwe na "*Old* Dar es Salaam" na "*New* Dar es Salaam". Tutilie pia mkazo kwa wawekezaji wajenge vituo vya Mkutano ili tuendeleze "*Conference Tourism*".

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuomba kuuza meno ya tembo huko "*cites*" pamoja na yote yatakayofanyika, ni muhimu kujiandaa vizuri kabla ya kwenda kwenye kikao. Tuwe na "*International lobbyist"* ili tujue nini tunafanya. Pia katika hii miaka mitatu tuwe tunajibu hoja mbalimbali kupitia magazeti na *internet* pale ambapo tunachafuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wengi wa Vijijini na hata baadhi wa mjini hatuna mkaa na hivyo kuendelea kukata miti. Ni muhimu programu iliyoanza katika baadhi ya Wilaya ya kudhibiti na kuvuna miti ikaendelezwa katika Wilaya zingine. Hii itawezesha wanavijiji kupanda miti inayoweza kuvunwa katika miaka michache na kuwa na mzunguko wa kuvuna miti na hivyo kupunguza kwa sehemu kubwa ukataji miti kwa ajili ya uchomaji wa mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini malengo ya Mkutano wa Diaspora. Mbali ya kubadilishana mawazo na kadhalika, ni muhimu watu wenye asili ya Afrika waje kuwekeza Tanzania na waonekane waziwazi kufaya hivyo. Bila ya kufanya hivyo mkutano huo utabaki tu kama "*one of those meeting*". Ni muhimu pia matangazo ya utalii yaende sambamba na hali ya teknolojia ya habari ambayo ndiyo inatawala dunia hii sasa. Kwa hivyo, *websites*, *internets*, n.k viweze kutumika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nawapongeza na nawapa pole pia kwa kifo cha Mira ambaye ni mmoja wa Wakurugenzi wa *Bradford Group* huko Marekani.

MHE. ANNA M. KOMU: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, naomba niwapongeze wale wote wanaofanya bidii kuhakikisha mali ya Watanzania inahifadhiwa kwa ajili ya Watanzania, nikianza na Waziri Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Ezekiel Maige na bila kumsahau Katibu Mkuu Dr. Ladislaus Komba na wote wanaoshirikiana pamoja kuhakikisha Mheshimiwa Waziri anafanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii ni nguzo nyingine muhimu inayotoa fedha za kutosha kuifanya nchi hii iweze kuendelea, tusipoiangalia Wizara hii muhimu kwa umakini, tutaendelea kulalamika kila siku na neno umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivutio vyetu vya utalii lazima tuviangalie kwa umakini mkubwa, naomba kutoa rai:-

(1) Vivutio vyote vipitiwe na kuangaliwa upya, kwa kufanyiwa ukarabati na kuhakikishiwa wale wanaotunza vituo hivyo wanalipwa vizuri ili wawe wanatunza mali hiyo muhimu;

(2) Kuhakikisha kuna uaminifu wa kutosha, kuwalinda na kuwatoa hadharani wale wote wanaohusika kuangamiza wanyama wetu kama Tembo, Pundamilia, Twiga, Simba na wanyama wote ambao ni vivutio vya watalii;

(3) Kuhakikisha tunalinda misitu yetu kwa kutokutoa vibali vya ukataji miti kiholela kwa manufaa ya watendaji, tutamaliza miti iliyobaki kwa uroho;

(4) Kulinda vyanzo vya maji, kuhakikisha maporomoko yetu hayakauki *(water falls)* kwani ni kivutio cha kutosha unapoona maji safi, mazuri yanateremka kwa mbwembwe milimani; na

(5) Kuulinda Mlima wetu Kilimanjaro na moto unaowaka kila siku ya Mungu na kuharibu uoto wa asili na misitu, miti mikubwa na kadhalika. Hii inafanya mlima huu kutoa joto kali ambalo linayeyusha barafu na kuharibu uzuri wote wa mlima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia Jedwali Na. 6(a) na kuona kifungu namba 270371, 270372, 270368, 270369, hakuna mishahara ni matumizi mengineyo tu, ningeomba kujua vyuo hivi havina Walimu wala wafanyakazi? Eneo kama Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BT) ambapo hivi sasa tunasema tujitahidi kukuza ufugaji wa nyuki ili tuweze kupata asali na kuongeza fedha za kigeni, kama hakuna Walimu vyuo hivyo vinaendeshwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri, ukurasa wa 58 inayoelezea sekta ndogo ya mambo ya kale, kama tutazingatia na kutekeleza hayo yaliyoorodheshwa hapo itakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningewaomba tena Wizara hii kuacha kuongea na kuandika vitabu mwaka hadi mwaka kama mwendelezo wa kutekeleza *Budget* Bungeni, sasa tutekeleze kwa vitendo. Tuhakikishe yote yale ambayo yataleta fedha ili tumudu *Budget* yetu bila kusubiri misaada basi tusiache tutekeleze kwa ufanisi na nguvu zote ili tupate hayo maisha bora tunayoyataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kusahau, naomba sana kusaidiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ili Wizara hizi mbili ziangalie njia mbadala ya wananchi kuweza kupata nishati ya kutumia kwa kupikia na kuachana na mlipuko huu wa kukata miti kiholela hasa miembe kwa ajili ya mkaa na pia baadhi ya viwanda ambavyo huwa wanaona umeme ni ghali basi na wao kukata magogo ya miembe ili kuendesha viwanda vyao. Naomba sana muangalie hili kwa dhati kwani miti inakwisha na tutakuja kujikuta tumebakia na majangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naomba tena tuwe Watanzania wa kulinda mali sio wa kufuja mali kwa maslahi binafsi, hatufiki popote ila tutaacha watoto wetu kwenye umasikini uliokithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya kale, Tabora Mjini kuna Kituo cha Mambo ya Kale pale Kwihara, je, Serikali inapaangaliaje maana ni sehemu ambayo kama haipo chini ya Serikali hata *solar* tu hawana na kituo chenyewe hata hakitangaziki kuna mpango gani wa kukiboresha? Je, kuna utaratibu gani hivi sasa kuangalia barabara iliyopitishwa Kilatumwa nayo ikatangazika na wananchi wa Tanzania wakafahamu hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Rais Mstaafu Marehemu Mwalimu Nyerere alikuwa ni Mwalimu na hata mahala alipokuwa akifanyakazi papo na wala hatuoni kama hiyo ni historia ya kuangalia? Pia hata maeneo yaliyopigiwa kura TATU ya kutufikisha hapa hatupatambui, je, historia yetu tunakubali kuitupa bila ya kufuatilia, tunasubiri Wazungu waje kutusomea historia yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu, naunga mkono hoja.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu ya Dr. Livingstone Ujiji. Jengo la kumbukumbu ni duni sana, hakuna vifaa vya kutunzia kumbukumbu, mfano picha na baadhi ya maandishi zikiwemo barua alizoandika Dr. Livingstone, magazeti na kadhalika yanawekwa juu ya meza duni mno kiasi kwamba vinaharibika kwa vumbi, rahisi kunyeshewa na mvua.

Cha kushangaza zaidi jengo lenye kumbukumbu halina hata umeme. Kwa nini Serikali isirekebishe lile jengo, likawekwa umeme na zikatafutwa *shelf* (makabati) ya vioo ambayo yatasaidia kuhifadhi vitu vyote muhimu kwa kumbukumbu iliyokusudiwa kutunzwa kwa ajili ya vizazi vijavyo ili watalii waangalie vikiwa kwenye ma-*shelf* maalum. Naomba majibu ya Serikali ni lini pataboreshwa, panatia aibu. Hapafanani na historia iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gombe ni hifadhi nzuri sana, wapo wanyama aina ya *gorilla*, lakini haitambuliki sana duniani kwa sababu ya ubovu wa miundombinu, vivyo hivyo hifadhi ya Mahale. Je, Serikali ina mpango gani wa ku-*promote* ili kusaidia *information* ziwafikie watalii wengi zaidi? Je, hifadhi hizo huendeshwa kwa hasara kiasi gani maana watalii wanaotembelea kule ni wachache lakini wapo walioajiriwa katika hifadhi hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, inabidi tuhifadhi maeneo muhimu yenye vitu asili, wanyama na hifadhi zote za Taifa. Lakini naomba nipatiwe majibu kwa nini Serikali imeruhusu uchimbaji madini ndani ya Hifadhi ya *Selous*? Sheria ililetwa ikakataliwa, iweje Serikali iruhusu? Kwa nini Bunge haliheshimiwi? Nini maana ya mgawanyiko wa majukumu na madaraka? Ilikataliwa kwa maslahi ya Taifa kwani bado maeneo mengi yaliyowazi yanachimbwa madini kwa nini tuingie hadi ndani ya hifadhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, gawio toka uwindaji wa kitalii, naomba Serikali ieleze kwa nini gawio la 25%, halitolewi kwa Halmashauri zote zenye vitalu vya utalii wakati pesa zilishalipwa toka mwaka 2008/2009? Ni lazima Serikali itambue walinzi wa kwanza wa maliasili zinazowazunguka ni wananchi na taarifa zilizopo ilishatolewa pesa Shs.1,516,839,511.1 ambazo zilitolewa na Makampuni yenye vitalu kwa ajili ya Halmashuri 37 zilitolewa Shs.890,000,000.00 tu. Serikali ieleze kwa nini haikutoa fedha kwa Halmashauri kwa wakati husika, haioni kuwa inachelewesha maendeleo hivyo kudhulumu haki ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibiwe yote niliyohitaji.

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kwanza kutoa pongezi kwa Wizara hii kwa jinsi ilivyojisafisha na kujiepusha na matatizo ya kiutendaji yaliyokuwa yakiikabili Wizara hii na kusasabisha kashfa kubwa kwa Taifa. Naamini hayo yote ni kwa sababu ya umakini uliopo na Rais wetu Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Mwangunga na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Maige (Mb) bila ya kuwasahau watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Komba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam tumeweza kutambua maeneo muhimu yenye historia ya kale kama vile Misikiti na magofu mbalimbali ambayo tunayaona ni muhimu kuyaingiza katika mpango wa Jiji na Taifa kwa jumla katika sekta ya utalii ikiwa ni pamoja na sehemu za visiwa vilivyomo katika mamlaka ya Jiji hilo. Nashauri Wizara ichukue juhudi za makusudi kuunga mkono Jiji la Dar es Salaam kuibua maeneo hayo mapya ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado naomba kutoa rai kwa Serikali kuangalia uwezekano wa Dar es Salaam kufaidika na maliasili tuliyonayo ya bahari. Halmashauri za Manispaa za Temeke, Kinondoni na Ilala hazipati faida yoyote kutokana na rasilimali ya bahari tuliyonayo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Serikali ikaanzisha utaratibu wa kulipatia Jiji la Dar es Salaam, Temeke, Ilala na Manispaa ya Kinondoni malipo ya mrahaba kutokana na rasilimali hiyo kama wenzetu wenye dhahabu na madini mengine wanavyopata mrahaba kutokana na maliasili hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara kuandaa hotuba na kuileta hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo usawa wa utekelezaji wa shughuli za ukusanyaji mapato ya mazao ya misitu katika Halmashauri zote Tanzania Serikali Kuu ijiondoe kwenye Wilaya ambako inakusanya kwenye ardhi ya vijiji, ijikite kukusanya kwenye maeneo ya mashamba/miradi ya misitu kama Meru, *Sao Hill*, Kiwira na ulinzi

uimarishwe kwenye misitu ya vyanzo vya maji. Idara ya Wanyamapori imekasimu tayari kazi hiyo, sekta ya misitu bado kwa baadhi ya Halmashauri za Mkoa wa Tanga, Kilimanjaro na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvamizi wa mifugo kwenye maeneo ya hifadhi tunajifunza nini kutoka Bonde la Ihefu? Kilio cha kukauka kwa Mto Ruaha kilianza mwaka 1997 kwa mhifadhi wa hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lilikuwa Bwawa la Lutena na Kidatu likapungua maji, umeme ukawa wa mgao tatizo likatanuka na kuathiri uzalishaji wa viwanda nchini, uchumi ukaguswa na kudorora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetumia mabilioni ya fedha kuainisha tatizo, baadaye uvumbuzi ukawa ni kuhamisha tatizo la mifugo toka eneo moja kwenda eneo lingine. Kwa kiasi kikubwa mifugo ilitua Morogoro haikwenda tulikolenga. Ardhi zake tutegemee Mto Wami/Ruvu kujaa matope kuhama mwelekeo, kuziba mitambo/mabomba ya kusukuma maji, kukosa maji ya viwanda majumbani na katika mbuga za wanyamapori, wanyamapori kusogelea maji na kuhatarisha maisha ya wananchi. Serikali italazimika kutoa tena fedha kutibu hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya utalii kwenye Halmashauri zetu siyo kipaumbele na hivyo zinaendeshwa kama yatima. Bunge la mwaka 2008/2009 na 2009/2010 lilitambue idara zisizopata ruzuku na kushauri Serikali itoe shilingi 200,000 na baadaye shilingi 300,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Idara ya Maliasili inayoratibu shughuli za sekta saba za wanyamapori, misitu, nyuki, mazingira, uvuvi mambo ya kale na utalii kwa fedha hizo ni wastani wa shilingi 44,000 kwa sekta wanunue shajara, mafuta ya doria na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii yenye mchango mkubwa kwenye vyanzo vya maji hali ya hewa na kilimo kwanza na umeme majumbani. Wizara ambazo hunufaika na matokeo ya uwepo wa hifadhi hizo za maliasili tumezifanya nyeti na kuzipa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo ushahidi wa kutosha Idara hii kutofikishiwa kinachoamuliwa hapa Bungeni na uratibu wake ni mgumu kwani Idara hii ipo TAMISEMI kiutawala na kitaaluma ipo Wizarani. Kilio chao nani atakifichua? Ndio maana nimefananisha Idara hii na yatima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujangili bado unakuwa na kubadilika. Vyombo vya usafiri vya boda boda hupeleka majangili maeneo nyeti na baadaye kusafirisha nyara. Zana za usafiri zipelekwe kwenye Halmashauri zenye kuonyesha fukuto la utambuzi wa matukio haya ya mbinu mpya na ujangili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie utaalam wa kutumia vinasaba ili kutambua nyara, kupunguza nyama ya swala kuwa ya mbuzi au pembe ya faru kuwa ya ng'ombe. Kesi nyingi za ujangili hufutwa kwa *Cap.* 225(5) kesi za ujangili hupelekwa kwenye uhujumu uchumi na liikuwa na lengo mahususi. Serikali iangalie ukweli matumizi ya kifungu hiki kufuta kesi za ujangili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza kinaweza kuwa janga kwa uhifadhi kama matumizi bora ya ardhi hayatahusisha sekta za maliasili. Shoroba ziainishwe na kuwekwa kwenye ramani za Halmashauri kupunguza migogoro ya watu na wawekezaji na wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999, migogoro mingi baina ya wananchi na hifadhi yamesababishwa na utekelezaji wa sheria hii. Watu wajanja wanawarubuni wananchi kwa kuomba ekari 50 kila msimu na kijiji kushtukia maelfu ya ekari yapo kwa mtu mmoja kwa kutumia muhtasari ya kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine vijiji hugawa maeneo ya hifadhi kwa wageni bila kujua kwa mfano *Pagale Forest Reserve* imegawanywa kwa wageni. Wenyeji wengi wanatambua hifadhi lakini mamlaka ya Serikali za Vijiji (viongozi) hupotosha wananchi.

MHE. ENG. DR. JAMES A. MSEKELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutamka kwamba naunga mkono hoja hii. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kipindi cha miaka mitano wakitekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia yangu katika mchango wangu mfupi ni kusisitiza juu ya umuhimu wa Wizara hii na TAMISEMI kufikia muafaka kabla ya kuingia na kuchoma moto makazi ambayo yanakuwa yamefanya hata chaguzi na kupata Serikali za vijiji na vitongoji na hata maeneo hayo kuwa yamejenga hata shule, zahanati na huduma zingine kwa wananchi kuwa wameshirikiana na Serikali, ikiwa ni pamoja na kupata fedha za Halmashauri za Wilaya katika kutekeleza miradi hiyo. Mtafaruku baina ya hata Wakuu wa Idara katika Halmashauri moja kuhusiana na uhalali wa makazi fulani (kwamba yamo ama yapo nje ya hifadhi) hautakiwi kuwepo, hasa pale ambapo hata rasilimali fedha na watu kuwa zimepelekwa na Halmashauri wanayosimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kukuta *DNRO* na *DED* wake, wanaokaa pamoja katika *CMT*, wanahitilafiana kuhusu uhalali wa makazi/vijiji/vitongoji huku tayari Serikali imepeleka fedha na hata watumishi wa kada ya afisa misitu katika Kata, Maafisa ambao pia hata kuhudhuria *WDC* chini ya Diwani anayekuwa madarakani akijua maeneo yake halali kama msimamizi wa uchaguzi *(DED)* alivyoyatambua maeneo hayo na hata kuweka vituo vya kupigia kura na kuendesha uchaguzi wa viongozi katika maeneo hayo.

Ni aibu kubwa kwa Serikali na hili halitakiwi kuwa tatizo la wananchi hata kidogo. Serikali haiwezi kupeleka fedha/rasilimali katika kijiji/kitongoji kwa mkono wa

kulia na mkono wake wa kushoto ukaenda mahali hapo na kuziondoa rasilimali hizo na kuvunja makazi, tena kwa kuchoma moto na pengine kwa baadhi ya watumishi wake kuwatendea wananchi wake matendo ya kikatili na pengine kupoteza hata mali zao. Hili linakera, hili linasikitisha na kwa kweli matendo kama haya yanaitia aibu kubwa Serikali na kukipaka matope Chama Tawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaliyotokea kwa wananchi wa Kitongoji cha Fila, Kata ya Bukumbi Wilayani Uyui hayapaswi kutokea tena kama Serikali ni moja na inafanya kazi kama chombo kimoja cha maamuzi na utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ihamasishe Watanzania kutembelea hifadhi za wanyama. Pia Wizara ijenge hoteli za gharama nafuu kuwawezesha raia wa hali ya chini kuweza kugembelea hifadhi zetu. Pia yawepo mabasi ya gharama nafuu kuweza kukodishwa na wananchi wasio na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ihamasishe wanachi kutembelea makumbusho ya Taifa. Watoto wahamasishwe kutembelea makumbusho kujua historia ya nchi. Nchi zingine mfano Uturuki hupata watalii wapatao 15,000 kwa siku kwa eneo moja hivyo hupokea fedha nyingi kwa utalii wa ndani tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iwasimamie/kuwawajibisha watendaji idara ya misitu wasio waaminifu wanaoshiriki pamoja na majangili kuvuna mbao bila kufuata autaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, maliasili ina changamoto nyingi na inahitaji uvumilivu mwingi. Hifadhi ya Msitu wa Kalambo haijatendewa haki hata kidogo. Maofisa Maliasili wa Wilaya ndiyo chanzo cha uharibifu wa msitu huu kwa kutoa vibali vya uvunaji mkaa kiholela na kuwanufaisha watu wasio na uchungu na msitu huu.

Himizeni mkaa wa mawe uanze kutumika mijini ili kuokoa misitu yetu la sivyo miaka michache ijayo misitu itatoweka, mvua itatoweka na matokeo yake ukame na njaa vitafuata katika Mkoa wa Rukwa, Wilaya ya Sumbawanga na Wilaya mpya ya Kalambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Kalambo Falls* Wizara haijafanya lolote kuyaendeleza kwa utalii. Magofu ya Bismark pia Wizara imeacha yatumike na *detach* ya jeshi je, watalii toka Ujerumani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji moto ya Kizambwe na Makal, je, maliasili mnayafahamu? Je, mnefanya nini? Karibu mapango yaliyopo Tatanda hayajulikani hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itusaidie tuokoe maliasili, misitu, wanyama na vivutio vya utalii katika Wilaya ya Kalambo kwa kuwa na doria za mara kwa mara. Naomba kuwasilisha.

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza kazi za Wizara na mipango yake ya baadaye pamoja na kazi iliyofanyika mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukataji wa miti na uchomaji wa mioto katika maeneo mengi nchini bado umekithiri. Aidha, elimu inahitajika zaidi hasa katika maeneo ya vijijini tuuelimishe umma kuhusu athari za kupata mafuriko na jangwa kwa vizazi vijavyo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka michache iliyopita katika banda la utalii, wakati wa Saba Saba, ilielezwa kuwa vinyonga vyenye pembe tatu vinapatikana tu katika Msitu wa Hifadhi ya Vikindu iliyopo kati ya Dar es Salaam na Mkuranga katika Wilaya ya Pwani, katika miaka ya 1990 msitu huo bado ulikuwepo. Nyakati za jioni wanyama kama simba na kadhalika walikuwa wakionekana hata barabarani. Jambo la kusikitisha sana, hivi sasa wanyama hao wametoweka na Msitu wa Vikindo umekaa wazi na *bushes* tu bila miti! Nataka Wizara hii inifahamishe wale vinyonga wa pembe tatu watakuwa wemekimbilia wapi? Ni aibu tena kwa Taifa kupoteza rasilimali ya viumbe kama hivyo, tulivyopewa na Mwenyezi Mungu, kutokana na uzembe wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango upi wa kuwahifadhi vinyonga hao na pia kuwatengea eneo linalowastahili ambapo watawweza kuzaana tena kwa wingi. Wizara pia ina mpango gani katika kuhakikisha Msitu wa Vikindo unapandwa miti tena?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lililopita nilizungumzia na kama mtu wa kwanza kuzungumzia kuhusu mjusi mkubwa wa Lindi *(Dinosaur),* aliyepelekwa Ujerumani na kuitaka Serikali yetu izungumze na Serikali ya Ujerumani ili wawezeshe kurudishwa kwa masalia ya mjusi huyo. Hivi sasa tunaamini kuwa mipango inaandaliwa na Serikali zote mbili kurudisha masalia ya mjusi huyo. Tunashukuru kwa hatua hiyo iliyochukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania bado tuna masalia na vifaa vingine vingi tu vilivyochukuliwa na nchi ya Kenya, Uingereza na nchi zingine. Hivi Serikali inafanya mpango gani katika kuhakikisha vifaa hivyo vinarudishwa nchini Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hizo zimefaidika sana na kupata mapato kwa miaka mingi. Hivi Serikali haioni sasa ni wakati ufike katika kuhakikisha kuwa baadhi ya mapato hayo kwa pamoja tunagawana ili na sisi Tanzania tupate haki yetu. Jambo la muhimu ni kuhakikisha kuwa masalia yetu na vifaa vinarudishwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, fundisho la vyura vya Kihansi waotoweka kutokana na uharibifu wa makazi ya viumbe hivyo na kupelekea nchi ya Amerika kuchukua baadhi ya vyura hao ili wakazalishwe huko Amerika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali bado inaendelea kuweka miundombinu katika maeneo mbalimbali nchi kama vile katika Mto Maragarasi, Serikali sasa ina mpango gani katika kuweka mazingira mazuri wakati wa ujenzi wowote katika mto huo, kuhakikisha viumbe hao kama vile konokono, vyura na kadhalika vinalishwa na kupewa haki yao ya makazi yao waliyoyazoea, sehemu ambayo haina maji yaliyochujwa na kuacha maji ya asili yao yenye tope na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate majibu ya uhakika tafadhali na naunga mkono ila nahitaji ufafanuzi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaeleza, tumewapa nafasi wachangiaji kama 14 kwenye Wizara hii, lakini kama mnavyotambua, Wizara ilikuwa imetanguliwa na Kauli za Serikali ambayo nayo ilikula muda. Kwa hiyo, naona tuingie kwenye hatua nyingine ya wenye hoja kuanza kujibu. Sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye itabidi ajibu hoja zenu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niseme ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na kwa kuzingatia kwamba Bunge hili ni la mwisho, mengi yamefanyika, nilikuwa naomba ruhusa yako niseme angalau mambo mawili au matatu ya utangulizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninaomba nimshukuru sana kwa mara nyingine Mheshimiwa Rais, Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani kubwa aliyonipa kwa kunipa dhamana hii ya kumsaidia katika kusimamia raslimali za nchi yetu kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kwa namna ya pekee sana nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mizengo Kayanza Pinda, kwa uongozi wake nzuri na mahiri. Amekuwa ni Mwalimu wangu mzuri sana wa mambo ya uongozi, nimekuwa nikijifunza kwake mambo mengi kwa kumwona anavyofanya na ninaamini kabisa kwamba Mungu atazidi kumbariki na atazidi kutuongoza, na mimi kama mwanafunzi wake basi nimuahidi kwamba nitaendelea kuwa mwanafunzi mzuri, mwenye bidii katika kulinda raslimali za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pie nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu mama Shamsa Mwangunga ambaye kwa kiasi kikubwa sana amekuwa ni mwongozaji wangu mkubwa wa kunifundisha na kunielekeza nini cha kufanya. Sina cha kumlipa zaidi ya kumtakia kheri njema kule Ubungo, ninaamini Mwenyezi Mungu atambariki na tutaweza kujumuika pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, niwashukuru sana wataalam mbalimbali kwenye Wizara ambao wamekuwa ni Walimu wangu wa kunifundisha taaluma hii ya uhifadhi kutoka kwenye taaluma yangu ya awali ya uhifadhi wa fedha. Sasa ninajifunza kuhifadhi vitu na wanyama. Ninawashukuru sana, wamenisaidia sana kujifunza jambo hili jipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie shukurani zangu kwa namna ya pekee kabisa kwa kuwashukuru wananchi wangu wa jimbo la Msalala kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika kufanikisha maajabu ya kimaendelea tulioyafanya kwenye jimbo letu katika kipindi kifupi. Tunaita maajabu kwa sababu wengei waliofika kwenye jimbo lile sasa na waliowahi kufika miaka mitano nyuma wanakiri kwamba, mengi yamefanyika.

Nawashukuru kwa uhakikisho ambao wamekuwa wakinipa kwamba pamoja na kauli yao kwamba, wao hawababaiki na mavuvuzela, wanaendelea na mchakato wa kunithibitisha tena kuwa Mbunge wao na wamesema kwamba, watu wanaofikiria jambo hilo watawaonesha kwa kunipigia kura zote, ili kuonyesha kwamba kweli wanachokisema wamekidhamiria.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie kwamba niko tayari kuendelea kuwatumikia kwa moyo zaidi lakini kwa kutumika uzoefu ambao nimekwishaupata, ninaamini tuliyokwishayaanza tutayafanikisha kwa nguvu zaidi, ari zaidi na kasi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuishukuru familia yangu, mke wangu Liberatha na vijana wetu God na Kabula ambao leo walisema waje hapa Bungeni kunitakia kheri na kama ambavyo wamekuwa wakiniombea siku zote ninawashukuru kwamba, wamekuwa ni watu wa msaada sana kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, naomba sasa nipitie baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Ziko hoja nyingi kama unavyofahamu, lakini pia kwa kuzingatia muda ambao umekuwepo hasa wa kuandaa inakuwa siyo rahisi kuzijibu moja moja. Hakika zipo nyingine ambazo tunaweza tusizifikie, lakini tunaamini kwamba Waheshimiwa Wabunge watapata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na baadhi ya hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Dada yangu Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kwa mchango wake katika taarifa ya Kambi ya Upinzani, amezungumzia suala la maduhuli yaliyobakizwa ya shilingi bilioni 6.6 na akasema kwamba hayakuonyeshwa matumizi yake akirejea taarifa ya *CAG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli *CAG* aliripoti hivyo, lakini kuna maelezo ambayo yalitolewa kuhusu fedha hizo. Fedha hizo ni fedha ambazo zinahusu makusanyo yanayofanyika kupitia *LMDA* pamoja na mifuko inayojitegemea ukiwemo mfuko wa *TWPF* pamoja na mfuko wa mambo ya kale.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazokusanywa za *LMDA*, huwa ni kiambatisho cha taarifa za fedha za Wizara na ukaguzi unapofanyika huwa inapaswa kuwa hivyo. Kwa bahati mbaya katika upekuzi wake Mheshimiwa *CAG*, jambo hili hakuliona na baadaye na maelezo yalitolewa na halikuwa jambo tena la utata.

Fedha nyingine ambazo zimezungumzwa ni zile ambazo ziko kwenye mfuko wa *TWPF*, fedha hizi ziko kwenye mfuko ambao ulianzishwa kipekee na kwa sheria inayojitegemea na ukaguzi wake huwa unafanyika kwenye mfuko wenyewe. *CAG*

aliliona hilo, lakini maelezo yalitolewa, lakini sio kwamba fedha zimepotea bali zipo kwenye hiyo mifuko ambayo nimekwishakuielezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeelezwa kwamba kuna maduhuli yasiyokusanywa ya dola 46,000 kutoka Wakala wa Utalii. Maduhuli yanayotajwa yalikuwa sio maduhuli halisi, mkaguzi alipokuwa akifanya ukaguzi wake alikusanya *working papers* na haya yalikuwa ni makisio ambayo yangeweza kukusanywa, lakini kutoka na hali ya biashara ilionekana kwamba katika makampuni 23 yaliyotegemewa kutoa maduhuli, makampuni 21 hayakufanya biashara mwaka 2008/2009.

Kwa maana hiyo, haya maduhuli sio kwamba hayakukusanywa bali ilikuwa ni *projection* ambazo zilikuwepo kwenye *working paper* zetu na hivyo baada ya wafanyabiashara baada ya kutokuwa wamefanya biashara, basi haikuweza tena kuwa sehemu ya fedha za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumezungumziwa pia mishahara isiyolipwa ya shilingi milioni 414.56. Katika fedha hizi, shilingi milioni 316.8 ni mishahara ya watumishi iliyorudishwa benki, na shilingi milioni 97 ni mishahara iliyozuiliwa na Wizara kutoka kwa watumishi waliofariki au kuacha kazi.

Mishahara isiyolipwa, yaani *un-claim salaries* ni fedha zinazorudishwa benki kutokana na watumishi ambao ama *account* zao zilikuwa hazijawa kamilifu kwa sababu walikuwa wameajiriwa mapema, au wengine walikuwa wamewasilisha kumbukumbu ambazo sio sahihi. Kwa hiyo, fedha hizi ziliwekwa benki ili kwamba baada ya kumbukumbu zao kuwa sahihi waweze kulipwa. Fedha nyingine ambazo zilikuwa zimebaki kwenye mchanganuo huu zilikwishakurejeshwa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni kuhusu shamba la *SAO HILL* kwamba halikutengewa bajeti ili kuhakikisha matumizi ya shilingi bilioni 5.1. Ufafanuzi ni kwamba shamba la miti la *SAO HILL* hupandwa miti, liko katika utaratibu wa kukusanya fedha kwa mtindo wa *LMDA.* Kama nilivyokwisha kusema awali fedha za *LMDA* hubakizwa na kutumika ili kuimarisha usimamizi wa huduma na kuhudumia shamba lenyewe.

Matumizi ya fedha za *LMDA* huonyeshwa kama kiambatisho katika hesabu za Wizara ambazo hukaguliwa na *CAG*. Changamoto iliyokuwepo ni namna ya kushirikisha wafanyabiashara wa misitu katika kujadili bajeti ya matumizi yake kwa kuwa kimsingi wadau ndiyo wamekubali kuchangia fedha hizo kwa ajili ya kuimarisha uendelezwaji wa mashamba ili yaweze kuendelea kuwepo kwa muda mrefu zaidi. Kwa hiyo, na zenyewe ni fedha ambazo zinakaguliwa na *CAG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Sakaya ni kwamba kuna fedha shilingi bilioni 1.4 ambazo zilihamishiwa kutoka kwenye Shamba la *SAO HILL* na ikaonekana kana kwamba ni pesa zimepotea. Katika utaratibu wa makusanyo ya *LMDA* sio mashamba yote yanayovunwa kwa sasa na sio mashamba yanayokusanya *LMDA* ya kuweza kutosheleza usimamizi na uendelezaji wa mashamba hayo.

Kwa hiyo, kumekuwepo utaratibu ambao unakubalika kabisa kiwizara kwamba kuna fedha zinazotolewa na kupelekwa kwenye maeneo mengine. Katika hizi ambazo zilitoka *SAO HILL* zilipelekwa kwenye vituo vya Mtibwa, zilipelekwa kwa *DFO* Mpanda, Tabora, kwa Mheshimiwa Sakaya, *DFO* Misenye, Ukaguru na Mikoko Pwani. Upungufu uliojitokeza ni kwamba baada ya *CAG* kuwa amepewa taarifa hizi au jambo hili kuwa limeonekana hakufanya *subsequent follow up* kuangalia kule zilikokwenda kama zilifika na angeweza kufanya hivyo jambo hili lingeweza kuonekana. Kwa hiyo sio kwamba zilipotea, lakini zilikwenda kusaidia kwenye maeneo ambayo hawakusanyi *LMDA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine imezungumzwa na Mheshimiwa Janeth Massaburi, yeye amezungumzia Hifadhi ya Katavi kwamba ni hifadhi muhimu. Miundombinu yake inahitaji kuendelezwa, ni wazo zuri na nimhakikishie kwamba jambo hili tunalo kwenye bajeti ya *TANAPA* mwaka huu ambao bajeti yake tunaijadili leo, zimetengwa shilingi milioni 700 kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya *Katavi National Park. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine, imezungumzwa na Mheshimiwa Diana Chilolo, ameomba kwamba Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri watembelee makumbusho ya Singida au wataalam wao ili kuona namna ya kuweza kuwasaidia. Ni ushauri mzuri ambao tumeuchukua, tutaufanyia kazi mapema iwezekanavyo, tutatuma watu wetu kuona namna ya kuweza kushirikiana na uongozi wa Mkoa.

Mheshimiwa Janeth Kahama ameipongeza Wizara, ametushukuru kwa jitihada tulizochukua za kurejesha masalia ya vitu mbalimbali ambavyo vilikuwa nje. Tuseme tu kwamba kimsingi kuna hatua ambazo zimeanza kuchukuliwa za kurejesha mali kale. Mwezi Septemba, 2009 mali kale zilizokuwa katika Taasisi ya Saikolojia ya Nairobi zilirejeshwa Mei, 2010. Serikali imerejesha sanamu ya kimakonde na jambo hili limetangazwa sana, lakini mazungumzo yanaendelea sasa hivi ya kuona namna ya kunufaika na Mjusi ambaye amehifadhiwa Ujerumani. Kwa hiyo, tunaamini kwamba majadiliano hayo yatafanikisha kusaidia Taifa kuweza kunufaika na rasilimali zake.

Mheshimiwa Dada yangu Estherina J. Kilasi ameomba kwamba kuna baadhi ya vitongoji ambavyo bado vina utata na akaomba kwa mujibu wa barua ambayo amemwandikia Mheshimiwa Waziri kwamba vimeondolewa kwenye maeneo ambayo yanahesabika kwamba yako hifadhini, kimsingi ombi lake hili tumelichukua na kwa sababu inahitaji kidogo mchakato wa kitaalam tutalifanyia kazi. Lakini kwa hakika *common sense* inaonyesha kwamba maombi yake yanakidhi haja. Kwa hiyo, tutaona namna gani kuweza kufikia azma hiyo, lakini mchakato utachukua muda kidogo mrefu.

Amezungumzia pia suala la fidia kwamba fidia zilizotolewa kwa baadhi ya wananchi wa mbalimbali zilikuwa ni kidogo, utaratibu uliotumika ni kwamba *government valuer* kutoka Halmashauri ndiyo aliyefanya *valuation* na malipo yakafanyika. Baada ya kuwa tumepokea malalamiko haya tumekuwa tukiwashauri wananchi wa Mbarali kwamba ni vizuri kuwasiliana na Halamashauri ili *valuation* kama ilikuwa ina mapungufu yoyote iweze kurekebishwa.

Lakini mara kadhaa tumepata ufafanuzi kwamba *valuation* imefanyika kwa mujibu wa sheria zilizopo. Sasa hapo kidogo inakuwa ni vigumu kwa sababu sheria yenyewe ndiyo inayosema kwamba kitu fulani kilipwe kwa *rate* fulani. Lakini sisi kama Wizara, tuko tayari kuendelea ku-*support* na pale ambapo *valuation* itaonekana kwamba kuna mtu alipunjwa basi tutafanya jitihada za kuona kwamba tunaweza tukamlipa.

Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya pia amezungumzia kwamba kuna tofauti ya takwimu kati ya asali iliyozalishwa na takwimu iliyotolewa na taasisi binafsi ya *PASS*. Tofauti ya takwimu hizi ni kwamba takwimu iliyotolewa na *PASS* ilikuwa inaonyesha *potential* na ilifanyika mwaka 1998. Takwimu ambazo zinatolewa hivi sasa zinaonyesha uzalishaji halisi ambao umefanyika.

Jambo lingine ameuliza Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya kwamba, ni mikakati gani imetayarishwa na Serikali kwa ajili ya kuwapa fursa kuwanufaisha wananchi kwa ufugaji Nyuki?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili tumelizungumzia kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 29 aya ya 62, kuna mikakati mingi ambayo imeelezwa pale, naamini kwamba Mheshimiwa Mbunge anaweza akapitia ili kuokoa muda.

Kaka yangu Mheshimiwa Felix N. Kijiko, napenda urudi na tutashirikiana na wewe umezungumzia suala la wananchi kuruhusiwa kuingia kwenye hifadhi na uliuliza swali kwenye Bunge hili hili tukasema kwamba kimsingi tunakubaliana na wazo hilo isipokuwa wataingia kwa utaratibu maalum wa vibali na siyo kuingia kiholela. Kwa maana hiyo, jambo hili tutaendelea kulitekeleza hivyo na kwa ushirikiano ambao tumeonyesha naamini tutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa mara nyingine, niseme naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitamwita Mtoa hoja - Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, utakuwa na dakika za kutaja majina halafu tunaanza kuhesabu dakika 30 baada ya kumaliza kutaja majina.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii. Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni wengi na hoja walizochangia ni nyingi hususan za maandishi. Hali hii inaonyesha wazi kwamba Waheshimiwa Wabunge wanathamini sana Wizara hii na wanathamini pia kulinda mali za asili za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru kwa ushauri walioutoa kwa kuboresha utendaji wetu wa kazi kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Napenda pia nichukue fursa hii ya pekee nitoe shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya

Bunge ya Ardhi na Maliasili na Mazingira kwani licha ya kutoa michango mingi katika kuandaa bajeti hii, kwa kweli Kamati hii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Job Y. Ndugai imekuwa na umuhimu mkubwa kwa jinsi walivyokubali na utayari wa kupokea na kushughulikia changamoto za Wizara yangu kwa moyo wa dhati na kutaka kuona mafanikio yanaonekana kwa kipindi chote cha Awamu ya Nne na hata kuchangia kujibu baadhi ya hoja zilizojitoleza leo. Aidha, naomba kumshukuru Naibu Waziri - Mheshimiwa Ezekiel M. Maige kwa kutoa majibu ya baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge na ninawatakia kila la kheri na ninafahamu kwamba kijana huyu ni hodari Mungu atamjaalia atarudi tena Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ni nyingi kuhusu Wizara yangu zimejikita katika maeneo ya migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji, kuhimiza ujirani mwema kati ya hifadhi na wananchi wanaoishi jirani na hifadhi zetu, tatizo la wanyamapori waharibifu na hatari, mahitaji ya kuibua na kuendeleza vivutio vipya vya utalii kwenye maeneo mbalimbali nchini na udhibiti wa ujangili na uharibifu wa mazingira na maliasili kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujadili hoja ya Wizara yangu, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 16 wamechangia kwa kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge 50 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, naomba kwanza niwatambue kwa majina Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuongea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Fuya G. Kimbita kwa niaba ya Kamati yeye ndiye alikuwa Msemaji. Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Alyoce B. Kimaro, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Eng. Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi na mwisho ni Mheshimiwa Ezekiel Maige - Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Wale waliochangia kwa maandishi ni kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Asha M. Jecha na Mheshimiwa Eustace O. Katagira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Oscar R. Mukasa, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Maulidah A. Komu, Mheshimiwa Abdallah, samahani hapo jina lilikuwa limeandikwa moja, sasa sikujua Mheshimiwa Abdallah yupi. Mheshimiwa Riziki Said Lulidah,

Mheshimiwa Fredrick Werema - Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Benedict Olenaiko na Mheshimiwa George M. Lubeleje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Mwanaidi A. Jecha, Mheshimiwa John Paul, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Mwanchoum A.Msomi, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Khadija S.A. Al-Qassmy, Mheshimiwa Abdullah J. Marombwa, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Basil P. Mramba na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Charles O. Mlingwa na Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa muda, ni dhahiri kuwa nitashindwa kujibu hoja zote hivi sasa. Hivyo, naomba kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwa wale nitakaoshindwa kujibu majibu yao nitawafikishia kwa maandishi baada ya ufafanuzi huu. Naomba baada ya hapo, nianze sasa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita alitoa ushauri kwamba mamlaka ya hifadhi ya mapori ya akiba ianzishwe haraka. Napenda kumjibu kwamba mamlaka hiyo itaanzishwa mwaka huu wa fedha.

Halafu Mheshimiwa Madgalena H. Sakaya yeye kuna hoja nyingi ametoa, nitajitahidi kuzijibu nitakazoweza na nitakazoshindwa nitaomba nimwandikie na kumletea. Katika hoja za Mheshimiwa Magdalena Sakaya mojawapo ilikuwa anataka kufahamu uchimbaji wa madini ya *uranium* katika pori la akiba la *Selous* na pia kwenye *WMA* ya Mbarang'ando.

Utafiti wa madini ya *uranium* katika pori la akiba la *Selous* umeanza tangu miaka ya 1970 kwa kampuni tofauti na nyakati katika kipindi hicho sheria ya zamani ilikuwa kimya kuhusu taratibu za uchimbaji wa madini. Kampuni ya *Mantry* ilipewa kibali cha utafiti wa madini kwa miaka mitatu na Wizara ya Nishati na Madini mwaka 2006. Katika ukanda wa Kusini ikiwemo sehemu ndogo ndani ya *Selous* na eneo la Mbarang'andu na *WMA.* Aidha, Wizara ilitoa idhini kwa kampuni hiyo kuingia na kufanya utafiti katika pori la *Selous* kwa kipindi cha hiyo miaka mitatu. Mwaka 2009, Bunge lilipitisha sheria ya uhifadhi wa wanyapori Na.5 ya mwaka 2009 ambapo kifungu cha 20(3) kinaruhusu utafiti wa uchimbaji wa mafuta, gesi na madini ya *uranium* kwa masharti kuwa Serikali lazima itoe kibali kufanyika kwa tathimini ya mazingira, kulipa ada na fidia ya uhifadhi.

Kilichofanyika hadi sasa ni utafiti pekee na siyo uchimbaji wa madini. Kampuni tajwa imekwishawasilisha taarifa ya tathimini ya mazingira, yaani *EIA* katika Wizara yangu, imewasilishwa jana. Kwa hali hiyo, sasa Wizara itapitia kuona kama taarifa hiyo inakidhi kabla ya kutoa kibali kwa mujibu wa sheria na kanuni zitakazokuwepo.

Suala lingine kwa Mheshimiwa Sakaya lilikuwa linahusu kuongezeka kwa ujangili wa tembo kwa sababu ya kutokuwepo mikakati mahususi ya uhifadhi. Napenda kujibu hilo kwamba maelezo hayo ya kuhusu kwamba mikakati haitoshelezi, kidogo nafikiri limekuwa halikutendewa haki na ile ya kusema kwamba tembo 50 kila mwezi wanauawa hiyo ni propaganda zilizotolewa na shirika la *EIA* nchi ya jirani na baadhi ya nchi kuzuia Muswada wa kuzuia meno ya tembo. Sasa katika hali hiyo, *TAWIRI* shirika letu la utafiti lenyewe limethibitisha na kutoa taarifa kwamba hiyo siyo sahihi na taarifa ya sensa ya *TAWIRI* ambayo pia inafanyiwa na doria imeonyesha kwamba mizoga 16 ya tembo katika kipindi cha miaka mitatu hii kwenye pori la *Selous* ndiyo ambayo iliweza kuonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimalize mchango wa Mheshimiwa Sakaya ndiyo niingie na mengine. Mheshimiwa Magdalena Sakaya pia alipenda kujua kwamba Watendaji Wakuu wa Idara ya Wanyamapori kujihusisha na ujangili bila kuchukuliwa hatua. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba watumishi wa Serikali wakivunja sheria za nchi taratibu husika hufuatwa na ikiwa ni pamoja na kufikishwa kwenye vyombo vya dola ili sheria ichukue mkondo wake. Kwa upande wa wanyamaporo kwa sasa hivi kuna jumla ya kesi 21 dhidi ya watumishi wanaotuhumiwa kujihusisha na ujangili. Kesi hizo zinahusisha watumishi wa ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Maafisa Wanyamapori.

Pia kwa sababu muda ni mdogo, hata orodha yenyewe ya hao Maafisa ambao wamejihusisha na ambao sasa hivi wako katika hatua mbalimbali za kesi, ninayo hapa, tunaweza baadaye tukaoanana nikakupatia uhakiki.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Magdalena Sakaya alizungumza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, siyo kwa ajili yeye mwenyewe.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuendelea na majibu ya Mheshimiwa Sakaya kwa sababu mengi yalitokea kwenye Kambi ya Upinzani naomba niyajibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo katika mambo ambayo yalikuwa ni hoja, Mheshimiwa Sakaya alisema kwamba uimara wa miundombinu ya barabara kwenye hifadhi ya Taifa ya Katavi alikuwa anaulizia hilo kuona kwamba barabara hizo hazikidhi.

Napenda kumfahamisha kwamba *TANAPA* imekuwa ikijitahidi kuimarisha miundombinu katika hifadhi zote za Taifa Tanzania. Kwa hifadhi ya Taifa ya Katavi shirika lilitenga kiasi cha shilingi za Kitanzania 202,850,000/= kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Kiasi hicho kimetumika katika ukarabati wa barabara zilizopo na pia barabara mpya yenye urefu wa kilomita 150 kutoka Stakile kupitia Chorwangwa hadi Lukima

ambako imeshafunguliwa. Vile vile, barabara mpya ya urefu wa kilomita kutoka Stakile kupitia Wamweru hadi Kisanga ilishafunguliwa ingawa haijakamilika. Mwaka huu wa fedha 2010/2011 kiasi kama hicho kimetengwa tena kwa ajili ya kuimarisha barabara za hifadhi na kumalizia ufunguzi wa barabara mpya zilizoanzishwa miaka iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hoja nyingine ya Mheshimiwa Madgalena H. Sakaya ambayo aliongelea kuhusu migogoro ya mipaka kwenye hifadhi, napenda kusema kwamba ili kukabiliana na tatizo la migogoro ya mipaka kwenye vijiji vilivyo karibu na hifadhi ya Taifa *TANAPA* imetenga fedha kwa ajili ya kuhakiki mipaka hiyo kwenye bajeti ya mwaka wa fedha ya 2010/2011. Uhakiki huo wa mipaka utafanyika kwa kutumia utaratibu shirikishi ambao utasimamiwa na Kamati iliyoundwa na Wizara ambapo wakati wa asubuhi wakati wa hotuba yangu niliitaja hiyo Kamati ambayo itashughulikia migogoro yote ya mipaka.

Lakini pia Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya alitoa hoja ambayo inahusu hatua iliyochukuliwa na Serikali kuhusiana na askari wa hifadhi ya Taifa ya Kitulo. Askari Natusi John aliyekuwa mtumishi wa *TANAPA* alishambuliwa hadi kufa na wanakijiji kwa silaha mbalimbali kama mapanga wakati akiwa katika shughuli za doria katika hifadhi ya Taifa ya Kitulo.

Tukio hilo lilitokea tarehe 22 kwenye msitu wa *Livingstone* ambao uko ndani ya hifadhi ya Taifa ya Katavi, watuhumiwa wa mauaji hayo wanatoka katika Kijiji cha Nyalwela. Hadi sasa watuhumiwa wote nane waliohusika katika tukio hilo walishakamatwa na kufikishwa Mahakamani. Hata hivyo, Mkurugenzi wa Mashitaka *(DPP)* aliona kuwa watuhumiwa wawili hawana hatia na hivyo kuachiwa. Watuhimiwa sita waliobakia wapo rumande na tarehe ya kuanza kusikilizwa kesi hiyo bado haijatajwa.Lakini pia uliongelea kuhusu ongezeko la ujangili wa Tembo.

Napenda kukufahamisha kwamba shirika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa mfano Jeshi la Polisi limeongeza doria zake katika maeneo ya ndani ya hifadhi za Taifa na hata nje ya hifadhi ili kukakabiliana na ujangili wa tembo pamoja na ujangili wa maliasili nyingine. Kwa mfano, operesheni iliyofanyika hivi karibuni katika Hifadhi ya Taifa, Katavi iliweza kukamata silaha 33 aina ya gobole, R4 mbili gram 16,000, risasi 138 za Gobole na Risasi sita za *SMG* zilikamatwa. Pia majangili 39 walionekana na kati ya hao 26 walikamatwa na 13 walitoroka. Operesheni kama hiyo imefanyika pia Mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye Kambi ya Upinzani kulikuwa kuna hoja nyingine inasema kwamba wanasiasa kuingilia uwekaji wa mipaka kusini mwa hifadhi ya Saadan. Mimi napenda kusema kwamba Wizara yangu itafuata sheria na pale sheria ilipo tutafuata mamlaka inavyosema. Lakini kuna wakati mwingine napenda niseme hilo wazi kunaweza wakati mwingine kukatokea katika mipaka yetu mgongano kati ya wanavijiji na hifadhi. Sasa hivi tuna uhakika kwamba watu wameongezeka kiasi fulani na baadhi ya watu wamebanana kiasi ambacho bila kufahamu wanajikuta wameingia ndani ya mipaka. Sasa ndio sababu tumeamua kuweka hii Kamati maalum au kikosikazi kwa kuweza kutatua mambo hayo yote na ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba wanasiasa

hawataingilia. Tutafuata sheria na pia makubaliano shirikishi sisi na vijiji husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, pia napenda nijibu hoja kutoka Kambi ya Upinzani kutoka kwa Mheshimiwa Magdalena Sakaya, nitalijibu nikilikuta kwa sababu naogopa muda unazidi kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijibu hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa James D. Lembeli na Mheshimiwa Job Y. Ndugai, walichangia mwanzoni na waliongelea kuhusu barabara ya hifadhi itakayopita huko Serengeti.

Mimi napenda kusema kwamba Serikali haina nia mbaya au makusudi mabaya, ni kwamba imedhamiria kutafuta njia mbadala ambayo inaweza ikaleta maendeleo kwa wananchi na pia kuweza kusambaza zaidi huduma mbalimbali. Sasa njia hii ambayo itapita Serengeti itatokea Nata hadi Mto wa Mbu kupitia hifadhi ya Serengeti. Ni njia ambayo itapitia mto wa Mbunge na kupita Tabora (B) mpaka *Clensi Camp* na kushuka katika hifadhi ambapo ndani ya hifadhi itachukua kilomita 50. Hata hivyo, napenda kusema yafuatayo:-

Bado ujenzi haujaanza kwa sababu barabara kawaida haijengwi kienyeji, lazima kuna utaalam wa aina mbalimbali unaotumika. Kwa hiyo, sasa bado kwanza kutafanywa upembezi yakinifu na baada ya upembezi yakinifu, michoro itachorwa, lakini pia tathimini ya mazingira itafanywa.

Kufuatana na hayo, ndiyo Serikali itapata ufumbuzi wa kujua barabara hii itakuwaje. Kwa wale ambao sasa hivi Serikali imeamua imeanza kujenga barabara, hayo ni majungu na ni uzushi. Serikali ni sikivu na Serikali inafahamu taratibu za kufanya kazi na lazima kwanza mambo ya kitalaam yote yatapitiwa na yatatolewa ushauri husika.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba niwatoe wasiwasi kwa jambo hilo kwa sababu wakati mwingine inaweza ikawa pia ni propaganda za wenzetu majirani huko katika kutafuta ushindani katika mambo ya utalii.

Naomba pia sasa nijibu swali la Mheshimiwa Oscar Mukasa ambaye yeye alizungumzia tatizo la tembo kwenye kijiji chake cha Nyakahura Wilayani Biharamulo. Napenda kumwambia kwamba tutakachofanya Wizara yangu tutaongeza uwezo wa kikosi cha kuzuia kupambana na ujangili kwa karibu zaidi kuwakabili tembo.

Lakini pia tutatenga fedha za kuendesha siku za msako wa wanyamapori waharibifu na pia tutaongeza idadi ya askari pori la akiba katika pori la akiba la Burigi ambalo liko Biharamulo. Pia tutaongeza idadi ya risasi huko kwa ajili ya kushughuli shughuli hizo za kudhibiti wanyama wakali, lakini pia wakiwemo tembo.

Pia tunatarajia kufanya mafunzo mbalimbali mbadala kwa ajili ya njia zingine za kuweza kuwatishia tembo wasiweze kusogea karibu na vijiji.

Kwa hiyo, kwa hali hiyo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, sisi tuko na wewe na pia tunafahamu tatizo la tembo haliko kwako peke yako liko sehemu nyingi na katika sehemu mbalimbali pia tumeshakutana mkutano wa kimataifa na wadau wote wanaohusika na mambo ya tembo kujadiliana suala la jinsi la jinsi ya kuhifadhi tembo na kwa sasa hivi pia tuna watalaam ambao wanafanya utafiti kuona njia nyingine mbadala ambayo itaweza kudhibiti tembo.

Hayo yote tumo mbioni tutakapokuwa tayari tutaweza kuyatumia na pia Waheshimiwa Wabunge tutawafahamisha kwa wale sehemu zao ambazo zinahusiana na uhalibifu wa tembo na wenyewe waweze kutumia njia hizo mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa kuna swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo ambaye yeye alitoa maombi yake ya kuhusu watalii wasipunguzwe idadi kwa sababu ana wasiwasi kwamba watapunguza kutoka 400 hadi 100.

Napenda kusema nimepokea maoni hayo na nitashirikiana na watalaam kupata ushauri ili tuone kwamba kiasi gani jambo hilo tunaweza tukalinusuru au kiasi gani cha watalii wanaweza kupunguzwa.

Pia Mheshimiwa Fuya G. Kimbita ulikuwa alikuwa na swali lako sasa hili la kwako la binafsi kuhusu njia mpya ya Masama umeomba ifunguliwe. Sasa napenda kukujibu kwamba kazi hiyo ya kuhusu njia hiyo, uwezekano wa kufungua umeshafanyika na kilichobakia ni majadiliano yatakayohusisha wadau mbalimbali ili kuweza kufanya uamuzi wa mwisho kwa ajili ya njia hiyo.

Mheshimiwa Aloyce Kimaro, yeye pia aliulizia kuhusu mapato ya Mlima Kilimanjaro ili wanavijiji waweze kunufaika zaidi na kwamba wapewe asilimia 25. Jambo hilo alishawahi kulisema tena na mimi nilipokea hayo mawazo na nilipeleka kwa wataalamu tuweze kuliangalia kwa sababu kwa sasa hivi asilimia 25 inatolewa tu kwa uwindaji wa kitalii kwenye hizi *WMAs* lakini kwenye upande wa hifadhi zetu za aina nyingine zote hii bado haijaamuliwa kutolewa. Lakini ni suala ambalo linajirudia, kila wakati tutajaribu kushirikisha pia na Wizara zingine husika tuone jambo hili tutalijadili kwa mtindo wa aina gani.

Lakini pia napenda kumfahamisha kwamba kwa sasa hivi tutaendelea na ile ile ya ujirani mwema lakini jinsi ya ujirani mwema ningependa kumshauri kwamba waibue miradi na miradi hiyo ipelekwe ili miradi iweze kufadhiliwa kuliko labda kupewa fedha kidogo mkononi. Hiyo itakuwa imenufaisha zaidi wanakijiji kuliko njia nyingine yoyote.

Pia Mheshimiwa Kimaro alikuwa anaulizia njia ile ya Maua. Kweli hiyo njia iko Kilema, mimi mwenyewe nilimuahidi, nilikwenda kuiangalia na nilipanda na hiyo njia mpaka katikati sehemu tu ya juu ya mlima lakini njia hiyo inatumika kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali. Niliwapa wataalamu wangu na wafanyakazi wangu wa *TANAPA* waangalie uwezekano wa hii njia kama inaweza kutumiwa na watalii, lakini baada ya kufanya stadi wakakuta kwamba njia hii iko karibu sana na njia ile ya Marangu na yote itafikia hatua watakutana kwenye kituo kimoja waendelee na safari.

Kwa hiyo, pale kutakuwa na watu wengi sana na msongamano na pia kutakuwa na msuguano kwa sababu idadi ya watu itakuwa ni kubwa mno na pia inaweza ikaleta athari za kimazingira. Kwa hali hiyo kwa sasa hivi hilo jambo kwanza tumeliweka pembeni tukingojea baadaye tutaweza kulitatua kwa njia gani lakini kwa sasa hivi njia hiyo kidogo itakuwa ngumu kufunguliwa kwa sasa, ila itaendelea kutumika tu kama njia ya huduma mbalimbali ambapo kwa sababu kule tunatumia gari kupanda mpaka sehemu za juu za mlima.

Mheshimiwa Niabu Spika, mimekuta swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, hili nafikiri la kwake yeye kama Mbunge ambaye anasema kutofautiana kwa takwimu zinazohusu uzalishaji wa asali baina ya zile za Serikali na Kampuni inayojihusisha na sekta ya kilimo *(PASS).* Napenda kujibu kwamba takwimu zilizotolewa na Kampuni inayojihusisha na maendeleo ya sekta ya kilimo *(PASS)* zimetoka kwenye Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya mwaka 1998 na takwimu hizo ni uwezo wa uzalishaji wa asali na nta nchini yaani *potential* tuliyonayo katika uzalishaji na sio tafiti zilizofanyika kiutaalamu kwamba hiyo ndiyo sahihi. Kwa hiyo, napenda kumfahamisha kwamba yale ambayo sisi tuliyoyatoa takwimu zetu ni sahihi kwa sababu zimefanyiwa utafiti na ndio tuko moja kwa moja katika kushughulikia shughuli nzima ya uzalishaji wa asali.

La pili, pia alipenda kujua mikakati gani imetayarishwa na Serikali kwa ajili ya kuwapa fursa na kunufaisha Watanzania katika ufugaji nyuki. Napenda kusema kwamba kwa kweli katika eneo ambalo Wizara yangu imejitahidi sana ni eneo la ufugaji nyuki. Katika hotuba yangu ya Bajeti ukurasa wa 29 aya ya 62 imeelekeza mikakati iliyopo na ambayo itaendeleza katika kuboresha ufugaji nyuki hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, yeye anasema kwamba fidia kwa wananchi wa kata ya Ilunga ambao maeneo yao yamechukuliwa na Serikali kwa kuhifadhiwa katika Hifadhi ya Kitaifa ya Kitulo. Pia wananchi hao hawajalipwa fidia tangu maeneo yao yachukuliwe zaidi ya miaka miwili iliyopita. Napenda kumfahamisha kwamba Hifadhi ya Kitaifa ya Kitulo ilipitishwa rasmi na kuwa Hifadhi ya Taifa kwa Sheria ya Bunge ya mwaka 2005. Kimsingi wakati wa mchakato wa kuanzishwa kwake Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ilirithi mipaka ya awali ambayo kwa upande wa Mwakaleli ambapo lipo eneo la Ilungu, kulikuwa na eneo la msitu wa hifadhi ya maji *(water catchment forest).*

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi hafifu uliokuwepo wakati huo kuhusiana na chanzo hicho cha maji ulisababisha wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya msitu huo kuvamia eneo la msitu na kuanza kuendesha shughuli za kilimo pamoja na mifugo pasipo kuruhusiwa na mamlaka yoyote ile. Hali hii ilidumu kwa muda mrefu na wananchii walidhani kuwa eneo hilo ni milki yao. Aidha, hakuna makubaliano yoyote yaliyofanyika ya kulipa fidia kati ya *TANAPA* na wananchi hao kwa msingi walikuwa ni wavamizi katika eneo hilo. Wapo wananchi ambao kwa kutambua hili waliamuliwa kuondoka na kwa kutambua hili waliondoka ili kupisha Hifadhi ya Taifa ya Kitulo. Eneo la Ilungu ni sehemu ya msitu wa Livingstone ambao ni chanzo muhimu sana cha maji ambacho

wananchi hawatakiwi kabisa kuharibu chanzo hicho kwa shughuli mbalimbali za kilimo na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nijibu swali la Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia ambaye yeye aliomba kuhusu barabara kutoka Ngarambe kwenda Kingupira ni mbaya na pia aliomba vijiji viruhusiwe kuvua kwa *permit* maalum wakati wa msimu. Napenda kumfahamisha kwamba nimepokea haya yote mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kuhusu barabara kwa kweli hilo ni jukumu letu na katika mpangilio wa Bajeti yetu ni mojawapo ambayo tutashughulikia na hili la kuvua naomba nilichukue nikashauriane na wataalamu. Lakini pia ameongelea kuhusu *WMA* ya Ngarambe na Tapika kwamba hawafuati fedha kwa sababu zinakwenda moja kwa moja Wizarani. Nimelipokea hilo nitamshauri mtaalamu aende akazungumze na *WMA* wajue tatizo liko upande gani ili kusuluhisha jambo hilo waweze kunufaika na fedha zao. Pia umeomba *WMA* nyingine ianzishwe nitatuma wataalamu watakuja kuhamasisha kwa ajili ya uanzishwaji wa *WMA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi yeye amesema vijiji 22 vya Wilaya ya Kilwa kuna mwekezaji anataka kuja pale kwa nguvu sana na yeye kidogo amekuwa na wasiwasi. Mimi napenda kumfahamisha kwamba sisi kama Wizara ya Maliasili na Utalii tunahusika tu na uwekezaji ambao umo ndani ya hifadhi zetu ambao vijiji havimo ndani ya hifadhi zetu, hiyo ni Halmashauri husika ndiko huko ambako zinahusika na mambo hayo. Kwa Kifunguupi ni kwamba Wizara yangu hatuna habari na huo mpango wa vijiji hivyo 22 ambavyo vinaingia huko. Lakini kwa sababu umelileta kwetu, jambo la kwanza nitaangalia kama vijiji hivyo vinahusiana na mipaka yetu vimo ndani ya hifadhi na kama ni nje ya hifadhi nakushauri kwamba jambo hilo lipeleke kwenye Halmashauri husika na pindi ikishindikana peleka kwenye mkoa husika linaweza likapata jibu lake. *(Makofi)*

Pia umesema wananchi wenye silaha unatoa ombi warudishiwe silaha zao. Napenda kusema kwamba hilo mara nyingi wanaokamatwa na silaha huwa ni aidha, wameingia kwenye hifadhi zetu na kwa sababu kule hakuruhusiwi mtu kuingia na silaha au alikuwa katika hali akatia wasiwasi, akafirikiwa huenda ni jangili au anaweza akawa ni jangili. Sasa kwa sababu umetoa ombi nitafuatilia kujua kwamba hawa chanzo cha wenyewe kupokonywa silaha zao ilikuwa ni nini. Kama inahusu kesi kwa upande wa kesi kitu cha Mahakamani hatuwezi kuingilia, lakini kama ilikuwa tu ni kwa bahati mbaya au kuna tatizo lingine lolote nakuahidi nitalishughulikia na nitalifuatilia kwa karibu. Kwa sababu yako mengi sana pia na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo aliongelea kuhusu *Airport* ya Moshi na reli ya Mombasa kuja Moshi.

Napenda kumfahamisha kwamba hayo sisi ni wadau ambao tunatumia njia hizo kwa ajili ya watalii kuja lakini kuna wahusika, wenye mamlaka hiyo ni Wizara ya Miundombinu na ambapo mimi nitachukua shauri hili nitampelekea Waziri wa Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Estherina Kilasi yeye aliongelea kuhusu fidia inayolipwa ni kidogo lakini suala hili Mheshimiwa Naibu Waziri yeye ameshalizungumzia na napenda tu kusisitiza kwamba mara nyingi fidia inayotolewa inatokana na sheria na ambapo

tunawashirikisha kikamilifu sana Halmashauri husika na ndiyo ambayo yenyewe inapanga bei gani ziweze kutolewa. Lakini pia la pili aliomba kwamba vijiji vingine vitatu vitolewe kwenye hifadhi. Napenda kumfahamisha kwamba kwa sababu hilo ni jambo la kitaalamu pia hilo tutashauriana na kuweza kuona kwamba hiyo mipaka je, bado itakuwa ya aina gani na itatoa athari za aina gani?

Mheshimiwa Emmanuel Luhahula yeye amezungumzia kuhusu ufugaji nyuki wa huko Bukombe, napenda kumfahamisha kwamba tumezingatia na pia Serikali tumeshaanzisha mradi wa ufugaji nyuki Bukombe na sasa hivi na mizinga imeshaanza kugaiwa. Mheshimiwa Felix Kijiko nafikiri Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu swali lake.

Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko yeye alitaka kuuliza kuhusu katika mapori ya misitu ya nyuki ya akiba ya *Forest Reserve* ya *Makele North South Yamkuti Kasulu* kwamba amependa kushukuru sana Wizara kupitia Kurugenzi ya Misitu kwa kutuma wataalamu kwenda huko kuona hali halisi ya mambo yaliyoko huko. Napenda nimshukuru sana kwa shukrani alizotupa na tumezipokea na pia ameomba kwamba Tume ikamilishe ripoti yake mapema ili yeye akiwa kama Mbunge aweze kupata nakala, napenda kumuahidi kwamba tutampatia nakala hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Diana Chilolo yeye aliulizia kuhusu kupatiwa mizinga 120 kama alivyoahidiwa na Naibu Waziri. Mheshimiwa Chilolo napenda kukuhakikishia na kukwambia kwamba mizinga hiyo kama ilivyoahidiwa mtaipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Basil Mramba yeye pia alizungumzia kama suala la Mheshimiwa Aloyce Kimaro la kuhusu mapato ya wananchi kunufaika na Mlima Kilimanjaro, lakini napenda kurudia ni ile ile kama nilivyosema kwamba tutaendelea na ujirani mwema. Nimejitahidi kumaliza yamebakia machache sana. Baada ya hapo naomba kutoa hoja. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Hujaomba kutoa hoja wenzio hawajakuunga mkono.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema kwa sauti ndogo. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono na hata waliopewa mizinga pia wamesimama. Waheshimiwa Wabunge, hoja hii imeungwa mkono sasa tuingie hatua inayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii

Kifunguungu 1001 – *Administration and General*…Sh. 3,414,766,400

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilielezea suala la Kilwa kwamba Kilwa inaboreshwaje kwa sababu ni mji mkongwe kati ya miji mikongwe ya Lamu Mombasa nchini Kenya, Mogadishu na Sofala. Sasa Kilwa Tanzania je, Serikali inauendelezaji mji huu?

Vile vile makumbusho ya Majimaji yapo Songea ilibidi vile vile iingizwe Kilwa kwa sababu Kilwa ndiko kulikokuwa na chanzo cha vita vya majimaji na Kinjeketile. Vita imeanza Kinjeketile ikaenda Songea. Sasa inaanzaje kuwa na Makumbusho Songea peke yake bila kuingiza Kilwa, sasa hii fedha haitoshi tunataka Kilwa iingizwe katika Makumbusho ya Majimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitaka tujue tu kwamba Tanzania inatoa kauli gani baada ya Berlin kukubali suala la kuleta *memorandum* yao ya utafiti na elimu na ushirikiano wa Makumbusho ya Tanzania na Berlin. Ahsante.

MWENYEKITI: Toka amuone huyo mjusi hamu ya kumleta hana. *(Makofi/Kicheko)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Fatma Mikidadi kama ifuatavyo; kuhusu uboreshaji wa Kilwa Wizara yangu tuna mikakati mingi na Kilwa na tuko tayari, kuna kazi ambazo tunazifanya na tunashirikiana pamoja na wafadhili wetu Serikali ya Ufaransa katika kuanza kushughulikia ule msikiti wa zamani na soko lililoko kule na pia ni sehemu mojawapo ambayo tumeisaidia sana katika utalii wa utamaduni kwa ajili ya kuweza kunyanyua utalii wa Kilwa na Kilwa ianze kuboreshwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu Makumbusho ya Majimaji. Makumbusho ya Majimaji tulianzia Ruvuma lakini pia sasa kutakuwa na sherehe maalum ya kumbukumbu ya kufikisha miaka 100 ya Makumbusho ya Vita ya Majimaji ambayo itafanyikia Kilwa na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru ndio mlezi wa hiyo.

Pamoja na Mheshimiwa Rais ameombwa kuwa mgeni rasmi kama atakuwa na nafasi atakwenda huko pia na sasa tunaanza kushughulikia Makumbusho ya Majimaji na baadaye tutaanza kujua kiasi gani ya yenyewe tuyaweke katika hali ya Makumbusho.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa kila mtu atakuwa na *issue* moja tu. Huyu kwa sababu ya huyo mjusi wake ndiyo maana nimemruhusu mawili.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifunguungu hicho hicho. Wakati nimechangia kwa maandishi niliwaomba Wizara kutueleza juu ya maombi ambayo tumewasilisha Wizarani kupitia Mkoa na Wilaya ya Singida kuomba kibali kuwaruhusu wananchi waweze kunywesha mifugo yao kwenye mabwawa yaliyo kando kando ya mbuga ya Muhesi. Mabwawa hayo ni Itwaga na Kiengegi. Wananchi wa maeneo hayo ya Ipande sasa hivi wanakabiliwa na ukame mkubwa sana na kama mnavyojua mwaka huu mvua hazikunyesha vizuri maeneo mengi. Kwa hiyo ninachoomba ni kupata maelezo au majibu kuhusu ombi hilo.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi imewekwa kwa kufuata Sheria na Sheria hizo ni Waheshimiwa Wabunge ambao mliweka sasa kweli nakiri kwamba katika mchango wako umeelezea kuhusu ombi hilo lakini kwa bahati mbaya kwa ajili ya muda mdogo hatukuweza kumaliza baadhi ya majibu lakini jibu ni kwamba jambo kama hilo hatuwezi kukurupuka na kusema ndiyo kuna mambo mengi ya kuangalia kuona athari mbalimbali na haya mabwawa mawili yako umbali gani na shughuli zingine za wanyama. Lakini nakumbuka kwamba umeniomba aidha, mimi au Naibu aje na tumekubaliana kwamba Naibu anakuja na nimeshamruhusu. Atakapokuja mtaangalia na suala hilo. *(Makofi)*

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka Waziri anipe ufafanuzi kwa nini katika Wilaya yangu hususani katika Kata ya Chita mpaka ambao umedumu kwa takribani miaka 56 ulibadilishwa kati ya kijiji cha Makutano na Shule ya Sekondari ya Chita na kuathiri wananchi kama 400 wanaolima katika Bonde lile. Mpaka huo ulishawekwa alama ya mitiki kwa kupandwa lakini ghafla mpaka ukahamishwa ukapelekwa katikati ya mashamba ya watu kiasi cha kuwafanya wananchi waishi kwa wasiwasi kwa kuwa walikuwa wanalima miaka yote hii katika bonde hili. *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo nalifahamu na Mheshimiwa Mbunge tulishawahi kulijadili hilo na kazi hiyo niliwatuma *TANAPA* waweze kulishughulikia na tujue tutafanyaje. Kazi za kwenye mipaka ni nyingi sana kwa hiyo, kila kitu kinakwenda kwa awamu lakini pia napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sasa hivi suala hilo litakwenda haraka kwa sababu zaidi ya *TANAPA* wenyewe kuweza kuzunguka kila sehemu, tumeunda kikosi kazi na chenyewe kitakwenda. Sasa naomba nimhakikishie kwamba nilitoa ahadi kwamba wamemaliza Tabora, wanakwenda Geita wakitoka Mkoa wa Geita sasa watakuja mkoa wako wa Morogoro. *(Makofi)*

MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba nianze kwa kumshukuru Waziri kwa kujibu hoja za Kambi ya Upinzani vizuri sana na nyingi amejitahidi ila najua kwa sababu ya muda ambao umekuwa mdogo ameshindwa kujibu baadhi ya hayo. Lakini kuna hoja ni ya muhimu sasa ambayo tukipatiwa majibu hapa kwa sababu inahusiana na maisha ya wananchi, inahusiana na suala zima la wafanyakazi wa waliokuwa wa kiwanda cha *Nkanda SaoHill* cha Tanga ambacho kilibinafsishwa mwaka 1998 kwa Inisho. Wafanyakazi hawa

wameachishwa kazi 75 na hadi hii leo hawajalipwa mafao yao wanashindwa kurudi nyumbani na wanahangaika. Tungeomba Serikali itupatie majibu katika hilo. *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jibu la haraka sasa hivi sitakuwa nalo na nisingependa kutoa ahadi ya uongo. Naomba nilifuatilie hili na niweze kujua sababu zenyewe ni nini na nitakujibu kwa maandishi au hata kwa kupigia simu nikupe hali halisi ilivyo na kama ni jambo la kuweza kutatulika mimi mwenyewe nitasimamiwa litatuliwe kama litakuwa ni uwezo wa Wizara yangu pia nitatoa ushauri wangu litakuaje. Ahsante.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wakati nachangia hotuba ya Bajeti nilizungumzia tatizo ambalo sasa hivi linagubika mashirika ya hifadhi ya Ngorongoro na *TANAPA* kuhusiana na maamuzi mbalimbali ambayo Serikali inakuwa inayatoa hasa hasa michango ambayo mashirika haya inakuwa inatoa kwa Serikali kwa maelekezo ya Hazina. Lakini pili michango ya kikodi ambayo haizingatii gharama ambazo mashirika yanakuwa yameingia kwenye miradi ya kimaendeleo ndani ya zile hifadhi. Kwa mfano, ujenzi wa barabara, ujenzi wa miradi ya umeme na kadhalika.

Lakini pia maamuzi kama haya yanapotoka maana yake ni kwamba mashirika yanakuwa hayana fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ya ujirani mwema na sisi kama Wabunge ambao tunatoka kwenye maeneo ambayo yana hifadhi inakuwa hatupati fedha za kutosha za miradi ya ujirani mwema kwa sababu fedha nyingi Serikali inakuwa imezielekeza maeneo ambayo hayahusiani moja kwa moja na uhifadhi na Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma kwa mara mbili mfululizo imekuwa ikitoa mapendekezo na yakipitishwa na Bunge kufanya mabadiliko ya suala kama hili na hakuna majibu yoyote ambayo Serikali imekuwa ikitoa. Wizara ya Maliasili na Utalii inasema nini kuhusiana na hali hii ambayo inahatarisha sana uhifadhi? *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru Mheshimiw Kabwe Zitto kwa kuweza kutumia uzoefu wake akiwa kama Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na masuala hayo. Lakini pia napenda niseme yafuatayo, tukichukulia mfano wa Shirika mojawapo ikiwa kama ni *TANAPA* zaidi lazima ichangie Serikalini kwa sababu haya mashirika yote yako pale kwa ajili kuzalisha kipato ili Serikali iweze kutumia kwa kazi nyingine mbalimbali. Lakini pia *TANAPA* yenyewe inahitaji kufanya maendeleo, ni lazima iwe endelevu katika kuwekeza katika mambo mbalimbali ya miradi yake ili kuhakikisha kwamba inakuwa endelevu. *(Makofi)*

Lakini la tatu pia mimi napenda kusema kwamba sidhani kwamba *TANAPA* au Ngorongoro au mapori ya akiba yatashindwa kutoa pesa kwa ajili ya ujirani mwema kwa sababu ya michango mingine. Mimi nafikiri hilo nitawauliza haya mashirika ambayo yako chini ya Wizara yangu. Kwa kweli uwezo wa pesa wanazochangia kwa ujirani mwema hazina matatizo na wana uwezo nazo. Kama ni sababu mojawapo kwamba ni hiyo, hapana. Napenda niseme hapana labda kuna aina moja au nyingine mambo hayakai sawasawa, lakini naomba mimi niyafuatilie. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ni jambo la kisera hilo. Kama sera imeamua asilimia ngapi kwa majirani na asilimia ngapi kwa Serikali itakuwa haina ubishi. Sasa naona kuna wakareketwa wengi wa mpira hapa. Brazil *out,* Uholanzi goli mbili Brazil goli moja. Kwa hiyo tunaendelea. *(Makofi)*

MHE. DANSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 51 wa hotuba ya Waziri anasema Wizara itajenga kituo cha doria katika eneo la Mtambaswala, Wilayani Nanyumbu na Daraja la Umoja, hilo naomba niwapongeza na ninawashukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia kuhusu kero kubwa ya tembo Wilayani kwangu. Nilisema kwamba watu wamekufa mwezi uliopita na vilevile nikaomba Wizara iongeze nguvu kusaidia, kwa kweli Wilaya ya Nanyumbu tupunguze hii kero ya tembo kwa sababu inaharibu mali na wananchi wanapoteza maisha. Lakini vilevile niliomba nyavu kwa ajili ya wanyama waharibifu kama nyani na ngedere.

MWENYEKITI: Kwa sababu na Mheshimiwa Mukasa ana tatizo la tembo hebu uliza.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Nina mambo matatu nitaongea kwa haraka.

MWENYEKITI: Ni moja.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, kwenye orodha ya mikakati ambayo Mheshimiwa Waziri ametusomea inaingia akilini lakini suala lenyewe linahusu maisha ya watu na mali zao na hivi tunavyoongea inawezekana tembo wanaandaa mkutano usiku Nyabugombe na vijiji vingine, yapi machache kati ya hayo ambayo kwa kweli yatakuwa ya kufanyiwa kazi kwa haraka na kwa dhararu wakati tunasubiri mengi yakamilike ?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru Mheshimiwa Danstan Mkapa, huyu ni mdau wangu wa muda mrefu kwenye mambo ya tembo na nilishaidhinisha mpaka gari akapelekewa kwa ajili ya kusaidia katika uhifadhi na kuwafukuza tembo. Lakini sasa suala la tembo kwa upande wa Kusini pia linaweza likawa lina kero zaidi kwa sababu kule tuna mpaka wa kwenda mpaka Nyasa ambako ni Msumbiji ile ni *corridor* ambayo tembo wanatoka *Selous* wanakatisha kule kwenu ndiyo wanakwenda Msumbiji.

Kwa hiyo, pale suala hilo litaendelea kuwepo lakini nguvu ambayo sasa tunaweza kuongeza ni kwamba nitashauriana na Mkurugenzi wa Wanyamapori ili tuweze kuona uwezekano wa kuweza kujenga kituo badala ya Halmashauri peke yake kuwapeni gari na silaha labda pia tujenge na kituo ili tuweze kuleta na askari wa kuja kukaa kule kwa sababu baada ya muda kweli lile eneo litakuwa ni mojawapo ya eneo lenye vurugu na ndiyo sababu tumeamua kujenga hicho kituo kingine tulichokwambia. *(Makofi)*

Kwa upande wa Mheshimiwa Mukasa, la kwanza kabisa la kuanzia ni lile ambalo tutashauriana na Halmashauri yako kusaidia kuongeza risasi na la pili nitashirikiana na nitamshukuru Mkurugenzi wa Wanyamapori alete hata askari wa muda kuja kuwafukuza hao tembo baada ya hapo ndiyo tutaendelea na yale mengine niliyokwisha yatamka. *(Makofi)*

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi naomba kwa ruhusa yako tu kwanza niwape hongera sana ndugu zetu wa *TANAPA* kwa mradi wao mzuri wa ujirani mwema ambao wametujengea Maktaba pale Kasulu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, maktaba ya kisasa kabisa ambayo nina hakika ni ya kisasa katika ukanda wetu wa Magharibi kwa maana ya Kigoma na Tabora. *(Makofi)*

Mimi langu dogo sana naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, katika mchango wangu wa maandishi niliuliza kuhusu haya maeneo tengefu. Kwenye hotuba yake ukurasa wa 50 amezungumzia maeneo tengefu mawili kuendelezwa kwa mwaka 2010/2011. Amezungumzia eneo tengefu la Ziwa Natron na *Kilombero Valley*, Mheshimiwa Waziri hakuendelea akaweka nukta.

Naomba kumkumbusha kwamba Maragarasi ni eneo tengefu ambalo pia ni uhai wa *Lake Tanganyika Basin* na Maragarasi asilimia 80 liko katika Jimbo langu. Sasa sijui kama ali-*over sight* au sijui ni kitu gani? Naona kwenye hotuba yako umezungumzia Wilaya 10, ukazungumzia Wilaya tatu, Natron, Kilombero na Ulanga. Lakini kwenye *development* naona kuna fedha karibu 1.3 kwa ajili ya *development* ya maeneo tengefu. Nataka niwe na hakika katika hizo Wilaya kumi eneo tengefu la Maragarasi na kwenye chepechepe ya Kasulu imeingizwa? *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba katika hizo Wilaya 10 na Wilaya ya kwako imo. *(Makofi)*

MHE. ESTHERINA J. KILASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na sina haja ya kutoa mshahara. Kwa upande wa mipaka namshukuru Waziri na wataalam wake kwamba wanalishughulikia sana na wataalam wake wanalishughulikia kwa karibu sana na wananchi wamesikia wamefurahi. Naomba nitoe ufafanuzi kuhusu fidia kwa sababu majibu yetu yamekuwa yanatofautiana na Halmashauri wanatelewa vibaya. Swali limekuwa likiulizwa kwamba pesa zilizoletwa Mbarali kwa maana ya fidia ya shilingi bilioni sita zile jibu linalotolewa na Halmashauri kwamba walengwa wote sawa walilipwa. Lakini kwenye upande wa mapunjo uko pale pale. Kuna watu ambao mashamba yao hayakufanyiwa tathimini, nyumba hazikufanyiwa tathimini inavyopaswa na hata miundombinu ambayo ni ya Halmashauri kwa mfano shule, misikiti na majengo pesa yake ni ndogo. Shule nzima huwezi kulipa shilingi milioni tatu au tano au tisa yenye madarasa saba. Kwa hiyo malalamiko yako pale pale na kwa sababu Halmashauri walishirikishwa tu wakisaidiana na watu wa ardhi kufanya tathimini na pesa ikaletwa na ikalipwa na Halmashauri.

Kwa hiyo, ninalozungumzia mimi ni wale ambao bado mashamba yao ambayo hayajafanyiwa tathimini na hawajalipwa na wengine wamelipwa kidogo sana. Yako zaidi ya 100 pale Halmashauri na mengine tumewapelekea watu wa *TANAPA* wanafahamu ndicho ninachokizungumzia. Lakini mkisikia kwamba kila kitu kimelipwa, sisi hatupingani na viwango, tunachotaka ni kile mtu anachotaka kulipwa. Nina shamba heka 100 je, nimepewa, ndiyo suala ambalo liko pale Halmashauri wanajua, Madiwani wamekaa, tumeshafanya tathimini. Sasa tunasubiri *TANAPA* waje washirikiane na Halmashauri wale watu walipwe, wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu. *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukumbuka kwamba kuna wakati Mheshimiwa Estherina Kilasi alinifahamisha kwamba kweli kuna watu wamepunjwa fidia zao na kuna baadhi ya watu walisema kwamba walipewa mpaka shilingi 15,000 wengine shilingi 7,000 lakini nilifuatilia hilo kwa *TANAPA.*

Mheshimiwa Mwneyekiti, *TANAPA* wakasema pesa zote zilikabidhiwa Halmashauri na Halmashauri walipoulizwa ndiyo wakawa wanasema kwamba wenyewe ndiyo wamefuata Sheria. Lakini hata hivyo mimi napenda tu nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa naomba kwa wale wote ambao wamepunjwa na wale ambao hawajapewa kwa kusahauliwa au kwa wale ambao tathimini bado inafanywa ili walipe, sasa naomba tukubaliane tuorodheshe kila mmoja tujue tutaifanyia nini. Lakini naomba sasa kwa wale ambao wamepunjwa Mheshimiwa atusaidie wajitokeze na kila mmoja akiri amepewa shilingi ngapi ili tuweze kujua kwamba huenda kweli watu wamedhulumiwa na tuweze kujua. Ndiyo sababu mimi napenda twende chini zaidi kuhakikisha kwamba haki imetendeka.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, wataalam wenu na wale wakutane wakalitatue hili kwa sababu inawezekana hatuelewani katika kusema hapa. Kwa hiyo, wakutane kusudi waweze kupata majibu.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uwezo wa juu aliouonesha Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na jinsi walivyoonekana kwamba Wizara hii ina-*team work,* mimi sina shida ya mshahara bali napenda tu kupata maelezo kwamba Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba atatuma wataalam au wao wenyewe kuja kuona makumbusho ya Singida.

Je, watakuwa tayari kuja kuangalia pia vivutio mbalimbali vilivyopo mkoani Singida kwa mfano *centre* ya Tanganyika iko Manyoni Sukamahela. Kuna kitu kimewekwa juu ya mlima na Wajerumani hatujui ni kitu gani, lakini Wizara iKifunguika pale wanaweza wakaona namna ya kupanda kuona kuna nini pale, inasemekana kuna mali iko pale. *(Makofi)*

Vilevile kuna jiwe kubwa ambalo lina sanamu kama Yesu vitu ambavyo watalii wanaweza wakashawishika kwenda kule na kuna mapango ya Kijerumani ambayo wamezika mali humo ndani. Sasa kwa ajili ya kuona makumbusho na mengine mtaunganisha ili na sisi Singida tuingie kwenye chati ya vivutio vya kuleta watalii? Lakini pia nashukuru sana, kwa kukiri kwamba mizinga 120 tutapata. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Unajua ukikaribisha mgeni akisema anakuja wewe ndiyo unatengeneza ratiba. Mheshimiwa Naibu Waziri maelezo.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana mama yangu Mheshimiwa Diana Chilolo kwa pongezi nyingi ambazo ametupa na katika mchango wake ametuomba twende na kama tulivyomwambia ni kwamba tutaenda. Na nimhakikishie kwamba ni nia ya Wizara kuhakikisha kwamba tunaibua au kutambua vivutio vyote vya utalii kwenye maeneo mbalimbali nchini, changamoto ambayo tumekuwa nayo ni rasilimali fedha na hivyo tumekuwa tukiweka vipaumbele kwamba tuanze na maeneo gani, lakini kwa ombi mahususi la Mbunge na kwa sababu tayari tuna ratiba ya kwenda kule haitakuwa na tatizo sana kupeleka wataalamu wa utalii wakaambatana na wale wataalamu wa makumbusho wakaenda wakafanya hiyo kazi kwa pamoja, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wataalamu watakapokwenda wataifanya hiyo kazi pia. *(Makofi)*

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimezungumzia juu ya Kambi ya Mateso ya Mlele na matumizi yake lakini pia nikajikita katika eneo la *WMA* ya Ubende. Pamoja na maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa sasa hivi katika kujibu hoja mbalimbali kwamba kuna Tume ambayo itasimamia na kuangalia migogoro iliyojitokeza kati ya wananchi na Hifadhi lakini nina hofu kubwa sana kwamba itachukua muda mrefu kuweza kutanzua migogoro hii kwa maelezo yake kwamba wakitoka Geita watakwenda Morogoro na sijui lini watakuja Rukwa, nataka Mheshimiwa Waziri awaeleze wananchi wa vijiji vya Kapalamsenga, Sibwesa, Mbugani, Kakesa, Itenka A na Itenka B, Kapanda, Ibindi na Stalike ni lini Serikali itamaliza mgogoro wa tatizo hili la *Ubende Wild life Management Area. (Makofi)*

WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hilo kumalizika kwake ni kwamba mpaka tukaone hiyo mipaka imekaaje. Kwa sababu *WMA* baadhi ambazo mpaka sasa hivi tumeshindwa kumaliza na tatizo kubwa ni mipaka. Aidha, mipaka kati ya wenyewe na Hifadhi au mipaka ya vijiji kwa vijiji wana hitilafiana katika kutoa sehemu za *WMA*, sasa kwa sababu hili zaidi limehusiana na *WMA* basi sasa kwa kuanzia Mheshimiwa Said Amour Arfi, ninamtuma Mkurugenzi wa Wanyamapori ambaye *WMA* ziko chini yake, yeye na afisa wake watakuja kuliangalia hilo suala na *WMA* hiyo. *(Makofi)*

MHE DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi sikusudii kutoa shilingi lakini *sub-vote 101* nafikiri Mheshimiwa Waziri atakuwa ameona Wabunge wengi tulivyozungumza. *Selous Game Reserve* ni *game reseve* kubwa duniani na ni rasilimali kubwa sana kwetu, sisi tunataka tupate maelezo fedha zinazoingia kwa shuguli za utalii pale siyo zinazorudi kuendeleza utalii au kuendeleza *infrastructure* yaani kuendeleza eneo la uhifadhi kwa hiyo, tulitaka tupate maelezo kulikoni. *(Makofi)*

WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mapori ya akiba mengi lakini kubwa ni hilo la Selous, lakini tukiyajumlisha yote yanaweza yakafika

mpaka karibu 30. Lakini haya mengine bado hayana uwezo wa kujitegemea kwa hiyo, *Selous Game Reserve* ndiyo ambayo inayatunza na kuyalea haya ma-*game reserve* mengine. Lakini napenda kusema kwamba sasa hivi kwa sababu Sheria ya Bunge mmetupitishia na mmeturuhusu tuanzishe Mamlaka ya haya Mapori ya Akiba wakati huo tutakapoyaanzisha katika mwaka wa fedha au kama nilivyoahidi ndiko huko sasa tunaweza tukatengeneza *structure* nzuri ya kuhakikisha kwamba kila *game reserve* inaweza kuwa na mapato ya kujitegemea na kuweza kuwa *independent* kuliko kwa hivi sasa, kwa hali hiyo ni kwamba hela nyingi ya *Selous Game Reserve* ndiyo inalea *Game Reserve* zingine. *(Makofi)*

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa ujumla kwa jinsi wanavyotupa ushirikiano Bukombe. Lakini katika haya nilikuwa nauliza tulileta Bajeti ya shilingi milioni 78 za kuchimba Lambo la Nsangu kwa ajili ya wafugaji ambao wanaishi kando kando ya Hifadhi ya Kigosi Myowozi na lambo hili tulitegemea lingenufaisha wananchi wa kijiji cha Nsagwe, Nyashimba na Busambiro lakini mpaka leo bado hawajaanza uchimbaji wa lambo lile.

Sasa nilitaka kujua ni lini pesa zile zitaletwa kwa ajili ya kuchimba lile lambo ili hawa wananchi wasiendelee kuingia kwenye Hifadhi ambako kuna mto mkubwa sana haukakuki uko kilomita moja kutoka Kijijini au mtupe kibali sasa wafugaji wale kwa sababu ni kiangazi wakanyweshe kule mifugo yao wakati mnajiandaa kuleta fedha.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu na kutoa ufafanuzi anaouhitaji Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, nianze kumpa pole sana kwa matatizo aliyopata, nashukuru kumuona anaendelea vizuri na nina muomba Mungu aendelee kumbariki ili tuendelee kuwa naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi kuhusu kuchimbiwa Bwawa la Nsangu tulishayapokea na mara kadhaa tulishazungumza na kaka yangu kumueleza kwamba mfuko wa *TWPF* ulikwisha tenga fedha kwa ajili ya shughuli hiyo na kwa mara ya mwisho mazungumzo ambayo yalikuwa yakiendelea ni kati ya mfuko na Halmashauri ili wawapatie watu wa mfuko *account* kwa ajili ya kutuma fedha za kuanzia mradi huo, kwa hiyo, liko kwenye hatua ya mwisho kabisa kilichobaki ni suala tu la utendaji na kwa sababu Mkurugenzi wa Wanyamapori yuko hapa ambaye ndiye Mkurugenzi wa mfuko basi naamini katika muda mfupi ujao fedha zitaweza kutumwa tayari kuna shilingi milioni 25 za kuanzia ambazo tumekwisha tenga. *(Makofi)*

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja kuhusu uchimbaji wa madini katika Hifadhi ya Selous ni suala *very serious.* Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba suala hili kibali kilitolewa mwaka 2006 na kwamba Sheria ilikuwa kimya kuhusiana na uchimbaji wa madini kwenye hifadhi na kwamba wale watu wa kampuni ya *MANTER* wameleta taarifa jana tarehe 1 Julai, 2010 kuhusiana na suala la taarifa hii ya *Environmental Impact Assessment,* lakini hifadhi hii Serikali inajua kwamba iko kwenye *UNESCO* na ni hifadhi ya kihistoria tangu mwaka 1982 kwa hiyo, kitendo cha kukubali utafiti wa madini tayari kinyume cha taratibu kwa sababu tayari tuna mkataba na *UNESCO* wanasema kabisa kwamba sehemu yoyote ambayo ipo

kwenye ule mkataba hairuhusiwi aina yoyote ya shughuli ambayo italeta uharifu wa rasilimali ama viumbe vilivyoko kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa nini inaendelea na mchakato huu hata baada ya Sheria kuwepo kwa sababu Sheria ikishapitishwa na Rais akishasaini ni Sheria tayari, kwa nini bado wanaendelea kumruhusu kwenye mchakato wa *EIA* wa kufanya utafiti wakati Sheria imekataza na hili ni eneo la kihistoria la dunia siyo Tanzania yenyewe? *(Makofi)*

WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009 haijakataza kuchimba madini lakini Waheshimiwa Wabunge wenyewe waliruhusu madini ambayo ni *strategic* ambayo waliamua ni ya aina tatu tu yaani *uranium, gas* pamoja na mafuta kama nilivyosema hapo mwanzo kuwa wakati huo mwaka 2006 hawa *MANTER* walipoomba waliomba kwa Wizara ya Nishati na Madini kwa sababu sisi kwa upande wa Maliasili kulikuwa hakuna sheria yoyote inayozuia au inayokubali kwa hiyo, ilikuwa ni jambo la kawaida sasa hawa walipokubaliwa wakati huo kwa sababu sisi Maliasili ni kwamba mteja yeyote ambaye anataka kuja kufanya utafiti wa madini anatokea Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu akija wanaomba *permit* aweze kuingia kufanya utafiti na kwa wakati huo aliruhusiwa afanye huo utafiti na kwa sababu ule utafiti ulikuwa unaendelea lakini na kwa bahati kwamba sheria tuliyoipitisha iliruhusu kwamba utafiti wa *uranium* unaweza ukafanyika na kwa sababu walishaingia gharama ya kulipia kwa ajili ya yeye kufanya utafiti inabidi amalize. Lakini kama nilivyosema ni sisi tumepata hiyo *EIA* ambayo alitengeneza sasa tunasubiri tuisome *EIA* inasema nini na baada ya pale sisi tuna uchungu wa manbo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuna uchungu kwa sababu tuna mkataba wa *UNESCO* kwa sababu hiyo pia inaweza ikatuletea matatizo mengine. Lakini pia tuna uchungu na nchi kuweza kupata kipato cha kutosha, sasa hayo yote sisi tutayaangalia lakini tunachosema ni kwamba Wizara yangu haijakubali chochote kwa hiyo, hatujakubali chochote kwa sababu na ninyi mmetoa ushauri na kila ushauri sisi tutaendelea kuupokea, unaweza kutusaidia kuboresha jinsi ya kutoa jibu ili tuwashauri wenzetu wa Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

MHE. MWANAWETU S. ZARAFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilielezea kuhusu vijiji 22 vya Lindi na Wilaya ya Kilwa. Mheshimiwa Waziri amenijibu kwamba hiyo inahusu Halmshauri ya Kilwa sawa nakubali lakini vijiji hivi na mchakato huu unaoendelea na vikao vya dharura pamoja na *full council* za dharura hivi vijiji vinahusu madhumuni ya huyu mwekezaji ni kufuga wanyama kama simba, tembo na wanyama wengine na vijiji vingine viwili hivi vya Kiswela ambavyo vijiji vyote vinachukuliwa Kiswele na Lushungi ni kwa ajili kuweka vivutio vya utalii kama *beach* hivi na hoteli, sasa nataka kuuliza hivi pia Wizara ya Maliasili na Utalii siyo sehemu yao kujua? Kwa sababu inasemekana kwamba inahusu Halmashauri lakini hivi vitu

ninavyovitaja ufugaji wa hawa wanyama inahusiana na utalii na ninyi mmenieleza kwamba haviwahusu, nataka kujua ufafanuzi wake ni nini kwa nini haviwahusu?

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1) inasema "Iwapo zimesalia dakika 10 kabla ya kufikia muda wa kuahirisha Kikao cha Bunge na Kamati ya Matumizi bado haijamaliza kupitisha mafungu, Mwenyekiti kuongeza muda usiozidi dakika 30 bila kuihoji Kamati ili kumaliza shughuli ya kupitia mafungu yaliyobakia" kwa hiyo, nitaongeza muda wa dakika 30 Mheshimiwa Waziri maelezo.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurudia jibu lile lile, nafikiri Mheshimiwa Mbunge huenda hakulipata sawasawa, sijasema kuwa hatuhusiki nimesema kwamba sisi tunahusika na sehemu za uwekezaji ambazo zimo ndani ya hifadhi zetu ikiwa vijiji 22 viko ndani ya hifadhi, sasa hilo litatuhusu lakini kama vikiwa nje ya hifadhi sasa hapo mamlaka wanayo Halmashauri, lakini kwa mimi ninavyofahamu kwa sababu jambo hilo halijafika ofisini kwetu huenda haviko katika **h**ifadhi vingekuwa ndani ya hifadhi tungeshirikishwa moja kwa moja na ndiyo nikasema moja kwa moja na mimi nitalifuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kama anataka kuweka wanyama sisi katika Sheria hii ya Wanyamapori tumeruhusu kwamba watu wanaotaka kuanzisha *sanctuary* za wanyama, kuanzisha *zoo* za wanyama inaruhusiwa. Ili mradi wataomba kibali maalumu kwetu na wataalamu wetu watakwenda kuchunguza waone kweli kama kuna athari yoyote au panafaa kufanya kitu kama hicho kwa hao hata kwetu hawajaja kwa suala kama hilo kwa sababu watakapokuja pia na sisi tutakuja kuchunguza kuona kama kweli pale mahala panastahili kuweka simba, pale mahala panastahili kuweka hiki na hiki hiyo na sisi tutatumia utaalamu wetu kuchunguza na tukiona haifai tutaawambia kuwa haifai, lakini napenda kusisitiza Mheshimiwa Diwani ingawa kwa bahati mbaya ndiyo tunaumalizia au diwani sivyo nilitakwa kusema kwamba kwenye Halmashauri wewe kule nenda kashinikize kwa sababu inaweza ikawa hilo suala humo kwenye Halmashauri nyie wenyewe Madiwani mnazungukana**.** *(Makofi)*

MWENYEKITI: Na zaidi ya hapo nafasi yetu kama Wabunge ni *institution* ya juu sana na hizi Halmashauri nazo ni *institution* za juu sana katika maeneo yao, sasa wewe uko huku wao wanakaa kule. Kwa kawaida wenzio huwa tunakimbia kwenda kuanzia kule maana huwezi kuanzia huku uka-*block* wale wengine wanaofanya kazi zao huenda wao wenyewe wanazo sababu wewe ambazo huzifahamu kwa hiyo, hili ndiyo maana Waziri ni vizuri ukaanze kule kule mtabishana pale pale na mtaelewana vizuri zaidi. *(Makofi)*

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina swali dogo sana kwa Mheshimiwa Waziri kama kumbukumbu zangu ni sahihi, mwaka jana wakati Wizara hii inawasilisha Bajeti yake hapa nilizungumza kwa uchungu sana kuhusu bei ya misitu ya Serikali. Kama kumbukumbu zangu bado ni sahihi mwaka jana tulikwenda ofisini kwa Waziri Mheshimiwa Shamsa Mwangunga akatuambia yeye mwenyewe alikuwa anashindwa kununua mbao kwa sababu gharama ni kubwa, sasa

swali langu ni kwamba iwapo Waziri anashindwa kununua mbao hivi huyu mwananchi maskini wa Tanzania atanunuaje mbao na Serikali ina mpango gani wa kupunguza bei ya misitu.

WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mheshimiwa Benito Malangalila alikuja na timu ya wadau ambao ni wadau wetu sisi wa Chama cha Uvunaji wa Miti na Mbao wa huko Iringa na ni kweli kabisa walipokuja malalamiko yao ilikuwa ni kuhusu mbao hazishikiki bei kwa sababu miti wananunua kwa bei kubwa na sababu zenyewe ilikuwa ni kwamba kulikuwa kuna tozo inatozwa mara mbili ambayo tulikuwa tunaita *VAT. VAT* ya kwanza wanatozwa kabla ya kuvuna mti na *VAT* ya pili inatozwa baada ya kuwa imekuwa mbao yaani *final product* lakini pia kulikuwa na tozo nyingine la *LMDA* ambalo hilo tunatoza sisi kwa ajili ya ile kata mti panda mti, wakikata miti ile sisi inabidi tena tupande lakini pia tusafishe na barabara na kuweka mandhari ikae vizuri, katika makubaliano yetu pale mimi nilimwambia kabisa kwamba la *LMDA* sisi tuna uwezo nalo kwa sababu liko chini ya Wizara yangu na niliwauliza wale wadau aliokuja nao mnataka iweje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakasema tunaomba ipungue mpaka 70 kwa 100 na ndivyo hivyo tumepunguza mpaka 70 kwa 100. Lakini ukija kwenye upande wa *VAT* mimi nilileta Serikalini na pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha nilimkabidhi suala hilo kwa sababu yeye ndiyo atashughulika na suala hilo pamoja na *TRA* na alinipa ahadi kuwa suala hilo analishughulikia kwa hiyo, sasa halipo chini ya mikono yangu liko katika Wizara ambayo inahusika na mambo ya *VAT* lakini pia napenda kusema kwamba bei ya sasa hivi kidogo hali ya msitu pale hata watu na wavunaji kwa sababu sisi tulifanya utafiti kwa sababu watu walikuwa wanashindwa kuvuna na bei ya mbao kutoka Malawi ilikuwa ni ndogo kuliko bei ya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaamua kupeleka wataalamu wetu wakachunguze Malawi kuna nini. Wakaenda wakaa na wenzetu wa Malawi kumbe Wamalawi walikuwa wanapata hasara juu ya hasara, walikuwa hawatozwi chochote. Lakini tulivyowaelimisha na wenyewe sasa wanatoza na tangu wameanza kutoza sasa bei ya mbao zao imepanda na sasa hivi sisi shamba letu wateja wetu wanavuna vizuri na zimekuwa *hot cake* kwa maana ya kuwa wanazikimbilia. *(Makofi)*

(Kifunguungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*…….Sh. 954,874,400
Kifungu 1003 – *Policy And Planning*…….Sh. 3,735,478,400
Kifungu 1004 – *Education, Information and Communication*….....Sh. 111,637,700
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*…..……Sh. 265,224,500
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*…..Sh. 277,877,600
Kifungu 1007 - *Legal Unit*……..Sh. 105,839,000
Kifungu 1008 – *Management Information System*…..Sh. 230,000,000
Kifungu 2001 – *Wildlife Development*…..……...Sh. 13,847641,900

Kifungu 3001 – *Forestry and Bee keeping*……..Sh. 16,419,781,100
Kifungu 4001 – *Tourism*……...Sh. 11,520,590,700
Kifungu 4002 – *Antiquities*……..Sh. 4, 515,268,300

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 69 -Wizara ya Maliasili na Utalii

Kifungu 1001 – *Administration and General* ……..Sh. 577, 816,600
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*…… Sh. 399,735,600
Kifungu 2001 - *Wildlife*…….Sh. 3,549,483,200
Kifungu 3001 – *Forestry and Bee keeping*…….Sh. 5,472,964,600
Kifungu 4001 – *Tourism* ……...…….Sh. 62, 260,000
Kifungu 4002 – *Antiquities Unit*……..…….Sh. 45,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)
(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoa hoja, taarifa.

WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lililokaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake ya kujadili hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011. Naomba sasa taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono naona sasa mmeshaendelea mnaunga mkono watu wote wanaoamini hivyo. Siyo wajibu wa Mawaziri kuunga mkono ni wajibu wa Wabunge wote. Kwa hiyo, hoja hii imeungwa mkono sasa nitawahoji na wote wameafiki. Kwa hiyo, Makadirio ya Wizara ya Maliasili na Utalii yamepitishwa na Bunge hili rasmi na sisi tunapenda tuwapongeze kwa dhati Waziri na Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii na kama

mnavyofahamu Wizara kama hii haihitaji mvua, haihitaji kulima na haitaji mbolea bali suala zima la kusimamia kizalendo maliasili zetu kwa manufaa ya Watanzania. Waheshimiwa Wabunge, na kila senti inayopitishwa hapa ikafanye kazi inayostahili, nadhani tutatoka hapa tulipo na kufika mahli pazuri sana. Tunawapongeza kwa kazi zote mlizozifanya. *(Makofi)*

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa Fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Kesho ni siku ya Jumamosi, tutakuwa na Wizara zifuatazo ambazo zitawasilisha Bajeti zao itakuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, hawa watasoma hotuba zao ataanza Waziri wa Afrika ya Mashariki na baadaye Waziri wa Mambo ya Nje halafu na Wenyeviti watasoma hivyo hivyo tutaingia kwenye mjadala pamoja halafu mwisho tunapitisha *vote* baada ya *vote* nyingine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu Jumamosi zetu zinaisha, siku zinaisha kwa *speed* sana, kwa hiyo, inabidi tuunganishe Wizara mbili kwa hiyo kesho asubuhi tutaanza na hizi Wizara mbili. Tunaomba Waheshimiwa muwahi kufika, najua hakuna maswali kwa hiyo ya kuwachangia motomoto muwahi hakipo, lakini basi mjitahidi saa tatu tuwe hapa. Waheshimiwa Wabunge naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

(Saa 1.50 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku Jumamosi, Tarehe 3 Julai, 2010 saa tatu asubuhi)